Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 7 Agosti, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka 2010/2011 *(The Annual Report and Accounts of Arusha International Conference Centre for the Year 2010/2011).*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2011/2012 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

**MHE. CECILIA D. PARESSO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Kazi na Ajira Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

# MASWALI NA MAJIBU

Na. 334

## Posho kwa Wenyeviti wa Serikali ya Vijiji

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA** aliuliza:-

Kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha Wenyeviti wa Serikali za Vijiji kutopata posho zao za kila mwezi wakiwa ndio wasimamizi wakubwa wa miradi ya maendeleo katika vijiji vyao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wenyeviti hao posho yao ya kila mwezi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu makubwa ya Wenyeviti wa vijiji na Mitaa, Halmashauri zimekuwa zikilipa viwango vya posho ambavyo hutofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine. Viwango vya posho vinalipwa kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri na hivyo kutofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine. Ili kuboresha kiwango hiki Halmashauri zimesisitizwa kuhakikisha zinaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka 2012/2013 imerejesha ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa baada ya kuonekana ni kero kwa kiasi cha shilingi bilioni 63.5. Kurejeshwa kwa ruzuku hii kutawezesha Halmashauri kumudu uendeshaji wa ofisi ikiwa ni pamoja na kulipa posho za Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji. Mpango wa Serikali ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri iil kuwezesha ulipaji wa posho kwa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji.

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Lakini pamoja na majibu hayo nilikuwa na swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri nyingi nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji uwezo wake wa kukusanya mapato na vyanzo vyake vya mapato ni duni sana.

Je, Serikali haioni sasa kuwa kuna haja ya kuziangalia upya Halmashauri zile ambazo hazina uwezo ili iweze kutoa ruzuku iweze kuwapatia viongozi hawa wanaongoza vijiji vyetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdul J. Marombwa Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili tatizo analosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli limekuwepo. Labda nieleze kwamba ni kwa nini lilijitokeza, mwaka jana na mwaka huu wa fedha uliopita, Serikali ilikuwa imeondoa hiki chanzo ambacho tumekisema hapa, kulikuwa kuna kitu tunakiita *nuisance taxies* tulifuta ile halafu baadaye Serikali ikaweka ruzuku pale.

Lakini mwaka jana Waheshimiwa Wabunge walikumbuka hapa kwamba ruzuku ile ilipoondolewa ilibakia bilioni 10 tu na ndio iliyoleta matatizo hayo ambayo yanasababisha Mheshimiwa Marombwa azungumzie jambo hili. Nina hakika Wabunge wengine wote watakaosimama hapa watasemea jambo hilo.

Lakini katika Bajeti hii tunayoizungumzia sasa tumepitisha hapa, tumeiomba Serikali irudishe kitu kinachoitwa the *general purpose grant,* hii ndio inayotumika kwa ajili ya kuendesha ofisi, kwa ajili ya mambo ya *re-tooling,* mambo ya *capacity building* na mambo mengine yanaingia mle ndani.

Hii ni pamoja na hizi posho ambazo zinazungumzwa za Wenyeviti zinazosemwa hapa ambazo zinasaidia sasa kwenda kusaidia hizo Halmashauri ambazo Mheshimiwa Mbunge, anaziona wakati mwingine kwamba ziko hoi ndio maana yake, hii hela ya shilingi bilioni 65.5 ambayo mmempitishia Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio inayokwenda kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Naelewa anachosema kwamba ni kweli Halmashauri hizi zinatofautiana lakini kilichosemwa hapa ni kwamba tuimarishe mapato yetu ya ndani na humu ndani msije mkasahau tumepitisha tena na maamuzi mengine makubwa na posho za madiwani zimepita na vitu vingine vya namna hiyo.

Kwa hiyo, napenda kumwambia Mheshimiwa Marombwa tunashukuru kwamba unatukumbusha kuhusu wajibu wa hawa watu muhimu, wenyeviti wa vijiji wanafanyakazi nzuri hata kule kwako Mheshimiwa Spika, Njombe kule Wenyeviti wa vijiji na Mitaa wanakazi nzuri sana. Kwa hiyo, tuombe hii itakapokuja sasa muisimamie vizuri ili mhakikishe kwamba Wenyeviti wa Vijiji wanaweza wakapata hizo posho zao kama tulivyoeleza hapa.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa anachosema Naibu Waziri katika Halmashauri zetu hawana habari kwamba fedha za ruzuku zilizorudishwa zinapaswa kuwalipa wenyeviti wa vijiji. Je, Serikali sasa itaweka amri kwamba kila Halmashauri iwalipe Wenyeviti wa Vijiji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido na jirani yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyosema hapa ndio tunasema hivyo, ndio tunawaambia hivyo, ndivyo tulivyosema wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anapitisha Bajeti yake hapa alisema kwamba *general purpose grant* inarudishwa hapa kwa ajili ya kwenda kufanyakazi hiyo.

Sasa nasema hivi sasa tunawaambia Halmashauri hela zinapokuja, hela hizi ni pamoja na kwenda kuwapa posho Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa. Kwa hiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nasema hapa mtu yeyote atakayekwenda kinyume na maelekezo yanayotoka hapa huyu ajue kwamba sisi tutashuka naye jumla jumla.

Haiwezekani Bajeti imepitishwa na Waziri Mkuu anasema kwamba hii ni pamoja na kufanya kazi hiyo wala hututegemei kwamba wale wenyeviti wa vijiji ambao walikuwa wanadai ambao wanaonekana kwamba hawajalipwa tunaambiwa kwamba hawajalipwa *no way.* Tutafuatilia na Mheshimiwa Lekule Laizer pamoja na Wabunge wote tunaomba mtusaidie kuwaambia hela hizi zinapelekwa kule ni pamoja na kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri *circular* ndio zinafanya kazi siyo maneno peke yake.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilitaka kuuliza swali ambalo mwenzangu Mheshimiwa Lekule Laizer ameuliza, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Na. 335

**Upungufu wa Walimu na Vifaa Shule za Nkasi Kusini**

**MHE. DESDERIUS JOHN MIPATA** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini wameitikia wito wa ujenzi wa shule ya Sekondari kwa kila Kata lakini bado shule hizo zinakabiliwa na changamoto za upungufu wa walimu, vitabu vya Sayansi ya Jamii *(Arts),* madawati, ukosefu wa madawati ukosefu wa maabara na madarasa ya kidatu cha V na VI:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza kabisa tatizo la ukosefu wa walimu na vitabu vya sayansi ya jamii *(Arts)?*

(b) Je, Serikali itakubaliana na ushauri wa kupanua na kuziwezesha shule za Sekondari za Kate, Chala na Wapembe ili ziweze kupokea wanafunzi wa Kidato cha V na VI?

(c) Je, ni lini tatizo la ukosefu wa maabara litatatuliwa katika shule za sekondari nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu A, B, na C kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa wananchi, Serikali na wadau wa maendeleo katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa na shule ya Sekondari mpaka ngazi ya Kata umeleta mafanikio ya ongezeko la shule za sekondari kutoka shule 1,745 (2005) hadi kufikia 4,367 (2012) ambazo kati ya hizo 3,337 ni shule za Sekondari ni Serikali na 1030 ni shule binafsi.

Mafanikio haya yameenda sambamba na kuongezeka kwa mahitaji ya walimu, miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeongeza idadi ya vyuo vya ualimu, vyuo vikuu na udahili katika kozi za ualimu pamoja na kuajiri walimu kadri wanavyofaulu.

Mkakati huu umewezesha Serikali kuajiri na kuwapanga katika shule za sekondari walimu 9,226 (2010/2011) na walimu 12,188 (2011/2012). Serikali itaendelea kuajiri walimu na kuwapanga katika shule kadri wanavyohitimu na ifikapo mwaka 2014 upungufu utakuwa umekwishafika zaidi asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari, Serikali imekuwa inatenga fedha za ruzuku ya uendeshaji (*Capitation*) katika shule za sekondari. Mwongozo wa matumizi ya fedha hizi unaelekezwa asilimia 50 kutumika katika ununuzi wa vitabu ambapo walimu wenyewe huonesha mahitaji ya vitabu husika. Mwaka 2012/2013 jumla shilingi bilioni 41 zimetengwa kama ruzuku ya uendeshaji (*Capitation*) kwa shule za sekondari hivyo shilingi bilioni 20.5 zitatumika katika ununuzi wa vitabu.

(b) Mheshimiwa Spika, ongezeko la wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne limesababisha ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano. Shule za sekondari Chala, Kata na Wapembe zinahitaji kuboreshwa ili kukidhi vigezo vya kuwa shule za *A' Level.* Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina shule moja ya kidato cha tano na imedhamiria kuzipandisha hadhi shule za sekondari za Kate na Milundikwa kuwa kidato cha tano na sita.

Mwaka 2011/2012 Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 61 kwa shule ya sekondari Kate ili kukamilisha mapungufu yaliyobainishwa na wakaguzi wa shule katika kuifanya shule hiii kuwa na kidato cha tano na sita. Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa mchango mkubwa alioutoa katika kuikamilisha shule ya sekondari Kate kuwa ya *A' Level* ambapo alichangia jumla ya shilingi milioni 5 nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012 Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa Maendeleo ilitumia jumla ya shilingi biiloni 30 katika Halmashauri zote kukamilisha miundombinu mbalimbali ya shule ya sekondari. Kati ya hizo shilingi bilioni 3.5 zilitumika kujenga Maabara 127 ambapo shilingi milioni 72 zilitumika kujenga maabara katika shule za Kate na Mkole zilizopo Wilayani Nkasi. Aidha, shule za Sekondari Mtenga, Mkanolo na Kipande zilizopo Nkasi.

Aidha, Shule za Sekondari Mtenga, Mkanolo na kipande zilizopo Nkasi ni mojawapo ya shule zilizonufaika na shilingi bilioni 3 zilizotolewa katika Halmashauri zote kununua maabara hamishika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi bilioni 7.8 zimetengwa na Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa maabara nchini.

**MHE. DESDERIUS JOHN MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Pamekuwepo na upungufu mkubwa wa walimu katika mwambao mzima wa Ziwa Tanganyika katika Shule za Sekondari na msingi naomba Serikali ilishughulikie kama tatizo maalum kwa sababu upungufu ulioko ni upungufu ambao si wa kawaida ukilinganisha na sehemu zingine?

(b) Hivi Sasa Halmashauri zote karibuni zimesimama kufanyakazi za maendeleo kwa sababu ya kutofanya malipo kwa kile kinachoitwa kuingia kwenye Mfumo wa *EPICA* jambo ambalo limeleta usumbufu mkubwa katika Halmashauri. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa shughuli hizo zilizosimama za Serikali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

La kwanza la upungufu wa mkubwa wa walimu ni kweli kwamba bado tuna mahitaji makubwa ya kupata walimu kwenye shule zetu za msingi hata sekondari na tunatambua mkakati tulionao wa kuwezesha shule zilizopo pembezoni mwa Tanzania kwamba zina upungufu mkubwa pia.

Lakini nashukuru pia kurudia kauli ya Naibu Waziri wa Elimu ambayo aliitoa hapa juzi kutambua mahitaji ya walimu kwenye maeneo ambayo yana upungufu mkubwa.

Alishauri Waheshimiwa Wabunge na popote pale ambapo Wakurugenzi wanatusikia kwamba kama iko Halmashauri ya Wilaya inao upungufu mkubwa wa walimu lakini na vijana ambao wangependa wapate mafunzo ya ualimu wenye sifa na kuombewa nafasi ya kuja kufundisha kwenye Halmashauri husika jambo hilo linawezekana ili kukabili upungufu.

Tunachokifanya sasa mgao tulioufanya mwezi Januari mwaka huu 2012 na Februari mwaka huu 2012 tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kwamba walimu hawa tunaowapeleka kwanza wasambazwe kwenye shule zilizoko pembezoni ili zile shule zilizoko katikati ya Makao Makuu ya Wilaya tukiamini zitapata walimu kwa njia ya kuhamia lakini pia wajaze kwenye shule zile ili zisipate upungufu mkubwa. Hilo tumelifanya hivyo. *(Makofi)*

Hili la pili la usumbufu ambao Halmashauri nyingi nchini zinakumbwa kwa mfumo wa mabadiliko ya Mfumo wa *EPICA* ni kweli tatizo lipo katika Halmashauri nyingi na tumeendelea kupata taarifa hiyo lakini Halmashauri na Makao Makuu ya TAMISEMI inawasiliana na Hazina ili kuimarisha mfumo huo ili Halmashauri ziondokane na tatizo ambalo sasa lipo. *(Makofi)*

**MHE. MCH. ISRAEL YOHANA NATSE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Nina swali dogo la nyongeza.

Ni kweli tatizo la walimu ni kubwa kwa nchi yetu na ni kweli Serikali inawekeza fedha nyingi kusomesha walimu. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi pamoja na kuboresha mazingira ya walimu, walimu wanaomaliza mafunzo wanapangwa kazi, wanaripoti wanaondoka?

Serikali ina mpango gani wa makusudi kuhakikisha kwamba kuna *Bond* kati ya walimu na Serikali angalau hata kufanya kazi kwa miaka mitano pale

anapopaswa kuwepo kabla ya kuondoka kwenda kwingine na mkakati wa kurudisha mikopo hiyo inakuaje, maana Serikali haijatuambia kama kuna mikataba? Watupe kauli. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Natse, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya ushauri wa kuwawekea *Bond* au kufanya makubaliano na wale ambao wanakubali kwenda kwenye ualimu, ili wanapomaliza wafanye kazi ya kusomesha kwa miaka kadhaa, ni ushauri mzuri, tunaukubali Serikalini, tutaufanyia kazi kwa kina, ili tuweze kulimaliza tatizo hili la upungufu wa walimu katika shule zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini hili la pili la utaratibu wa kurejesha mikopo. Utaratibu huu tunaendelea kuukazia kwa kusimamia Bodi ya Mikopo kwa umakini zaidi kwa sababu, Bodi ina majukumu mawili, kutoa mikopo, lakini pia kukusanya marejesho ya mikopo ile. Hivi karibuni tutawasilisha Bungeni, marekebisho ya Sheria ambayo nia yake ni kuwabana zaidi wale ambao wamekopa waweze kurudisha mikopo hiyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tutakapokuja na marekebisho hayo, tutaomba mtusapoti ili tuweze kuwabana zaidi wale waliochukua mikopo, sio tu walimu, hata ambao sio walimu wamefanya kozi mbalimbali. *(Makofi)*

Na. 336

## Tatizo la Maji Kata ya Kakese

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kakese ni Kata mpya ambayo ina matatizo mengi hususan maji:-

Je, Serikali, iko tayari kuondoa kero ya ukosefu wa maji katika vijiji vya Mwamkulu, Kakese, Kakese Mbugani, Kawanzige na Kamakuka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshiwa Spika, Kata ya Kakese inajumuisha Vijiji vya Kakese Mbugani, Kamakuka, Kawanzige, Mwamkulu na Mkwajuni yenye jumla ya wakazi wapatao 29,620. Wananchi hawa wanapata huduma ya maji kutoka kwenye visima vifupi 2 na visima virefu 4. Upatikanaji wa maji safi na salama ni 5% ya mahitaji ya wakazi wa Kata hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo, Halmashauri katika mwaka wa fedha 2012/2013 imeomba fedha nje ya ukomo wa Bajeti kiasi cha shilingi milioni 90 kwa ajili ya ujenzi wa visima 5 vikiwemo

visima katika vijiji vya Kamakuka, Kakese mbugani na Mkwajuni katika Kata ya Kakese. Vijiji vilivyobaki vya Kawanzige na Mwamkulu vitaendelea kujengewa miundombinu ya maji kwa kadri rasilimali fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nimeyapokea majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa masikitiko makubwa sana. Inaonesha ni namna gani Serikali, haijatilia nguvu katika suala la kuwapatia wananchi wake maji; iwapo wakazi wa Kata ya Kakese ni 5% tu ya watu 30,000 watu 6,000 wanapata maji. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, amesema kumekuwa na ombi nje ya ukomo wa Bajeti. Nataka atuhakikishie kwamba, ombi hilo limekubaliwa na fedha hizo zitapelekwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, tatizo hili linavigusa vijiji vyote vitano (5) na mpango ni kujenga, kuchimba visima virefu vitano (5).

Je, unaweza ukaiagiza Halmashauri kwamba, sasa visima hivyo 5 visambazwe katika Vijiji vyote 5 vya Kata ya Kakese?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi namwomba Mheshimiwa Said Arfi, asijisikie vibaya, maana amesema anapokesa kwa masikitiko. Haya maeneo nimekwenda, nayafahamu. Serikali, ikikiri kwamba, ni 5% tu ya wananchi wanapata maji safi na salama hapa, maana yake ni *realization,* maana yake unakiri kwamba, kuna tatizo hapo, yaani kwa kusema tu kwamba tunajua kwamba, kuna tatizo pale. Hatuwezi kusimama hapa tukapingana na Mbunge hapa, tukasema hakuna tatizo pale. *Only 5%* ndio wanapata maji safi na salama, *which means* Chuchuri, Siminyo, Tegu na kila kitu, ndio huko kwa sababu, huna hakika na maji wanayokunywa pale.

Mheshimiwa Spika, nataka niliambie Bunge hili, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Halmshauri hii, inazo bilioni 2.5 ambazo zimetengwa. Yeye hapa, ameji-*confine* kwenye hiyo Kata inaitwa Kasese, ndio anayoizungumza hapa na ambayo ndio anaipigia kelele na anasema kwamba, sasa tutoe zile hela. Ile *procurement* imeshafanyika, *no objection* imeshafanyika na vijiji vile nitaenda nikacheki mle ndani kama hivi Vijiji anavyovisema vimo au havimo. Kwa hatua hii tuliyofika hapa kwamba, unaweza ukabadilisha ile, *it is not possible,* nitakuwa naongopa hapa. Tunachoweza kufanya hapa na ndicho alichouliza, nimemwuliza Mkurugenzi Mtendaji, hizi milioni 90 zimepitishwa?

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapa leo, nakwenda kuzitafuta hizi milioni 90 hizi, ili twende tukamsadie kwenye hilo eneo maana sina hakika kwamba, wao wale wameshapitishiwa. Kwa hiyo, anasikitikia hapo,

usisikitike, sisi tutakusaidia jambo hili, tutakuondolea tatizo hilo lililoko hapo. Kwa hiyo, wewe utembee hapa wala usiwe na wasiwasi, Serikali, inajua kwamba, kuna tatizo pale. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Katika Kata ya Kabungu, Tarafa ya Kabungu, kuna tatizo kubwa sana la maji, hasa katika Vijiji vya Kasinde, Vijiji vya Kamsanga, Nyagala na Kijiji cha Sijonga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tatizo hilo ni kubwa sana na liko jirani na Vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini, alizungumzia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abwao, rudi kule ulikokaa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Je, Serikali, iko tayari kupeleka huduma hiyo ya maji katika Vijiji hivyo tajwa nilivyovitaja?

**SPIKA:** Anasema viko jirani, mimi sijui. Haya, hebu jibu, nadhani ulipotembelea uliviona.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii hapa anayoisema hapa, itabidi niende nikacheki. Ninachokumbuka ni kwamba, Waziri wa Maji, alipokuwa ana-*wind up* hapa,

alitwambia tupunguze hivyo vijiji vibakie vitano vitano, ndio maelekezo aliyokuwa ametoa. Sasa kuna wengine ambao walikuwa wamekwenda zaidi ya vijiji vitano.

Mheshimiwa Spika, kwa vile imejitokeza hapa, ninaomba nimwahidi Mheshimiwa Kakoso, tutakwenda kucheki kwenye hii orodha kujua kwamba, vimeingia au havikuingia, ili tuweze kujua kwamba, tunafanya nini kusaidia hivyo vijiji vyake. *(Makofi)*

Na. 337

**Matibabu ya Ugonjwa wa Saratani Kutolewa Bure**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Tatizo la ugonjwa wa Saratani limekuwa ni tishio kwa Watanzania na Dunia nzima, lakini matibabu yake pamoja na dawa zake hutolewa kwa gharama kubwa:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kutoa bure kabisa matibabu na dawa za ugonjwa huo, hasa ikizingatia kuwa idadi kubwa ya Watanzania, bado ni maskini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Nchi, imeainisha kuwa huduma za uchunguzi na tiba aina zote za saratani kwa waginjwa wote ni bure. Tiba hizo ni pamoja na upasuaji, mionzi, dawa za kemikali na vichocheo na zimekuwa zikitolewa bure katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* Hospitali ya Rufaa Bugando na Rufaa za nje ya nchi, mfano India.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti ya serikali, dawa zinazonunuliwa zimekuwa hazitoshi kukidhi mahitaji ya wagonjwa wote wa saratani kwa muda wote wa tiba, hivyo huwalazimu wengine kununua dawa pale zinapokosekana Hospitalini, ambapo dawa hizo ni ghali sana. Kwa mfano; saratani ya utumbo mpana inagharimu kiasi cha shilingi 300,000/= kwa sindano moja, na hivyo mgonjwa atahitaji sindano 12 ambazo gharama yake kwa jumla ni milioni 3,600,000/= na mara nyingine wagonjwa huendelea na tiba ya awamu ya pili, ambayo ni ghali zaidi. Kwa wagonjwa ambao ni wanachama au wategemezi wa wanachama wa mfuko wa Taifa wa Bima ya afya, dawa hizo zimekuwa zikilipwa na Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara, inawashauri na kusisitiza kwa wananchi wote kwamba, ni muhimu kuchunguza afya kila mwaka na pale ambapo huduma ya kupima dalili za Saratani zinatolewa, wananchi washiriki kwa wingi kwa sababu, kugundulika mapema, kunaongeza fursa ya kutibu. Juhudi za kuimarisha utambuzi huo katika ngazi za Rufaa na Mkoa zinaendelea, tiba ya mionzi na tiba ya dawa, vyote vinaimarishwa. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Majibu ambayo Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa jumla, wameona hali halisi jinsi wanavyoendelea kuathirika na gonjwa hili, ambalo limekuwa tatizo kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Tanzania, tumekuwa na wanawake wengi ambao wako vijijini. Waathirika wakubwa wa gonjwa hili ni wanawake, ukizingatia wanapata sana kansa ya kizazi na kansa ya titi. Uchunguzi unaofanywa ni kwa wale ambao wako katika maeneo ya karibu. Wanawake waliko Vijijini, si rahisi kufikiwa kupata huo uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Je, Serikali, inaonaje kuanzisha vituo vya uchunguzi katika kila Wilaya, ili wananchi waweze kugundua matatizo yao mapema kabla hayajafikia katika *stage* kubwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Watanzania wengi wanaathirika sana na tatizo hili. Na kwa kuwa, tiba ya ugonjwa huu, Mheshimiwa Waziri, kakiri kwamba, ni ghali sana dawa zake na si rahisi kwa Mtanzania kuweza kupata 300,000/= kwa kila sindano.

Je, Serikali, inaonaje, ingeanzisha utaratibu kama vile gonjwa la *UKIMWI* lilivyopewa uzito? Ugonjwa huu ukapewa uzito mkubwa, ili wananchi waweze kupatiwa matibabu bure? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Riziki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, wagonjwa wa saratani ni wengi na ni kweli, utambuzi wa haraka wa mapema, juu ya saratani yenyewe unasaidia sana katika kutoa tiba za awali ambazo zinakuwa nyepesi na sio ghali. Serikali, imeongeza juhudi hizi kwa kuanzisha vituo karibu 81, vikihusisha vituo vya afya pamoja na zahanati, katika kuwapa mafunzo Wataalamu waliko pale katika kutambua saratani za matiti na zile za shingo ya kizazi, ili zenyewe ziweze kuchangia katika kutoa matibabu mapema, kuwagundua watu mapema.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Serikali, inatambua kwamba, wagonjwa wengi wanaopelekwa nje ya nchi zaidi ya 30% ni wagonjwa wa saratani. Kwenye bajeti ya mwaka huu Waheshimiwa Wabunge, mmetoa ridhaa kwa Serikali, kupitisha bajeti ambayo inaongeza fedha katika Taasisi yetu ya *Ocean Road,* ambayo itanunua mashine nyingine ambazo zitapunguza idadi ya wagonjwa ambao watakuwa wanalazimika kupelekwa nje ya nchi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, saratani si ugonjwa wa kuambukiza, lakini, mara mtu apatapo ugonjwa huu ni ngumu sana kupona. Je, Serikali, inakabiliana vipi na magonjwa ya kuambikiza kama *EBOLA,* ambapo hivi

karibuni, tumesikia umeingia kwa majirani zetu wa Uganda?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali tulilokuwa tunajibu hapa ni swali la ugonjwa wa saratani, ambalo limo katika kundi la magonjwa yasiyoambukiza. Lakini kwa vile, mwenzetu ametaka kufahamu juu ya ugonjwa wa *EBOLA,* taarifa tumezitoa, lakini kwa kutoa taarifa tena hapa Bungeni, ni kwamba, kwa sasa ugonjwa huu upo Uganda na Tanzania, tulikuwa na mgonjwa ambaye alikuwa anakisiwa kuwa na ugonjwa huo. Mpaka sasa, katika uchunguzi ambao amewekwa huyo mtoto pamoja na mama yake na daktari, ambao wamewekwa katika eneo la uangalizi, huyo mtoto anaendelea vizuri na bado haijathibitika kwamba, tunao ugonjwa wa *EBOLA* nchini kwetu.

Lakini tahadhari zote zimechukuliwa na Wataalamu wetu wako katika maeneo yote ya mipaka, ili kuweza kuhakikisha mgonjwa anapotaka kuingia kwenye nchi yetu, anaweza akatambulika mapema na hatua stahili zinaweza zikachukuliwa mapema. *(Makofi)*

Na. 338

## Huduma za Afya Bure kwa Wazee

**MHE. MICHAEL L. LAIZER K.n.y. MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** aliuliza:-

Iko Sera ya Kuwapatia Huduma ya Matibabu Bure Wazee, lakini huduma hiyo imekuwa ikilalamikiwa na wazee kuwa, hawapatiwi huduma hiyo kikamilifu:-

Je, Serikali, ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa, huduma hiyo inatolewa kikamilifu kwa walengwa mahali popote nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishiniga Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kuwepo kwa malalamiko kuhusu wazee kutopatiwa huduma za afya kikamilifu kama inavyoelekezwa katika Sera na Miongozo mbalimbali. Sera hii ya kuwapatia wazee huduma za afya bila malipo, imekuwa haitekelezwi kikamilifu kwa sababu mbalimbali, ikiwemo upungufu wa Wataalamu, vifaa na dawa ambayo ni malalamiko kwa wagonjwa wa makundi mengine.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ili kuboresha huduma kwa makundi mbalimbali, Serikali, imefanya mapitio ya Mwongozo wa Uchangiaji ambao uko katika hatua za ukamilishwaji ambapo mwongozo huo umetoa mapendekezo ya matibabu bila malipo kwa wazee walio na umri wa miaka 60 na kuendelea. Aidha, usimamizi wa utekelezaji wa Sera ya kutoa Huduma za afya kwa Wazee bila Malipo utaimarishwa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja dogo la nyomngeza. Kwa kuwa, hawa Wazee, Serikali, imekiri kwamba, wanalalamika kila wakati. Na wakati mwingine utata wa uzee unaleta matatizo.

Je, ni kwa nini wasipewe vitambulisho, kila mzee mwenye miaka 60 na kwenda juu, awe na kitambulisho cha kumtambulisha kwamba, anahitaji huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba kutoa jibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumekwishakuzielekeza Halmashauri zote kwamba, ziandae orodha ya wazee wote waliko katika Halmashauri na tumewaambia kwamba, wafungue Dirisha Maalum kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, tunatoa maelekezo hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, kwamba, Halmashauri zote zifanye hivyo. Ni vizuri kuwa na vitambulisho, na vitambulisho vinavyosemwa sio hivi vya Taifa, ni vitambulisho vya Halmshauri, ambavyo vitawatambua

hawa wazee na wapate hizo huduma kutoka ngazi ya Zahanati mpaka katika ngazi ya rufaa.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ninashukuru majibu yote yaliyotolewa pande zote mbili kwa Naibu Waziri *TAMISEMI* na Naibu Waziri wa Afya. Lakini tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na kumekuwepo na mkanganyiko aidha, ni nani atoe kitambuslisho hicho.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali, iko tayari kulieleza Bunge hili, kwamba, mpango uliopo wa kuwapata hao wazee utaanzia ngazi ipi? Na utachukua muda upi? Ili kupunguza malalamiko ya wazee hawa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba kutoa majibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wote mzima unafanyika kutoka ngazi ya vitongoji, vijiji, mpaka unapofikia katika ngazi ile ya Kata na Halmashauri. Ninataka nimthibitishie hapa kwamba, hili jambo limekuwa halifanyiki kwa sababu, ni kweli kwamba, hatujakuwa na orodha ya hawa wazee kama ilivyokuwa imezungumzwa. Sasa Serikali, imetoa maelekezo kwamba, tuwatambue hawa wazee na tutoe vitambulisho.

Kwa hiyo, mchakato wake unaanzia kutoka kule Kitongojini na Watendaji wote wa Kata wanatakiwa wafanye hivyo, ili orodha ijumuishwe pale katika Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji, awe na hiyo orodha ya wazee, ili waweze kuhudumiwa kama ilivyoelekezwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunioa. Kama Mheshimiwa Naibu Waziri, ambavyo amejibu kwenye swali la msingi kwamba, moja ya sababu zinazochangia huduma hii kwa wazee, akina mama wajawazito na watoto ishindwe kupatikana ni kutokana na ukosefu wa vifaa pamoja na dawa.

Kama tunavyojua wenye jukumu la kusambaza hizi dawa na vifaa ni *MSD,* lakini *MSD* wamekuwa wakitoa visingizio kwamba Wizara inachelewesha kupeleka fedha za kuagiza vifaa na dawa. Je, kwanini Hazina isipeleke fedha moja kwa moja kuliko kupitia Wizara ya Afya ambako yanacheleweshwa?

Yaani sina uhakika lijibiwe namna gani. Kwa sababu hii inazungumzia fedha wale wazee ni identity zaidi kuliko hiyo dawa, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, jambo hili tulipokuwa tunapitisha bajeti hapa tulizungumza wote zipo hela ambazo zinatoka kupitia Halmashauri kupitia mfuko wa *NHIF* na ziko hela ambazo zinakuja moja kwa moja kutoka

Serikalini na hizi zinatoka kutoka katika Wizara ya Afya. Sasa hizi *MSD* zimeanzisha maeneo ya kanda ambapo kule kumeanzishwa kitu kimoja kinaitwa *integrated logistic system.* Hiyo *integrated logistic system* kazi yake ni kubaini aina ya matatizo yaliyoko kule. Sasa najua swali linaloulizwa hapa linauliziwa kuhusu hela tumekubaliana kwa utaratibu huo kwamba hizi hela zitakuwa zinaelekezwa katika Halmashauri.

Lakini hizo zilizotengwa zitakuwa zinakwenda kule na wale zinazotoka katika Wizara ya Afya zitapelekwa moja kwa moja na Mheshimiwa Mwinyi yupo hapa anafahamu kwamba zitakuwa zinapelekwa moja kwa moja kwenye *MSD* ili kuona kwamba tatizo hili haliendelei kutokea kama ilivyokuwa kule nyuma lakini zinatokea katika Halmashauri.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda niongezee majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba fedha zikitoka Wizara ya Fedha zinapita Wizara ya Afya kabla ya kwenda *MSD* kwa hiyo nadhani mchelewesho hautokei Wizara ya Afya kwa sababu hatuna sababu ya kukaa nazo tatizo ni pale ambapo zinapochelewa kutoka Hazina.

Lakini ni wazo zuri na napenda niseme kwamba tutaangalia upya utendaji wa *MSD* kwa ujumla wake na endapo itabainika kwamba kuna tatizo la uchelewesho basi tutawaomba wenzetu wa Hazina

wapeleke moja kwa moja huko ili kuondokana na tatizo hili. *(Makofi)*

Na. 339

**Kumaliza Tatizo la Upimaji wa Ardhi Nchini**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua za dhati ili kumaliza tatizo la upimaji wa ardhi nchi zima?

(b) Je, ni nini kikwazo cha utekelezaji wa zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu bado haijapangiwa matumizi na kupimwa ni moja ya vyanzo vya migogoro ya ardhi. Napenda pia nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ilikwishaanza kuchukua hatua za kupima ardhi na kuimilikisha kwa mwananchi mmoja mmoja, taasisi au

vikundi ama umiliki wa pamoja. Kutokana na hatua zilizochukuliwa hadi sasa takribani asilimia kumi ya ardhi ya nchi yetu imekwishapimwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha upangaji matumizi na upimaji wa sehemu ya ardhi iliyobaki, Serikali imekuwa ikichukua hatua zifuatazo:-

(i) Imepima mipaka ya vijiji vipatazo 11,261 kati ya vijiji 11,817 vilivyosajiliwa nchini;

(ii) Kutayarisha mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 1200;

(iii) Imesimika alama za upimaji wa ardhi 800 katika maeneo mbalimbali nchini ili kurahisisha upimaji wa ardhi. Kati ya alama hizo sita zinapima moja kwa moja kwa kutumia satellite; na

(iv) Kupima mashamba ya wananchi yapatayo 230,671 na kutoa Hatimiliki za kimila zipatazo 179,195.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imepanga kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya 20 ambayo itahusisha vijiji vipatavyo 150. Narudia kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wahimize Halmashauri zao za Wilaya zitoe kipaumbele kwa program za upangaji wa matumizi ya ardhi kwa kujumuisha kwenye mipango yao ya maendeleo na kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji kwani Serikali Kuu pekee haitaweza kutekeleza jukumu hilo kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji wa kazi za upimaji ardhi ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuna upungufu mkubwa wa rasilimali watu wa kada zote kwenye sekta ya ardhi nchini.

(ii) Kuna ufinyu wa Bajeti kwa ajili ya kulipa fidia na upimaji wa viwanja na mashamba mijini na vijijini;

(iii) Kuna upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya upimaji wa ardhi hususan kwenye Halmashauri za Wilaya na miji;

(iv) Kuwepo kwa migogoro ya ardhi kati ya watumiaji mbalimbali kama kijiji na kijiji, wilaya na wilaya, wawekezaji na wananchi, hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na vikwazo hivyo Serikali inachukua hatua kadhaa zikiwemo zifuatazo:-

(i) Kuomba kibali cha kuajiri wahitimu wa stadi za ardhi moja kwa moja wanapohitimu vyuoni;

(ii) Kuanzisha mfuko wa ardhi kwa mujibu wa maelekezo ya kifungu cha 173 cha Sheria ya ardhi Na. 4 Mwaka 1999 tuko katika hatua ya juu katika utekelezaji wa maelekezo haya;

(iii) Serikali imeandaa mpango wa matumizi wa mwaka 2011 hadi 2031. Pia imeanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya kugharamia utekelezaji

wa mpango huo ambapo mwaka 2012/2013 imetenga shilingi bilioni 4.58; na

(iv) Kutoa mafunzo kwa watendaji katika Halmashauri za wilaya kuhusu matakwa ya sheria za ardhi, ikiwemo sheria ya matumizi ya ardhi ya 2007 na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana licha ya majibu ambayo yanawiana na yanaridhisha kutoka kwa Mheshimiwa nina maswali kadhaa ya nyongeza.

Kumekuwa na malalamiko makubwa sana kutoka kwa wananchi hasa maeneo ya miji kwamba ugawaji wa viwanja na upimaji wa viwanja una matatizo. Sasa nini hatua ya Serikali kuweza kuondoa kero hii kwa mfano kama maeneo ya Gezaulole?

Utaratibu wa upimaji wa ardhi, kazi ya ardhi, *club* ya Mwembeyanga imeombwa kupimiwa ardhi, kwa kipindi cha zaidi ya miaka 23 wamelipa ada na lilitolewa agizo, na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Chilligati kwamba wapewe umiliki wa eneo hilo. Ni sababu zipi zinazopelekea mpaka leo wasipewe umiliki wa eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu malalamiko ya wananchi yahusuyo taratibu za ugawaji wa ardhi, umetoa mfano wa huko Dar es Salaam ningependa tu kusema kwamba Serikali inazo taratibu kadhaa za kugawa ardhi.

Moja tunagawa ardhi kupitia taratibu za kiutawala *Administration Allocation of Land,* na pili ni *market allocation.* Ugawaji kwa mfano uliofanyika mwezi uliopita na Halmashauri ya wilaya ya Manispaa ya Temeke kule Gezaulole kule ilitumika *Market allocation* ambapo wananchi walialikwa kuomba viwanja na kwa taarifa nilizonazo jumla ya wananchi wapatoa 16,000 waliomba viwanja lakini viwanja vilivyokuwepo ni 1800 na kwa hiyo viko vigezo vilivyokuwa vimewekwa ambavyo ndivyo vimetumika wananchi hawa 1800 ambao wamepata viwanja.

Ningependa kupitia Bunge lako Tukufu niondoe lawama ambazo zimekuwa zinatolewa kwa viongozi kwamba eti wamepewa viwanja vingi kuliko wananchi wengine.

Viongozi ni wananchi. Viongozi wana haki nao ya kumilikishwa ardhi kama mtu mwingine yeyote. Viwanja vinapogawanya hawaangalii kwamba huyu ni kigogo maana yake wametumia neno kigogo au siyo kigogo wanachoangalia ni vigezo vilivyowekwa mojawapo ni uwezo wa kuendeleza eneo hilo ambalo unalouziwa katika fomu ya maombi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba Mwembe Sport waliomba kupimiwa ardhi, kwa zaidi ya miaka 23 lakini bado hawajapimiwa. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu kwa mapenzi yake kwa wanamichezo na kuwaunga mkono wana

michezo kwani michezo ni ajira ambayo tunaihitaji sana kwa ajili ya kukwamua vijana wetu wasio na ajira.

Suala la msingi kwamba namshukuru kwa taarifa hii kwamba kuna ombi limetolewa na *Mwembe Sports Club* kwamba wapimiwe ardhi, nami nitaomba nishirikiane naye kufuatilia hili na tutachukua hatua zifaazo ili kuhakikisha kwamba Mwembeyanga Sports, umesema Mwembeyanga Sports wanapimiwa ardhi ile wanamilikishwa ikiwa itathibitika kwamba matumizi ya ardhi ile ni yale ambayo wao wanataka kumilikishwa kwayo.

**SPIKA:** Hili swali limetumia dakika kumi. Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Ezekia Wenje swali lingine, kwa niaba Mheshimiwa Mnyika kwa niaba ya Mheshimiwa Wenje.

Na. 340

**Hatua Zilizochukuliwa Kutokana na Makosa Yaliyofanyika Wakati wa Ununuzi wa Rada**

**MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y. MHE. EZEKIA D. WENJE)** aliuliza:-

Kampuni ya Uingereza ya Silaha za Kivita *(BAE SYSTEMS)* ilishakiri kwamba ilifanya makosa ya kutoweka kumbukumbu za fedha na mahesabu katika mchakato wa mauzo ya Rada kwa Serikali ya Tanzania; ni dhahiri kwamba kuna makosa yalifanyika ya kimanunuzi kati ya pande zote mbili. Hali

iliyosababisha kuwepo kwa tozo ya pauni milioni 29.5 kama fedha zilizochukuliwa na kampuni ya *BAE SYSTEMS* kutoka kwa Serikali ya Tanzania:-

(a) Je, Serikali ya Tanzania ina mpango gani wa kuchukua hatua dhidi ya kampuni hiyo ambayo ilishiriki kufanya makosa hayo?

(b) Je, Serikali imewachukulia hatua gani waliohusika na mchakato wa ununuzi huo kwa upande wa Serikali ya Tanzania?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimatifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimekwishaeleza kuhusu *BAE* katika Bunge hili wakati nikiwasilisha kauli ya Serikali Bungeni tarehe 23 Juni, 2011 na pia wakati nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati nikiwasilishwa Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012. Serikali ya Tanzania ilihusishwa katika kufikia makubaliano kati ya *SFO* na *BAE SYSTEMS* iliyopelekea *BAE* kukiri kosa la kutoweka kumbukumbu zaidi S zake vizuri na hivyo kuamuliwa kulipa tozo la faini ya *pound* milioni 29.5 wananchi wa Tanzania.

Moja ya kipengele cha makubaliano hayo yaliyoidhinishwa na Mahakama ya Uingereza tarehe 21 Desemba, 2010 imeweka bayana kwamba kuwa kukiri

kosa na kukubali kutoa tozo hilo *BAE* haitachukuliwa hatua yoyote nyingine ya kisheria itokanayo na suala hilo. Utaratibu huo wa makabiliano nje ya mahakama ni utaratibu wa kawaida katika sheria za Uingereza na una nguvu ya kisheria.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa *BAE* wametimiza wajibu wao katika makubaliano hayo na sasa wameshatoa fedha hizo kwa Serikali ya Tanzania. Hivyo kwa muktadha huo Serikali ya Tanzania haina mpango wa kuchukua hatua yoyote dhidi ya *BAE* kwa kuwa imeshahukumiwa na imeshatekeleza hukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kipekee nachukua nafasi hii kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa hatua ilizozichukua kufanikiwa kurudishwa kwa fedha hizi. Aidha napenda kukupongeza wewe mwenyewe binafsi Naibu Spika Mheshimiwa Job Ndugai kwa namna mlivyolishughulikia suala hili kwa umakini mkubwa.

Mwisho nawashukuru Wabunge wote wa Kamati ndogo ya Bunge walioambatana na Naibu Spika pamoja na maafisa waandamizi wa Bunge na Serikali walioshughulikia suala hili hadi fedha hizo kurejeshwa. Wizara ya Mambo ya nje, ilikuwa na jukumu la kuwezesha kufanikisha mawasiliano baina ya Serikali na kampuni ya *BAE SYSTEMS* ya Uingereza.

Katika kuratibu mchakato huo haukushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali mathalani Kamati maalum ya Bunge iliyoongozwa na Naibu Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai ilifanikiwa kuhakikisha

kuwa *BAE SYSTEMS* inakiri kuilipa Serikali kiasi cha tozo la *pound* milioni 29.5 kama fedha zilizokwapuliwa kutoka Serikali ya Tanzania wakati wa ununuzi wa rada.

Kuhusu kuchukua hatua dhidi ya kampuni hiyo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote waliohusika na mchakato wa ununuzi wa rada ni wazi kwamba masuala haya yanahitaji umakini mkubwa kwa vyombo vyetu vya Serikali hususan ushahidi na uchunguzi wa kina ili kujiridhisha juu ya hatua hizo na matokeo yake kwa Serikali ya Tanzania na vyombo vyake.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru makubaliano kati ya kampuni ya *BAE* na *SFO* yanahusu zuio la mashitaka nchini Uingereza dhidi ya kampuni ya BAE lakini makubaliano hayo shughuli ni kwamba yanazuia nchi ya Tanzania kuchukua hatua za ndani za kisheria dhidi ya watu wake. Kwa kuwa Tanzania ni dola huru je, Waziri anayatafsiri makubaliano ya Uingereza kuwa ni Serikali ni ya Tanzania?

Kwa kuwa katika miaka ya karibuni wamepelekwa mahakamani baadhi Mawaziri ya Serikali kwa makosa ya uzembe, uhujumu uchumi na kuisababishia hasara Serikali.

Je, katika kashfa hii ya rada, Serikali iko tayari kuendelea na uchunguzi na kuchukua hatua dhidi ya uzembe ufisadi na kusababishia hasara Serikali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, suala hili nilipata nafasi ya kulizungumzia tena jana wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba nijirudie kwanza Serikali ya Uingereza haingilii vyombo vyetu huru.

Kilichofanyika Uingereza ni makubaliano baina ya *SFO* na *BAE SYSTEMS* kwamba kutokana na makubaliano hayo maafisa wa *BAE* wote si tu kwamba hawawezi kushitakiwa *actually* hawawezi hata kutajwa kwenye sakata lolote linalohusiana na sakata lile la rada. Kwa hiyo, kutokana na ukweli huo na haya masuala yote nayajibu kwa pamoja.

Kutokana na ukweli huo kwanza inakuwa ni vigumu kumchukua Mtanzania yeyote ukamshitaki halafu ukategemea ushahidi kupata Tanzania.

Ushahidi wote utatoka *BAE SYSTEMS* ndiyo makosa ya rushwa yalivyo unatoa, kuna mtoaji na mpokeaji sasa haiwezakani mtoaji awe Mtanzania, mpokeaji Mtanzania halafu *BAE SYTESMS* ikakaa pembeni utahitaji mashahidi kutoka *BAE SYSTEMS* huwezi kuwapata, utahitaji mashahidi kutoka *SFO* huwezi kuwapata wamejifunga na hata ukiwaandikia Uingereza watakuambia kwanza lazima tupitie kwenye mahakama zetu ili hawa waweze kupata kibali, huwezi kupata hiyo *mutual legal system*.

Lakini la pili hili la kusema kwamba kuna viongozi wa Watanzania wameshitakiwa ni kweli wapo na

ushahidi upo na ndiyo maana tuliona kuna kesi sasa hivi sina ushahidi na nilisema jana na nasema tena leo. Ndani ya Bunge hili kama yupo mtu, nje ya Bunge hili kama yupo mtu, nje ya nchi hii kama yupo mtu mwenye ushahidi ambao ni *credible* wa kushitaki mtu yeyote Mtanzania tutamchukua mtu huyo na ushahidi huo tutakwenda naye mahakamani kesho, *this is the challenge.* Yoyote mwenye ushahidi huo alete, nilisema mwaka jana tarehe 5 Julai, 2011 nasema tena leo na nilisema tena jana. *(Makofi)*

Na. 341

**Idadi Ndogo ya Wanawake Kwenye Ngazi za Maamuzi/Uongozi**

**MHE. MOZA ABEID SAIDY** aliuliza:-

Nchi yetu imeridhia mikataba au maazimio mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa juu ya ukombozi, fursa sawa na kumpa haki Mwanamke lakini bado idadi ya Wanawake nchini imekuwa ndogo katika ngazi za maamuzi/uongozi.

(a) Je, Serikali itakubaliana name tatizo la utashi wa kisiasa hasa ikizingatiwa kuwa nafasi nyingi kama za Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya na kadhalika ni za uteuzi?

(b) Je, ni kweli kwamba wanawake wengi hawapewi nafasi hizo kwa sababu hawajasoma au hawana maono?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, kuwa nchi yetu imeridhia mikataba na maazimio mbalimbali ya kimataifa na kikanda kuhusu ukombozi, fursa sawa na haki za wanawake.

Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kitendo cha Tanzania kuridhia na kusaini makubaliano hayo ni mojawapo ya ishara kubwa ya kuonyesha kuwepo kwa utashi wa kisiasa katika kushughulikia haki za wanawake na usawa wa kijinsia nchini.

Aidha utashi huu pia unajidhihirisha wazi katika kutekeleza makubaliano hayo kwa mfano kuingiza masuala ya haki za wanawake na usawa wa kijinsia katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika sera, mipango na mikakati mbalimbali ya kitaifa na kisekta kama vile dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA I & II).

(b) Mheshimiwa Spika, kihistoria wanawake wengi hawakupata fursa sawa za kupata elimu kama wanaume. Hali hii iliathiri kwa kiwango kikubwa uwiano wa nafasi za wanawake katika uteuzi kipindi hicho na sio kuwa hawana maono kama wanaume.

Hata hivyo kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa kwa makusudi na Serikali na zinazoendelea kufanywa hali hiyo imebadilika sana na sasa kuna wasomi wengi wanawake katika ngazi ya maamuzi ukilinganisha na miaka ya mwanzoni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Moza swali la nyongeza.

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri umesema katika jibu lako la msingi wanawake hivi sasa wengi ni wasomi na humu ndani tuna Wabunge wanawake wa Majimbo. Je, haikuonwa haja ya kuwapatia nafasi ya uteuzi wanawake hawa kuwa Waziri Mkuu?

Pili, kwa kuwa hivi sasa tunaendea *fifty-fifty.* Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wanawake kufikia kwenye lengo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba uwepo wa Mheshimiwa Moza ndani ya Bunge hili ni utashi tosha wa uongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kuwapatia wanawake nafasi za uongozi. Lakini suala la kwanini wanawake wa Majimbo hawakuteuliwa kuwa Waziri Mkuu, *Ishaalah* Mwenyezi Mungu akijaalia siku moja tutakuwa na mwanamke Waziri Mkuu lakini pia uteuzi ni itakavyompendeza mwenye mamlaka inayoteua na si kwamba wanawake hawana uwezo lakini wanawake wana uwezo mkubwa sana na wakipewa nafasi wanafanya vizuri sana tena kuliko hata wanaume naweza nikasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mkakati wakufikia hamsini kwa hamsini, tayari kama Wizara tumeandaa mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha kwamba tunafikia hamsini kwa hamsini katika nafasi zote za maamuzi kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya juu. Lakini ninaamini kwamba kama Katiba yetu ya sasa ibara ya 66(1)(b) ilivyoweka msingi huo wa kuhakikisha kwamba wanawake wasipungue 30% katika Bunge na katika Halmashauri, tunategemea kwamba hata katika hiyo Katiba mpya ambayo tutaiandika basi msingi huo utaendelea kuwepo ili

kuhakikisha kwamba tunafikia zaidi ya 50% katika nafasi za wanawake.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba wanawake na wanaume wote kutoa maoni katika Tume ya kukusanya maoni ya Katiba kuhakikisha ni kwa kiasi gani tutafikia lengo hili la hamsinig kwa hamsini katika nafasi zote za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, naamini inawezekana na wanawake wanaweza.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sussan Lyimo!

**MHE. SUZANA A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa, elimu tu ndiyo Mwarubaini na njia sahihi ya kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi za maamuzi. Kwa kuwa, wasichana wengi wamekuwa wakikatisha masomo yao kwa sababu mbalimbali ikiwemo za kupata mimba.

Je, Wizara hii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, itawahakikishiaje kwamba wasichana hao wanafikia malengo yao ili waweze kuwa na usawa katika ngazi zote za maamuzi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Susana Lyimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Suzana kwamba elimu ndiyo Mwarubaini wa kuhakikisha kwamba wanawake wanashiriki kikamilifu katika nafasi zote za maamuzi na kama Serikali tumefanya vizuri katika kuwa na usawa katika shule za msingi na sekondari. Lakini changamoto yetu kubwa ipo katika kuhakikisha kwamba wanawake wanapata nafasi katika elimu za juu.

Sasa hivi takwimu zinaonyesha kwamba wanawake ambao wako katika vyuo vya elimu ya juu ni 36% kwa hiyo bado tuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, mkakati uliokuwepo Mheshimiwa Suzana kama umeona Mheshimiwa Waziri wa Elimu aliwasilisha rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambapo inatoa nafasi kwa wasichana ambao wamepata mimba waweze kuendelea na masomo yao. Najua lilileta sana maneno ndani ya Bunge, lakini bado tunaendelea kutoa maoni ili kuhakikisha kwamba sera ya elimu inatoa fursa ya kuhakikisha kwamba wasichana wanapata elimu.

Lakini kama Wizara tutaendelea kuwahamasisha watoto wa kike na wenyewe kuhakikisha kwamba wanajitunza ili kuhakikisha kwamba wanaendelea na masomo yao na pale ambapo wanateleza tutahakikisha kwamba wanapata hiyo nafasi ya kuendelea na masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Martha Mlata, atauliza swali linalofuata.

Na. 342

**Mikopo ya Zana za Kilimo**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Wanawake wengi wa Mkoa wa Singida wameshindwa kutekeleza kikamilifu kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kutokana na kushindwa kukopa pembejeo kama *Power Tiller* na matrekta.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuangalia masharti ya mikopo ya zana za kilimo ili kuwawezesha walio wengi kukidhi vigezo vya mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfuko wa Tafa wa pembejeo za kilimo unatoa mikopo ya aima mbalimbali kama vile ununuzi na usambazaji wa mbolea, mbegu bora, madawa ya mimea na mifugo, matrekta makubwa, matrekta madogo *(Power Tillers)* zana za kukokotwa

na wanyama kazi, zana za kilimo cha umwagiliaji na kadhalika. Walengwa na mikopo hii ni pamoja na wakulima binafsi, vyama vya ushirika vya msingi, vyama vya akina na Mikopo *(SACCOS)* na vikundi vya uzalishaji mali vilivyosajiliwa katika sekta ya kilimo na ufugaji, makampuni ya kusambaza pembejeo za kilimo na taasisi za kijamii.

Mkopaji anatakiwa akamilishe mambo yafuatayo katika maombi yake ya mkopo:-

(a) Andiko la mradi kwa maana ya *write up,* linalochambua mahitaji ya mkopaji, mapato, faida na utaratibu wa urejeshaji wa mkopo. Muda wa mkopo ni miaka mitano (5) kwa riba ya asilimia saba (7%) kwa mwaka. Mikopo ya vikundi vya kijamii yaani *social groupings* itatozwa riba ya asilimia sita (6%) kwa mwaka.

(b) Ankara vifaa *(Proforma Invoice)* kutoka kwa muuzaji au kampuni inayofahamika. Ankara vifani ioneshe aina ya trekta na liwe limethibitishwa na *Centre for Agricultural Mechanisation and Rural Technology (CAMARTEC).* Kwa hili ningependa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge kwa ufahamu zaidi ya hili wanaweza kwenda hata pale kwenye uwanja wa Nanenane kwenye maeneo ya *CAMARTEC* na *MACHANISATION* na Wizara ya Kilimo.

(c) Uthibitisho wa kumiliki shamba lisilopuimngua ekari hamsini (50) ambalo tayari limeanza kuendelezwa.

(d) Kwa waombaji binafsi au kampuni waambatanishe kivuli cha Hatimiliki itakayodhamini mkopo na mwombaji sharti awe ndiye mmiliki.

(e) Kwa maombi ya vikundi au mashirika ya kijamii yaambatanishwe na muhtasari wa kikao kilichoazimia kukopa kama lilikuwa kundi la watu 30 ionyeshe kwamba watu hao 30 waliazimia kukopa, mahitaji ya wanachama watakaokopeshwa, kivuli cha Hati ya usajili, uthibitisho wa dhamana ya mkopo ambayo ni Halmashauri ya Wilaya au taasisi itakayowadhamini. *(Makofi)*

(f) Mkopaji atatakiwa kuchangia gharama za trekta na zana zake kwa asilimia kumi (10) ya kiasia cha mkopo anaokopeshwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuona kuwa masharti haya yanamwezesha mkopaji kumudu kupata zana bora za kilimo.

Aidha, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuwahimisza wananchi wa mkoa wa Singida kutumia fursa hii ili waweze kupata mikopo ya matrekta ikiwa ni pamoja na matrekta madogomadogo (*Power Tillers*) kutoka mfuko wa pembejeo za Taifa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri.

Naomba tu kumwuliza kwamba kwa kweli masharti aliyoyasoma hasa ya andiko pamoja na Hatimiliki ni kitendawili kikubwa sana kwa wakopaji kwa sababu namna ya kuandika tu hilo andiko mara sijui Hatimiliki ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi kwamba watapataje msaada kutoka Serikalini ili kuweza kukamilisha hayo maandiko pamoja na Hatimiliki.

Lakini pili, ni kwamba wanawake wa Mkoa wa Singida wamenipigia simu na wameniomba kwamba wao wako tayari kulima mazao yatakayoleta tija katika kilimo chao. Kwanza, Mtama, Uwele, Alizeti pamoja na Mahindi. Sasa naomba awahakikishie watapataje pembejelo za mazao hasa kwa mfano zao la Mahindi ambalo sasa hivi limekuwa ni kitendawili kikubwa sana katika Mkoa wa Singida kwa kupigwa marufuku na wakati kuna maeneo ambayo yanastawisha zao hili?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha M. Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la masharti ya andiko kwa maana ya *write up* na Hatimiliki limegawanyika katika sehemu mbili.

Hili la andiko tunatarajia kwamba kikundi chenyewe kikisha kuja kinakuja na *write up* yake kusema mambo waliyokubaliana nayo. Tumeona kweli

kwamba vikundi vingi hasa vya kijijini vinapata taabu kuleta *write up* ambayo ni *bankable* kwa hiyo, tumekubaliana kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwamba tutakuwa na eneo maalum ambalo hivi vikundi vinapokuja kabla ya kutaka kupeleka *write up* watuletee ili tuwasaidie kuiweka sawa. Hili tumekubali tunalipokea.

Lakini suala la Hatimiliki liko baina ya Wizara ya TAMISEMI na watu wa ardhi kwamba kwa kusema kweli inasaidia pia kuweka *guarantee* kwenye mikopo lakini pia Mheshimiwa Mwanri alikuwa ananishauri kwamba wanaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hili la vikundi vya uzalishaji wa kilimo, tulichosema sisi Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa ni kwamba mazao kwa kanda ya Dodoma, Singida, sehemu ya Iringa, Igunda, Tabora na Nzega mpaka Kwimba na Kishapu tunataka tupeleke Mtama, Uwele na Alizeti mbegu bora kwa sababu ndizo zinazohimili mazingira ya ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya kilichotokea Singida ni kwamba Singida yote yaani mkoa mzima umechukuliwa kama ni Mkoa ambao ni kame. Kuna maeneo ya Singida kama Mpambaa, Mkarama, Mgandu kwa Mheshimiwa John P. Lwanji, Mtekete karibu na Arusha na kuna maeneo ambayo kusema kweli ni maeneo ambayo ni mabichi *they have enough hydraulic*.

Kwa hiyo, tulichosema ni kwamba kwa maeneo kame ya Singida yatakwenda kwenye ruzuku ya Mtama, Alizeti na Uwele, yale mengine ambayo kwa sasa hivi tunajua kuna wakulima kuna wakulima maeneo ya Singida karibu na Arusha na karibu na Manyara pia kuna wengine wanazalisha mpaka magunia 70 kwa ekari moja.

Mheshimiwa Spika, tunachosema ni kwamba wale tutawapa ruzuku ili kuwe na *mix* ya mazao kwa maana ya Mahindi pia kwa maeneo hayo machache ya Singida na siyo yote.

Na. 343

**Tatizo la Umeme – Mpanda**

**MHE. ANNA MARYSTELLA JOHN MALLAC** aliuliza:-

Licha ya Mji wa Mpanda kupanuka na kutarajiwa kuwa Makao makuu ya Mkoa wa Katavi yanatumia jenereta kusambaza umeme ambao mara nyingi hauna uhakika.

Je, ni lini Wilaya hiyo itaunganishwa na mpango wa gridi ya Taifa ili kuondokana na usumbufu wa mgao wa umeme?

**NAIBU WAZIRI WANISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Annamarystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpanda ina kituo cha kufua umeme kinachoendeshwa kwa kutumia mafuta ambacho kwa sasa kinakidhi mahitaji ya umeme. Kituo hicho kina mitambo minne yenye uwezowa kufua umeme kiasi cha MW 2.664. Ili kuendana na ongezeko la mahitaji linalotarajiwa kuwepo siku za usoni kutokana na kushamiri kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Wilaya hiyo kuna mpango wa kujenga kituo kipya ambapo mitambo yenye uwezo wa kufua MW 2.5 itafungwa. Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uholanzi chini ya Mradi wa *ORIO*. Mradi utajumuisha pia ufungaji wa mitambo ya kufua umeme kwa miji ya Biharamuolo na Ngara. Miradi hii itagharimu kiasia cha *Euro* 34,000,000.

**MHE. ANNA MARYSTELLA JOHN MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Waziri lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Wilaya ya Mpanda mpaka sasa inatumia umeme wa *generator* mashine mbili katika nne zilizoletwa huku mbili zikiwa mbovu na chakavu.

Je, ni lini Serikali itajenga kituo hicho kipya chenye uwezo wa kufua umeme *Megawatt* 2.5?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallac kama ifuatavyo.

Labda ni dhana tu ya kudhani kwamba mara zote umeme wa gridi si miongoni mwa umeme unaozalishwa kwa kutumia *generators.* Hata kwenye *grid* kwenyewe tuna *feed* karibu zaidi ya meg*awatt* 100 ambazo zinatokana na *generators* hizihizi. Kwa hiyo, nidhana tu. Lakini pengine inaonekana ni mtu anaonekana ni mtu anakuwa na uhakika ambapo anakuwa *connected* na *grid*. Nadhani tuliwapa ramani tukionyesha mtawanyiko wa gridi na gridi tunamaanisha ni pamoja na *generators* ambazo zinakuwa zinaendeshwa na Shirika la Umeme la *TANESCO*.

Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi kwamba kuunganishwa kwenye *grid* ya taifa au kuwa na umeme wa *generator* ni kitu kilekile lakini suala la msingi ni hoja yake kwamba zipo *generator* nyingine ambazo ni mbovu yaani katika mashine zile nne mbili ni mbovu na siyo kwamba ni chakavu na nikuhakikishie kwamba zinafanyiwa ukarabati. Lakini pia kupitia uhusiano wetu mzuri na Uholanzi basi tunakusudia kufunga mashine mbili ambazo zitatoa *megawatt 2.5* ambazo ni mpya kabisa. Kwa hiyo, tatizo la umeme Mpanda litakuwa halipo tena. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na tupo nje kabisa ya ratiba ya maswali. Naomba niwatambue wageni waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Kwanza kabisa nina wageni wa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira ambao ni Ndugu Ayoub Nyakimori ambaye ni binamu yake

Mheshimiwa Waziri. Pia yupo mwandishi wa *ITV* Ndugu George Marato. Karibuni sana. Pia tuna wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, ambao ni familia yake wakiongozwa na Bi. Florence Mahanga, ambaye ni mke wake mpendwa, asimame na familia yake yote na *members* wa *family* wengine. Ahsanteni sana na tunashukuru. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watatu wa Mheshimwa Cecilia Pareso yeyeni Naibu Msemaji wa Kambi ya Upinzani Wizara hii wakiongozwa na Ndugu Stephen Mboba, ambaye ni mume wake mpendwa. Maana yake kila siku wamekazana wazo wapendwa lakini leo ni mume wake mpendwa kaja. Karibu sana. (*Makofi*)

Tuna wageni kutoka Wizara ya kazi na ajira ambao ni Katibu Mkuu Bwana Erick Shitindi. Pia kuna Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa *NSSF* Bwana Aboubakar Rajab, huyu zamani alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara mbali mbali. (*Makofi*)

Pia yupo Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Dkt. Ramadhan Dau. Pia yupo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamiziwa wa *SSRA* Bi. Irene Isaka. Pia yupo Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Bwana Cosmas Msigwa. Yupo Mkurugenzi Mkuu Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi yaani OSHA, Dkt. Acqulina Kayumba. Yupo Mtendaji Mkuu Wakala wa Huduma za Ajira Bwana Elieza Mwasele.

Pia yupo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tija Bwana Leonidas Rwejuna. Yupo Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika Umma *PPF,* Bwana William Erio. (*Makofi*)

Lakini pia yupo Mkurugenzi Mkuu *ILO* Kanda ya Afrika Mashariki Bwana Lexio Msindo. Pia yupo Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri, Dkt. Aggrey Mulimuka. (*Makofi*)

Pia wapo Wakurugenzi Wakuu wa Idara, Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa wote kutoka Wizarani na Taasisi zake, wote wasimame walipo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna Viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania yaani *TUCTA* wakiongozwa na Bi. Norbart Maskini Makamu wa Rais wa *TUCTA* pamoja na Bwana Nicholous Mgaya ambaye ni Katibu Mkuu wa *TUCTA*. Naomnba wote wasimame walipo. Karibuni sana na ahsanteni sana. (*Makofi*)

Yupo Bwana Joseph Masama ambaye ni Rais kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Fedha, Mabenki na Huduma za Usindikaji yaani ZIBUKA. Karibu sana.

Pia yupo Bwana A. P. Mushi, ambaye ni Mwenyekiti wa Muungano wa Washauri Elekezi Tanzania *TACO*. Asimame huyu bwana. Ahsante sana. *(*Makofi*)*

Halafu tunao Mabalozi wa kampeni ya kuchangia ujenzi wa hosteli za wasichana wa shule za sekondari Tanzania, kampeni ambayo inaendeshwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)*. Hawa ni Bi. Rebecca Buyuni, Mtangazaji wa *Fema Talk Show*. Yuko wapi huyu? Ahaa, ahsante yule pale juu. Yuko Faraja Nyalandu, Miss Tanzania 2004. Huyu ni mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye Nancy Sumari, yeye ni *Miss* Tanzania 2005. Ahsante sana. Kwa hiyo, hawa wameona wafanye kazi sasa ya kuhakikisha wasichana wanapata mahali pa kulala kule mashuleni ili kusudi waweze kuepukana na mambo ya mimba. Kama alivyosema Mheshimiwa Suzan Lyimo pale, ukombozi wa kweli wa mwanamke ni elimu. Kwa hiyo, tunawashukuruni sana Mabalozi wetu na nadhani mtaungwa mkono na watu wengine. Ahsante sana. (*Makofi*)

Halafu kuna wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 190 pamoja na walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Wasichana inaitwa La - Miriam. Wako wapi hawa? Wasimame walipo pamoja na walimu wao. Ahaa, ahsante sana. Hii shule sijui iko wapi! Karibuni sana tunaomba msome kwa bidii ndiyo hao tunaowasema, msome kwa bidii, achaneni na maneno hayo, mengine yanayozungumzwa hayawafai kabla hamjamaliza kusoma. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 35 pamoja na Walimu wao kutoka shule ya msingi ya Paroma iliyopo Manispaa ya Musoma katika Mkoa wa Mara. Naomba na hawa

wasimame na walimu wao. Ahsante sana. Mmependeza sana watoto wazuri. (*Makofi*)

Tuna wageni 36 kutoka Babati, Mkoa wa Manyara wakiongozwa na ndugu Abdallah Soki Sogara, Mwenyekiti wa CCM Wilaya. Hawa wageni sijui wako wapi? Ahsanteni sana na tunawatakia kazi njema huko Babati. (*Makofi*)

Tuna kikundi cha akina mama 30 kutoka Karatu ambao ni wageni wa Mheshimiwa Cecilia Paresso. Hao nao wako wapi? Ahsante sana akina mama na karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge: wako wageni watatu wa Mheshimiwa Jitu Soni, kutoka *Jain Irrigation* ya India ambao ni Mrs. Rupa Shushak, *where is Mrs* Rupa Shushak? *Okay, she is there!* Mr. Sharma and Mr. Chaudry, *you are welcome to our country and I hope you will do a good service to us*. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wageni wangu walikuwa wengi na muda unakwenda, *I hope* tutatumia muda vizuri.

Matangazo ya kazi sasa; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.30 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Chumba Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew Chenge anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5.00 asubuhi hii kutakuwa na kikao cha Kamati kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2012. Kikao hiki kitafanyika katika ukumbi Na. 231. Hawa nimewapa ruhusa kwa sababu tunakaribia mwisho, hivyo ni vizuri wakaifanya vizuri kazi ile ya ule Muswada.

Tuna Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa ambaye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa.

Halafu Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Kaika Telele anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi wa *basement*.

Halafu Mwenyekiti wa *TWPG,* chama cha wanawake Wabunge wote Mheshimiwa Anna Abdallah anaomba niwatangazie Wabunge wanawake wote kuwa tarehe 7 kuanzia Saa 7.15 mchana na tarehe 8 kuanzia Saa 4.00 asubuhi kutakuwa na semina ya Wabunge wanawake itakayofanyika katika ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wanawake wote wanahimizwa kuhudhuria semina hiyo muhimu. Kwa hiyo, leo ni saa 7.15 mchana na kesho kwa sababu ni sikukuu mtaanza saa 4.00 asubuhi. Waheshimiwa

Wabunge wanawake wote, naomba mhudhurie elimu ina namna za kipekee.

Waheshimiwa Wabunge pia Mheshimiwa Alhaji Mohammed Missanga anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote waliofunga na wasiofunga pamoja na watumishi wote waliofunga kwamba wanaalikwa katika futari ya pamoja leo Jumanne tarehe 7 mwezi wa Nane saa 12.30 jioni katika ukumbi wa Bunge hapo chini *basement*. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa.

Halafu tena Alhaji Mohammed Missanga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya futari, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya maandalizi ya futari kwamba, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo Saa 7.15 mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Kama mtagongana huko mtapanga wenyewe maana yake nimesoma Msekwa tena. Kwa hiyo, Kamati ya utendaji nadhani inabidi iende huko.

Halafu kampuni ya *energy masters* kutoka Dar es Salaam wapo katika viwanja vya Bunge wakionesha vifaa mbalimbali vya umeme, vifaa vya *solar*, umeme wa upepo pamoja na *CCTV Camera*. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kutembelea sehemu hiyo mkajifunze.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Kazi na Ajira

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* kwa mwaka 2011/2012. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Tume kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

*(Hapa kulikuwa na minong'ono ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wakitoka nje ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnaotoka, mtoke kwa utulivu.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Nane wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu na

jamaa za Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki cha mwaka mmoja ambao ni marehemu Jeremia Solomon Sumari aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki (CCM), marehemu Mussa Hamis Silima aliyekuwa Mbunge wa Uzini (CCM) – Zanzibar, marehemu Salum Amour Matondoo aliyekuwa Mbunge wa Bububu (CCM), Zanzibar na marehemu Regia Estelatus Mtema aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) na Waziri Kivuli wa Wizara hii.

Vilevile napenda kuungana na watanzania wengine kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu, jamaa na wananchi wote waliofikwa na maafa kutokana na ajali ya meli ya Stagit. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu wote waliofariki na kuwajalia afya njema wale waliojeruhiwa na vilevile moyo wa subira na matumaini kwa familia, ndugu na jamaa.

Mheshimiwa Spika, pili naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kutuongoza na kutoa maelekezo katika utekelezaji wa kazi katika sekta ya Kazi na Ajira hasa katika masuala ya kusaidia kusaidia hatua zitakazowezesha kutatua tatizo la ajira hususan kwa vijana. *(Makofi)*

*(Hapa minong'ono kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ikiendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaomba utulivu.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio makubwa. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuja nchini kwetu na wadau wa maendeleo kuona haja ya kuendelea kutuunga mkono. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kwangu na heshima kubwa aliyonipa ya kuendelea kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi ndogo wa kule Igunga na Arumeru Mashariki. Aidha, nawapongeza kwa dhati Wabunge wenzangu wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na vile vile Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa akiwemo Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum na Mheshimiwa James Francis Mbatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Alhaj Adam Kimbisa, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Shy-Rose Sadruddin Bhanji, Mheshimiwa Angela Charles Kizigha, Mheshimiwa Abdallah Ali Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Maryam Yahaya Ussi, Mheshimiwa Twaha Issa Taslima, Mheshimiwa Nderakindo Perpetua Kessy na Mheshimiwa Bernard Musonyi Murunya. Ni matumaini yangu kuwa watatuwakilisha vyema kwa manufaa na maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Mbunge wa Bunda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vema mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Malengo, maelezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia Mbunge wa Kondoa Kusini, iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu tarehe 7 na 8 Juni, 2012.

Wizara yangu imezingatia ushauri walioutoa na ambao umesaidia sana kuiboresha bajeti hii ninayoiwasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya awali naomba sasa kuelezea mapitio ya utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, utekelezaji wa Mpango na Kazi kwa mwaka 2011/2012, Mpango wa Kazi wa mwaka 2012/2013 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelezea kwa kifupi utekelezaji wa malengo ya kazi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2012 na maelezo ya kina yapo katika ukurasa wa 5 -35 wa kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuandaa mazingira bora ya utekelezaji wa viwango vya kazi, usawa, kazi za staha na nafasi za ajira za kutosheleza kwa kutoa na kusimamia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo kuhusu masuala ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, mikakati tuliyojipangia ili kufikia malengo hayo kwa ufanisi ni pamoja na kuboresha na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kukuza Ajira kwa kuimarisha taarifa za soko la ajira, kutoa elimu ya ujasiriamali na kuhamasisha watu kuweza kujiajiri ili kupunguza umaskini wa kipato na ukosefu wa ajira, kusimamia urekebishaji na utekelezaji wa sheria za kazi ili kuleta amani na tija sehemu za kazi, kuwa karibu na wafanyakazi na kutatua matatizo yao kwa wakati,

kusuluhisha na kuamua migogoro ya kikazi, kufanya ukaguzi za kazi, ajira na usalama na afya mahali pa kazi mara kwa mara na kusimamia masuala ya hifadhi ya jamii ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na uhakika wa kupata mafao yao pindi wanapostaafu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango kazi wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka 2011/2012 umezingatia Sera, Mipango na Mikakati ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Katika kipindi hiki tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Kazi na Ajira imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi na viwango vya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia sheria za kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi sehemu za kazi, kuboresha hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Wizara (Fungu 65) iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya sh. 18,509,965,321/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo sh. 12,565,090,321/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 5,944,875,000/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 Wizara ilikuwa imetumia jumla ya sh. 10,447,748,103.45/= ambazo ni sawa na asilimia 83.1 ya sh. 12,565,090,321/= zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida. Aidha, Wizara ilitumia jumla ya sh. 599,812,466.43/= sawa na asilimia 10.1 ya sh. 5,944,875,000/= zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa kazi na huduma za Ukaguzi; kufanya ukaguzi sehemu za kazi. Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi; ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Aidha, Wizara imeendelea kuwa karibu na Wafanyakazi na kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Wizara imeendelea kuhimiza maelewano mema baina ya Waajiri na Wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya kaguzi sehemu za kazi pamoja na kutoa elimu ya Sheria za Kazi ili kuboresha utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria za Kazi na kuchukua hatua stahiki pindi haki za Wafanyakazi zinapokiukwa. Wizara imefanya ukaguzi 2,401 katika sehemu mbalimbali za kazi nchi nzima kwa lengo la kuona namna Sheria za kazi zinavyozingatiwa na kutekelezwa na waajiri na wafanyakazi, utekelezaji wa viwango vya kazi, haki za msingi za kazi pamoja na haki za vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa sheria za kazi zinafuatwa na kuzingatiwa kikamilifu, jumla ya waajiri 14 walifikishwa Mahakamani ambapo usikilizaji wa kesi moja umekamilika na mwajiri aliyepatikana na hatia ametozwa faini ya shilingi 500,000/=. Kesi mbili zilisuluhishwa nje ya Mahakama kwa wafanyakazi husika kulipwa haki zao walizokuwa wakidai na kesi zingine 11 zipo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuheshimu viwango vya kazi vya kimataifa kama vinavyoelezwa katika Mikataba na Mapendekezo mbalimbali ya Shirikia la Kazi la Kimataifa *(ILO)*. Napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mnamo mwaka 2010, Mkutano Mkuu wa *ILO* ulipitisha Pendekezo Na. 200 kuhusu UKIMWI na Virusi vya UKIMWI mahali pa kazi linalolenga kuzisaidia nchi wanachama katika mapambano dhidi ya janga hili.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mwaka 2011, Mkutano Mkuu ulipitisha Mkataba Na. 189 na Pendekezo Na. 201 kuhusu Kazi za staha na haki za msingi kwa wafanyakazi wa majumbani. Wizara itaendelea kudumisha ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo waajiri, wafanyakazi na vyama vyao ili kuhakikisha kwamba maslahi ya pande zote yanazingatiwa wakati wa utekelezaji wa Mkataba na Mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu ya Sheria za Kazi katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Jumla ya wafanyakazi 3,926 na Waajiri 256

wamenufaika na zoezi hili. Aidha, Elimu hii inayotolewa na ukaguzi unaofanyika unasaidia sana kuongeza uelewa na kubaini ukiukwaji wa sheria, kuzuia migogoro na kuboresha mahusiano mema mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia uundwaji na uimarishwaji wa vyombo vya ushirikishaji wa Wafanyakazi na waajiri ili kuwawezesha kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayowagusa. Kwa kuzingatia dhana ya UTATU (*Tripatism*), Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* imetoa mafunzo kwa Wajumbe 89 wa Bodi 12 za mishahara kisekta kuhusu upangaji wa kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi. Bodi hizo ni ya sekta za Ujenzi; Mawasiliano; Shule binafsi; Madini; Viwanda na Biashara; Ulinzi Binafsi; Afya; Maji; Majumbani; Mahoteli; Kilimo na Usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeratibu vikao vitatu vya Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii *(Labour, Economic and Social Council - LESCO)* ambapo wajumbe wa Baraza walipata fursa ya kujadili na kutoa ushauri wao katika masuala mbalimbali ambayo ni pamoja na marekebisho ya Sheria za Sekta ya Hifadhi ya Jamii, kanuni za Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*) na kanuni za Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya 2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikisha malipo ya fidia kwa watumishi wa umma 176 baada ya kuumia

au kupata madhara wakiwa kazini. Jumla ya sh. 19,999,000 zimetumika kulipa madai hayo.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha na kuendeleza Hifadhi ya Jamii nchini; Wizara imekamilisha marekebisho ya Sheria za Taasisi sita za Hifadhi ya Jamii nchini na kupitishwa na Bunge tarehe 13 Aprili, 2012. Marekebisho haya yatawezesha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* kufanya kazi zake vizuri na yanalenga kuboresha huduma za hifadhi ya jamii nchini. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha Mamlaka ya *SSRA* ambayo imeanza kufanya kazi mwezi Oktoba, 2010. Kuanzishwa kwa Mamlaka hii kumesaidia sana katika kuweka utaratibu wa kudhibiti sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Selemani Jafo nitaitolea maelezo mwishoni kuhusiana na suala hili la Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mkutano Mkuu wa *ILO* uliofanyika Mwezi Juni, 2012 ulipitisha Pendekezo Na. 202 linalolenga kutoa mwongozo kwa nchi wanachama katika kupanua wigo na kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii. Wizara inajipanga vizuri ili kutekeleza vyema pendekezo hili katika maboresho ya sekta ya hifadhi ya jamii yanayoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya ajira ya mtoto na mazingira hatarishi ya kazi; Wizara

imeendelea kuratibu juhudi mbalimbali za kukomesha utumikishwaji na ajira mbaya ya mtoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Serikali za mitaa. Katika kipindi hiki, jumla ya watoto 22,243 wametolewa katika utumikishwaji na kupatiwa mafunzo ya fani mbalimbali ikiwemo elimu ya msingi watoto 8,402, elimu ya MEMKWA watoto 1,428 na elimu ya ufundi watoto 12,413.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* na kwa ufadhili wa Serikali ya Brazil imetoa elimu kuhusu Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto katika Wilaya za Lindi Vijijini, Mtwara Mjini na Vijijini, Masasi, Liwale, Ruangwa, Mikindani na Lindi Mjini. Mafunzo yaliyotolewa yamewezesha kuundwa kwa kamati ndogo za kuratibu masuala ya utumikishwaji wa watoto katika wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Masuala ya Utumikishwaji wa Mtoto iliwezeshwa kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali. Aidha, siku ya kupinga utumikishaji wa mtoto duniani iliadhimishwa Kitaifa tarehe 12 Juni 2012 Jijini Dar es Salaam kwa kauli mbiu isemayo “Haki za binadamu na usawa wa kiraia - Tokomeza utumikishwaji wa watoto”.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa suala la kutokomeza utumikishaji na ajira mbaya ya mtoto linapewa kipaumbele na kuhakikisha kuwa wale wote wanaokiuka na kutenda kosa hili wanafikishwa katika vyombo vya sheria, katika mwaka 2011/2012 jumla ya

kesi tatu zipo katika hatua ya kufikishwa mahakamani. Kesi hizi mbili zipo Mjini Songea Mkoani Ruvuma na moja Mjini Mafinga Mkoani Iringa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi. Wizara imeendelea kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa usalama na afya mahali pa kazi, ambapo Rasimu ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Rasimu ya Sheria Mpya ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi zimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukuzaji wa ajira nchini. Hali ya umaskini uliokithiri ikiambatana na ukosefu wa ajira hususan kwa vijana imeendelea kuwa changamoto kubwa duniani. Ripoti ya mwaka 2012 ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* inaonesha kuwa, mwaka 2011 nguvukazi inayofikia milioni 205 haikuwa na ajira sawa na ongezeko la watu milioni 27 kwa kipindi cha miaka minne (ukilinganisha na mwaka 2007).

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ukosefu wa ajira duniani kwa mwaka 2011 ulikuwa ni asilimia sita ukilinganisha na asilimia 5.6 mwaka 2007. Vijana ambao hawakuwa na kazi duniani kwa mwaka 2011 (miaka 15–24) walikadiriwa kuwa milioni 74.8 ukilinganisha na milioni 73.5 kwa mwaka 2007 sawa na asilimia 12.7 ikilinganishwa na asilimia 11.8 kwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara,Tanzania ikiwa mojawapo, ukosefu wa ajira kwa mwaka 2011 ni asilimia 8.2 na

tatizo hili ni zaidi kwa vijana ambapo ukosefu wa ajira ni asilimia 12.8.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukosefu wa ajira katika Tanzania kulingana na takwimu zilizopo ni asilimia 11.7 kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 15 na zaidi. Jumla ya vijana walioajiriwa wenye umri wa miaka 15 hadi 34 ni 9,056,217 sawa na asilimia 86.6 na vijana wasio na ajira ni 1,398,677 sawa na asilimia 13.4 ya jumla ya nguvukazi yote ya vijana*.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu juhudi za kukuza ajira nchini na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira 2008 kwa kuhamasisha na kuwahusisha wadau mbalimbali katika utekelezaji wake. Katika kipindi hiki Wizara imetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za ajira nchini hususan katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali. Taarifa zilizopatikana zinaonesha kwamba, katika mwaka 2011/2012, jumla ya ajira 250,678 zilipatikana kutokana na baadhi ya miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* 34,516; miradi ya ujenzi wa barabara kupitia *TANROADS* 42,107; miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali 17,685; Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (*TIC*) 82,834; Mamlaka ya Ukanda wa Kiuchumi *(EPZA)* 15,100 na Serikali 38,289.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa takwimu za ajira linachangia sana katika kutoa picha hasi

kwamba hakuna fursa za ajira zinazoundwa nchini. Wizara yangu imechukua hatua ya kuhakikisha taarifa za fursa za ajira zinapatikana kwa faida ya watafuta ajira hususan vijana. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* imempata mshauri mwelekezi anaye andaa mfumo wa taarifa za soko la ajira utakaokamilika katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Utambuzi wa fursa za Ajira katika Mipango na Programu za Maendeleo. Wizara imetoa mafunzo elekezi kwa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu kuainisha fursa za ajira na kujumuisha masuala ya ajira na kazi za staha katika Sera, Mipango na programu za maendeleo za kisekta. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara imetoa mafunzo kwa Wizara nne (4) na Mikoa miwili (2).

Mheshimiwa Spika, mafunzo yametolewa kwa kutumia mwongozo maalum ulioandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha. Tangu tulipoanza utaratibu huu mwaka 2010/2011, jumla ya Wizara kumi (10) na Mikoa minne (4) imepatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hizo ni Ofisi ya Rais Tume ya Mipango; Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Fedha. Mikoa iliyopatiwa mafunzo ni Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa Taasisi za Umma kuainisha fursa za ajira katika mipango na programu za ajira umeanza kuonesha mafanikio. Tayari baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma zimetoa taarifa inayoashiria kwamba fursa za ajira zaidi 800,000 zitatengenezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, katika fani mbalimbali, kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya mpango wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano *(FYDP I)*.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeshirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika utekelezaji wa mradi wa "Kazi Nje Nje" unaotekelezwa na Shirika la Kazi Duniani. Mradi huu umewapatia mafunzo vijana 28 (wasichana 13 na wavulana 15) wasomi waliomaliza vyuo vikuu ambao wamedhamiria kujiajiri katika sekta ya ushauri wa biashara na ujasiriamali ili wahusike katika kuwaelekeza vijana wenzao jinsi ya kuibua fursa za ajira zilizopo mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu ulimalizika mwezi Desemba 2011 na ulizifikia Wilaya 10 za Tanzania Bara ambazo ni: Mbeya Mjini, Kibaha, Handeni, Mtwara Mjini, Singida Mjini, Bagamoyo, Urambo, Tabora Mjini, Magu na Lindi Mjini. Vijana hao wamehamasisha wenzao 76,241 kuhusu masula ya ujasiriamali na utambuzi wa fursa za kujiajiri. Kati ya hao 1,741 wameweza kujiajiri. Awamu ya pili imeanza kutekelezwa mikoa yote kwa utaratibu wa Kanda.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu ushiriki wa wajasiriamali wadogo wadogo 82 wa Tanzania waliojiajiri (wanawake 71 na wanaume 11) kushiriki maonesho ya 12 ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki huko Jijini Kampala, Uganda mnamo tarehe 3 –10 Desemba, 2011. Washiriki walifanikiwa kupata masoko ya baadhi ya bidhaa zao katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa watu wenye ulemavu. Wizara imehamasisha wadau mbalimbali kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 inayosisitiza kukuza usawa wa fursa za ajira na mapato kwa makundi yote wakiwemo watu wenye ulemavu. Kwa kushirikiana na wadau kama vile *Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT)*, *CEFA* na *Radar Development* kupitia mradi wa "*LESS is More*" uliofadhiliwa na Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Spika, jumla ya watu wenye ulemavu 308 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi wa fani mbalimbali kama vile kushona, upishi, sanaa na ufundi seremala. Kati ya wahitimu hao, 145 wameajiriwa na 163 wamejiajiri. Makampuni 32 yametoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi walemavu katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu na ukaguzi wa vibali vya ajira za wageni; Wizara imeimarisha taratibu za usimamizi, utoaji na ukaguzi wa vibali vya ajira za wageni kwa lengo la kuhakiki na kulinda nafasi za ajira za watanzania. Jumla ya maombi 3,773 mapya ya vibali vya ajira za wageni daraja "B" yalipokelewa,

ambapo 2,740 yalikubaliwa, 668 yalikataliwa, 333 yalisitishwa kwa uchunguzi zaidi na 32 yalipelekwa Kituo cha Taifa cha Uwekezaji *(TIC)* kwa uhakiki. Maombi ya kuongeza muda yalikuwa 1,222 ambapo 963 yalikubaliwa na 269 yalisitishwa kwa uchunguzi na uhakiki wa taarifa za kampuni husika ili kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya maombi 2,233 ya vibali vya ajira daraja "A" kutoka makampuni ya uwekezaji yaliwasilishwa kupitia Kituo cha Taifa cha Uwekezaji *(TIC)* ambapo 2,120 yalikubaliwa na 113 yalikataliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya ukaguzi wa vibali vya ajira katika kampuni 42 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Morogoro kwa lengo la kuhakiki na kubaini ukiukwaji wa taratibu za ajira kwa wageni. Kampuni zilizoonekana kukiuka taratibu zilichukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kupewa onyo na kusitishwa vibali vyao. Kampuni zilizoonekana kutokuwa na mpango wa kurithisha ujuzi kwa wazalendo (*succession plan*) ziliagizwa kutekeleza mpango huo ili kuwaandaa wazawa kujaza nafasi za wageni.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya vibali vya ajira kwa wageni. Lengo la Muswada huu ni kuwa na Sheria moja ya kusimamia masuala ya vibali vya ajira za wageni, hivyo kuondoa utata na migogoro katika utaratibu unaotumika sasa

ambapo kuna Mamlaka na Sheria tofauti zinazoshughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri; Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka 2011/2012 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Kupokea na kushughulikia maombi mapya 11 ya usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri kutoka sekta za usafirishaji, afya, viwanda, majumbani, mahoteli, huduma za elimu, reli na migodini. Kati ya maombi hayo, chama kimoja cha waajiri kinachojumuisha vyama vya waajiri vilivyosajiliwa katika nchi za Afrika Mashariki *(EAEO)* kilisajiliwa.

(ii) Jumla ya wadau 150 wakiwemo waombaji wa usajili wa vyama vipya vya wafanyakazi na vile vilivyosajiliwa walielimishwa juu ya masuala mbalimbali ya vyama kwa mujibu wa sheria za kazi zikiwemo taratibu za kujumuika, uhuru wa kujiunga na taratibu za kusajili wanachama wapya.

(iii) Ukaguzi wa kumbukumbu za wanachama ulifanyika katika Mikoa mitano ambayo ni Tabora, Pwani, Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam ili kuibua changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kisheria kwa watendaji wa vyama vilivyopo katika mikoa iliyotajwa. Aidha, taarifa za fedha zilizokaguliwa na taarifa za mwaka za idadi ya wanachama kutoka

vyama vya wafanyakazi sita zilipokelewa na kushughulikiwa.

(iv) Migogoro 13 ya kiuongozi na ile ya wanachama katika vyama vya wafanyakazi na maeneo mbalimbali ya kazi ilipokelewa na kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kujenga uwezo wake ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuwapatia mafunzo watumishi 80 kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara. Watumishi 63 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 17 walipata mafunzo ya muda mrefu.

(ii) Watumishi 59 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo na Watumishi 15 walithibitishwa katika nafasi zao.

(iii) Watumishi wanne (4) wa Wizara wanaoishi na virusi ya UKIMWI wanaendelea kupata huduma stahiki.

(iv) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kukarabati baadhi ya ofisi na kununua vifaa vya Ofisi katika ofisi za Makao Makuu ya Wizara na ofisi za Mikoani.

(v) Wizara imeshirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi kama vile ulinzi, usafi na matengenezo mbalimbali ya vifaa vya ofisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi sita za umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)*, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)*, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)*, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*. Utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2011/2012 kupitia taasisi hizi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* umesimamia na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwa kufanya ukaguzi 5,995 wa kawaida (*General Workplace Inspections*), ambao ni sawa na asilimia 85.6 ya ukaguzi uliopangwa na ukaguzi maalum 12,549 sawa na asilimia 89.6 ya ukaguzi uliopangwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo unajumuisha ukaguzi wa umeme, *boilers*, mitungi ya hewa, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira. Aidha, wafanyakazi 16,767 walipimwa afya zao, sawa na asilimia 129 ya wafanyakazi 13,000 waliotegemewa kupimwa afya zao. Aidha, mafunzo ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yalitolewa kwa wafanyakazi 1,004 kutoka sehemu mbalimbali za kazi.

Mheshimiwa Spika, Wakala umetoa ushauri kwa waajiri na kuwataka kuzingatia sheria na kanuni za usalama mahali pa kazi. Aidha, wale waliokaidi maagizo walipelekwa Mahakamani na wengine

kufungiwa kabisa shughuli zao. Hadi kufikia Mei 2012 jumla ya kesi 16 zipo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Kitaifa iliadhimishwa mkoani Dar es Salaam tarehe 28 Aprili, 2012 ikiwa na kauli mbiu isemayo, "kuboresha Afya na Usalama Mahali pa kazi katika uchumi kijani" ambapo makampuni 14 yalionesha na kutoa elimu kuhusu shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Wakala umejitangaza kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari na tovuti yake ya *www.osha.go.tz*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)* umetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuhudumia wateja 4,040, kati ya hao watafutakazi ni 2,610 na waajiri 304 na wadu wengine 1,126. Aidha, watafuta kazi 571 waliunganishwa kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi.

(ii) Wakala ulisimamia na kuratibu ajira za Watanzania nchi za nje, ambapo watafuta kazi 1,132 walipata ajira katika nchi za UAE, Oman, Dubai, Denmark na Saudi Arabia.

(iii) Serikali ya Tanzania na Serikali ya nchi ya Qatar zimefanya mazungumzo na kukubaliana watanzania wenye sifa waende kufanya kazi katika nchi hiyo. Mkataba wa makubaliano umeandaliwa na utasainiwa mwaka huu wa fedha 2012/2013.

(iv) Wakala umetembelea waajiri 164 katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro, Iringa, Singida, Arusha, Mara, Shinyanga, Kagera na Tabora kwa lengo la kuwaelewesha waajiri na umma kwa ujumla kuhusu huduma zitolewazo na Wakala pamoja na kubaini fursa za ajira.

(v) Maombi ya Kampuni Binafsi arobaini (40) ya usajili wa kutoa huduma za ajira yalipokelewa na kuchambuliwa ambapo kampuni 28 zimesajiliwa na maombi 12 yanashughulikiwa.

(vi) Wakala umejitangaza kupitia tovuti yake ya *www.taesa.go.tz* ambapo wadau zaidi ya 41,850 wamefikiwa na kufahamishwa kuhusu huduma zitolewazo na Wakala.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* limetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Shirika limekusanya mapato ya kiasi cha shilingi milioni 653,085.7 sawa na asilimia 85.5 ya lengo na kutumika katika kulipa mafao ya Wanachama, kuwekeza katika vitega uchumi, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo.

(ii) Limeendesha semina 464 kwa waajiri na wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii.

(iii) Shirika lilifanya Mkutano Mkuu wa pili wa wadau mwezi Februari 2012 ambao ulihudhuriwa na wadau wapato 701.

(iv) Shirika limeandikisha wanachama wapya 93,455 ambao ni asilimia 66.20 ya lengo lililokusudiwa. Aidha, Shirika limelipa mafao mbalimbali ya jumla ya shilingi milioni 134,183.83 ambazo ni asilimia 117.7 ya lengo kwa wanachama 131,900.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *NSSF* limechangia katika shughuli za maendeleo ya nchi yetu kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali muhimu kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 150 katika eneo la Mkuranga umeanza kutekelezwa ambapo umefikia hatua ya kupata washauri wasanifu (*Consultants*) kwa ajili ya usanifu wa njia ya kusafirishia umeme (*Transmission line*) kutoka Mkuranga mpaka Kinyerezi kwenye gridi ya Taifa.

(ii) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni umeanza ambapo mkandarasi amepatikana na kukabidhiwa eneo la kazi, na yuko katika hatua ya ukusanyaji vifaa kwa ajili ya kuanza ujenzi.

(iii) Ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mkoa wa Njombe na Chuo cha Nelson Mandela Arusha umekamilika.

(iv) Vile vile Shirika limeshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na kutoa

misaada kwa waliopatwa na maafa ya milipuko ya mabomu - Gongolamboto, waliopatwa na ajali ya meli ya *Spice Islanders* na meli ya *Skagit* - Zanzibar, Ujenzi wa madarasa na maktaba katika Shule ya Msingi Mnazi Mmoja, Ujenzi wa kituo cha wanafunzi – Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na taasisi ya Mkapa *Fellows* dhidi ya mapambano ya Malaria na upimaji wa Afya za wanachama.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* limetoa mafunzo mbalimbali, ushauri pamoja na kufanya utafiti ili kuinua tija sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Shirika la Tija la Taifa limetoa mafunzo 70 ya tija na kujenga uwezo sawa na asilimia 87.5 ya lengo lililopangwa, ambapo washiriki 916 sawa na asilimia 76 ya lengo wamenufaika na mafunzo hayo. Aidha, lilifanya utafiti mbili sawa na asilimia 50 ya lengo na kutoa huduma za uelekezi katika kukuza tija kwa wateja 15 kutoka Taasisi za umma na binafsi sawa na asilimia 50 ya lengo. Vile vile Shirika limejitangaza kupitia tovuti yake ya *www.niptz.org*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/12, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya tathmini ya uwezo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Actuarial Assessment of the Pension Schemes in* Tanzania Mainland) kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania. Matokeo ya tathmini hii yamesaidia kuandaa mapendekezo ya mfumo na

mafao bora kwa wanachama na pia kuhakikisha kuwa Mifuko iliyopo inakuwa endelevu.

(ii) Kufanya utafiti kuhusu vitega uchumi vya Mifuko *(Portfolio Review)* uliwezesha kuandaa Mwongozo wa Uwekezaji kwenye Mifuko *(Social Security Schemes Investment Guidelines*, 2012). Mwongozo huu umeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Mei, 2012.

(iii) Kufanya ukaguzi wa uangalizi kwa kila Mfuko kwa mujibu wa kifungu cha 40 cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2008. Lengo la ukaguzi huu ni kupima uzingatiaji wa matakwa ya sheria na kanuni zinazohusu usimamizi na udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

(iv) Kutoa elimu kwa umma ili kuwahamasisha wananchi wengi zaidi wajiunge na Mifuko ya hifadhi ya jamii ili kujikinga na majanga mbalimbali yanayotokana na umasikini wa kipato wakati wa uzeeni.

(v) Aidha, mwezi Novemba 2011 Wiki ya Hifadhi ya Jamii ilizinduliwa kwa mara ya kwanza nchini na kuonyesha mafanikio makubwa kwa kuhimiza wananchi wengi kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*Commission for Mediation and Arbitration*) ni chombo chenye jukumu la kusuluhisha na kuamua migogoro ya kikazi. Upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Tume unaweza kupeleka shauri hilo Mahakama ya Kazi. Vile vile, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya Sheria

za Kazi na uimarishaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu15), iliidhinishiwa jumla ya Sh. 2,938,263,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo sh. 1,933,763,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 1,004,500,000 ni kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, Tume ilikuwa imetumia jumla ya sh. 1,827,648,572 sawa na asilimia 62.2 ya sh. 2,938,263,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Tume iliendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Migogoro 7,722 ilisajiliwa ambapo migogoro 5,354 sawa na asilimia 69.3 ilisikilizwa na kupatiwa ufumbuzi. Migogoro 3,281 sawa na asilimia 61.3 ilimalizika kwa njia ya usuluhishi na migogoro 2,073 sawa na asilimia 38.7 kwa njia ya uamuzi. Migogoro 2,368 sawa na asilimia 30.7 inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali.

(ii) Tume imewezesha uundwaji wa Mabaraza 40 ya wafanyakazi katika Taasisi mbalimbali kama ifuatavyo; Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji (14),

Taasisi za Serikali (Wizara, Idara, Wakala na Mashirika) (21) na Sekta binafsi (5).

(iii) Taasisi 73 zilipewa mafunzo ya uimarishaji wa mabaraza yaliyosajiliwa kuhusu wajibu wa wajumbe wa mabaraza juu ya majukumu yao ambazo ni Halmashauri za Wilaya na Miji (13), Taasisi za Serikali (Wizara, Idara, Wakala na Mashirika 51 na Sekta binafsi (9).

(iv) Tume imeratibu uchapaji na uzinduzi wa juzuu ya kwanza ya kitabu cha rejea cha maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Vol.1.*) yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi. Aidha, imekamilisha rasimu ya juzuu ya pili ya kitabu cha rejea cha maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide* Vol. 2.) kwa kushirikana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*.

(v) Tume imeandaa na kuchapa kitabu cha mwongozo wa kuzuia na kutatua migogoro ya kikazi (*Dispute Prevention and Resolution Training Guide*). Vilevile imechapisha toleo la pili la vitabu vya kiswahili vya Sheria Na.6 ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 na Sheria Na. 7 ya Taasisi za Kazi zote za mwaka 2004 pamoja na kanuni zake kwa kushirikana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*.

(vi) Tume imewaendeleza watumishi tisa katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani za sheria, uhasibu na utunzaji wa kumbukumbu ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013 Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia sheria na viwango vya kazi; ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Utekelezaji kwa mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Kazi na Huduma za Ukaguzi:-

(i) Kufanya jumla ya ukaguzi 4,800 katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima.

(ii) Kukamilisha utafiti wa vima vya chini vya mishahara katika sekta kumi na mbili ikiwa ni pamoja na kuweka vima vya chini vya mishahara katika sekta hizo.

(iii) Kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kufanya tathmini ya kuanzisha Idara ya Hifadhi ya Jamii na kukamilisha maandalizi ya kuanzisha mamlaka ya Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara wakiwa kazini.

(iv) Kuwezesha vikao vya Baraza la ushauri wa masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii *(LESCO)*.

(v) Kuwezesha vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kuratibu masuala ya kukomesha utumikishwaji wa

watoto (*National Intersectoral Coordination Committee - NISCC*).

(vi) Kutoa elimu kwa wadau (Wafanyakazi na Waajiri) na umma kwa ujumla kuhusu Sheria za Kazi.

(vii) Kukamilisha na kutekeleza Mkakati wa maboresho katika sekta ya Hifadhi ya Jamii ikiwa ni pamoja na mpango wa pensheni kwa Wazee.

(viii) Kukamilisha utafiti na kutoa mapendekezo ya namna ya kutengeneza mfumo bora na endelevu kwa ajili ya kutoa Pensheni kwa Wazee (*Universal Pension*) nchini.

(ix) Kukamilisha Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Afya na Usalama mahali pa Kazi Na. 5 ya mwaka 2003.

(x) Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Usalama na Afya mahali pa Kazi ya mwaka 2010.

(xi) Kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba Na.189 wa 2011 wa Shirika la Kazi Duniani kuhusu haki za wafanyakazi wa majumbani (*ILO Convention for Domestic Workers).*

(xii) Kufanya marejeo ya kanuni za utatu kuhusu masuala ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI mahali pa kazi ya mwaka 2008 ili iendane na Pendekezo Na. 200 la *ILO* na mikataba mingine ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa Ajira nchini:-

Kupitia miradi yake ya maendeleo chini ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaotelekezwa na Wizara na Taasisi mbalimbali, Serikali inategemea katika mwaka wa fedha 2012/2013 kutakuwa na upatikanaji wa fursa za ajira zaidi ya 800,000. Fursa hizi zitapatikana kutokana na utekelezaji wa baadhi ya miradi na programu za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Sekta ya Kilimo itazalisha zaidi ya ajira 169,189; Ujenzi wa Miundombinu ya barabara itazalisha ajira 646,615; Mawasiliano itazalisha ajira 27,600; Viwanda na Biashara itazalisha zaidi ya ajira 5,000. Halmashauri za Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani zitazalisha zaidi ya ajira zipatazo 6,885. Takwimu hizi ni mbali na ajira za watumishi 56,678 watakaoajiriwa Serikalini kama ilivyobainishwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika Hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaimarisha mfumo wa kukusanya na kutoa taarifa za soko la ajira ambao utawezesha kufuatilia na kukusanya taarifa na takwimu za ajira zinazotokana na utekelezaji wa miradi yote inayotekelezwa na Serikali chini ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano pamoja na fursa za ajira katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa taarifa za soko la ajira ni suala muhimu kwa sababu ni moja ya kiashiria muhimu katika ukuaji wa uchumi katika nchi na husaidia kuonesha wananchi fursa za ajira zilizopo. Hivyo, hili ni eneo linalopewa kipaumbele na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara itatoa mafunzo ya namna ya kuainisha fursa za ajira na kujumuisha masuala ya ajira na kazi za staha katika Sera, mipango na programu za maendeleo kwa Wizara, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazijapatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuhakikisha kwamba malengo na viashiria vya kukuza ajira na kazi za staha yanazingatiwa. Aidha, tutashirikiana na Ofisi ya Rais – Tume ya mipango na Wizara ya Fedha kuandaa Mwongozo kwa Wizara na Taasisi wa namna ya kukusanya na kuwasilisha takwimu za ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la ukuzaji wa Ajira ni suala mtambuka ambalo haliwezi kuachiwa Wizara ya Kazi na Ajira au Serikali peke yake. Ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kunahitajika kuimarisha ubia baina ya Serikali, Sekta binafsi, vyama vya wafanyakazi na waajiri pamoja na Asasi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza fursa za ajira, Wizara itahamasisha na kushirikiana na mamlaka mbalimbali ili ziweze kuchukua hatua na kuweka mazingira mazuri zaidi ya ukuzaji wa ajira na kazi za staha nchini. Maeneo yatakayopewa kipaumbele katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 ni:-

(i) Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kuwekeza, kuzalisha mali na kufanya biashara, kama vile kupatikana kwa umeme wa uhakika na nafuu,

miundombinu ya usafirishaji pamoja na mfumo wa sheria za biashara na ajira. Hatua hizi zitasaidia kuongeza uwekezaji na uzalishaji mali na kurahisisha kufanya biashara katika maeneo mbalimbali na hivyo kuongeza fursa za ajira.

(ii) Taasisi za fedha za Umma na Binafsi kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu na rafiki kwa wawekezaji na wafanyabishara hasa wa kati na wadogo. Taasisi hizi zitachangia katika kuongeza fursa za ajira kwa kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika, *SACCOS* na wajasiriamali binafsi hususan vijana kwa ajili ya uzalishaji mali na kufanya biashara.

(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwatengea wananchi maeneo ya kuzalisha mali, kufanya biashara na shughuli za sanaa na michezo. Tunapozungumzia maeneo tunamaanisha mashamba kwa ajili ya kilimo na ufugaji, maeneo maalumu ya kufanyia biashara, viwanda vidogovidogo, viwanja vya michezo na sanaa mbalimbali. Kwa ujumla haya yote yapo katika Mamlaka ya Tawala za Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa.

(iv) Taasisi za elimu za umma na binafsi kutoa mafunzo yanayowapatia ujuzi na stadi za kazi watafuta kazi hasa vijana ili kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa kwa urahisi zaidi. Tatizo la kukosa sifa au stadi stahiki katika baadhi ya kazi kumechangia sana vijana wetu kukosa ajira. Kwa hali hiyo Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itawekeza zaidi katika kuimarisha eneo la rasilimali watu hususan vijana.

(v) Taasisi na mamlaka mbalimbali kuanzisha utaratibu wa kuwapatia vijana vifaa na nyenzo za uzalishaji mali. Hatua hii inalenga kuwahamasisha na kuwawezesha vijana kuzalisha mali, kujiajiri na vile vile kuwaajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la vijana wetu kukosa ajira kutokana na kutokuwa na ujuzi na stadi za kazi zinazohitajika katika soko la ajira, lipo tatizo la vijana wengi kuwa na mtazamo hasi kuhusu kazi (*negative attitude towards work*).

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko kutoka kwa waajiri kuwa baadhi ya vijana wanaoajiriwa wana matatizo kadhaa kwa mfano: ukosefu wa maadili, kuchagua kazi, kutokuwa wabunifu na kutokupenda kazi. Kwa mtazamo huu, naomba kutoa rai kwa wadau wote, wazazi na jamii kwa ujumla kushirikiana katika kuwaelimisha na kuwajengea vijana misingi bora itakayowabadilisha mitazamo kuhusu kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza ajira na kazi za staha nchini, katika mwaka 2012/2013 Wizara imepanga pia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwapatia Wadau miongozo stahiki ya namna ya kuhuisha malengo na viashiria vya kukuza ajira na kazi za staha katika Sera, Mipango na Programu za maendeleo za kisekta;

(ii) Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wadogo kwenye maonesho ya 13 ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika nchini Burundi mwezi Novemba/Desemba 2012;

(iii) Kushughulikia maombi ya vibali vya ajira za wageni na kufanya kaguzi za kuhakiki kampuni zilizoajiri wageni;

(iv) Kuandaa Muswada wa Sheria ya vibali vya ajira za wageni nchini;

(v) Kufanya maandalizi ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi nchini (*Integrated Labour Force Survey*) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Utafiti huo utatoa picha halisi ya hali ya ajira nchini hususani viashiria vya soko la ajira ambavyo ni pamoja na kiwango cha ukosefu wa ajira, ajira isiyo timilifu, ujuzi na viwango vya elimu vya nguvu kazi, ajira mbaya ya watoto, shughuli za kiuchumi katika sekta rasmi na isiyo rasmi na kipato kinachotokana na kazi;

(vi) Kuandaa Sera ya Taifa ya Uhamaji wa Nguvukazi nchini *(Labour Migration Management Policy);* na

(vii) Kuhamasisha wadau kuhusu ajira za watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha kuwa walemavu wanapata fursa za ajira ya kuajiriwa na kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kushughulikia maombi na kusajili vyama vya wafanyakazi na waajiri na kuwaelimisha wadau juu ya umuhimu wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri.

(ii) Kufanya ukaguzi wa kumbukumbu za wanachama na fedha katika mikoa na matawi ya vyama vya wafanyakazi na waajiri.

(iii) Kushughulikia malalamiko mbalimbali ya vyama na kutoa ushauri stahiki kwa lengo la kujenga mahusiano mazuri kati ya waajiri na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga uwezo wa Wizara. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara ili waweze kutoa huduma bora.

(ii) Kutoa mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na Utawala Bora sehemu ya kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

(iii) Kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi kama vile ulinzi, usafi na matengenezo ya vifaa vya ofisi katika kuboresha utendaji kazi.

(iv) Kuratibu ushirikishwaji wa kuimarisha mahusiano bora kwa watumishi wa Wizara kwa kufanya mikutano ya Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Umma chini ya Wizara:-

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia taasisi za umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)*. Ili kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wakala utatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya ukaguzi 12,000 wa kawaida na 16,000 maalumu wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi na kupima afya za wafanyakazi 20,000 katika sehemu mbalimbali za kazi.

(ii) Kutoa kozi nne (4) za mafunzo ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi kwa Maafisa wa Afya na Usalama mahali pa kazi.

(iii) Kukamilisha taratibu za kuridhia mikataba mitatu (3) ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO Conventions*); mikataba hii ni Mkataba Na. 155 wa mwaka 1981 (*Occupational Safety and Health Convention*), Mkataba Na. 167 wa mwaka 1988 *(Occupational Safety in Construction Convention*) na Mkataba Na. 187 wa mwaka 2006 *(Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention).*

Pili, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA).* Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wakala huu umepanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri ndani na nje ya nchi na kufanya utafiti katika nyanja za upatikanaji wa fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

(ii) Kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za soko la ajira.

(iii) Kuendeleza rasilimali watu ili kuongeza tija na ufanisi.

(iv) Kusimamia na kuratibu shughuli za Wakala binafsi zinazotoa huduma.

Tatu, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. Katika mwaka 2012/13 Shirika litatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukusanya jumla ya Shilingi milioni 1,016,029.7 na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia gharama za uendeshaji, mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali na miradi ya maendeleo.

(ii) Kuimarisha uandikishaji na ukusanyaji michango ya Wanachama, kuendelea na ukusanyaji wa madeni kwa waajiri na pango kwa wapangaji wa majengo ya *NSSF*.

(iii) Kuboresha huduma kwa wateja kwa kuhakikisha Ofisi zote za Shirika zinaunganishwa na mkongo wa mawasiliano wa Taifa na kujenga uwezo katika Shirika na kutafuta vyanzo vingine vya kugharamia miradi ya muda mrefu inayohitaji fedha nyingi kwa njia ya ubia (*joint venture*).

(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa hifadhi ya jamii, kupima afya za wanachama na kufanya Mkutano Mkuu wa Tatu wa wadau wa *NSSF*.

(v) Kufanya tathimini ya uwezo wa mfuko kifedha ili kulipa mafao kwa wanachama wake kwa muda mrefu ujao na kuandaa Mpango wa muda mrefu *(Corporate Plan*) wa Dira ya Shirika kwa miaka mitatu 2013/2014- 2015/2016.

(vi) Kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigamboni na mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 150 katika eneo la Mkuranga.

(vii) Kukamilisha mradi wa ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika mikoa ya Arusha na Kigoma, pamoja na Wilaya ya Kahama na kuendeleza ujenzi katika Mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Mbeya, Moshi, Mara, Mwanza, Wilaya ya Ilala na ujenzi wa nyumba za Jeshi la Wananchi *(TPDF)* kwa kutumia mitambo ya *UBM*. Aidha, kukamilisha ujenzi wa ofisi za kumbukumbu katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mara na ujenzi katika Wilaya ya Temeke utaanza pindi mzabuni atakapokuwa amepatikana.

(viii) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Apollo Jijini Dar es Salaam, na kuendelea na ujenzi wa ofisi za *RITA* (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency),* kuanza ujenzi wa jengo la Mzizima jijini Dar es Salaam, hoteli ya kisasa Mwanza, ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu *Farm*) na

Ujenzi wa Jengo la Maadili Dar es Salaam, endapo taratibu za mazungumzo zitakamilika.

(ix) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Hisabati (*College of Earth and Mathematics)* katika Chuo Kikuu cha Dodoma na nyumba za polisi awamu ya tatu endapo majadiliano na Serikali yatakuwa yamekamilika.

(x) Kuendeleza Ujenzi wa makazi, biashara na ofisi katika eneo la Mchikichini Ilala, endapo manispaa ya Ilala itakuwa imewahamisha wapangaji wa nyumba zilizopo na kukabidhi Hati miliki za ardhi kwa Kampuni ya Hifadhi *Property Limited* ambayo itasimamia mradi huu. Aidha mradi wa ujenzi wa nyumba Magomeni Kondoa Kinondoni Dar es Salaam, utafanyika pindi kutakapofikiwa makubaliano kati ya Shirika na Manispaa ya Kinondoni.

(xi) Kufanya upembuzi yakinifu (*detailed feasibility study*) wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam mpaka Chalinze.

Nne, Shirika la Tija la Taifa *(NIP).* Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika limepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendesha mafunzo 80 ya uongozi yatakayohudhuriwa na watumishi 1,200 kutoka taasisi za umma na binafsi.

(ii) Kutoa huduma za ushauri kwa wateja 30 katika sekta za umma na binafsi.

(iii) Kufanya utafiti minne (4) katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija.

Tano, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)*. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka itaendelea na hatua za kuboresha sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali ambayo itajikita katika kuboresha sekta ya Hifadhi ya Jamii na kuifanya kuwa endelevu na yenye mchango katika maendeleo ya wanachama wa Mifuko na nchi kwa ujumla.

(ii) Kusajili Mifuko, Mameneja uwekezaji (*fund managers)* na watunza mali *(custodians)* kwa ajili ya kutenganisha majukumu kwenye uendeshaji wa Mifuko ili kuleta ufanisi zaidi.

(iii) Kuratibu mikakati ya kupanua wigo wa hifadhi ya jamii nchini ili makundi mbalimbali hasa ambayo yako kwenye sekta isiyo rasmi yaweze kufaidika na huduma zitolewazo na taasisi za hifadhi ya jamii.

(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu sekta ya hifadhi ya jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni, makongamano, Wiki ya Hifadhi ya jamii na mtandao.

(v) Kufanya ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha kuwa Mifuko hiyo inatekeleza

majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

(vi) Kutoa mafunzo kwa Bodi za wadhamini na watendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii juu ya kanuni na miongozo inayotolewa na Mamlaka ili kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2012/2013, Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) inatarajia kutumia kiasi cha Sh. 15,945,298,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wake wa mwaka. Kati ya fedha hizi Sh. 13,109,498,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 2,835,800,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Tume imeweka kipaumbele katika kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusuluhisha na kuamua migogoro ya kikazi na kuandaa taarifa.

(ii) Kufanya utafiti na kushughulikia migogoro ambayo haijaripotiwa katika Tume.

(iii) Kuendesha mafunzo ya uelewa na ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya kuzuia na kutatua migogoro sehemu za kazi.

(iv) Kusimamia uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi.

(v) Kujenga uwezo wa Tume kwa kuwaendeleza watumishi, kutembelea nchi zinazoendesha shughuli za utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa lengo la kujifunza.

(vi) Kuboresha mazingira ya uandaaji na utunzaji taarifa kwa njia ya elektroniki (*Case Management System).*

(vii) Kuijengea uwezo Kamati ya Huduma Muhimu *(Essential Services Committee*) za kazi.

(viii) Kuratibu uchapaji na usambazaji wa juzuu ya pili ya vitabu vya rejea vya maamuzi mbalimbali ya Tume yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi pamoja na kitabu cha mwongozo wa namna ya kuzuia na kutatua migogoro ya kikazi sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2012/2013, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inaomba jumla ya Sh. 2,131,329,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudi

zao kubwa walizoonesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa kaka yangu Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Mbunge wa Segerea kwa ushirikiano na ushauri wake wa karibu anaonipatia mara kwa mara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu Bwana Eric F. Shitindi na Naibu Katibu Mkuu Mstaafu, Bibi Edine E. Mangesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru sana Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Bodi zao kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa njia ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii – *(LESCO)*, Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)*, kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo ikiwemo Shirika la Taifa la *(ILO)* kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya

Washirika wa Maendeleo ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na Washirika wa maendeleo mbalimbali ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yetu. Hivyo, napenda shukurani za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani *(ILO), UNDP, UNICEF, UNFPA,* Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark *(DANIDA)*, Idara ya Kazi ya Marekani, Serikali ya Brazil, Benki ya Africa *(AfDB)* na Benki ya Dunia *(WB)*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. Pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao ya mara kwa mara na kwa ushauri wao pia kwangu binafsi na Wizara yangu wanaotupatia kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa mkoa wangu wa Mara hasa akinamama walionipa fursa ya kusimama hapa mbele yako kwa mara nyingine kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Aidha, naomba nishukuru kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa mchango mkubwa wanaonipatia na faraja hususan binti yangu Patricia Rhobi Kabaka na wajukuu zangu Christina na Angelo kwa upendo na faraja kubwa wanaonipatia kila mara ninapokuwa nawahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwajulisha Wafanyakazi wote kwamba, Wizara yangu pamoja na Taasisi zake itatekeleza mabadiliko ya Sheria za Hifadhi ya Jamii kwa uangalifu mkubwa na tutahakikisha kwamba, tunawashirikisha na kuwaelimisha kwa kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha na kuomba fedha, naomba nitoe maelezo mafupi kama nilivyoahidi kuhusiana na hoja aliyoitoa Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo hapo jana kuhusiana na mabadiliko na marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Jamii yaliyofanyika hapa tarehe 13 Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Azimio la Bunge lililowasilishwa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe jana tarehe 6 Agosti, 2012 juu ya umuhimu wa kuletwa Bungeni Muswada wa Dharura wa Marekebisho ya Sheria Na. 5 ya Mwaka 2012 inayozungumzia Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo ndani yake imeelezea kuzuiwa kwa fao la kujitoa *(withdrawal benefit*) kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba, kwanza nasikitika kwamba sheria hii imepokelewa kwa hisia tofauti na imetangazwa na vyombo vya habari kwa hisia tofauti. Wapo watu waliotafsiri kuwa utekelezaji wa Sheria hii unatokana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kufilisika kutokana na uwekezaji mbaya katika miradi ya Serikali kama vile ujenzi wa Chuo Kikuu na miradi mingine na hasa wakigusia *NSSF*. Ukichukua kwamba kuna chombo kimoja cha habari kilidai

kwamba *NSSF* iko hatarini kufilisika baada ya Serikali kushindwa kulipa Shirika hilo kutokana na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wapo wanaodai kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ina hali mbaya kifedha kutokana na uwekezaji mbaya kwa ujumla. Wapo watu waliokwenda mbali zaidi sina hakika, lakini nimesikia wanatafsiri kwamba utekelezaji wa sheria hii unatokana na hali ya Chama cha Mapinduzi kutaka kutunisha Mifuko ya Hifadhi hii ili baadaye zichotwe kwa ajili ya kugharamia uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, yote haya sio kweli huu ulikuwa utekelezaji ambao ulitokana na sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu. Tatizo kubwa tulilogundua ni kwamba hatukutoa elimu ya kutosha kabla ya kuleta marekebisho haya hapa Bungeni. Utaratibu wa wafanyakazi kujitoa na kuchukua mafao yao katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii umekuwepo kwa muda mrefu. Utaratibu huu ulihusu wafanyakazi wote wa Mikataba ya Ajira na Masharti ya Kudumu na Malipo ya Pensheni pamoja na wale wa Mikataba ya Masharti ya Muda Maalum.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Na. 5 ya Mwaka 2012 yaliyofanywa na Bunge lako Tukufu tarehe 13 Aprili, 2012, utaratibu wa kujitoa na kuchukua michango ambayo mwanachama amechangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ulifanyiwa marekebisho na kuzuia utoaji wa fao la kujitoa, ambalo kwa kweli lilisababisha malalamiko mengi sana hasa wafanyakazi wa migodini.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Jafo kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kutembelea migodi yote amekwenda *GGM*, Bulyankulu, Nyamongo amekutana na wafanyakazi na kama tunavyosema amesikia *from the horse's mouth* kwamba tatizo lao ni nini na kutokana na kazi hiyo aliyoifanya Mheshimiwa Jafo sasa hivi migodi imetulia. Naomba nimpongeze na nimshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imesikia malalamiko ya wafanyakazi na wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na hoja za Waheshimiwa Wabunge na ya Mheshimiwa Jafo na kwamba imepokea na kuzingatia mapendekezo yaliyomo katika Azimio la Bunge na imekubali kuletwa kwa Muswada wa Sheria hapa Bungeni ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuujadili upya katika Mkutano ujao wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua pamoja na kwamba Muswada huu utaletwa kwa hati ya dharura, lakini mchakato wa kuwasilisha Muswada huu lazima upitie vipengele muhimu ikiwemo na kupitia vikao vyote, lakini kubwa zaidi ambalo tumeliona sisi Wizarani pamoja na Mamlaka ni kutoa elimu ili wananchi kabla hawajasaidia kuamua pamoja na Waheshimiwa Wabunge tuweze kupata elimu kwa nini tunasema kujiwekea akiba ni muhimu kuliko kuchukua akiba mapema.

Mheshimiwa Spika, nasema mchakato huu utaanza mara moja kwa kuwashirikisha wadau wote wa sekta ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo Kamati yetu makini sana ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nimalizie hoja yangu kwa kufanya hitimisho kwamba, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu na kazi za Wizara kwa mwaka 2011/2012 na Mpango wa Kazi kwa mwaka 2012/2013, Wizara inawasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 na Fungu 15 kama ifuatavyo:-

Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira; matumizi ya Kawaida Sh. 13,109,498,000.00 na Miradi ya Maendeleo Sh. 2,835,800,000.00; Jumla Sh. 15,945,298,000.00.

Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi; Matumizi ya Kawaida Sh. 2,131,329,000.00; Jumla Sh. 2,131,329,000,00.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi hii na jinsi unavyoendesha vikao vyetu, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote naomba niwashukuru kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya *www.kazi.go.tz*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo imehusika na Wizara hii, mwakilishi wake Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA (K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninayo shukrani mbele ya Mungu kwa upendeleo wake alionipa tena kwa siku ya leo kuwa mzima na napenda nitoe shukrani kubwa kwa kwa Wanankenge kwa kunifanya nifanye kazi yangu bila matatizo yoyote. Pia namshukuru Mungu kwa ajili ya mume wangu anavyonisaidia kufanya kazi yangu vizuri, Mungu ambariki sana. Pamoja na watoto wangu, namwomba Mungu awasaidie waendelee kumtumia Mungu, J. *Sisters*.

Mheshimiwa Spika, mbele yangu ninayo taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa Watanzania wote waliofikwa na majanga mbalimbali likiwemo lile la ajali ya meli ya *MV. Skagit* iliyotokea maeneo ya Chumbe tarehe 18 Julai, 2012. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira na uvumilivu wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika ajali hiyo. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 na Kanuni ya 114 (7), nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge (2007), majukumu ya Kamati hii ni pamoja na kufikiria na kuchambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira, Dar es Salaam tarehe 7 na 8 Juni, 2012 na kupata maelezo ya Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira, ambayo yalihusu utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 na malengo yaliyomo katika bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kufikiria taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira ya mwaka 2011/2012 na bajeti ya mwaka 2012/2013 ilizingatia miongozo muhimu ya Wizara ikiwa ni pamoja na dira, dhima, majukumu na malengo ya Wizara. Katika kikao hicho, Kamati ilihoji utekelezaji wa sekta mbalimbali za Wizara ya Kazi na Ajira. Aidha, Kamati iliipitia bajeti ya mwaka 2012/2013, malengo yaliyowekwa pamoja na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Bajeti ya mwaka 2011/2012. Katika mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali na hasa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Serikali iendeleze juhudi ya kutoa elimu kwa waajiri kuhusu sheria na kanuni za ajira na kuhakikisha zinafuatwa ili kuondoa migogoro katika sehemu mbalimbali za kazi. Pia Serikali ione umuhimu wa kuitambua migogoro yote na kuitengenezea mpango kazi ili kuitatua; na

(b) Serikali iongeze bajeti ili kuiwezesha *OSHA* iendelee kufanya kaguzi za viwanda na makampuni mbalimbali nchini na kuleta taarifa ya kaguzi hizo.

Vilevile Serikali ihakikishe uongozi wa viwanda na makampuni unaweka utaratibu wa kupima afya za wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi na elimu ya usalama na afya mahali pa kazi itolewe;

(c) Serikali ihakikishe inafanya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii kuondoa upungufu uliopo. Pia kuhakikisha mifuko yote inakuwa chini ya Wizara moja na inatenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka pamoja na kuanzisha utaratibu wa kumwezesha mwanachama kuhama kutoka Mfuko mmoja kwenda mwingine;

(d) Serikali ianze kutoa pensheni kwa wazee ili kutimiza ahadi ya Waziri Mkuu na kuondoa matatizo mengi yanayowakabili, kwani wengi wao ni walezi wa yatima;

(e) Elimu itolewe kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hasa katika maeneo ya Wilayani na kujenga vitega uchumi hasa katika Wilaya zilizo nyuma kimaendeleo. Pia waajiri wapewe mafunzo kuhusu sheria za uchangiaji na wale ambao hawachangii wawajibishwe kisheria;

(f) Serikali iweke kipaumbele katika kushughulikia tatizo la ajira na hasa kwa vijana. Aidha, Serikali iwezeshe uwekezaji katika sekta ya mawasiliano, sekta binafsi, sekta ya rasilimaliwatu, ujasiriamali na sekta isiyo rasmi ili kuleta suluhisho la tatizo la ajira; na

(g) Serikali ilifanyie kazi tatizo la ajira kwa wageni, ione kama ni kweli wasomi wetu wameshindwa kushika nafasi hasa katika ajira, uwekezaji na ajira binafsi za viwandani na migodini na kuhakikisha elimu ya kuwaamsha vijana ili kuwanufaisha na mianya yote ya ajira itolewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ufafanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi na Ajira kuhusu maagizo ya Kamati unaonesha kuwa, Wizara imejitahidi kutekeleza maeneo kadhaa kwa kiwango cha kuridhisha. Hata hivyo, Kamati inaweka bayana kwamba bado inahitaji kujua zaidi kuhusiana na utekelezaji wa maagizo yaliyobaki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara (Fungu 65) iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya Shilingi bilioni 18.14 na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) iliidhinishiwa Shilingi bilioni 2.81.

Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2011/2012. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na mafanikio yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara imeelimisha waajiri 256 na wafanyakazi 3,926 kuhusu sheria za kazi nchini kote. Vile vile imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za kazi Na. 7 ya mwaka 2004.

(ii) Wizara imefanya jumla ya kaguzi 5,600 za kawaida ambazo zinajumuisha kaguzi za umeme, *Boiler*, mitungi ya hewa, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira. Vile vile, Maafisa Kazi 79

wamepewa mafunzo maalum ya mbinu za kisasa za kufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi.

Pia jumla ya wafanyakazi 14,000 walipimwa afya zao na mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi yalitolewa kwa wafanyakazi 770 wa sehemu mbalimbali za kazi.

(iii) Wizara imechambua maombi 3,773 mapya ya ajira za wageni nchini ambapo maombi 2,740 yalikubaliwa. Aidha, maombi ya kuongeza muda yalikuwa 1,222 ambapo maombi 963 yalikubaliwa na maombi 269 yalisitishwa kwa uchunguzi zaidi.

Vile vile, Wizara imefanya ukaguzi katika Makampuni 42 yaliyoomba na kuajiri wageni katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Morogoro ili kubaini uhalali wa mahitaji hayo. Wizara imeshauri Makampuni kuwa na mpango wa kurithishana madaraka ili kuwaandaa wazawa kujaza nafasi hizo.

Ili kutambua na kuainisha fursa za ajira na kazi za staha, Wizara imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara sita Wizara ya Mambo ya Ndani, Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Fedha.

(iv) Wizara ilisajili migogoro 6,279 ambapo migogoro 4,039 ilisikilizwa na kupatiwa ufumbuzi. Migogoro 2,487 ilimalizika kwa njia ya usuluhishi, migogoro 1,552 kwa njia ya uamuzi na migogoro 2,240 inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali.

Wizara imesajili Mabaraza ya Wafanyakazi 31 na Taasisi 44 zilipewa mafunzo kuhusu matumizi ya Sheria za Kazi Na. 6 na 7 zote za mwaka 2004 na Taasisi 45 zilipewa ushauri wa faida ya ushirikishwaji wa wafanyakazi.

(v) Pia Wizara imeweka Mpango Kazi kwa mwaka ujao wa fedha kwa kufanya kaguzi 17,000 za kawaida na 17,000 maalum za Afya na Usalama Mahali pa Kazi na kupima afya za wafanyakazi 20,000 kutoka sehemu mbalimbali.

Kutoa kozi nne za mafunzo ya afya na usalama mahali pa kazi kwa Maafisa wa Afya na Usalama mahali pa kazi, kozi nane kwa huduma ya kwanza na kozi tatu za uanzishwaji na utendaji wa Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi.

Vilevile mpango kazi huu umepanga kuratibu taratibu za kuridhia mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani ambayo ni Mkataba Na. 155 *(Occupational Safety and Health Convention,* 1981); Mkataba Na. 167 *(Occupational Safety in Construction Convention*, 1988) na Mkataba Na. 187 *(Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention*, 2006).

Pia wamepanga kuendelea kuratibu mkakati wa utekelezaji wa sera, uandaaji wa Sheria mpya na Kanuni kumi za Afya na Usalama Mahali pa Kazi. Kanuni hizo kumi ni kama ifuatavyo: *Gas Safety (installations and use) Rules; OSH (General Administratio) Rules; Lifting Appliances and Gears Rules; Occupational First Aid Regulations; OHS (Hazardous*

*Chemical Substances) Rules; OHS (Welfare Facilities) Regulations; OHS (Building and Construction Industry) Rules; Recording and Reporting of Occupational Diseases, Injuries and Dangerous Occurences Rules; Vessel under Pressure Regulations and OHS (Electric Machinery Safety) Rules*.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2012/2013, imeomba kuidhinishiwa Shilingi bilioni 18.08. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi bilioni 15.94 ni kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 (Wizara) na Shilingi bilioni 2.13 ni kwa ajili ya matumizi ya Fungu 15 (Tume ya Usuluhishi na Uamuzi). Kiasi hiki cha fedha za Wizara kimepungua kwa takribani Shilingi bilioni 2.9 (sawa na asilimia 13.8) ikilinganishwa na Shilingi bilioni 20.96 zilizoidhinishwa kwenye bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati haifurahishwi na upungufu huu wa bajeti ya Wizara, kwani utaathiri utekelezaji wa vipaumbele ambavyo Wizara imepanga kuvitekeleza katika mwaka huu wa fedha. Kwa kuzingatia kuwa bajeti ya Wizara kwa mwaka uliopita wa 2011/2012 ilikuwa imeongezeka kwa takribani Shilingi bilioni 4.19 (sawa na asilimia 25) ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliotangulia wa 2010/2011, ni wazi kuwa Wizara ilikuwa imeanza utekelezaji wa baadhi ya majukumu ambayo sasa itabidi yaathirike kutokana na kupungua kwa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia ukweli kwamba hii ni Wizara ambayo kwa kutumia taasisi mbalimbali zilizo chini yake ina dhamana ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria za ajira zenye kuweka mazingira ya kuhakikisha kuwa Watanzania wanakuwa na viwango bora vya kazi, usawa na staha katika kazi ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ina wajibu wa kuainisha nafasi za ajira, kutambua vijana walio na sifa za kuajiriwa ambao wako katika soko la ajira wakitafuta ajira na kuwaunganisha na nafasi za ajira zilizopo na kutoa hamasa ya ajira binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti hii ya Wizara inahusisha pia bajeti ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*, ni wazi kuwa kupungua kwa bajeti hii kutaathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo ambayo miongoni mwake ni kupokea na kusajili migogoro ya kikazi, kuisuluhisha na kuitolea uamuzi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; Wizara ya Kazi na Ajira inasimamia sekta muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu kama vile:-

(1) Hifadhi ya Jamii:-

- Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii *(SSRA)*;

- Pensheni kwa Wazee; na

- Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(National Social Security Fund – NSSF)*.

(2) Migogoro ya Wafanyakazi.

(3) Hali ya ajira nchini:-

- Tatizo la ajira; na

- Ajira za Wageni.

(4) Vyama vya wafanyakazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni vyema sekta hizi zikaangaliwa kwa umakini kutokana na ukweli kwamba, maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla yanategemea sana ufanisi wa sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Jamii ni utaratibu wa kujiwekea akiba dhidi ya hatari za kupoteza kipato kutokana na kustaafu, ulemavu au kifo, ambao hufanywa na karibu kila mtumishi au mwajiri. Utaratibu huu upo kisheria na hivyo huunganisha Sera na Mipango katika kupunguza umaskini na kumlinda mchangiaji na wategemezi wake dhidi ya tishio la kuathirika kiuchumi pale atakapokuwa amestaafu au amepoteza uwezo wa kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, katika Mataifa yaliyoendelea, Hifadhi ya Jamii imekuwa msaada mkubwa katika kuwalinda wananchi dhidi ya majanga kama vile ugonjwa, ulemavu na kukosa ajira na hivyo kujenga hali ya usawa wa kipato jambo linalopunguza kiwango

cha umaskini. Mfano, utafiti uliofanywa mwaka 2010 na iliyokuwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana (sasa Wizara ya Kazi na Ajira) ulionesha kwamba kipato cha Sh. 10,000/= kitasaidia kupunguza kiwango cha umaskini wa chakula *(food poverty rate)* kwa wazee wa miaka 60 na kuendelea kwa asilimia 58 (kutoka asilimia 15.3 hadi asilimia 6.4). Pia kiasi hicho hicho cha fedha kingeweza kupunguza pengo la umaskini wa mahitaji muhimu *(basic needs poverty gap)* kwa asilimia 59 (kutoka asilimia 10 hadi asilimia 4.1).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali pia kuiga utaratibu huo wa Mataifa yaliyoendelea wa kutumia hifadhi ya jamii katika kupambana na umaskini na kuwaondolea wananchi kero zinazosababishwa na ukosefu wa kipato. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa viwango vya pensheni vinavyolipwa vinawawezesha watu wa rika zote kuishi maisha yenye staha kwa kuwawezesha kupata mahitaji na huduma muhimu kama vile afya. Hata hivyo, kabla ya kuanza kutekeleza utaratibu huo, elimu ya kutosha inapaswa kutolewa kwa wananchi, kwani ni kitu kigeni kwao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Muswada ulioliwezesha Bunge kutunga Sheria Na. 8 ya mwaka 2008 ambayo inaanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)*. Sheria hiyo pamoja na Sheria zote za Hifadhi ya Jamii zilifanyiwa marekebisho mwaka huu kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Sheria Na. 5 ya mwaka 2012 (*The Social Security Laws (Ammendments) Act, No.5 0f 2012)* ili kuondoa kukinzana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tangu kufanyika kwa marekebisho hayo ya sheria kumekuwa na migogoro baina ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii na baadhi ya Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya jamii hapa nchini ambao wanadai marekebisho hayo ya sheria yatawaumiza kutokana na kuondoa fao la kujitoa (*withdraw benefit*). Kutokana na hali hiyo Kamati ilibaini kwamba *SSRA* imeanza kutekeleza Sheria hiyo kabla ya kuandaa Kanuni za utekelezaji hali iliyochochea migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya madai ambayo yanayotolewa na wafanyakazi wanaopinga utekelezwaji wa sheria hiyo ni pamoja na:-

- Baadhi ya sekta kama vile madini ambayo inahusisha matumizi ya dawa na mionzi watumishi wake hawana uhakika wa kufanya kazi mpaka miaka 55 au 60, hivyo kuondoa fao la kujitoa ni kuwanyima wafanyakazi haki zao;

- Watumishi wa sekta binafsi hawana uhakika na ajira zao na Tanzania haina utaratibu wa kisheria wa malipo ya watu wasio na kazi (*unemployment benefit*); na

- Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa umri wa kuishi wa Mtanzania *(demographic health survey*, 2002) ni kati ya miaka 47 hadi 53 hivyo kutokuwepo kwa fao la kujitoa ni kuwanyima wafanyakazi haki zao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Muswada wa marekebisho ya Sheria hii eneo hili liliibua mjadala mkali na wadau pamoja na Kamati walihofia kwamba kuondolewa kwa fao la kujitoa (*withdraw benefit*) kunaweza kuleta tatizo. Ili kuepusha hali ambayo ingeweza kutokea, Kamati ilitoa ushauri kwa mujibu wa taratibu zake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya kutokea kukinzana kwa matumizi ya Sheria hiyo na hali halisi ya mahitaji ya wafanyakazi, Kamati inaona upo umuhimu wa kupitiwa haraka na kufanyiwa marekebisho kwa Sheria hiyo kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

- Sheria irejeshe fao la kujitoa (*withdraw benefit*);

- Mwanachama aruhusiwe kutumia sehemu ya mafao yake ya uzeeni kulipia mkopo wa nyumba (*home mortgage*); na

- Mwanachama aruhusiwe kutumia sehemu ya mafao yake ya uzeeni kwa ajili ya kugharamia shughuli yoyote nyingine kwa lengo la kuandaa mazingira mazuri ya maisha baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuzingatia masuala hayo, Kamati inaiagiza Serikali kuhakikisha kuwa mara baada ya kupitiwa upya kwa sheria hiyo, inaandaa kanuni na miongozo itakayosaidia kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuifanya iwe endelevu huku ikichangia na kujali maendeleo ya wanachama na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali kupitia *SSRA* iandae mikakati ya kupanua wigo wa hifadhi ya jamii nchini ili makundi mbalimbali hasa ambayo yako kwenye sekta isiyo rasmi yaweze kufaidika na huduma zinazotolewa na Taasisi za Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inakubaliana na hatua ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008 kuruhusu waajiriwa wapya kuchagua Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao watapenda kujiunga nao tofauti na awali ambapo walilazimika kujiunga na Mfuko ulio kwenye sekta wanayoifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itaondoa ukiritimba katika utendaji wa Mifuko na hivyo kuifanya itekeleze majukumu yake kwa ushindani ili kuvutia wanachama. Kamati pia inazidi kuiagiza Serikali juu ya umuhimu wa kuandaa mazingira ya kuiweka Mifuko yote chini ya Wizara moja ili iwe rahisi kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Pensheni kwa Wazee. Wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote ile duniani na kwa Tanzania, wazee wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya Kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa wazee hapa nchini ambao wanakadiriwa kufikia

asilimia 5.7 ya Watanzania wote ndio wanaolea yatima milioni 2.1 (sawa na asilimia 53 ya yatima wote waliopo nchini) ambao wamepoteza wazazi kwa namna mbalimbali. Pengine ni kutokana na ukweli huu, ndiyo maana Wahenga wakaja na msemo kwamba, “utu uzima dawa”, wakimaanisha kwamba panapokuwa na mtu mzima, suluhu ya tatizo hupatikana.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa licha ya umuhimu huo, wazee wamesahaulika katika jamii na wakati mwingine wananyanyasika kutokana na madhila ya uzee. Mara kadhaa vimeripotiwa vitendo vya unyanyasaji na mauaji ya vikongwe kwa madai ya kujihusisha na imani za ushirikina, sababu kubwa ikiwa ni vikongwe hao kuwa na macho mekundu. Mfano, kwa mujibu wa Asasi Isiyo ya Kiserikali ambayo inajihusisha na masuala ya wazee ya *Concern for the Elderly (COEL*) zaidi ya vikongwe 2,800 waliuawa katika kipindi cha miaka mitano (2007 – 2011) iliyopita kutokana na imani za kishirikina.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na hali hii hasa pale ambapo jamii inashindwa kutambua kuwa ni hali ngumu ya kiuchumi ambayo inawanyima wazee uwezo wa kupata nishati bora ya kupikia, hivyo kujikuta wakihangaika na kuni zenye moshi na hivyo kuathiri macho yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kundi hili ndilo linalea sehemu kubwa ya yatima, hali ngumu ya uchumi inawafanya wazee kushindwa kuwapatia yatima hao elimu, huduma bora za afya na lishe na matokeo yake ni watoto hao kukimbilia mitaani na

wengine kuingia katika masuala ya familia mapema na hivyo kupata watoto katika umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, athari za watoto hao kuzaa katika umri mdogo tena wakiwa tegemezi ni kwamba, wanaongeza mzigo kwa wazee, vifo vya akinamama na watoto vinaongezeka na mwishowe kuongezeka kwa kiwango cha umaskini pamoja na maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na mantiki hiyo basi, Kamati imekuwa inaagiza Serikali kuangalia namna ya kuwawezesha wazee kiuchumi, kwani hatua hiyo itakuwa na manufaa kwa jamii. Wazee wakiwezeshwa kiuchumi ni wazi watawahudumia wajukuu (yatima) wanaowalea. Uzoefu unaonesha kwamba wazee wachache (asilimia 4.1) ambao wako katika mfumo rasmi wa pensheni wanaishi katika hali bora ikilinganishwa na wenzao ambao hawako katika mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, mfano, utafiti uliofanywa mwaka 2010 na iliyokuwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana (sasa Wizara ya Kazi na Ajira) ulionesha kwamba kipato cha Sh. 6,000 kwa wazee walio na umri wa zaidi ya miaka 60 kingewawezesha kupunguza kiwango cha umaskini wa mahitaji muhimu *(basic needs poverty rate)* kwa asilimia 32.7 (kutoka asilimia 33 hadi 22.2). Utaratibu huo ukitekelezwa utawawezesha wazee kuishi juu ya mstari wa kiwango cha chini cha umaskini wa mahitaji muhimu (*basic needs poverty line*).

Mheshimiwa Afrika Kusini, Kenya, Mauritania na kadhalika) unaonesha kuwa Wazee huridhika hata wakipatiwa kiwango kidogo cha fedha na huduma za tiba. Mafanikio mengine yanayotokana na pensheni kwa wazee ni pamoja na afya njema kwa wazee, kupungua kwa gharama za huduma za afya ambazo Serikali inazitoa kwa wazee, kuongezeka kwa mzunguko wa fedha vijijini na hivyo kuimarisha hali ya uchumi ambayo itaboresha huduma nyingine katika jamii kama vile elimu, afya na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali kwa ahadi ambayo kupitia Waziri wa Kazi na Ajira, iliahidi jana tarehe 6 Agosti, 2012, kwamba itaanza kutoa pensheni kwa wazee katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014. Kauli hiyo ya Serikali ilifuatia swali la nyongeza lililoulizwa na Mbunge wa Peramiho na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama ambaye aliitaka Serikali kutamka wazi kwamba, ni lini itaanza kuwalipa pensheni wazee ambao wanateseka kutokana na ugumu wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafanya utafiti wa kutosha juu ya suala hili ili litakapoanza kutekelezwa hapo mwakani liwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo itatoa matumaini kwa wazee ambao ni nguvu kazi ya zamani iliyolitumikia Taifa hili katika nyanja mbalimbali za uzalishaji mali na utoaji wa huduma na watatambua kwamba, Serikali inawajali na kuwathamini. Pia ni

vyema kuzingatia kuwa uzee siyo laana, bali ni baraka na kila mmoja wetu hapa ni mzee mtarajiwa.

Mheshimiwa Spika, pia ni muhimu kukumbuka kwamba, hifadhi ya jamii ni haki ya kila mtu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara).

Ibara ya 11(1) ya Katiba inaeleza kwamba: "Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kupata elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi..." Pia ibara ya 22 ya Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu *(UDHR)* la mwaka 1948 inataja kuwa ni haki kwa kila mtu kupata hifadhi ya kijamii kupitia utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ndiyo chombo cha hifadhi ya jamii kikongwe nchini. Mfuko huu ulianza kama Idara ya Serikali mwaka 1964 kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Akiba ya Wafanyakazi (*NPF*) kwa sheria Na. 36 ya mwaka 1975. *NPF* iliendelea hadi mwaka 1997, Serikali ilipopitisha Sheria Na. 28 iliyoanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ili kuwa na mfumo wa hifadhi ya jamii unaozingatia kanuni na viwango vya Kimataifa vya hifadhi ya jamii. Mfumo huo ndiyo umeiwezesha *NSSF* kutoa mafao mengi na bora zaidi yakiwemo mafao ya pensheni, kwani kabla ya hapo, yalikuwa yakitolewa

mafao ya uzeeni ambayo yalikuwa hafifu na yalitolewa kwa mkupuo.

Mheshimiwa Spika, licha ya mfumo wa hifadhi ya jamii kuwepo miongo kadhaa, bado ni sehemu ndogo sana ya nguvu kazi katika Taifa letu ndiyo inanufaika na huduma ya hifadhi ya jamii. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, ni asilimia 6.2 tu ya nguvu kazi ya Watanzania wanaokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 21, ndiyo inapata huduma ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, hii ni ishara kuwa bado ipo safari ndefu ya kuwaelimisha wale wote ambao wanapaswa kuwa wadau wa hifadhi ya jamii ambao ni watunga sera na sheria, waajiri, waajiriwa, wanachama na wananchi kwa ujumla. Kamati inaishauri Serikali kuangalia utaratibu ambao utafikisha elimu zaidi kuhusiana na mfumo wa hifadhi ya jamii nchini. Aidha, Mfuko husika *(NSSF)* uendelee kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na wananchi wengi walio katika sekta binafsi ili waweze kuelewa vizuri mfumo wa hifadhi ya jamii kwamba unawagusa na waweze kujiunga.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* inaigusa jamii moja kwa moja kutokana na uwekezaji wake kwenye sekta za elimu (Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa hosteli za Mabibo kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya makazi (Kigamboni na maeneo mengine), afya (kushiriki ujenzi wa hospitali ya Apolo), nishati na daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza *NSSF* kwa kuendeleza uwekezaji katika vitega uchumi ambavyo mbali na kulenga kuongeza kipato cha Mfuko, pia vinatoa huduma za kimsingi kwa jamii. Katika mwaka wa fedha uliomalizika Juni 20, 2012, Mfuko uliweza kukamilisha ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mkoa wa Njombe na Chuo cha Nelson Mandela, Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Spika, Mfuko pia ulifanikiwa kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa miwili ambayo ni mradi wa kuzalisha umeme wa Megawati 300 katika eneo la Mkuranga na ujenzi wa daraja la Kigamboni ambao umekuwa ukisubiriwa kwa hamu kubwa na Watanzania.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2012/2013, Mfuko unatarajia kukamilisha miradi ambayo haijakamilika, kuendelea na miradi iliyoanza ambayo itachukua muda mrefu kukamilika na kuanza utekelezaji wa miradi mingine ambayo ni pamoja na:-

(a) Uboreshaji wa huduma za wateja kwa kuhakikisha ofisi zote za Mfuko zinaunganishwa na mkongo wa mawasiliano wa Taifa (*fibre cable*);

(b) Kushiriki katika ujenzi wa Hospitali ya Apolo jijini Dar es Salaam;

(c) Ujenzi wa jengo la Mzizima, Jijini Dar es Salaam;

(d) Ujenzi wa hoteli ya kisasa Jijini Mwanza;

(e) Ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu *Farm*);

(f) Kuanza ujenzi wa jengo la Maadili Dar es Salaam endapo taratibu za mazungumzo zitakamilika; na

(g) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Hisabati (*College of Earth and Mathematics*) katika Chuo Kikuu cha Dodoma na nyumba za Polisi awamu ya tatu iwapo majadiliano na Serikali yatakamilika.

Mheshimiwa Spika, licha ya Mfuko huu kutimiza wajibu wake kikamilifu, Serikali ambayo imekuwa ikitoa dhamana ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, imekuwa ikichelewa kuanza kulipa gharama za miradi mara inapokamilika na kukabidhiwa. Kamati inaishauri Serikali kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati muafaka ili kuuwezesha Mfuko uendelee na shughuli za kiutendaji na pia kuwekeza katika vitega uchumi vingine ikiwemo miradi ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mafanikio makubwa, Mfuko huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa na kubwa, miongoni mwa hizo ni baadhi ya waajiri kutowasilisha au kuchelewa kuwasilisha michango ya wafanyakazi na pia kutozingatia viwango vya uchangiaji vinavyotakiwa.

Hali hii inasababishwa na baadhi ya waajiri ama kutoelewa vyema umuhimu wa mfumo wa hifadhi ya jamii au kufanya kwa makusudi. Kamati inashauri

Wizara kupitia *NSSF* isichoke kutoa elimu kwa waajiri, wanachama na umma kwa ujumla kuhusiana na hifadhi ya jamii pamoja na sheria na kanuni zinazosimamia uchangiaji katika uhifadhi wa jamii.

Aidha, Mfuko uwe na ukomo wa uvumilivu kwa waajiri ambao wamekuwa hawachangii wafanyakazi wao kwa kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria ili kukomesha tabia hiyo ambayo siyo kwamba inaathiri uendeshaji wa mfuko, bali pia inawanyima wafanyakazi haki ya kujiwekea akiba kwa ajili ya pensheni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mfuko kuangalia namna ya kuwekeza vitega uchumi katika maeneo ya nchi yetu ambayo yako nyuma kimaendeleo ili kupeleka chachu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mfuko uangalie namna ya kuboresha zaidi mafao ya wanachama wake kwa kutumia faida ambayo inatokana na vitega uchumi vinavyowekezwa na Mfuko huo kwani fedha zinazotumika kama mitaji zinatokana na michango ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya wafanyakazi; licha ya kuwepo sheria kadhaa zinazosimamia masuala ya kazi na ajira nchini kama vile Sheria Namba 6 na 7 zote za mwaka 2004, bado kumekuwepo na migogoro mingi ambayo imekuwa ikijitokeza katika maeneo ya kazi kama vile viwandani, katika makapuni na mashirika, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, migogoro hiyo imekuwa ikitokana na wafanyakazi kudai maslahi (mishahara na stahili nyingine) na mazingira bora ya kazi. Zipo pia sababu nyingine za migogoro ambazo ni kukiukwa kwa mikataba, ubaguzi katika sehemu za kazi, kunyimwa haki ya kuwa na Vyama vya Wafanyakazi na uelewa mdogo wa sheria za kazi miongoni mwa waajiri na waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia takwimu kuhusiana na migogoro inayopokelewa na kusajiliwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*), Kamati imebaini kuwa sekta inayochipukia ya usalama (ulinzi) binafsi inaongoza kwa kuwa na migogoro mingi sana. Mfano kati ya migogoro 3,069 ambayo ilisajiliwa katika kipindi cha kuanzia Oktoba, 2011 hadi Machi, 2012, sekta hii ilikuwa na jumla ya migogoro 652 ambayo ni sawa asilimia 21.2 ya migogoro yote. Kiwango hiki cha migogoro kinatisha hasa kwa kuzingatia kwamba, sekta hii ni ndogo ikilinganishwa na zile za viwanda, migodi, makampuni na nyingine ambazo zinaajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ingawa kwa maelezo ya *CMA* hali hii ya migogoro katika sekta hii ya ulinzi inatokana na wamiliki wengi wa makampuni ya ulinzi kuwa wastaafu wa Majeshi ya Polisi na Ulinzi, ambao wamekuwa wakitumia amri zaidi kuliko kufuata sheria na kanuni za kazi, bado Kamati inasisitiza kuwa linapokuja suala la sheria, ni wajibu wa kila mmoja kuziheshimu, kwani hakuna aliye juu ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* kwa kutambua kuwa njia kubwa ya kupunguza migogoro maeneo ya kazi ni pamoja na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusiana na namna ya kutatua migogoro ya kikazi na pia sheria za kazi. Tume hiyo imeandaa rasimu ya kitabu cha Mwongozo wa Kuzuia na Kutatua Migogoro ya Kazi (*Dispute Prevention and Resolution Training Guide*) na tayari imefanikiwa kuchapa nakala takribani 1000 kwa ajili ya kuzisambaza kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatarajia kwamba, iwapo mwongozo huo utatumiwa vyema, utakuwa nyenzo muhimu itakayosaidia kupunguza tatizo la uelewa mdogo kuhusu taratibu za kutatua migogoro katika maeneo ya kazi. Hata hivyo, kwa mtazamo wa Kamati, idadi hiyo ya nakala ni ndogo na Wizara ione namna ya kuiwezesha *CMA* kuandaa nakala nyingi zaidi na kuzisambaza kwa wadau wengi zaidi ili kuongeza wigo wa uelewa kuhusiana na namna ya kushughulikia migogoro katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi hizo, Kamati inaishauri Wizara kupitia *CMA* iendelee kusajili migogoro yote ya ajira iliyopo nchini (ya muda mrefu na muda mfupi) na kuishughulikia kikamilifu. Pia elimu iendelee kutolewa kwa waajiri kuhusu Sheria na Kanuni za Ajira na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hatua hii italeta hali ya utulivu na amani sehemu za kazi, kwani wafanyakazi na waajiri watatambua haki na wajibu wao na hivyo

uzalishaji utaongezeka, utoaji wa huduma utaboreshwa na kwa ujumla uchumi wa nchi yetu utakua.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na inaipongeza Serikali kwa kuunda Bodi 12 za mishahara ya kisekta kwa lengo la kufanya tathmini na uchambuzi na hatimaye kutoa mapendekezo ya kima cha chini kwa sekta binafsi. Ingawa Serikali imeahidi kufanya utafiti wa kima cha chini cha mshahara katika mwaka huu wa fedha, Kamati inahimiza zoezi hilo kufanyika kwa umakini mkubwa na ikiwezekana likamilike mapema ili kupata suluhu ya malalamiko ya mishahara midogo kwa wafanyakazi wa sekta binafsi na ile ya Umma.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa matokeo ya utafiti huo pia yatasaidia Serikali inapopandisha mishahara kuzingatia ongezeko la gharama za maisha kwa wananchi, kwani mara nyingi nyongeza inayotolewa imekuwa hailingani na hali halisi ya ongezeko la gharama za maisha, au hulingana na baada ya muda mfupi gharama za maisha hupanda kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na nia hiyo njema yenye lengo la kuwakomboa wafanyakazi wa sekta binafsi na ile ya umma kwa kuhakikisha kuwa wanalipwa kima cha chini cha mishahara chenye staha, Kamati imebaini kuwa wako baadhi ya wawekezaji binafsi ambao wana nia ya kulipa wafanyakazi wao kiwango cha juu zaidi kama kima cha chini ikilinganishwa na kiwango kinachotamkwa

na sheria (Sheria ya Taasisi za Kazi, Kif. 35 (1) ambacho kinatumika tangu mwaka 2010 baada ya kile kilichotangazwa mwaka 2007 na kuanza kutumika mwaka 2008 kukataliwa na wadau hasa waajiri. Wawekezaji hao wamekuwa wakishindwa kutimiza azma hiyo kwa sababu ya kuzingatia matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuruhusu uwepo wa viwango tofauti vya kima cha chini cha mshahara katika sekta moja baina ya wawekezaji binafsi wa ndani na wale wa kigeni na iwapo utaratibu huo utaonekana kuwa na tija, basi wawekezaji wa kigeni waagizwe kulipa viwango vya juu vya kima cha chini ikilinganishwa na vile vinavyolipwa na wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kupitia Bodi mpya za Mishahara 12 ambazo zilizinduliwa mwaka 2011, kuharakisha mchakato wa kumtafuta Mtaalam Mwelekezi (*Consulatant*) ambaye atafanya tathmini ya viwango vya kima cha chini cha mshahara Kitaifa ili kuzisaidia Bodi hizo kupendekeza viwango husika kwa kuzingatia uwezo wa kila sekta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuwapongeza Wataalam wa Afya kwa hatua ya kukubali kurejea kazini huku suala lao likiendelea kushughulikiwa na vyombo husika. Hatua hiyo inaonesha moyo wa kizalendo walio nao wataalam hao hasa kwa kuzingatia kuwa taaluma yao ni muhimu kwa Taifa.

Kamati pia inasikitishwa na utata uliojitokeza baina ya Walimu na Serikali wakati wataalam hao wakidai maslahi yao. Kutokana na Maamuzi ya Mahakama kwamba, mgomo ambao ulikuwa umeitishwa na Walimu haukufuata taratibu, Kamati inajiuliza maswali kadhaa yakiwemo:-

Je, hakukuwa na mawasiliano ya kutosha baina ya Serikali na Chama cha Walimu kuhusiana na mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea baina ya pande hizo juu ya madai ya Walimu?

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inawashukuru Walimu kupitia Chama chao (CWT) kwa kutii uamuzi wa Mahakama na kurejea kazini. Hata hivyo, inazitaka pande mbili hizo (Serikali na Walimu) kurejea haraka katika meza ya mazungumzo ili kuhakikisha kuwa suala la madai ya walimu linamalizwa kwa njia ya muafaka bila kuifikisha nchi katika mgomo ambao mwishowe wanaoathirika ni watoto wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Wafanyakazi vipo kwa mujibu wa Sheria za nchi na lengo kubwa ni kusaidia kuleta tija katika kazi. Historia inaonesha kuwa chimbuko la vyama hivi ni hatua ya wafanyakazi kuunganisha nguvu zao kwa lengo la kudai haki zao (malipo bora, mazingira mazuri ya kazi na kadhalika) wakati wa Mapinduzi ya Viwanda kwenye karne ya 18 hasa katika nchi za Ulaya Magharibi.

Mheshimiwa Spika, ingawa tangu wakati huo kumekuwa na mabadiliko yanayochagizwa na

maendeleo ya teknolojia na demokrasia, bado malengo ya vyama hivyo yamejikita katika kupinga vitendo vinavyomkandamiza mfanyakazi, kudai maslahi bora zaidi na mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro katika vyama vya wafanyakazi ambayo imetokana na hali ya kutoelewana ama baina ya Chama na Chama au Vyama, Chama na Wanachama wake, Chama na Waajiri au Viongozi ndani ya Chama. Hata hivyo, licha ya makundi hayo ya migogoro, kwa hali ilivyo sasa, migogoro ambayo inaonekana kushamiri ni baina ya Vyama na Waajiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na tabia ya baadhi ya waajiri ambao hawataki kutimiza wajibu wao kwa wafanyakazi na hivyo kuona njia pekee ya kukwepa usumbufu ni kupinga Vyama vya Wafanyakazi. Waajiri hao ama wamekuwa hawataki kuruhusu Vyama vya Wafanyakazi kuwepo maeneo ya kazi au wamekuwa wakiviruhusu lakini kwa shingo upande, jambo ambalo linaondoa ushirikiano na umoja baina ya wafanyakazi na waajiri na hivyo kuibua mivutano isiyo na msingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kukemea tabia hiyo ya baadhi ya waajiri na wale ambao watabainika kufanya hivyo wachukuliwe hatua za kisheria, kwani wakati mwingine wamekuwa wakisababisha migogoro ya kikazi isiyo ya lazima na wafanyakazi wao na hivyo kuathiri uzalishaji na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Vyama vya Wafanyakazi kuwa imara katika kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kuwaelimisha kutambua wajibu wao kwa mwajiri na haki za msingi ambazo wanastahili kuzipata kutoka kwa mwajiri kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Ajira.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa iwapo wafanyakazi watatambua wajibu na haki zao na wakazidai kwa mujibu wa sheria na Waajiri wakatimiza wajibu wao, kiwango cha migogoro katika maeneo ya kazi kitapungua na hivyo uzalishaji utakuwa wenye tija na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, usalama na afya mahali pa kazi vinapaswa kuzingatiwa kwa kiwango cha juu sana, kwani siyo kwamba vikipuuzwa vyaweza kuwa na madhara kwa mwajiri au mwajiriwa pekee, bali hata kwa uchumi wa Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa katika kipimo cha Kitaifa, makadirio ya gharama za ajali na magonjwa mahali pa kazi yanafikia asilimia nne (4%) ya pato la Taifa. Kwa mfano, mwaka 2011 pato ghafi la Taifa *(GDP)* lilikuwa ni Shilingi trilioni 37.5.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba asilimia nne (4%) ya pato hilo ambayo ni sawa Shilingi trilioni 1.5 zilitumika kugharamia ajali na magonjwa yaliyotokea mahali pa kazi. Fedha hizi ni nyingi sana, kwani hakuna hata Wizara moja ya Serikali ambayo bajeti yake inafikia kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, ingawa ni jukumu la wadau wa ajira (waajiri na wafanyakazi) kuhakikisha afya na usalama mahali pa kazi, bado Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inaweka viwango vya usalama na afya mahali pa kazi na kusimamia kikamilifu utekelezwaji wake ili kunusuru afya za wananchi wake na hivyo kulinda ukuaji wa uchumi wa Taifa. Ili kuhakikisha wajibu huu muhimu unatekelezwa, ndiyo maana Serikali kupitia Wizara, ikaunda Wakala wa Serikali wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi *(OSHA)* ambao ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Utendaji Na. 30 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa, ingawa *OSHA* imepewa majukumu makubwa ya kuhakikisha kuwa afya na usalama vinazingatiwa mahali pa kazi, bado Serikali kupitia Wizara haijaiwezesha kikamilifu kutekeleza majukumu hayo. Wakala hii inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhaba wa rasilimali watu, rasilimali fedha pamoja na vitendea kazi na vifaa vya ofsini.

Kwa mfano, katika upande wa vifaa vya Ukaguzi (vikagua umeme na vifaa vya elektroniki) *OSHA* ina upungufu wa wastani wa asilimia 80. Hali hii inaashiria kwamba *OSHA* haiwezi kutimiza majukumu yake kikamilifu na athari zake, ni kwamba usalama na afya ya wafanyakazi vinawekwa rehani.

Mheshimiwa Spika, aidha, ofisi za *OSHA* haziko katika hali nzuri, kwani majengo ya ofisi zake ni ya kizamani na hayakidhi mahitaji ya nafasi na ubora unaotakiwa. Ni ukweli usiopingika kwamba, hali kama

hii inawapa *OSHA* kigugumizi katika utendaji wao, kwani hawawezi kuwa na ujasiri wa kuwataka wadau wa ajira kuhakikisha afya na usalama katika maeneo ya kazi wakati wao hawatimizi jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, licha ya Wizara kuongeza bajeti ya matumizi ya kawaida kwa *OSHA* katika mwaka huu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kuijengea *OSHA* mazingira mazuri ya kiutendaji ili iweze kuonesha mfano kwanza kabla ya kuwaendea wadau wengine kwa lengo la kuwakagua na kuwataka wazingatie viwango vya usalama na usafi katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la *OSHA* kujengewa uwezo wa kiutendaji ni la muhimu sana hasa kwa kuzingatia kwamba, kadri dunia inavyokumbwa na mabadiliko ya kiuchumi, sayansi na kiteknolojia, ndivyo ambavyo wafanyakazi wanakuwa katika vihatarishi na hatari za mahali pa kazi kama vile kemikali, mnunurisho hatari, viumbe hatari (viumbe maradhi) hatari za mitambo, hatari za mazingira ambazo zinaweza kuharibu mwili na mifupa na hivyo kuathiri uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miongoni mwa changamoto ambazo *OSHA* inakutana nazo wakati wa ukaguzi ni pamoja na baadhi ya waajiri kutosajili sehemu zao za kazi, kutotoa taarifa za ajali zinazotokea maeneo ya kazi pamoja na kutopima afya za wafanyakazi wao. Kamati inaisisitizia Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za afya na usalama mahali pa kazi na kusimamia utekelezaji wake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na kuhakikisha wafanyakazi wa mazingira hatarishi wanapewa vifaa maalum vya kujikinga *(Personal Protection Equipments)* ambavyo ni *masks*, *gloves, safety boots na overalls*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa tarehe 28 Aprili ya kila mwaka ni siku ya usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi, Kamati inashauri siku hiyo itumike hapa nchini kuwazawadia waajiri ambao walifanya vizuri katika kujali na kuzingatia afya na usalama wa maeneo yao ya kazi na hivyo kuwaweka salama wafanyakazi wao. Pia siku hiyo itumike kuwahimiza waajiri juu ya umuhimu wa kupima afya za wafanyakazi wao mara kwa mara ili kujua wako katika hali gani ya afya.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la ajira, ni lazima kuboresha uchumi ambao utawezesha kutengenezwa kwa nafasi nyingi za ajira. Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na programu mbalimbali kwa lengo la kukuza uchumi ili hatimaye kupunguza umaskini. Hata hivyo, mafanikio yamekuwa ni kwa kiwango kidogo sana. Kwa mfano, kutokana na juhudi hizo, ukuaji wa uchumi uliongezeka kutoka asilimia 4.1 mwaka 1998 hadi asilimia 7.4 mwaka 2008 ingawa ulishuka tena hadi asilimia 6.0 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, ukuaji huo wa uchumi wa kiwango cha asilimia 3.3 kwa kipindi cha miaka 10 au (wastani wa asilimia 0.3 kwa mwaka) haujaweza kuchangia kikamilifu katika kuondoa umaskini nchini, kwani kiwango cha umaskini (*basic needs poverty line*)

kilifikia asilimia 33.6 mwaka 2008 kutoka asilimia 35.7 mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, hii inadhihirisha kuwa itakuwa ni vigumu kufikia malengo ya milenia ya kupunguza umaskini kwa nusu ifikapo 2015 kwani wakati kiwango cha umaskini kikipungua kwa asilimia ndogo ongezeko la ukosefu wa ajira ni kubwa na hivyo kufanya Taifa kuwa na sehemu kubwa ya nguvu kazi isiyo na ajira au iliyo katika ajira zisizokidhi kiwango.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa ajira linazidi kukua duniani ambapo Ripoti ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* ya mwaka 2011 inaonesha kuwa nguvu kazi inayofikia watu milioni 205 hawakuwa na kazi. Idadi hii ni sawa na ongezeko la watu milioni 27.6 katika kipindi cha miaka minne ikilinganishwa na nguvu kazi ya watu milioni 177.4 ambao hawakuwa na ajira mwaka 2007. Ripoti hiyo inaeleza kuwa vijana wasio na kazi duniani ( miaka 15 – 24) walifikia milioni 77.7 mwaka 2010 ikilinganishwa na milioni 73.5 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kulinganisha taarifa hiyo ya *ILO* na hali halisi hapa nchini utagundua kuwa hali ya ukosefu wa ajira ni mbaya, kwani wastani wa kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana wa kati ya miaka 15 - 24 ni asilimia 14.9 (Wanawake asilimia 15.4 na Wanaume asilimia 14.3). Kundi linalofuatia la umri wa kati ya miaka 25 - 34 nalo haliko salama, kwani linakabiliwa na ukosefu wa ajira kwa wastani wa asilimia 11.8 (wanawake asilimia 13.2 na wanaume asilimia 10.3).

Mheshimiwa Spika, ukichambua takwimu katika makundi hayo mawili ambayo yanabeba sehemu kubwa ya vijana ambao wamehitimu shule na vyuo na wapo katika kipindi cha mpito (*transition period*) utagundua kuwa kwa ujumla kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana walio katika umri wa miaka 15 – 33 ni asilimia 13.4, athari zikionekana zaidi maeneo ya mijini ambapo asilimia 26.7 na asilimia 7.9 iliyosalia ni kwa vijana wa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, hii siyo dalili nzuri, kwani kundi kubwa la Watanzania (asilimia 47) ni la walio chini ya umri wa miaka 15 na kila mwaka kuna sehemu ya kundi hilo inavuka na kuingia katika kundi la nguvu kazi katika soko la ajira. Kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa nguvu kazi (*ILFS* 2006) ilibainika kuwa watu wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka ni kati ya 800,000 hadi 1,000,000.

Mheshimiwa Spika, ingawa maendeleo ya sayansi na teknolojia ni jambo jema katika jamii yoyote duniani, lakini yamekuwa yakichangia ukosefu wa ajira. Kwa mfano, katika siku za karibuni watu wengi wamepoteza ajira na wengine kukosa kuajiriwa kwa sababu utandawazi, maendeleo ya mawasiliano na mabadiliko ya teknolojia vimekuwa havihitaji nguvu kazi nyingi katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali inapaswa kuzingatia kwamba, wakati nafasi za kazi zikipungua au kuongezeka kwa kasi ndogo, idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa, makundi ya watu wanaohitaji ajira yameongezeka husus an wanawake

kutokana na kubadilika kwa majukumu, vijana wadogo ambao wanalazimika kuanza kujitegemea mapema na hata wazee ambao wamestaafu, lakini kutokana na ugumu wa maisha wanaendelea kushikilia nafasi za kazi kwa mikataba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni dhahiri kwamba sekta ya kilimo ndiyo inaajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi (74.6%) ya nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuboresha sekta hii na kuifanya ichangie katika kukuza uchumi na kuendelea kutoa ajira kwa nguvu kazi iliyopo, kwani hata nchi zilizoendelea kiviwanda, zilianza na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo kikiimarika, kitazalisha ziada, kitatoa msukumo wa kuanzishwa viwanda vya kusindika na kuyaongezea thamani mazao ambavyo siyo kwamba itaongeza kipato kitakachotokana na mauzo ya mazao hayo, bali pia vitatoa nafasi za ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa ni vigumu kufikiri kwamba, kama Taifa tutaweza kupiga hatua katika kukuza uchumi na kuondoa tatizo la ajira kwa kutegemea sekta nyingine pasipo kujipanga kikamilifu katika kilimo, kwani ni wastani wa asilimia 15 tu ya Watanzania ndiyo wako katika ajira rasmi zinazojulikana kama *white colour jobs.*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba kabla hofu inayoukumba ulimwengu kwamba ukosefu wa ajira kwa vijana ni bomu linalosubiri kulipuka (*timed bomb*) haijashika kasi hapa nchini na

kufikia kiwango cha kushindwa kuhimilika. Ni vyema tatizo la ajira kwa vijana likapewa kipaumbele katika kulishughulikia kwa kutumia kila mwanya unaoonesha dalili ya kutengeneza nafasi za kazi kuanzia katika ngazi za Kijiji hadi Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za wageni; utaratibu wa kutoa vibali na hatimaye kuwa na wafanyakazi wa kigeni katika nchi ni jambo la kawaida kabisa duniani na ndiyo maana leo kuna Watanzania wanafanya kazi katika Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kadri siku zinavyokwenda kunaibuka chuki kuwa huenda utaratibu huu unakiukwa au una kasoro kiasi cha kuruhusu wageni kuchukua nafasi za ajira hasa katika sekta isiyo rasmi ambazo zingefanywa na wazawa. Kwa mfano, leo hii siyo jambo la ajabu kukuta nafasi za juu na hata zile za kawaida katika sekta za hoteli, viwanda, ujenzi na maeneo mengine zikiwa zimeshikiliwa na wageni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ilivyo katika sehemu hizo za kazi, Kamati inajiuliza maswali kadhaa ikiwa ni pamoja na:-

(a) Hivi ni kweli kwamba licha ya kuwa na vyuo vinavyotoa wahitimu kila mwaka katika fani mbalimbali kama nchi hatujaweza kupata wataalam wanaoweza kumudu kushika nafasi za juu katika uwekezaji unaofanywa na wageni?

(b) Je, hatua ya wageni kushika nafasi za juu katika uwekezaji wanaoufanya, siyo mbinu wanayoitumia kuibia nchi raslimali zake na kuinyima mapato halisi ambayo ilistahili kuyapata?

(c) Je, hatua kama hiyo haihatarishi usalama wa Taifa? Kwani, hakuna anayejua kinachofanyika katika menejementi za wawekezaji hao.

(d) Je, mpango wa wageni wanaokuja nchini kwa kazi za kitaalam kuwarithisha wazawa ujuzi wao (*succession plan*) ili wanapoondoka nchi ibakie na ujuzi huo unafuatwa?

(e) Je, sheria inayoruhusu utoaji wa vibali kwa wageni kufanya kazi nchini inasema nini juu ya kazi ambazo wanapaswa kuzifanya na zile ambazo hawapaswi kuzifanya?

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ikitarajia kupata ufafanuzi kutoka kwa Wizara, ni vyema kama Taifa tukafumbua macho, tukaangalia na kutafakari tunakokwenda ni wapi. Iwapo hatutafanya hivyo, tena kwa haraka, hasa tukizingatia kuwa utandawazi unazidi kutumeza kutokana na maendeleo ya sekta ya mawasiliano, Soko la Pamoja la Afrika Mashariki linatukabili huku kila nchi mwanachama akiitazama Tanzania, basi tutakuja kujikuta tunapoteza utambulisho wetu kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina rasilimali nyingi na kutokana na ukweli huo tumejikuta tukitazamwa na Mataifa mengi duniani ambayo yanaona mianya

mingi ya kuweza kuitumia kupata raslimali zetu kwa kigezo cha uwekezaji. Kamati haipingi uwekezaji, kwani hakuna nchi inayoendelea bila kuwa na uwekezaji, bali inatoa rai kuwa tuwe na uwekezaji katika sekta zinazohitaji mitaji mikubwa na teknolojia, lakini siyo kuwa na wawekezaji hata kwenye biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa matarajio yetu kwa uwekezaji unaofanywa na wageni ni kwamba vijana wetu wapate ajira. Hata hivyo, tukiruhusu wageni wafanye kila kazi, basi mantiki ya uwekezaji haitakuwa na maana na tutaendelea kukabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inahisi kuwa huenda tunashuhudia ulegevu wa vibali vya wageni kuingia nchini na kufanya kazi hata ambazo tunadhani zingefanywa na wazawa kutokana na vibali vya ajira (*work permit*) kutolewa na mamlaka zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, taratibu za vibali kwa wageni nchini zinasimamiwa na sheria zifuatazo: Sheria ya Huduma ya Ajira Na. 9 ya mwaka 1999 (*National Employment Promotion Services Act*), Sheria ya Uhamiaji Na. 6 ya mwaka 1995 (*Immigration Act*), Sheria ya Uwekezaji Na. 26 ya mwaka 1997 (*The Tanzania Investment Act*); Sheria ya Maeneo Huru ya Biashara Na. 2 ya mwaka 2006 (*Special Economic Zones Act*) na Waraka wa Utumishi Na. 1 wa mwaka 2000 (*Civil Service Circular*).

Mheshimiwa Spika, ili kupata kibali, mwombaji analazimika kusubiri Wizara ya Kazi na Ajira, Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Idara ya Uhamiaji, sehemu hizo zote zifanye mawasiliano na kukubaliana kwamba watoe kibali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa utaratibu huu siyo sahihi na unapaswa kuangaliwa haraka kama Serikali ina nia ya kuondoa manung'uniko yanayojitokeza kila siku kuhusiana na ajira za wageni.

Uzoefu unaonesha kuwa, utaratibu uliofanikiwa kuhusiana na utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni ni ule wa kuwa na chombo kimoja ambacho kitakuwa na dhamana ya kushughulikia utoaji wa vibali vya ajira na kutoa hati maalum ya ajira (kibali). Kwa sasa Tanzania haina hati maalum ya ajira (*work permit*) ambayo inajitegemea, badala yake kibali hiki kimeunganishwa katika hati ya ukaazi (*residence permit*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia upya suala hili la utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni na ikiwezekana iandae utaratibu wa kuwa na mamlaka moja ambayo itashughulikia suala hilo, la sivyo tutaendelea kushuhudia wageni wakifanya kila kazi huku wananchi wakinung'unika kwamba wageni wanawanyang'anya hata zile kazi ambazo wanaziona ni stahiki yao tu.

Mheshimiwa Spika, hali hii ikiachwa iendelee inaweza kuwafanya wananchi wajenge hali ya uoga

na chuki dhidi ya wageni (*Xenophobia*) kwa tafsiri kwamba wageni ndiyo wanawasababishia ugumu wa maisha, kwani wamechukua kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni mbalimbali yaliyotolewa na Kamati katika vipengele kadhaa vya taarifa hii, Kamati ingependa kutoa maoni na ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

(1) Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na mamlaka moja ambayo itasimamia utoaji wa vibali vya wageni wanaokuja kufanya kazi nchini ili kuondoa mkanganyiko uliopo hivi sasa;

(2) Tatizo la utumikishwaji wa watoto katika migodi, bandari, mashamba makubwa, uvuvi na maeneo mengine bado linashamiri. Kamati inashauri Serikali iangalie namna ya kukomesha ajira hizo haramu na iandae utaratibu wa kuwasaidia watoto hao;

(3) Serikali kwa kushirikiana na Bodi za Mishahara za Kisekta iharakishe kumpata mtaalam elekezi atakayetathmini viwango vya kima cha chini cha mshahara ili kuziwezesha Bodi za Kisekta kupendekeza viwango vya kima cha chini kulingana na uwezo wa sekta husika;

(4) Serikali iiwezeshe Wizara kununua jengo la ofisi ambalo inalitumia kwa sasa, kwani mmiliki wa jengo hilo (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii -*NSSF*) uko tayari kuiuzia Wizara jengo hilo. Kinachotakiwa ni Serikali kutoa

dhamana. Hii itaisaidia Wizara kuepukana na kodi kubwa ya pango ambayo inalipa kwa sasa;

(5) Wizara iharakishe kukamilisha program ya Kitaifa ya kukuza ajira kwa vijana ili kuliwezesha Taifa kupambana na tatizo la ajira kwa vijana;

(6) Serikali ichukue hatua za Kisera na Kisheria ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kuwa na fursa sawa ya kupata kama ilivyo kwa watu wasio na ulemavu;

(7) Serikali itumie sensa ya watu na makazi itakayofanyika wiki chache zijazo kupata takwimu sahihi za watu wenye sifa za kuajiriwa na wenye kutafuta kazi na iwaunganishe na nafasi za kazi zilizopo. Sensa hiyo pia itumike kutambua idadi ya wazee ambao wanastahili kulipwa pensheni;

(8) Serikali iratibu shughuli za ujasiriamali na iwajengee vijana na wanawake uwezo wa kujiajiri;

(9) Serikali kupitia idara husika ikague vibali vya raia wa kigeni wanaofanya kazi nchini na wale ambao watabainika kutokuwa na vibali halali wachukuliwe hatua za kisheria;

(10) Serikali iwachukulie hatua waajiri ambao wamekuwa wakinyanyasa wafanyakazi wanaodai haki za kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi. Hili limekuwa tatizo kubwa na wafanyakazi wananyanyaswa na wengine kuachishwa kazi;

(11) Serikali iimulike Sekta ya Usalama (ulinzi) binafsi, kwani inaongoza kwa kuwa na migogoro mingi ya kikazi. Sekta hiyo ina asilimia 21 ya migogoro yote iliyosajiliwa katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi; na

(12) Kutokana na ongezeko la migogoro katika sehemu za kazi nchini, ni vyema bajeti ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* ambayo ina jukumu la kupatanisha waajiri na wafanyakazi ikaongezwa ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Niwapongeze pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo wanakusaidia kutekeleza majukumu yako. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Kazi na Ajira Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Militon Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Erick Francis Shitindi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake. Ninawatakia mafanikio zaidi katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa

ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati, pia kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mwenyekiti; Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kapt. John Damian Komba Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mjumbe; Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mjumbe; Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mjumbe; Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mjumbe; Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mjumbe; Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mjumbe na Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mjumbe; Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Nshunju Mshama, Mjumbe; Mheshimiwa Asha Mohamed Omar, Mjumbe; Mheshimiwa Ramadhan Haji Salehe, Mjumbe; Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mjumbe; Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mjumbe; Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mjumbe; Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mjumbe; Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo na Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah akisaidiwa na Makatibu wa Kamati, Ndugu Hosiana John na Ndugu Chacha Nyakega, kwa ushauri wa kitaalam kwa Kamati na pia kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Kazi na Ajira na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya ahsante, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hiyo.Spika, uzoefu wa nchi ambazo zinatoa pensheni kwa wazee barani Afrika (Uganda, Botswana,

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA KAZI NA AJIRA):** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kuniongoza vema katika kipindi chote cha utumishi wangu; tangu aliponifanya kuwa Diwani wa Watu wa Karatu miaka saba iliyopita na hata sasa ninapopigania maslahi ya Watanzania wote kwa nafasi yangu ya Ubunge, yeye muweza wa yote, ndiye amekuwa dira na ngome yangu kuu katika uongozi.

Mheshimiwa Spika, nitumie wasaa huu kutoa pole na salamu zangu za rambirambi kwa familia zote za Watanzania waliopoteza ndugu na jamaa zao katika ajali ya meli ya *MV. Skagit* iliyotokea hivi karibuni; Aidha, nampa pole na kumtakia moyo wa uvumilivu Mheshimiwa Joseph Selasini Mbunge wa Rombo katika

kipindi hiki kigumu anapoomboleza kifo cha baba yake mzazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa pole kwa kifo cha aliyekuwa mtumishi wa Bunge Marehemu Peter Mazengo pamoja na kutoa pole kwa Wabunge mbalimbali waliopatwa na misiba katika kipindi hiki. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote hao, mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa kipindi kifupi cha uwepo wangu hapa Bungeni kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira, Viongozi wote wa CHADEMA katika nafasi zao, wananchi wote wa Jimbo la Karatu na Mkoa wa Arusha kwa ujumla kwa kuniamini na kunifikisha hapa.

Mheshimiwa Spika, wote kwa ujumla nawaahidi kuwa nitakuwa mtumishi wa watu kwa maslahi ya watu na maendeleo ya watu. Aidha, nichukue fursa hii pia kutambua uwepo wa Viongozi na Wajumbe wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA, Wilaya ya Karatu, waliofunga safari kuja kuniunga mkono leo ndani ya Bunge hili, nawakaribisha sana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Wazazi wangu, Mama na Baba yangu Mzee Paresso kwa Malezi mema waliyonipatia hata kufikia hatua ya kuaminiwa kuwa kiongozi wa watu. Pia namshukuru mume wangu, Bwana Steven Mmbogo, kwa kuwa na

mimi bega kwa bega katika harakati zangu za kisiasa na kiuongozi, namshukuru sana!

Mheshimiwa Spika, leo nawasilisha maoni ya Upinzani, huku nafsi na akili yangu vikiwa vimegubikwa na hisia na kumbukumbu za majonzi; nikimkumbuka Mbunge mwenzetu, mpendwa wetu Mheshimiwa, marehemu Regia Estelatus Mtema aliyekuwa Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira na aliyetimiza wajibu kama huu mwaka jana kabla ya mauti kumfika; Mungu ampumzishe kwa amani Dada Regia na aniwezeshe kuitekeleza vema azma yake ya kupigania haki na maslahi ya Watanzania kwa uadilifu, ujasiri na umakini mkubwa hadi hapo muda wangu utakapofika! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la mwaka 2007) kifungu cha 99 (7), nachukua fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa Taifa maskini kama Tanzania, kazi na ajira vinapaswa kuwa ndiyo kipaumbele cha msingi kuliko vyote katika kuchochea maendeleo ya nchi. Aliyekuwa Rais wa 26 wa Marekani, Theodore Roosevelt (1858-1919) aliwahi kusema: *"It is only through labour and painful effort, by grim energy and resolute courage that we move on to better things"* tafsiri yake ni kwamba: "Ni kwa kupitia kazi na juhudi chungu, kwa nguvu yenye maumivu na

ushujaa wa kijasiri, ndivyo vinavyopelekea sisi kupiga hatua kuelekea kwenye maendeleo".

Mheshimiwa Spika, Serikali makini duniani huweka sera na mifumo thabiti ya kuhakikisha kuwa ajira za kutosha zinatengenezwa, mazingira ya kazi yanaboreshwa na wafanyakazi wanalipwa ujira na mishahara yenye staha, si tu kwa ajili ya kuwawezesha kumudu gharama za maisha, bali pia kuwapa morali wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo Taifa lolote duniani ambalo vijana wake wengi hawana ajira na wale walio vyuoni wanashindwa kusoma kwa sababu ya Serikali kushindwa au kupuuza kugharamia masomo yao; Taifa ambalo limejaliwa rasilimali nyingi za utalii na madini ya thamani, lenye vyanzo vingi vya kodi na mapato, lakini limegubikwa na migogoro mingi ya mara kwa mara na isiyokwisha ya wafanyakazi wanaodai haki na mafao yao halali, huku wakiishia kunyamazishwa kwa kauli za kibabe na nguvu za dola. Kwa namna yoyote ile Taifa hilo, ni kielelezo cha nchi inayoongozwa na Serikali isiyo na vipaumbele, yenye viongozi wenye ubinafsi wasiojali na wanaotekeleza sera zilizoshindwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya wafanyakazi; katika kitabu chake cha Uongozi Wetu na Hatma ya Tanzania, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema: "Uhalali wa Serikali yoyote ya kidemokrasia kuendelea kukaa madarakani na kuendelea kuongoza hautokani tu na

Katiba na Sheria iliyoiweka Serikali hiyo madarakani, bali ridhaa ya wananchi kuendelea kutawaliwa au kuongozwa inatokana na matendo mema ya Serikali kwa raia wake”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hii ya Baba wa Taifa, hebu Bunge hili lijiulize, yako wapi matendo mema ya Serikali yetu kwa Wafanyakazi wa Kitanzania, ikiwa kwa miaka mingi, tangu mwaka 2007 na kabla ya hapo, Walimu wamekuwa wakigoma kudai stahili na mafao yao, lakini mpaka leo hii wengi wao hawajalipwa? Yako wapi matendo mema ya Serikali hii ikiwa Wazee wengi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa miaka 35, tangu mwaka 1977 hadi leo 2012 bado wanateseka wakidai mafao yao, ilhali wenzao wa nchi nyingine walishalipwa?

Mheshimiwa Spika, yako wapi matendo mema ya Serikali hii kwa wafanyakazi wa migodini ikiwa hadi leo hii wanalipwa malipo duni kwa kazi ngumu ya kuchimbia madini ya wawekezaji wa kigeni, licha ya kuwa nchi yao Tanzania iko katika nafasi za juu kwa uzalishaji wa dhahabu na *Tanzanite* duniani?

Mheshimiwa Spika, yako wapi matendo mema ya Serikali hii, ikiwa wafanyakazi wanapunjwa huku sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na kodi na nguvu za wafanyakazi yanatumika kuneemesha viongozi wa juu wa Kiserikali na kisiasa, kwa kuwalipa mishahara mikubwa, posho na marupurupu mengi, huku wazalishaji wenyewe hususani wakulima na wafanyakazi wakizibwa midomo kwa kauli za kibabe na nguvu za dola? Iko wapi haki na huruma ya Serikali

hii kwa wananchi? Iko wapi ile CCM ya wakulima na wafanyakazi? Serikali hii inawezaje kujivunia uhalali wa kuwaongoza Watanzania hawa wanaoteseka hivi?

Mheshimiwa Spika, tunachukua fursa hii kwa mara nyingine tena kuliarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla, kwamba sababu kuu, lakini isiyo ya msingi, inayosababisha Serikali isiwalipe wafanyakazi mishahara na mafao yanayostahili kwa wakati, kama Madaktari, Walimu, wafanyakazi wa *TAZARA*, Polisi, Wanajeshi wa ngazi za chini, Wazee waliokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na wafanyakazi wa mashirika mengine, si kwamba madai yao hayalipiki au hakuna pesa, bali tatizo ni nchi kuongozwa bila kufuata vipaumbele vya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wakubwa wakisema madai ya walimu hayalipiki kwa sababu Serikali haina pesa; Kambi Rasmi ya Upinzani tuliionesha Serikali vyanzo vingi mbadala vya mapato na kuitaka ipanue wigo wa ukusanyaji kodi, lakini hatukusikilizwa. Tuliishauri Serikali izibe mianya ya ufisadi na ipunguze misamaha ya kodi ili kuokoa pesa nyingi zinazobaki kwa Wawekezaji wa Makampuni makubwa, lakini tulipuuzwa.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza Serikali ifute posho zote za vikao *sitting allowance* ili kuokoa matumizi makubwa ya fedha yasiyo ya lazima yanayofanywa kwenye taasisi nyingi za umma likiwemo Bunge, lakini tulibezwa. Tuliitaka Serikali kwa kutumia Madaraka ya Kikatiba aliyonayo Rais Kikwete,

ipunguze Baraza kubwa la Mawaziri, ili kuokoa fedha za wananchi na kuwa na Serikali ndogo inayofanya kazi kwa ufanisi, lakini hakuna kilichotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake nchi yetu imekuwa kama vile imesimama, wafanyakazi hawalipwi inavyostahili na Taifa haliendelei.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaiasa Serikali kuwa jitihada zake za kuzima migomo na migogoro ya wafanyakazi Mahakamani, athari yake itakuwa ni kubwa na mbaya sana kwa uhai wa Watanzania na maendeleo ya Taifa hili. Hakuna Mtanzania atakayekuwa na uhakika wa kupona ikiwa tutaendelea kutibiwa na Madaktari hawa wanaolazimishwa kufanya kazi kwa mishahara duni na wala raia wa nchi hii hawatakuwa na uhakika wa usalama wao na mali zao, ikiwa Askari Polisi wanalazimishwa kufanya kazi kwa malipo na maisha ya kudhalilisha. Nchi hii huenda kabisa ikakosa viongozi na wataalam wa fani mbalimbali ikiwa Serikali itaendelea kujiona shujaa kwa kuzima madai ya Walimu Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Aya ya 81 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 – 2015 iliahidi kwamba ili kuimarisha na kuendeleza hifadhi ya jamii CCM itazielekeza Serikali zake "… kufanya tathimini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kurekebisha viwango vya mafao vinavyotoa ili visipishane mno; kuanzisha na kuimarisha Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii na kuchukua hatua za makusudi za kupanua wigo wa

kinga ya Hifadhi ya Jamii, ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na huduma za Mifuko ya Jamii."

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa mujibu wa Ilani hiyo, Serikali za CCM zitapaswa kuelimisha jamii ya wafanyakazi na waajiri juu ya umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa maendeleo ya wafanyakazi na ya nchi kwa ujumla na kuendelea kutumia uwezo wa kifedha uliopo katika kila Shirika la Hifadhi ya Jamii, kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya kwanza iliyotajwa katika Ilani ya CCM, yaani kurekebisha viwango vya mafao ili visipishane mno haijatekelezwa hadi sasa kwani viwango vya mafao vinavyotolewa na Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii ni vile vile vya kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2010.

Mheshimiwa Spika, aidha, hakukuwa na sababu yoyote ya msingi ya kuingiza ahadi ya pili katika Ilani hiyo kwani Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* imekuwepo kisheria tangu mwaka 2008 wakati Bunge lako Tukufu lilipotunga Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utekelezaji wa ahadi ya tatu ya CCM kwa Watanzania, Taarifa ya Waziri wa Kazi na Ajira iliyotolewa kwa Kamati ya Huduma za Jamii mwezi Juni, 2012 inaeleza kuwa, asilimia sita tu ya nguvukazi ya Tanzania ndio wanaopata huduma za Hifadhi ya Jamii. Kwa maana

hiyo, ahadi ya kupanua wigo wa kinga ya hifadhi ya jamii ili Watanzania wengi zaidi wafaidike na huduma hiyo nayo haijatekelezwa!

Mheshimiwa Spika, ahadi ya nne kwenye Ilani ya CCM kuhusiana na hifadhi ya jamii nayo haijatekelezwa kwani, kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri kwa Kamati ya Huduma za Jamii, takwimu za Watanzania wanaopata huduma ya hifadhi ya jamii zinadhihirisha kuwa bado kuna uelewa mdogo wa masuala ya hifadhi ya jamii kwa watunga sera, waajiri, waajiriwa, wanachama na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama watunga sera, yaani Wizara na Serikali yenyewe, bado wana uelewa mdogo wa masuala ya hifadhi ya jamii kama anavyokiri Waziri katika Taarifa yake maana yake ni kwamba, Watanzania wasitegemee kwamba Serikali hii ya CCM ina uwezo wa kutekeleza ahadi zake za uchaguzi kuhusu kupanua wigo wa wapata huduma za hifadhi ya jamii!

Mheshimiwa Spika, ahadi pekee kuhusu hifadhi ya jamii iliyotekelezwa na Serikali ya CCM ni kuendelea kutumia fedha za wafanyakazi zilizomo katika Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika miradi ambayo haina manufaa yoyote kwa wafanyakazi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu, Serikali imechota mabilioni ya fedha za Mifuko hiyo na kuziingiza katika miradi ambayo haina manufaa yoyote kwa Mifuko yenyewe na hasa kwa wafanyakazi

ambao ndio wenye fedha hizo. Ushahidi wa jambo hili, unapatikana katika Taarifa Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zingine kwa mwaka 2010/2011 iliyowasilishwa kwa Rais Kikwete tarehe 28 Machi, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo, kuna udhaifu mkubwa katika vitega uchumi vinavyosimamiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa mfano, ukaguzi wa vitega uchumi vya *NSSF* ulionesha kwamba licha ya Mfuko huo kuwekeza shilingi bilioni 234.054 za wafanyakazi katika ujenzi wa awamu ya pili ya Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*, Mfuko ulikuwa haujasaini mkataba na Serikali juu ya fedha za mradi huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa mujibu wa taarifa hiyo, licha ya *NSSF* kusaini mkataba na Serikali ili kuwekeza shilingi bilioni 35.218 kwa ajili ya ujenzi wa Awamu ya Kwanza wa Chuo hicho na licha ya majengo yaliyojengwa katika awamu hiyo kuanza kutumika tangu Septemba 2008, Mfuko haujapokea fedha ya pango au malipo ya mkopo kutoka Serikalini ambao tayari umelimbikiza riba ya shilingi bilioni 14.157.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anaituhumu Serikali hii ya CCM kwa kukiuka masharti ya mkataba kwa kugeuza riba ya mkopo wa *NSSF* kuwa sehemu ya mtaji wakati *NSSF* ilitakiwa kupokea kodi ya pango ambayo ni gharama ya uwekezaji na riba ya asilimia 15 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, sio fedha za *NSSF* tu ambazo zimetumiwa na Serikali hii ya CCM kwenye *UDOM*. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaonesha kwamba Mifuko mingine nayo imepoteza mabilioni ya fedha za wafanyakazi kwenye ujenzi wa Chuo hicho. Hivyo, kwa mfano, *PPF* imekwishazamisha jumla ya shilingi bilioni 39.987; *PSPF* imechakachuliwa shilingi bilioni 105.921; *LAPF* imepoteza shilingi bilioni 22.030; wakati ambapo *NHIF* imekwishaunguza shilingi bilioni 13.403 za wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha za wafanyakazi wanachama wa Mifuko hii mitano ambazo zimeunguzwa katika ujenzi wa *UDOM* ni shilingi bilioni 450.615. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali, vitega uchumi vyote hivi katika *UDOM* vilikuwa *non-perfoming*, ikimaanisha kwamba havirudishi fedha za mikopo ya Mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, *UDOM* sio *White Elephant* pekee anayeteketeza fedha za wafanyakazi. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, *NSSF* ilikubali kutoa mkopo wa shilingi bilioni 5.33 kwa riba ya asilimia 15 kwa mwaka kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Idara ya Usalama wa Taifa. Mkopo huo na riba yake ulitakiwa kulipwa kwa njia ya kodi ya pango katika kipindi cha miaka kumi kuanzia 2007.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taasisi husika ya Serikali bado haijaanza kulipa mkopo huo na hakuna malipo yoyote yaliyofanywa hadi sasa. Vile vile, riba inayotokana na mkopo huo nayo bado haijalipwa.

Taasisi husika ya Serikali ilitakiwa ianze kufanya malipo tangu tarehe 31 Desemba, 2010. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Jengo hilo la Usalama wa Taifa pia lilikwishatafuna shilingi bilioni 6.5 za *PSPF*.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ukumbi huu wa Bunge lako Tukufu pia umefanywa na mikopo inayotokana na fedha za makato ya wafanyakazi ambazo pia hazijalipwa hadi sasa. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2011, *NSSF* ilikuwa haijalipwa shilingi bilioni 8.96 na *PPF* ilikuwa inadai malipo ya shilingi bilioni 7.9 zilizotumika katika ujenzi wa Ukumbi huu wa Bunge. Aidha, hadi tarehe 30 Juni, 2011, *LAPF* ilikuwa imechangia shilingi bilioni 2.91 kwa ajili ya ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaonesha fedha nyingine nyingi za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zimetumika katika miradi ya ujenzi yenye manufaa yenye mashaka kwa wafanyakazi na kwa Mifuko yenyewe. Hivyo, kwa mfano, mwaka 2007 *NSSF* ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 20 wenye riba ya asilimia 15 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, mkopo huo na riba yake ulitakiwa ulipwe katika kipindi cha miaka kumi baada ya mwaka mmoja wa huruma. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu: “Mfuko haujaanza kukusanya kodi ya nyumba hizo kwani Mkataba wa

Upangaji bado haujasainiwa licha ya kwamba nyumba zenyewe zimekuwa zinakaliwa."

Mheshimiwa Spika, mabilioni mengine ya wafanyakazi yameteketezwa katika ujenzi wa *Machinga Complex* ambayo ni mali ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, mwaka 2007 *NSSF* ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 12.9 kwa riba ya asilimia 14.9 kwa mwaka kwa ajili ya ujenzi wa Machinga *Complex* Jijini Dar es Salaam: "Mkopo haujaanza kulipwa bado na hakuna malipo yoyote yaliyofanywa". Hadi tarehe 30 Juni, 2011, mkopo huo ulikuwa umefikia shilingi bilioni 15.4."

Mheshimiwa Spika, mikopo mingine ambayo Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaitaja kama *not performing* ni pamoja na *Continental Venture Tanzania Limited.* inayodaiwa dola za Marekani milioni 3.5; *Meditech Industrial Company Limited.* (dola za Marekani milioni 1.45); *General Tyre* yenye kudaiwa dola za Marekani milioni 18.8 na Dar es Salaam *Cement Company Limited* inayodaiwa dola za Marekani milioni 4.7.

Mheshimiwa Spika, wadaiwa wengine wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni pamoja na Kagera *Sugar* yenye kudaiwa shilingi bilioni 12, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(HESLB)* shilingi bilioni 78.6 na Kiwira *Power Limited* shilingi bilioni 13.5.

Mheshimiwa Spika, Hukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu juu ya uendeshaji, udhibiti na usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika nchi yetu

inajieleza yenyewe: “Kushindwa kwa makampuni haya (baadhi yao yakiwa yamedhaminiwa na Serikali) kuheshimu majukumu yao ya mikopo kunatia shaka kama uchambuzi madhubuti ulifanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii juu ya uwezo wa wakopaji kulipa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, ukubwa wa biashara inayofanywa baina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na taasisi za Serikali na malipo yasiyokuwa na uhakika ya mikopo hiyo yanatia shaka juu ya uendelevu wa Mifuko husika katika siku chache zijazo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Waziri kwa Kamati ya Huduma za Jamii inaeleza kwamba *NSSF* imeanza kutekeleza mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 300 katika eneo la Mkuranga. Zaidi ya hayo, Taarifa ya Waziri inasema kwamba: “*NSSF* imeanza ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambapo mkandarasi amepatikana na kukabidhiwa eneo la kazi na yuko katika hatua ya ukusanyaji vifaa kwa ajili ya kuanza ujenzi”.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013, *NSSF* itaendelea na ujenzi wa Daraja la Kigamboni na mradi wa uzalishaji umeme wa Mkuranga. Vile vile, *NSSF* itawekeza katika ujenzi wa nyumba za Jeshi la Wananchi *(TPDF)*, kushiriki ujenzi wa Hospitali ya Apollo Jijini Dar es Salaam, ujenzi wa ofisi za *RITA*, Chuo cha Sayansi na Hisabati katika *UDOM* na miradi mingine mingi ya ujenzi kwa kutumia fedha za akiba ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia yote ambayo yametokea kutokana na uwekezaji wa fedha za wafanyakazi katika miradi iliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kusitisha mara moja matumizi haya makubwa ya fedha za wafanyakazi katika miradi ambayo inaelekea kuifilisi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hivyo kuhatarisha maslahi ya moja kwa moja ya wafanyakazi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze Bunge hili Tukufu kwa nini inatumia mabilioni ya fedha za akiba ya wafanyakazi kwa majengo yasiyokuwa na umuhimu wowote kiuchumi kama ofisi za Idara ya Usalama wa Taifa. Vile vile, Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu kwa nini hadi sasa haijalipa mikopo na riba iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ujenzi wa miradi iliyotajwa na lini inatazamia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ushahidi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ni wazi kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Tanzania inaongozwa, kuendeshwa na kusimamiwa na watu ambao hawana uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ujuzi na uadilifu unaohitajika kwa maslahi ya wafanyakazi wanachama wa Mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni wazi, kwa ushahidi huu, kwamba, mabadiliko makubwa ya kimfumo na kiutendaji katika Mifuko hii yanahitajika na kwa haraka kabla Mifuko hii haijafilisika kabisa. Kwa sababu hiyo na

ili kuinusuru Mifuko hiyo na kunusuru maslahi ya maelfu ya wafanyakazi wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Rais Kikwete kuwawajibisha watendaji wakuu wote wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambao wameacha mabilioni ya fedha za wafanyakazi yazamishwe kwenye miradi mikubwa ya uwekezaji ambayo, kwa ushahidi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, imefanywa bila uchambuzi madhubuti wa uwezo wa wamiliki wa miradi hiyo kurudisha fedha za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; baada ya kutapanya fedha za wafanyakazi kwa kuwekeza katika *grandiose projects* isiyokuwa na manufaa ya kiuchumi kwa wafanyakazi wanachama na hata kwa Mifuko yenyewe, sasa Serikali hii ya CCM imeamua kuwadhulumu wafanyakazi fedha zinazotokana na makato ya mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, vile vile, inaelekea Serikali hii ya CCM inataka kuficha uchafu ilioufanya katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kutunga Sheria inayowazuia wafanyakazi kupata fedha zao wakati wanapozihitaji zaidi, yaani wanapokuwa hawana ajira.

Mheshimiwa Spika, hii imefanyika kwa Serikali kupenyeza kinyemela na kinyume cha Kanuni za Kudumu, masharti yanayowazuia wafanyakazi wote wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Tanzania kuchukua mafao ya kujitoa uanachama wa Mfuko

husika kabla ya kufikisha umri wa miaka hamsini na tano au sitini.

Mheshimiwa Spika, kisheria, umri wa kustaafu kwa hiari ni miaka hamsini na tano wakati umri wa kustaafu kwa lazima ni miaka sitini. Kwa masharti haya, mfanyakazi hana haki au namna nyingine yoyote ya kupata fedha za makato yake ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hata akiachishwa kazi na mwajiri wake bila kosa lolote, hadi atakapofikisha umri huo wa kustaafu kwa hiari au kwa lazima.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, 2012 ulichapishwa katika *Gazeti la Serikali* la tarehe 12 Januari, 2012. Hakukuwa na masharti ya kuzuia mafao ya kujitoa uanachama wa Mfuko. Tarehe 1 Februari, 2012, Muswada huu uliletwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa kwa Mara ya Kwanza chini ya kanuni ya 83(1) ya Kanuni za Kudumu. Hapa pia hakukuwa na masharti ya kuzuia mafao ya kujitoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, Muswada ulipelekwa kwenye Kamati ya Huduma za Jamii kwa ajili ya kuujadili kwa mujibu wa kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu. Masharti hayo hayakujadiliwa wala kupendekezwa na Kamati ya Huduma za Jamii. Ingekuwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni ya 84(3) na (4) ya Kanuni za Kudumu, masharti hayo yangeletwa Bungeni wakati wa Muswada kusomwa kwa Mara ya Pili. Hilo halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, kutoka kwenye Kamati, Muswada huu ulirudishwa Bungeni tarehe 13 Aprili, 2012 kwa ajili ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na kujadiliwa na Bunge lako Tukufu chini ya kanuni ya 86 ya Kanuni za Bunge. Hotuba yote ya Waziri haina mstari hata mmoja unaoonesha nia ya Serikali ya kufuta mafao ya kujitoa kwa wanachama ambao hawajafikisha umri wa kustaafu kwa hiari au kwa lazima.

Mheshimiwa Spika, aidha, hotuba za Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni nazo ziko kimya juu ya kufutwa kwa mafao ya kujitoa uanachama. Ukimya huu unatokana na ukweli kwamba hadi kufikia hatua hiyo hakukuwa na jambo lolote la kuashiria nia ya Serikali kufuta mafao ya kujitoa.

Mheshimiwa Spika, aidha, sio Mwenyekiti wa Kamati au Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani pekee waliokuwa kimya kuhusu masharti haya. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge ya Mkutano wa Saba, Kikao cha Nne cha tarehe 13 Aprili, 2012, hakuna hata mmoja wa Wabunge wote thelathini na nane waliochangia mjadala wa Muswada aliyezungumzia suala la kufuta mafao ya kujitoa uanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, suala hilo halikuzungumziwa katika michango ya Wabunge kwa sababu halikuwepo kwenye mjadala. Wala halikuingizwa kwenye mjadala na Wabunge wengine watano waliowasilisha Majedwali ya Marekebisho ya vifungu mbalimbali vya Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia udhaifu wa uongozi wa Bunge katika kusimamia Kanuni za Kudumu na upungufu wa muda wa mjadala Bungeni ambao ni matokeo ya kuvurugwa kwa Kanuni za Kudumu zinazohusu muda wa Wabunge kujadili hoja za Serikali, Waziri aliwasilisha Jedwali la Marekebisho lililopendekeza marekebisho ya vifungu vipatavyo 45 na vifungu vidogo karibu 70 vya Muswada.

Mheshimiwa Spika, ni katika msitu huo wa Jedwali la Marekebisho ndiko Serikali ilikochomeka masharti ya kufuta mafao ya kujitoa kwa wafanyakazi wasiofikisha umri wa kustaafu kwa hiari au kwa lazima. Kwa sababu ya urefu wa Jedwali na uchache wa muda wa kulichunguza na kujadili, inaelekea hakuna Mbunge hata mmoja aliyeona mapendekezo hayo ya kufuta mafao ya kujitoa.

Mheshimiwa Spika, *Hansard* inaonyesha kwamba ibara za 9, 10 na 11, zilipitishwa na Kamati ya Bungeni Zima pamoja na marekebisho yake." Ibara ya 11 ndio iliyobadilishwa na Jedwali la Marekebisho la Waziri kwa kuweka masharti kwamba mfanyakazi atapata mafao ya kujitoa pale tu atakapofikisha umri wa miaka 55 au miaka 60.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelalamikia ukiukwaji wa kanuni zinazohusu muda wa mjadala Bungeni. Tumelalamika kwamba uongozi wa Bunge umeshiriki katika kupunguza muda wa mjadala kinyume cha Kanuni za Kudumu. Hatukusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, tumepigia kelele kupunguzwa kwa muda wa mjadala wakati wa kupitisha vifungu vya Miswada ya Sheria na mafungu ya bajeti. Hakuna aliyetaka kuelewa kelele zetu. Tumepaza sauti zetu kwamba, Bunge lako Tukufu linageuzwa kuwa muhuri wa kuhalalisha maamuzi ya Serikali tunayotakiwa kuisimamia na kuishauri. Tumepuuzwa.

Mheshimiwa Spika, haya ndio matokeo ya kuruhusu kanuni za mjadala kukanyagwa jinsi zilivyokanyagwa. Sheria hii inayodhulumu wafanyakazi kwa kuzuia mafao yao ya kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii sio tu ni matokeo ya hila za Serikali, bali pia ni uthibitisho wa ulegevu wa uongozi wa Bunge na udhaifu wa Bunge lenyewe katika kusimamia Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi, kifungu pekee kilichofanyiwa marekebisho ya kuzuia fao la kujitoa ni kifungu cha 21 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma. Hata hivyo, *SSRA* imedai kwamba Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yanahusu Mifuko yote na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu kama Sheria hii mpya imerekebisha vifungu vya Sheria nyingine *by implication*, kama inavyoelekea kuwa tafsiri ya *SSRA*. Kama Sheria mpya haijabadilisha vifungu vya Sheria za Mifuko mingine, ni kwa nini *SSRA* inang'ang'ania kwamba marekebisho ya Sheria ya *PPF*

yanawahusu wafanyakazi wote nchini mwetu bila kubagua sekta yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, aidha tunaelewa kuwa Pensheni ni suala la msingi sana na hatuwezi kuwaacha wazee wetu waishi bila Pensheni. Vile vile tunatambua kuwa kuna mahitaji ya sasa ambayo hayasubiri mpaka mtu azeeke ndipo aweze kuyatatua ndio maana tunaunga mkono wafanyakazi katika kupata fao la kujitoa na tunapendekeza sheria irekebishwe na kuzingatia yafuatayo:-

(a) Uanzishwe utaratibu wa kuwa na mafao kwa wanachama ambao ama wamekosa kazi kutokana na sababu mbalimbali *(Unemployment benefits)* kama vile kumalizika kwa mkataba, kuachishwa kazi, kufukuzwa kazi na kadhalika kwa kipindi cha miezi sita mwanachama wa Mfuko husika aweze kulipwa kiasi cha mshahara kamili na miezi sita mingine kama hajapata kazi alipwe nusu mshahara na Mfuko na baada ya mwaka mmoja kama atakuwa hajapata kazi basi Mfuko uache kuendelea kumlipa mwanachama huyo. Mifuko itenge fungu maalum kwa ajili ya kulipia mafao hayo.

(b) Mifuko itenge fedha kwa ajili ya masomo *(Education Fund)* kwa ajili ya wanachama wake pindi watakapokuwa wanakwenda masomoni wakiwa ni wanachama wa mfuko, hii itawafanya wanachama kuweza kujiendeleza kielimu na hivyo itapunguza idadi ya wanachama ambao wanajitoa kwa ajili ya kupata fedha za kusoma.

Mheshimiwa Spika, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kurejea pendekezo letu tuliloishauri katika bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2011/2012 katika kuona umuhimu wa kuiunganisha Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii na kubaki katika Wizara moja ambayo ni ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa lengo kuu la kuunganisha Mifuko hii ya Hifadhi za Jamii ni katika kuirahisishia Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi za Jamii (*SSRA*) katika kutekeleza Sheria moja na kuunda vifungu sawa vya kisheria vitakavyosimamia utekelezaji na uendeshaji wa Mifuko hii ambapo kwa sasa Mifuko hii imekuwa chini ya Wizara tofauti. Hivyo, hata utekelezaji wake unakua mgumu na kuleta ukinzani kwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Spika, tunasisitiza kuwa pendekezo letu ni kuifanya *PPF* na *NSSF* iunganishwe na kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta Binafsi. Vile vile *LAPF, PSPF* na *GEPF* iunganishwe na kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta ya Umma. Pia, Kambi ya Upinzani inapendekeza Mifuko yote isimamiwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, kodi ya pato la mishahara (*Pay as You Earn – PAYE)* Tarehe mosi Julai mwaka huu, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipokea taarifa kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imebadilisha viwango vya kodi ya mapato kwa watu ambao ni wafanyakazi wakaazi. *TRA* imesamehe kodi kwa wafanyakazi wanaopata mshahara mpaka Shilingi

170,000, lakini imeendelea kutoza kiwango kikubwa cha kodi kwa wafanyakazi wanaopata shilingi 360,000 kwa mwezi, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 14 ya mshahara huo.

Mheshimiwa Spika, mapato ambayo yanazidi sh. 360,000, lakini hayazidi shilingi 540,000, hutozwa asilimia 20 ya kiasi kinachozidi, mapato yanayozidi sh. 540,000, lakini hayazidi sh. 720,000 hutozwa aslimia 25 ya kiasi kinachozidi. Kiasi kinachozidi 720,000, lakini hakizidi 1,076,000 hutozwa asilimia 30 ya kiasi kinachozidi.

Mheshimiwa Spika, viwango hivi vya tozo mpya za kodi ya mapato ni vikubwa sana. Tunalitaka Bunge lako Tukufu kupitia viwango hivi upya na kwa umakini ili kutafuta kila namna ya kumwondolea mfanyakazi mzigo huu mzito wa kodi. Badala ya Serikali kulimbikiza kodi nyingi kwa wafanyakazi pekee, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri kuongeza wigo wa wananchi wanaotozwa kodi kwa kuzingatia vipato vyao, kama ilivyobainishwa na ripoti ya hivi karibuni ya Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* iliyoonesha kuwepo kwa idadi kubwa ya wananchi wanaopaswa kulipa kodi, lakini hawatozwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza mzigo mkubwa wa kodi wanayokatwa wafanyakazi, Kambi Rasmi ya Upinzani inarejea pendekezo lake la kuitaka Serikali ipunguze viwango vya sasa vya kodi mpaka asilimia tisa kwa kiwango cha chini na asilimia 27 kwa kiwango cha juu. Uamuzi huu utawezesha wafanyakazi kubakia na fedha kutoka kwenye mishahara yao na hivyo kuishi vizuri kumudu maisha yao ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria za Kazi na Haki za Wafanyakazi, pamoja na kuwepo na Sheria za Kazi ambazo zinajaribu kulinda haki za wafanyakazi, kama vile Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya 2004, bado kuna pengo la sheria katika kulinda haki za wafanyakazi pindi kunapotokea uhamisho wa shughuli yaani *(Transfer of Undertakings),* kwa upande wa muajiri hususani kwenye sekta binafsi ambapo kumekuwa na migogoro mingi baina ya pande mbili hizi inayotakana na kukosekana na sheria hii.

Mheshimiwa Spika**,** mkataba wa miaka 25 ambao Serikali iliingia na Kampuni ya *Rites* ya India mwaka 2009, katika kusimamia shughuli na uendeshaji wa Shirika la Reli Tanzania *(Tanzania Railway Limited- TRL)* ni mfano mzuri wa uhamisho wa shughuli. Mkataba huu ulileta mgogoro wa kazi baina ya menejementi na wafanyakazi baada ya mwajiri mpya kusitisha mikataba ya kazi na ajira na kufanya wafanyakazi wapatao 3,204 kuwa hatarini kupunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulipa uzito mkubwa suala hili kwa kuleta Muswada wa Sheria Bungeni utakaosimamia maslahi wafanyakazi katika suala hili. Afrika Kusini ni nchi inayokua kwa kasi kiuchumi na yenye fursa mbalimbali za uwekezaji, lakini kwa kugundua hili na kwa lengo la kulinda haki za wafanyakazi, wenzetu wameweza kutunga sheria inayoitwa *Transfer of undertakings Act (Protection of Employment)* ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba Serikali, ambayo ina sera mbalimbali zenye nia ya kuikuza sekta ya uwekezaji, bila shaka itaona umuhimu wa dhati wa kutunga sheria ambazo zitalinda haki za kazi pale panapotokea uhamisho wa shughuli ili kuepusha migogoro inayoweza kutokea kama kuvunjwa kwa mikataba, kupunguzwa kwa wafanyakazi kazini bila kufuata Sheria za Kazi, ushurutishwaji wa wafanyakazi kufanya kazi kwa mwajiri mpya, kupoteza haki za msingi za wafanyakazi na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Tanzania na Zambia *(TAZARA)*, Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ilifanya mazungumzo na uongozi pamoja na wafanyakazi wa *TAZARA* na kukiri kuwa mkataba ambao Serikali za Tanzania na Zambia uliingia miaka 36 iliyopita, umeisababishia Serikali hasara kubwa na umechangia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa migogoro isiyokwisha baina ya uongozi na wafanyakazi wa *TAZARA*.

Mheshimiwa Spika, moja ya athari za makubaliano ya mkataba huu, ni Wazambia kunufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na mapungufu ya kimkataba huo kuliko Watanzania; kwa mfano, wafanyakazi 52 kutoka Zambia wanaofanya kazi katika Tawi la *TAZARA* Tanzania wamekuwa wakipata marupurupu ya kufanya kazi kama wafanyakazi wa kigeni wakati kuna wafanyakazi wanne tu wa Tanzania wanaofanya kazi katika tawi la *TAZARA* nchini Zambia, lakini hawapewi marupurupu hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kuwa hali hii imesababishwa pia na kuhodhiwa madaraka na Mkurugenzi wa *TAZARA* ambaye ni raia wa Zambia. Kama ambavyo imeshauri Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali na Bunge hili kupitia mkataba huu ili kuweza kuleta usawa na haki katika Sheria za Kazi utakaolinda maslahi ya wafanyakazi wa nchi zote mbili bila kuleta mpasuko.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara kutoa maelezo ya kutosha juu ya hatua gani zimechukuliwa katika kutatua madai haya ya msingi ya wafanyakazi wa *TAZARA* na je, Wizara ina mikakati gani katika kuhakikisha kuwa mkataba huu unaangaliwa na kupitiwa upya ili kuleta Muswada wa sheria utakaolinda haki za wafanyakazi wa *TAZARA* pindi kunapotokea mabadiliko yoyote ya mkataba?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kazi za migodini, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)* kilikuwa cha kwanza kutoa taarifa kwa umma juu ya ukiukwaji mkubwa uliokithiri wa haki za wafanyakazi wa Geita *Gold Mine (GGM*), *Resolute 'Resources' Golden Pride* - Nzega, Tabora baada ya uchunguzi wa kipelelezi kwenye migodi hiyo miwili mwezi Mei, 2011. Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)* ilipeleka ripoti kwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, ambaye aliahidi kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani, inamtaka Waziri kulieleza Bunge hili ni hatua zipi

zilichukuliwa dhidi ya mwajiri kwa kukiuka Sheria na Kanuni za Kazi na kutoa majibu yasiyoridhisha juu ya fidia ambazo wafanyakazi walilipwa baada ya kuonekana kwa ukiukwaji wa haki zao.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Vyama vya Wafanyakazi toka vianzishwe mwaka 1929 lilikuwa ni kutetea maslahi ya wafanyakazi, lakini hadi leo ambapo tumefikisha zaidi ya miaka 50 ya uhuru bado wafanyakazi wanakabiliwa na matatizo yale yale yaliyopelekea kuanzishwa kwa vyama hii. Sheria zetu zinazoratibu masuala ya kazi ikiwemo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004, zinaruhusu wafanyakazi kuunda umoja wao ili kuwa na sauti moja katika kutetea maslahi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kwa mujibu wa tafiti (rasmi na zisio rasmi) wafanyakazi wa Tanzania wanakabiliwa na hali mbaya ya maisha kutokana na kushindwa kwa uongozi wa kisiasa katika kutawala uchumi na matumizi ya rasilimali katika kufikia malengo ya kuboresha maslahi pamoja na mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa sekta zote.

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha hili Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wafanyakazi *(International Trade Union Confederation- ITUC)* katika taarifa ya ripoti yake ya *Annual Survey of Violations around the World in 2011*, ripoti imeonesha kuwa haki za muungano wa wafanyakazi nchini mara nyingi hupuuzwa kwa kiwango kikubwa, wafanyakazi huwa na hatua ya migomo mikubwa kinyume cha sheria na

hii inasababishwa na mahitaji ya muda mrefu na upindishwaji wa sheria katika kuruhusu Vyama vya Wafanyakazi kutoa wito wa mgomo wa kisheria. Katika sekta binafsi, ripoti inaonesha kuwa baadhi ya waajiri mara nyingi wanawanyima wafanyakazi wao haki ya kuandaa na kushiriki katika majadiliano ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, licha ya wafanyakazi kufuata taratibu zote za kisheria pindi wanapotaka kuandamana au kugoma ili kushinikiza utelekezaji wa madai yao, bado Serikali imekuwa ikitumia mabavu kuwakandamiza wafanyakazi na vyama vyao. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha mara moja kutumia mabavu katika kushughulikia madai ya wafanyakazi, kwani kufanya hivyo ni kukiuka haki za binadamu na sheria halali za nchi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, *(CMA)* ni muhimu sana kutokana na majukumu yake katika kutatua migogoro sehemu za kazi kwa ufanisi, usawa na kwa haraka tofauti na ilivyo kwa Mahakama za kawaida. Pamoja na Tume kuwa na jukumu hilo kuu, bado yapo malalamiko mengi sana juu ya utendaji wake hasa katika kutoa haki sawa baina ya mwajiri na mfanyakazi au baina ya wafanyakazi na vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya maelezo ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ya Juni, 2012, katika maeneo yanaongoza kwa migogoro kazini, migogoro katika sekta ya Afya kwa kipindi cha Oktoba – Disemba, 2011 ilikuwa 33 na kutoka Januari – Machi, 2012 migogoro ilikuwa ni 53 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 23 kwa kipindi cha miezi mitatu tu.

Hii ni ishara kuwa kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za wafanyakazi na hii pia imeonesha ongezeko la usajili wa migogoro kwenye viwanda, migodi, mashirika ya umma, vyakula na vinywaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi ni kukosekana kwa haki katika maamuzi ya Tume kutokana na waajiri wengi kuwa na nguvu ya fedha. Pia waajiri wengi wanatumia mwanya wa baadhi ya wafanyakazi ambao hawana uelewa wa masuala ya kisheria ambapo maamuzi ya Tume hawazingatii na badala yake baadhi ya wafanyakazi hufukuzwa kazi mara tu maamuzi yakishatoka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa watendaji wa Tume hii kuzingatia weledi katika kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua waamuzi ambao hawazingatii taratibu za kazi pamoja na kutoa haki pale inapostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, vyombo vingine vya Kiserikali ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) vifuatilie kwa karibu Tume hiyo na mamlaka nyingine za wafanyakazi ili kudhibiti mianya ya ufisadi katika utetezi wa haki na maslahi ya wafanyakazi. Hata hivyo, bado kuna changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na Tume kuwa na mashauri mengi ambayo hayajafanyiwa maamuzi/usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzishwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)*, bado

wafanyakazi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu yasiyozingatia usalama wa afya zao. Taasisi hii haijafanya kazi vya kutosha ili kulinda usalama wa afya za wafanyakazi kazini.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuweka utaratibu wa kuhakikisha mashirika, taasisi na makampuni yote nchini yanatekeleza matakwa ya *OSHA* na kuongeza adhabu kwa taasisi ambazo hazizingatii taratibu hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa uongozi wa viwanda na makampuni unaweka taratibu wa kupima afya za wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yetu ya mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kambi ya Upinzani tuliendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa waajiri wanatengeza mazingira salama. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko mbalimbali kutoka kwa wafanyakazi wa Sekta ya Madini ambao wamekuwa wakiathiriwa na mazingira magumu na hatarishi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa matokeo ya tafiti hizo, idadi kubwa zaidi ya wafanyakazi wa Sekta ya Madini ambao walitibiwa katika hospitali mbalimbali, uchunguzi wa Madaktari umeonesha kwamba wengi wao maradhi yametokana au kuhusiana na shughuli za madini. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya utafiti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii, ambalo linaundwa na idadi ya wateule 17 ambao wanateuliwa na Waziri wa Ajira na Kazi, ni sawa na kuibebesha Serikali mzigo mkubwa hasa ukizingatiwa kuwa kazi na majukumu makuu ya Baraza hili ni masuala ya ushauri hasa katika kuishauri Serikali na Waziri kwenye masuala yanayohusiana na kazi, uchumi na jamii kwa kiasi kikubwa kama zilivyoainishwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza umuhimu wa Serikali katika kuhakikisha kuwa inapunguza matumizi yake kutokana na utegemezi wa bajeti yake ili kutoa unafuu na kuelekeza fedha hizi katika sekta nyingine ambazo zinaweza kutumia fungu hili.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza hili *(LESCO)* lilitengewa kiasi cha sh. 30,000,000/= ili kuwezesha vikao vya Baraza na kiasi cha sh. 12,508,500/= kuwezesha vikao viwili tu vya Baraza. Katika bajeti ya mwaka huu, Baraza hili limetengewa kiasi cha sh. 37,325,000/=, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kupunguza matumizi yake kwa kurekebisha sheria hii na kulifuta Baraza la Kazi kutokana na kuwa na taasisi nyingine zinazofanya kazi za kulingana nazo vikiwemo Vyama vya Kazi, Vyama Vya Waajiri pamoja na Wataalam wa Masuala ya Kazi katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Kamati ya Huduma Muhimu *(Essential Services Committee)* inaanza kazi

mara moja ili kutatua kisheria migogoro inayojitokeza katika sekta zitoazo huduma muhimu kama vile afya, usafiri na kadhalika kama ilivyoainishwa katika Vifungu Namba 29-33 vya Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2007.

Mhesimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)* ilianzishwa mwaka 2008 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997, ili kuleta ufanisi katika kuboresha utoaji wa huduma za ajira kwa watafuta kazi, waajiri na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya ajira na kazi ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tulitoa pendekezo la *TaESA* kujitangaza vya kutosha na kuhakikisha kuwa inaweka taarifa za shughuli zake ili kutoa fursa kwa nguvu kazi kuweza kufuatilia nafasi za kazi zinazotangazwa na vigezo rasmi kwa ajili ya nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inaendelea kutoa ushauri kwa TaESA tukiitaka iandae *database* ambayo itakua na taarifa muhimu kama namba ya wahitimu wa elimu ya juu nchini, taaluma zao na uzoefu wao ili kuweza kupata takwimu rasmi zitakazoweza kumuunganisha mtafuta kazi na mwajiri.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri *TaESA* kuhakikisha kuwa nafasi za kazi hazitolewi kwa upendeleo na kuwa sheria na kanuni zinazingatiwa kwa kutoa nafasi hizo za kazi, kwa kuwa kumekuwepo malalamiko mbalimbali kuhusu

uunganishwaji wa watafuta ajira na waajiri. Kwa mamlaka waliyopewa *TaESA*, yanaweza pia kufungua mianya ya rushwa na kupeana kazi kwa vimemo na hii itasababisha kupoteza watu walio na sifa kamili na uwezo ambao wangeweza kufanya kazi ka ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji; je, ni mikakati gani ambayo *TaESA* inatumia katika kuhakikisha kuwa nafasi za kazi zinatolewa bila upendeleo wowote? Je, ni kwa kiwango gani *TaESA* imefanikiwa katika kuhakikisha kuwa wadau pamoja na umma unapata taarifa sahihi kuhusu soko la ajira kwa kuzingatia viwango na taratibu zilizowekwa?

Mheshimiwa Spika, utafiti wa nguvukazi na ajira uliofanyika mwaka 2006 ndio utafiti wa mwisho katika kutoa takwimu za hali ya sekta ya ajira nchini na kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2011, huo ndio utafiti pekee uliofanyika miaka ya hivi karibuni ilhali tafiti za ajira hupaswa kufanyika kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu rasmi na kuhakikisha kuwa inatenga fungu la kutosha kuwezesha tafiti za nguvukazi na ajira kufanyika katika muda uliowekwa (yaani kipindi cha kila baada ya miaka mitano).

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya hali ya uchumi, takwimu zilizoendelea kutumika mpaka sasa ni za Sensa ya mwaka 2002 na pia imekuwa ikifanyiwa

makadirio kutokana na taarifa za Shirika la Takwimu za Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani, inapenda kujua ni lini taarifa rasmi za soko la ajira nchini zitatolewa kwa umma pamoja na hayo tunataka kujua idadi ya watu waliopata ajira 1,000,000 kama ilivyoahidiwa na Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inajua kuwa ukusanyaji wa taarifa za soko la kazi ni muhimu ili kutoa taswira ya ajira kwa Taifa letu, lakini kama Serikali itaendelea kutegemea fedha za wafadhili kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira ni wazi kuwa hata mianya ya wafanyakazi wa kigeni wanaofanya kazi nchini kinyume na sheria itazuia uwezekano wa Watanzania wenye uwezo kuweza kupata nafasi na kuonesha ujuzi na utaalam wao katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la raia wa kigeni na Mustakabali wake katika soko la ajira nchini, kuna wimbi la kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi wa nchi nyingine wanaoingia kwa mgongo wa wawekezaji kinyume cha taratibu na ambao hufanya kazi za kawaida ambazo Watanzania wana uwezo nazo. Wafanyakazi wetu wengi wanaonekana kuwekwa pembeni si kwa sababu hawana uwezo bali kwa sababu waajiri wanaleta watu wao toka nje.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Na. 26 ya mwaka 2007, Sura 38 Kifungu cha 24, inaruhusu Mwekezaji kuleta wataalam wasiozidi watano kutoka nje ya nchi. Aidha, iwapo Mwekezaji ataona haja ya kuongeza wataalam zaidi kutoka nje ya nchi,

atapaswa kuwasilisha maombi maalum Kituo cha Taifa cha Uwekezaji ambacho kitawaruhusu ikiwa tu itathibitika hakuna Mtanzania hata mmoja mwenye utaalam husika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka katika kampuni ya *SBC- Pepsi* kuzidisha idadi ya wafanyakazi ambao ni raia wa India ambao pia wamekuwa wakifanya kazi ambazo Mtanzania anaweza kufanya, kwa mfano, kuna raia wa India ambao wamepewa hadi kazi za ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imegundua malalamiko kama haya yapo kwenye kiwanda cha Jambo *Plastic* cha Dar es Salaam na pia Kiwanda cha M*able stones* cha Marmo kilichopo Mbeya ambako kuna ushahidi wa wageni kutoka india kufanya kazi zisizohitaji utaalam maalum wa kitaaluma kama ulinzi na kazi zingine za mikono kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, kinyume kabisa na Sheria hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kuwa migodi na kampuni nyingi nchini, wamekuwa wakiajiri raia wengi wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikiwanyima Watanzania wengi fursa ya kuajiriwa wakati kumbe nafasi zipo, lakini wanapewa wageni kinyume kabisa cha sheria. Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Wizara hii, kufanya ukaguzi maalum katika migodi, viwanda na mashirika yote yanayolalamikiwa kuajiri wageni kinyume cha sheria (yakiwemo

tuliyoyataja), ili kuhakikisha sheria husika inaheshimiwa na Watanzania wazawa wananufaika nayo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Sekta Isiyo Rasmi ni mhimili mkubwa sana katika uchumi wa Tanzania, lakini bado haipewi kipaumbele kinachostahili. Zaidi ya asilimia 80% ya Watanzania wapo sekta hiyo, sekta rasmi ni asilimia isiyozidi 10% ambapo kitakwimu Watanzania walioajiriwa rasmi hawazidi laki nne. Kwa hiyo, utaona kuwa wavuja jasho ndio wengi hapa nchini na ndio wanaoendesha maisha yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mara ngapi tunashuhudia au kusikia wafanyabiashara wadogo wadogo/wajasiriamali wakinyanyasika zaidi ya wakimbizi kwa kufukuzwa maeneo wanayojitafutia riziki bila ya kuoneshwa maeneo mbadala? Mara ngapi tunashudia mama lishe wakifukuzwa kama mbwa na kukatazwa kufanya biashara bila ya sababu za msingi wala kuwekewa mazingira ya kujiendeleza. Vijana walio wengi hawana ajira rasmi na wanajituma ili waweze kupata kianzio cha mtaji wafanye biashara/shughuli halali ili wajipatie kipato lakini hakuna taasisi yoyote inayoweza kuwapa mikopo kama mtaji.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22, 23 na ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano zinazungumzia haki ya kufanya kazi. Ibara hizi zimeweka bayana misingi ya kisheria na msimamo thabiti unaowalinda Watanzania wanaojishughulisha katika sekta zisizo rasmi. Kwa mfano, Ibara ya 22 kifungu kidogo cha kwanza kinasomeka hivi: “kila mtu anayohaki ya kufanya

kazi' na cha pili kinasomeka: "Kila raia anastahili fursa na haki sawa, kwa masharti ya usawa ya kushika nafasi yoyote na shughuli yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi".

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23(1) kinasomeka hivi: "Kila mtu bila ya kuwepo ubaguzi wa aina yoyote anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake, na watu wote wanaofanya kazi kulingana na uwezo wao watapata malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi wanayoifanya".

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa nguvukazi iliyo katika sekta isiyo rasmi inalindwa kwa kuzingatia misingi bora iliyowekwa na kuainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa. Kwa mujibu wa taarifa za watumishi wenye ulemavu zilizokusanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Desemba 2007, inaonesha kuwa ni asilimia 0.2 tu ya watumishi wote wa umma walioajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kama hali ni hiyo kwenye utumishi wa umma basi hali ni mbaya zaidi kwenye sekta binafsi kwani waajiri wengi binafsi wamekuwa wakikwepa kuajiri watu wenye ulemavu kutokana na visingizio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe ili kuongeza ajira kwa wenye ulemavu:-

- Serikali ifanye utafiti na kupata takwimu za watu wenye ulemavu walioko katika soko la ajira na walioajiriwa kwenye sekta binafsi.

- Serikali iimarishe na kuboresha miundombinu kwenye ofisi na maeneo ya kazi kote kwa sekta ya umma na binafsi.

- Serikali iharakishe utungwaji wa Kanuni za Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya 2010.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia taasisi zake mbalimbali, kuhakikisha kuwa makundi mbalimbali ambayo kwa kiasi kikubwa hukabiliwa na ubaguzi wa kazi kama, walemavu, wanawake na watu wenye maambukizi ya ugonjwa UKIMWI, yanapewa fursa sawa katika masuala ya kazi na ajira. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa, inawapatia mafunzo waajiri na waajiriwa yanayohamasisha masuala ya fursa sawa kwa wote, kufuatilia kwa usahihi na ukaribu mgawanyo wa kazi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, aidha tunaitaka Serikali ipitie kwa umakini vigezo vinavyoonesha stahili za mafao kwa waajiriwa, kuweka viwango vya wazi vya malengo ya fursa sawa kwa wote katika ngazi zote na kupitia taratibu za kuajiri na kupandisha vyeo pamoja na kuhakikisha kuwa majina yote yalipitishwa kwa ajili ya

usaili wa ajira na kupandisha vyeo yamejumuisha waombaji wa makundi yote wenye sifa stahili na kuweka mawasiliano ya moja kwa moja na taratibu za kutoa malalamiko ya ubaguzi katika maeneo na mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira hatarishi kwa watoto. Kauli mbiu ya mwaka huu katika kuadhimisha siku ya kupinga ajira kwa watoto iliyoadhimishwa tarehe 12 Juni, 2012 ilisema: “Haki za binadamu na haki za kijamii, tutokomeze ajira kwa watoto” ukiwa ni ujumbe wa kuikumbusha jamii kwa ujumla wake kuwa ajira kwa watoto siyo kitu kinachoungwa mkono, utumikishaji wa watoto ni ukiukaji wa haki za msingi za watoto. Nchini Tanzania asilimia 18.7 ya watoto wote wanatumikishwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwenye mashamba makubwa, migodini hasa ya wachimbaji wadogowadogo, majumbani na kwenye shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara kueleza mikakati endelevu ambayo itatatua tatizo la kutokulindwa kwa haki za watoto, hali inayochangiwa kwa Serikali yenyewe kuruhusu hali hii kutokea au kuchelea kukemea ajira kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa *(NIP* ni chombo muhimu kinachoweza kulisaidia Taifa katika kuhakisha shughuli zinafanyika kwa tija ikizingatiwa uchache wa rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili likitumiwa vizuri litapunguza upotevu wa fedha za umma unaofanyika katika nyanja za mafunzo toka kwa taasisi ambazo baadhi hazina nyenzo na uwezo wa kutoa mafunzo yenye ubora unaotakiwa. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa pendekezo la kuendesha shughuli za mafunzo ambazo *NIP* imekuwa ikiyafanya kwa kupitia chuo chake cha mafunzo nchini Swaziland zifanyike hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya taasisi hapa nchini ambazo zinatoa mafunzo kwa gharama nafuu na pia baadhi ya vyuo vikuu vyenye wataalam na wakufunzi wenye ujuzi wa kutosha, ambao wanaweza kutumika kama njia mojawapo ya kupunguza gharama ambazo Shirika hili linatumia katika mafunzo yanayofanyika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yakifanyika nchini si tu yatachangia kupunguza gharama na matumizi bali itachangia pia katika kuhakikisha uwezeshaji wa walengwa wa mafunzo haya katika kutumia yale waliyofundishwa katika mazingira halisi ya kazi kwa kuwa mafunzo yanafanyika kwenye maeneo sahihi, kuhamisha kujifunza, *(transfer of learning)*.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, imeomba kuidhinishiwa kiasi cha sh. 15,945,298,000/= ambacho ni sawa na punguzo la asilimia 12 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika katika maagizo na ushauri ulioletwa hapa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali ilipewa ushauri wa kutoa pensheni ya wazee kwani Waziri Mkuu alishaahidi Serikali kuanza kutoa pensheni kwa wazee lakini katika bajeti ya mwaka huu hakuna mahali ambapo bajeti inaonesha kuhusu utekelezaji wa shauri hilo zaidi ya maelezo ya Wizara ya kuandaa tafiti kwa kupitia Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa ni lini tafiti hizi zitakamilika na kutelekezwa kama ilivyoelezwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2010-2015. Ni dhahiri kuwa Serikali imeendelea kupiga danadana suala la posho la wazee kwa kuwa imeshindwa kusimamia ahadi zake walizotumia kwa ajili ya kupata kura za wazee masikini wasio na msaada, wenye maisha duni na ya kusikitisha, ikizingatiwa kuwa wazee wanakabiliwa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya maendeleo ya Wizara hii, imetengewa kiasi cha sh. 2,835,800,000/= fedha za nje ambazo ni kwa ajili ya uboreshaji wa ofisi za kazi na ajira, kuimarisha mfumo wa utawala na utunzaji kumbukumbu, masuala ya utokomezaji wa ajira ya watoto, utekelezaji wa sera na sheria, mapambano dhidi ya UKIMWI na uboreshaji wa mazingira wezeshi ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi, inamaanisha kuwa bajeti ya nchi yetu kwa Wizara ya Kazi na Ajira ni tegemezi kwa asilimia mia moja. Hii ni hatari sana kwa

maendeleo ya ajira na kazi hapa nchini kwani ni mara nyingi tumeona jinsi ambavyo fedha za ufadhili zisivyo na uhakika kwa kuwa mara nyingi hazifiki kwa muda uliopangwa na mara nyingine zinakuja lakini si kwa kiwango kile kilichotegemewa.

Mheshimiwa Spika, utegemezi huu wa wafadhili katika kutekeleza maendeleo katika sekta ya ajira na kazi ni ishara tosha kuwa Serikali imeamua nguvu kazi ya Taifa katika hatari kubwa ya kuporomoka kiuchumi na katika kuwapa maisha bora Watanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je ni vipi suala la ajira hatarishi kwa watoto litafanikiwa ikiwa bajeti ya maendeleo ni tegemezi kwa asilimia mia moja kutoka kwa wafadhili?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imeamua kuweka rehani maisha ya watoto ambao wanafanya kazi zilizo hatarishi kwa kuwategemea wafadhili na wahisani? Je Serikali imeamua kuweka pembeni mapambano dhidi ya UKIMWI na kuamua kutegemea wafadhili katika kutoa elimu ya hamasa ya masuala ya UKIMWI ambapo tunajua athari zake ni kubwa kwa nguvukazi ya Taifa letu? Ni vipi bajeti tegemezi itaweza kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025?

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha hotuba hii, ujumbe wangu kwa Walimu wa Tanzania, Madaktari na Askari Polisi, Wazee wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na wafanyakazi wote wanaonyanyasika kwa kudai haki na mafao yao, ni kwamba wasihofu, kwani kama alivyosema Mahatma Gandhi, Dunia

imekuwa na watu katili, lakini mwisho wa yote nao pia walianguka".

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba kueleza kwamba, tumepokea hapa barua kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekaimisha nafasi ya kusimamia shughuli za Serikali, hapa Bungeni, kwa Mheshimiwa Samwel Sitta, kutokana na kwamba, yeye anakwenda Mkoani Arusha kwa shughuli za kikazi, kuanzia tarehe 7 Agosti mpaka tarehe 9 Agosti. Kwa hiyo, wakati huu wote Mheshimiwa Sitta, atakaimu Ukuu wa kusimamia Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Kwa hiyo, tutakupa ushirikiano unaostahili kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

Ya pili Waheshimiwa Wabunge, ningependa kueleza, kwa mujibu wa Kanuni zetu Sehemu ya 8, Kamati za Kudumu za Bunge na hususan Kamati ya Uongozi. Kamati ya Uongozi kwa mujibu wa Taratibu zetu ina Wajumbe wafuatao, yuko Spika ambaye ni Mwenyekiti, Naibu Spika ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni au Mwakilishi wake, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni au Mwakilishi wake, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu au Makamu wao na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu wa Kamati hii ni Katibu wa Bunge. Kazi au shughuli ya Kamati hii, kujadili na kumshauri Spika, kuhusu mambo yote yanayohusu shughuli za Bunge kwa jumla, ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu utakaorahisisha maendeleo ya shughuli za Bunge au za Kamati yoyote.

Kwa hiyo, napenda kusema Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, anasema ni udhaifu wa Bunge ni udhaifu wa kila kitu; ni udhaifu pamoja na wao, sisi wote ndio tunaokubaliana utaratibu huu. Naomba tuwe na utaratibu wa kuheshimu kazi tunazozifanya. Kama tuna matatizo tunakaa tena kwenye Vikao vyetu, tunaangalia upya namna ya kuendesha shughuli zetu. Huwezi kumuoneshea mtu mmoja kidole kwa sababu, vyote vinakuonesha wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaendelea na wafuatao kwa sababu, ya muda wetu. Wachangiaji wa kwanza watakuwa Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mheshimiwa Subira Mugalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Juma Haji. Tuone kama muda utasemaje.

Mheshimiwa Profesa!

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza niweze kutoa mawazo yangu katika Hotuba hii muhimu. Ningependa nizungumzie suala la pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, ajenda hii ya pensheni kwa wazee, imeshika kasi sana hivi karibuni. Nakumbuka mwaka jana kipindi kama hiki, wazee waliandaa Mkutano pale Pius Msekwa, baadhi yetu tulihudhuria. Nawashukuru Shirika la *HELPAGE,* ambao ndio waliweza kufadhili huo Mkutano.

Mheshimiwa Spika, tulipotoka pale, wote tulikubaliana kwamba, ni muhimu na ni wakati muafaka kwamba, wazee washughulikiwe kwa suala la pensheni. Majibu ya Serikali, yamekuwa yakitia moyo toka wakati huo. Juzi na jana maswali yamejitokeza hapa Bungeni na Serikali, imetoa Tamko, na tunashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonesha kwamba, idadi ya wazee kwa tafsiri yetu, waliozidi miaka 60 hapa nchini, wanafikia milioni mbili ambayo ni 4% ya idadi ya watu na 82% kati ya hao, wanaishi Vijijini. Wazee wana kila stahili ya kuenziwa. Hii Tanzania tunayojivunia imefika hapa, ni wazee waliotufikisha hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru kwamba, Serikali, inatambua umuhimu wa wazee katika jamii. Ukiangalia katika Katiba, Kifungu cha 11(11) kinazungumzia Wazee, MKUKUTA *Cluster* ya II, Lengo la 4, linahusu wazee na katika Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003, wazee wana nafasi yao pale na Serikali, iliunda Sera ya Wazee mwaka 2003, ambayo imekuwa ikizungumzwa kwa muda mrefu bila kuundiwa Sheria.

Mheshimiwa Spika, hii Sera ya Wazee, kwa sisi ambao tumeisoma ni Sera nzuri kwa sababu, inatambua umuhimu wa wazee katika jamii kwamba, ni hazina ya hekima, lakini vile vile ni nguzo ya malezi ya watoto na nguzo ya uchumi. Lakini kundi hili la wazee ni kundi maalum, lenye mahitaji maalum. Katika

Sera, utaona kwamba, wameainisha maeneo matatu yanayowaathiri ya kijamii, ya kiafya na ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kijamii, wazee wamegubikwa na upweke, kutengwa, wengine wanauawa hasa Usukumani. Lakini vile vile tunajua kwamba, 53% ya watoto yatima wanalelewa na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kiafya, wana matatizo sana ya usahaulifu. Lakini vile vile kuna magonjwa ambayo yanawaandama kama vile kisukari, shinikizo la damu, saratani, magonjwa ya mifupa, magonjwa ya viungo na kadhalika. Matibabu ya magonjwa haya ni ya gharama kubwa na yakianza, yataendelea mpaka uhai wa mzee.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kiuchumi, wazee wanakuwa wamechoka; wamechoka kimwili, wamechoka kiakili. Kipato chao kinapungua, wale walioajiriwa kipato chao kinapungua, lakini hata ambaye amejiajiri kipato kinapungua; ndio maana 73% ya wastaafu, wanaendelea na ajira ya mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera, imeainisha nini kifanyike, ili kuyapatia ufumbuzi matatizo ya wazee, kwa mfano, kuhusu matibabu tunasema wazee wapatiwe matibabu bure. Pia imeelezwa kwamba, Mfuko Maalum wa Kuwakopesha Wazee Mitaji uanzishwe, wazee waweze kupata mtaji ili waweze kujikimu katika shughuli wanazoweza kuzifanya, lakini pia suala la pensheni ya wazee limezungumzwa katika Sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kwamba, baadhi ya mambo haya yameanza kufanyika, kwa mfano, matibabu kwa wazee kwamba, wapewe matibabu bure na kwamba, Waganga Wakuu wa Mikoa, wameelekezwa kufanya hivyo. Ninavyojua ni kuna maeneo mengi ambayo Dirisha limewekwa. Kwa hiyo, ni mambo mazuri ambayo Serikali, imeona iyafanye.

Mheshimiwa Spika, na leo hii hapa Bungeni, tumezungumza habari za kodi ya viwanja, kodi za nyumba za kupanga na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, nia naona ni nzuri. Mambo mazuri yamefanyika kwa ajili ya wazee, matatizo inakuwa utekelezaji tu. Lakini vile vile mambo mazuri yamepangwa kufanyika, matatizo ni kwamba, mambo yote haya hayana nguvu ya kisheria. Wazee hawawezi wakadai kwamba, mimi sikutibiwa bure kwa sababu, hakuna Sheria, ambayo imeelekeza kwamba, hii ni haki yako, yanayofanyika ni kama hisani tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wazo langu, naona jambo la haraka ni kwamba, hii Sera, itungiwe Sheria. Tumechangamkia sana pensheni ya wazee, kwa sababu, wote tunaishi na wazee, tunawahurumia, lakini nadhani vile vile tunajitengenezea mazingira kwa sababu na sisi tutakuwa wazee siku moja. Lakini, tumelizungumza sana suala la pensheni.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tu kwamba, *pension* sio muarobaini wa matatizo na ustawi wa hawa wazee. Tuna Mifuko kadhaa ya Pensheni, kuna Bima ya Afya, kuna Bima ya Serikali, Mfuko wa Serikali

*(LAPF), PPF, NSSF,* Mifuko yote hii wanufaika wanachangia pesa katika Mifuko hii na mwajiri pia anachangia katika Mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, Pensheni ya wazee, tofauti yake na hii Mifuko ni kwamba, hawa wanufaika hawatachangia katika huu Mfuko. Kwa maana kwamba, utaanza na *zero capital...*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Aaa, jamani!

**SPIKA:** Ya kwanza, Mheshimiwa.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni ya Wazee utategemea Bajeti ya Serikali, kwa asilimia mia moja. Ina maana bajeti yake itategemea pesa za walipa kodi mwaka hadi mwaka na huu Mfuko ukianza ni lazima uendelee. Ina maana kwamba, kwa mfano *OC,* kitu cha kwanza ni kutoa mshahara, halafu ndio mambo mengine yanakuja. Kwa Bajeti ya Serikali na wenyewe Mfuko wa Wazee itabidi iwe hivyo, hatuwezi tukaanza halafu mwaka kesho mseme hatuna pesa za kutosha, kwa hiyo, hatutawapa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tukumbuke kwamba, idadi ya Wazee itaongezeka mwaka hadi mwaka, magonjwa yanadhibitiwa, lakini vile vile mfumuko wa bei tunauona kwa hiyo, Serikali, iwe tayari kuongeza bajeti mwaka hadi mwaka. Tukitumia uzoefu wa nchi mbalimbali, pamoja na utafiti ambao tumefanya hapa

nchini, imebainika kwamba, pensheni kwa wazee, tukiwapa 16,800/= kwa mwezi, itapunguza umaskini kwa 58% kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, bajeti itakayohitajika ni shilingi bilioni 154 kwa mwaka. Tunahitaji kuwa na *data* ambayo ni madhubuti na ambayo tuta-*up date* kila wakati. Nashukuru kwamba, zoezi la kuwatambua wazee limeanza, lakini vitambulisho vya Taifa, nadhani vitasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwamba, Sheria itungwe haraka, lakini tutakapoitunga hii Sheria, ijumuishe pia na suala la Pensheni. Hatuwezi leo tukaletewa Sheria ya Wazee, halafu kesho ya Pensheni, nadhani tunahitaji *a Comprehensive Law,* ili iwe *one stop centre* kwa wazee, Sheria inayowahusu iwe katika Sheria moja.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kabla sijaanza kuchangia, kwa vile leo nitajikita sana kwenye hifadhi za jamii, naomba kutumia Kanuni ya 61, kutangaza maslahi kwamba, mimi mpaka sasa ninahesabiwa kwamba, ni mtumishi wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma; nipo likizo bila malipo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwaomba Waajiri, wawasilishe michango ya wanachama kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Wafanyakazi wamekuwa wakikatwa michango kwenye mishahara yao, lakini michango haiwasilishwi.

Mheshimiwa Spika, hii inaleta adha kwa Mtumishi, anapofikia wakati wa kustaafu. Kwa sababu, usipowasilisha michango, maana yake huwezi kulipwa kiinua mgongo chako. Kwa hiyo, nawaomba sana Waajiri watimize wajibu wao, maana Sheria, zinawataka wao ndio wawe wanapeleka michango ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nililokuwa nataka nilizungumze, naiomba sana Serikali, iutazame vizuri zaidi ya ilivyoutazama sasa mfumo wetu wa Hifadhi ya Jamii. Mfumo wetu wa Hifadhi ya Jamii, lazima uendane na mwenendo wa uchumi, lazima uendane na mazingira halisi ya Mtanzania wa sasa.

Mheshimiwa Spika, lazima Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, iongeze wigo kwa wanachama. Leo tunaizungumzia Hifadhi ya Jamii, inayowafaidisha Wanachama wa Tanzania 930,000 tu, leo hii. 6.2% ya watu milioni 22 ambao ndio nguvu kazi, wenye uwezo wa kufanya kazi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha. Tuna idadi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, mpaka sasa ni saba ukijumlisha na ule unaoitwa *CHF,* lakini *coverage* yake ni ndogo na hii inamaanisha nini? Maana yake ni kwamba, leo kijana anayeendesha Bodaboda, wenye

mradi wa Bodabo*da,* akipata ajali akaumia hataweza tena kuendelea na kazi ya kujitafutia kipato. Kama hakuwa mwanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, basi ndio anakuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifano iko mingi. Tuna watu wengi wanaofanya biashara zao binafsi, *informal sector* imekuwa, hawa wote hawajawa *covered* kwenye Hifadhi za Jamii kwa kiasi cha kuridhisha. Tuna watu wana ma-*saloon* makubwa, wanaajiri watu binafsi, hatujawaingiza kwenye huu mfumo; tuna *Contractors,* tuna mafundi cherehani wanaajiri watu, tuna mafundi *furnitures* wanaajiri watu, tuna maduka ya nguo, tuna *Super Markets* zimeajiri watu, hawa wote walipaswa kuingizwa kwenye huo Mfuko, kwenye Hifadhi ya Jamii ili na wao waweze kunufaika kwa sababu na wao wanaweza wakawa kwenye *middle income earning society.*

Mheshimiwa Spika, upo msemo unasema: *"We must make the market work for the poor."* Hiyo ndio rai yangu kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Lazima tuwasaidie, lazima tulisaidie Soko la Hifadhi ya Jamii lifanye kazi kwa watu maskini. Marekani leo ina 99.9% *coverage* yake katika Hifadhi ya Jamii, Malaysia ina 100% *coverage* yake katika Hifadhi ya Jamii; sisi tunashindwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wenzangu wamenituma nisiache kuzungumzia kero hii ya Fao la Kujitoa. Mimi nasema nini? Mimi nasema kutunga sheria ni jambo moja, maana sheria siyo Msaafu, inaweza ikabadilika. Lakini nilichojifunza mimi hapa ni kwamba

utekelezaji wa ile sheria uliharakishwa mno, wakati bado hatujatatua kero za msingi za wafanyakazi. Wafanyakazi wana kero nyingi sana siwezi kuzisema hapa kwa idadi maana muda wangu ni mchache na nina mengi ya kuzungumza lakini nina uhakika mengi yamekwishawafikia na nitayaleta vizuri kwa maandishi, nitawasilisha kwa Waziri ili aweze kuzifanyia kazi kero hizi. Mchakato mzima wa kuandaa sheria hii uliwashirikisha vipi wafanyakazi kwenye *field?* Tunaweza tukasema utatu lakini tunaojua kero ni sisi wenyewe wafanyakazi na nilidhani kwamba *SSRA* ndiyo yenye jukumu la kwenda kwa wafanyakazi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi Mwalimu wangu, Marehemu Prof. Chachage, nitaomba nitumie Kanuni, kunukuu maelezo yake, aliwahi kuniambia hivi. Kwa nini Tanzania ni maskini, ni kwa sababu watu wenye wadhifa kutopenda kusikiliza taasisi mbalimbali kama vile Vyama vya Wafanyakazi, wakulima wadogowadogo, wafanyakazi na wasomi na badala yake watawala, Mawaziri wawekezaji, waajiri, wataalam wa nje na ndani wanadhani kwamba wao ndiyo wanajua zaidi lipi la maana, lipi la kisasa na lipi linatakiwa kubadilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maneno haya ni machungu sana, yananichoma hata mimi kwa kuwa niko kwenye Serikali iliyopewa dhamana. Nina uhakika Serikali yangu inayafanya zaidi ya haya, ni *mess* tu lakini Serikali yangu haipo hivi. Ninaomba ili tuondoe tafsiri ya hii *mess*, *SSRA* nendeni *field*, nendeni mkaongee na wafanyakazi, timizeni wajibu wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo nilitaka niliseme kuhusu hifadhi ya jamii. Zamani historia ya Mifuko ya Jamii ilikuwa inawa-*cover* wafanyakazi waliokuwa wameajiriwa na mkoloni ambao ni wachache. Sasa leo hii haya tunayoyafanya na *coverage* nzima ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii bado ni ileile ya kikoloni. Naiomba Serikali iyafanyie kazi haya niliyoyaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa sekta ya kilimo wamenituma, wameniomba niwasemehe hivi, kima cha chini cha mshahara mpaka leo ni 65,000. Kiwango hiki ni kidogo sana, hakiwatoshi na mimi nasema ni kidogo lazima kiendane na hali halisi ya maisha yetu. Ninaomba kima hicho kiongezwe.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuweza kusimama na kuchangia hoja ambayo iko mezani kwetu. Nianze kusema naunga mkono hoja na pia nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nachukua fursa hii kupongeza taasisi zote zilizochini ya Wizara hii kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizojipangia mwaka 2011/2012. Mfano Wakala wa Huduma za Ajira kwa namna ambavyo imewaunganisha wanaotafuta ajira

na wenye nafasi za kuajiri, Shirika la Tija la Taifa kwa namna ambavyo wametoa mafunzo yenye tija zaidi ya asilimia 85, Shirika la Hifadhi la Jamii *(NSSF)* kwa namna ambavyo imetekeleza miradi, mfano mradi wa *megawatt* 150 katika eneo la Mkuranga, mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni ambako Mwandisi ameshapatikana na yupo *site* na pia ujenzi wa Chuo cha Nelson Mandela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati napongeza utekelezaji wa mipango ya mwaka 2011/2012, pia nijielekeze kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na naomba niwapongeze kwa kuona kwamba Ilani ya CCM inatekelezeka, lakini pia naomba niwaambie Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliwaahidi 2010 -2015, ni ya miaka mitano. Sasa hivi tuko kwenye mwaka wa pili, ni wazi kwamba yale ambayo tumeyaainisha yatatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kwa nafasi hii nipingane na maoni yao kwamba uwekezaji wa pesa za Mashirika ya Hifadhi ya Jamii ni uwekezaji ambao hauna tija. Kwanza nikianzia kwenye uwekezaji uliofanywa katika Chuo Kikuu cha *UDOM*. Kila Mtanzania anaona, Mataifa mbalimbali yanakuja yanatembelea kile chuo, kusema kwamba uwekezaji huu ni kufuja pesa za wafanyakazi wanaohifadhi fedha zao kwenye mashirika hayo siyo sahihi kwa sababu hata kwenye ripoti ya *CAG* hakuzungumza kwamba zile pesa zimetumika vibaya. Hoja kwamba Serikali haijalipa mpaka sasa hivi, Serikali ni mdaiwa kama kawaida lakini hata mikopo yenyewe ina *interest,* ni

wazi kwamba Serikali itakapolipa mikopo inalipa na hiyo *interest*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwa sababu Chuo cha *UDOM*, Wabunge hao au Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakitembelea sana, inatafuta pale wanachama sana, inakesha mara kwa mara kwenye chuo hicho na inajivunia kuwa na wanachama wapiganaji kupitia chuo hicho. Sasa mimi nashangaa tunavyozungumza kwamba eti uwekezaji huo hauna tija, wangepata sehemu gani ya kufanyia shughuli zao kama siyo chuo cha *UDOM*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, uwekezaji huo una tija na umefanywa vizuri kabisa na ninaomba niwaombe vijana wanaosoma *UDOM*, mwenye macho haambiwi tazama, wanaona kabisa ni nani mwenye nia ya dhati ya kuona vijana wetu wa Kitanzania wanapata elimu ya Chuo Kikuu, ni Serikali ya CCM ambayo imechukua michango ya wazazi wao kwa nia njema wamewekeza pale na wala haijasita kwamba itashindwa kulipa hiyo michango.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nisikitike kusema kwamba hata ujenzi wa ukumbi huu wa Bunge ambao inatupa fursa wote kusimama kuishauri Serikali, kuisimamia, eti kwamba sio matumizi sahihi ya mifuko hiyo. Lakini pia nisikitike hata lugha iliyotumika kwamba pesa zimechakachuliwa, pesa zimepotezwa, hii hoja hapa ni kwamba Serikali ifanye kila namna ilipe fedha ambazo zimetumika na mifuko hii kuwekeza kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, niseme fedha zimewekezwa sehemu sahihi na niombe *NSSF* na mashirika mengine ya hifadhi ya jamii yaweze kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali. Kwa mfano imewekeza kwenye jengo, jengo la Machinga pale Dar es Salaam, ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuwatafutia sehemu Wamachinga ambao tunadhani wanachangia uchumi wa Taifa hili kwa kuwa mara kwa mara walikuwa wanafanya shughuli zao katika maeneo ambayo siyo salama, barabarani na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hapa, hata viongozi wa siasa tutumie fursa hii kuwahamasisha vijana Wamachinga wanaofanya biashara katika maeneo siyo rasmi waende wakalitumie jengo lile lakini hoja si kwamba pesa zimewekezwa katika sehemu ambayo ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba taarifa ya *CAG* iliyowasilishwa Machi, 2012 inapowasilishwa taarifa pia inatoa fursa kwa wale wanaojua kutoa majibu na pia taarifa hizi zitajadiliwa katika Kamati zetu lakini kiuhukumu Serikali na Mashirika haya ya Hifadhi ya Jamii ambayo bado yana fursa kwa mujibu wa sheria ya kujibu hoja hizo na kuwasilisha kwenye Kamati na bado ndiyo Kamati zinataka zianze kukaa kujadili taarifa hiyo wala si sahihi na ni mapema mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nizungumzie tatizo la ukosefu wa ajira Tanzania. Kama ambavyo tunaona zaidi ya asilimia 34 ya vijana wenye umri wa miaka 15 mpaka 34 hawajapata ajira. Nipongeze

maeneo ambayo yamechangia ajira hizi kwa mfano shughuli za ujenzi zimechangia, miradi ya jamii *TASAF* lakini hapa niombe Wizara ijaribu kufuatilia Mifuko ya Maendeleo ya Vijana iliyopo kwenye Halmashauri zetu ambako inatakiwa watenge asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, lakini ni wazi kwamba sisi ambao tupo kwenye Halmashauri zile hazitengwi asilimia kumi ya pato la ndani ya Halmashauri, kinachofanyika ni Halmashauri kutenga tu kiasi ambacho inaona inafaa. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kama Halmashauri zetu zitatenga asilimia 10 ya mapato ya ndani na mifuko hiyo ikatumika kama ilivyokusudiwa kukopesha vijana kuchangia taasisi zao, ni wazi nayo inaweza ikachangia katika kupunguza tatizo la ajira hasa kwa vijana ambao wako katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wetu wa Pwani, Mama Mwantumu Mahiza alipokuja Pwani alilivalia njuga suala la ajira kwa kuanzisha kambi maarifa ya vijana iliyowakusanya vijana wote na sasa hivi vikundi vile takribani 30 vipo Mkoa mzima vimejielekeza kwenye shughuli mbalimbali za ujenzi, pia vimejielekeza kwenye shughuli mbalimbali za mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nipongeze taasisi hizi ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa mipango ambayo imejipangia mwaka 2012/2013, naomba utekelezaji wake ufanyike.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niiombe *NSSF* isijielekeze tu kwenye Mikoa ambayo pengine ina fursa nzuri ya kiuchumi, lakini yapo maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo. Mfano kwenye Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Tanga, naomba *NSSF* nao tuwaone kwa sababu na sisi tunao wafanyakazi wanachangia mifuko hiyo lakini hatujaona uwekezaji wowote ambao umefanyika katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia mashirika haya yapanue wigo kama alivyosema Mheshimiwa Zainab ya kuwafikia hata wafanyakazi walio katika sekta isiyo rasmi maana ni wengi na sisi tunaoishi nao vijiji wako tayari endapo watawafikia na wakafanya semina nyingi katika kuchangia katika mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini michango mbalimbali inayofanywa na mashirika haya au Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii itachochea katika kuongeza idadi ya ajira kwenye hiyo miradi. Watanzania wengi wanaajiriwa katika shughuli mbalimbali zilizofanywa na mifuko hiyo. Ni wazi kwamba tatizo linalosemwa la upungufu wa ajira kwa vijana wengi linaweza likapungua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nichangie kuhusu suala la Fao la Kujitoa. Naomba niseme kwamba Bunge kama Bunge lilitimiza wajibu wake, hamna namna ya kunyosheana vidole, wote tulikuwepo siku hiyo wakati tunajadili, hakuna *schedule of amendment* ambazo ziliwasilishwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Zainab, sheria inapopitishwa siyo Msaafu, kama Wabunge tunao wajibu pia kwa

mujibu wa kanuni kuwasilisha Muswada binafsi. Naomba tutumie fursa hiyo kama alivyofanya Mheshimiwa Jafo na wengine ili kifungu hicho kama kinalalamikiwa na watumishi wengi kiweze kubadilishwa na hatimaye iweze kuleta maslahi. Kusema kwamba kilibadilishwa, kwa sababu tulivyokuwa tunajadili Muswada huo hakuna ambaye alisema kwamba tunapitisha sheria hii kwa sababu tu ni kwa nia ya Chama cha Mapinduzi kichangishe fedha za uchaguzi, wala halikuwepo suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuweza kusimama hapa leo na kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kazi na Ajira. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, leo mimi ilikuwa mchango wangu hasa nauelekeza kwenye sekta binafsi. Wizara hii ina jukumu kubwa la wafanyakazi wa Serikalini na wafanyakazi wa sekta binafsi. Kuna vyombo mbalimbali ambavyo vimeundwa kwa ajili ya kuisaidia Wizara hii kwa shughuli za wafanyakazi mbalimbali kwa maslahi yao na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la kusikitisha katika sekta binafsi hasa nizungumzie kwenye mahoteli au kwenye magesti, kwa kweli huko bado Serikali hakujakuangalia vizuri na hasa hiki chombo chao sijui kama kipo lakini nasikia kuna chombo kinaitwa *TUICO*,

kwa kweli chombo hiki mimi nadhani kimelala usingizi mzito sana na sijui kama hakijazimia na kiko *ICU*.

Mheshimiwa Spika, kwenye mahoteli yetu, baadhi ya mahoteli kuna unyanyasaji mkubwa sana wa wafanyakazi, mishahara midogo, hawana mapumziko, likizo hawana, baya zaidi hata kama ikivunjika sahani, sahani mfanyakazi imemdondoka, wafanyakazi wote watakatwa mishahara yao shilingi 10,000, shilingi 5,000 inachangiwa sahani hiyo, shilingi ngapi hizo? Kwa kweli huo ni unyanyasaji mkubwa na dhuluma kubwa inatendeka katika vyombo hivi vya binafsi.

Mheshimiwa Spika, nije katika wafanyakazi wa majumbani, baadhi ya wafanyakazi kwa kweli wako katika utumwa mkubwa na haya yanawapata kutokana na unyonge wao. Wengi tuna wafanyakazi wa majumbani hapa, lakini kuna watu wengine wanawatumia wafanyakazi wa majumbani kana kwamba ni wanyama, hawana uhuru mzuri, kula akale *store* huko kama kwenye mabanda ya kuku akale hukohuko, hana uhuru wa kula kwenye *dining room*, hawezi kuchanganyika na watoto wa mwajiri wake, ni dhambi, ni najisi kwa kweli ni unyanyasaji mkubwa. Kama *TUICO* ipo basi imelala, imezimia. Mheshimiwa Waziri nakuomba uipatie dawa hii *TUICO* iweze kuamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfanyakazi wa majumbani hana uhuru wa kukaa kwenye sofa na kuangalia televisheni, huu ni unyanyasaji mkubwa na ni unyama, ni utumwa kabisa. Mimi nasema hili kwa mfano nilipata mfanyakazi mmoja mtu mzima tena lakini namwambia

akae pale kwenye kochi, naenda kwenye ukumbini pale namkuta kakaa chini. Namuuliza mbona hukai kwenye kochi? Anasema mimi sijazoea kukaa kwenye kochi. Huko anapotoka alikuwa hana uhuru wa kukaa kwenye kochi kabisakabisa, ni unyama kabisa, nasema hili kwa uchungu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikutana na mfanyakazi mmoja wa hoteli tulikuwa kwenye ziara ya Kamati Tabora, akanieleza unyanyasaji alioupata. Mtoto wake alikuwa anaumwa na bosi wake akaenda kumuona, mtoto yule alipata ule ugonjwa wa kuvimba kichwa, ghafla akapatiwa *transfer* ya kuja Muhimbili. Hana pesa ya kumleta Muhimbili kutoka Tabora akaona aende kwa mwajiri wake akaombe mkopo. Mfanyakazi huyu alinyimwa mkopo alichofanyiwa ni kupewa pesa zake zile alizofanyia kazi siku 14 na bahati mbaya mtoto yule alipomfikisha Muhimbili akafariki, kurudi kule anaambiwa kazi basi alishajazwa mtu mwingine. Ni lazima kiwepo hiki chombo na kiwe makini kutetea wafanyakazi kama hawa.

Mheshimiwa Spika, nije katika sekta hii ya ulinzi, kampuni hizi za ulinzi, hapa ndiyo pana kazi nzito haswa na hivi karibuni walionekana wanaashiria mgomo kwa ajili ya maslahi yao kuwa mabaya sana. Mfanyakazi wa ulinzi ameajiriwa zaidi ya miaka mitatu analipwa shilingi 80,000, ana watoto, ana familia nzito anataka kusomesha watoto, hana mapumziko kila siku yupo kazini, si Jumamosi, si Jumapili hana likizo lakini analipwa 80,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutuhitimishia hapa atueleze hiki chombo *TUICO* kinafanya kazi gani? Kama ndicho kama sicho sina hakika nacho atanisawazisha lakini nadhani ni *TUICO,* sijui inafanya kazi gani hawa watu wanadhalilika sana, wanapata tabu sana, wananyanyasika sana. Nimeshuhudia mimi mwenyewe mfanyakazi wa hoteli anapigwa na bosi wake, anapigwa kabisa kwa sababu aliambiwa umefanya jambo fulani akakanusha tu sijafanya kwa mara ya kwanza, alipoulizwa tena akasema sijafanya, basi bosi kakasirika kampiga, hilo lipo! Sasa hii *TUICO* inafanya kazi gani? Huu ni unyama!

Mheshimiwa Spika, mimi leo nazungumzia hapa tu, ni unyama, kwa kweli ni unyama lazima Serikali iwe makini na idhamirie kwa dhati kushughulikia suala hili. Kama hakuna chombo hiki basi kiundwe na kama kipo basi kiamshwe maana kimelala usingizi mzito.

Mheshimiwa Spika, leo sitaki kwenda mbali sana, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa kunipa nafasi, sasa namwita Mheshimiwa Mhagama!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini kwanza na mimi naomba kusajili *interest* yangu katika Kamati yangu kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na kwa kweli ni Kamati ambayo imechambua mapendekezo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwenye hoja yangu, naomba niseme ninaishukuru Serikali kupitia Mifuko ya Hifadhi za Jamii kuona umuhimu wa kuitumia hii mifuko kuleta maendeleo yenye tija kwa wananchi wa Tanzania. Tunajua kwamba ni kweli kabisa fedha hizi za wafanyakazi zinapowekwa kwenye mifuko ya jamii, ni mali ya wafanyakazi lakini ni mali ya wafanyakazi ambao ni Watanzania na ni Watanzania ambao pia wanapenda kuona kwamba wao na nchi yao maendeleo yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, nilitembelea nchi ya Malaysia, Malaysia Mifuko ya Hifadhi za Jamii ndiyo iliyotatua tatizo la umeme katika nchi ya Malaysia. Kwa hiyo, mimi sioni kama ni kitu kigeni eti sisi kwa Tanzania kwa mfano  kama kazi nzuri inayofanywa na Mifuko hii kwa mfano *NSSF* ilivyofanya kazi nzuri ya kuwekeza, sasa sisi kwenye nchi yetu tunaona kwamba eti inafanya kazi ambayo siyo kazi. Mimi naomba nianze kwa kulisema hilo na ninalisema hilo kwa sababu nimeshuhudia kwa macho yangu nilipokwenda Malaysia kazi nzuri iliyofanywa na Mifuko hii. Tena Mifuko hii ilikwenda mbali hata kuwezesha kilimo bora na cha kisasa katika nchi ya Malaysia. Sasa Watanzania wenzangu sijui tunataka nini, tayari tuna kitu mkononi lakini hatutaki kukitumia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana *NSSF* kama mfuko ambao uko ndani ya Kamati yangu. Mimi nimefanya ziara na Kamati yangu na tumeona miradi yenye tija inayohudumiwa na shirika hili.  Kwa kweli naomba niliseme kwa dhati ya moyo wangu na ninaamini katika ninachokisema na ninaomba wakaze

kamba, waendelee kuwasaidia Watanzania wahame huko waende hata katika miradi ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakubali kabisa kuna mjadala mkubwa kwa Watanzania karibu nchi nzima na hasa kwa wafanyakazi kuhusu Sheria mpya iliyofanyiwa marekebisho na kupewa madaraka *SSRA* kuona ni namna gani inaweza ikawasaidia wafanyakazi. Kwanza, ninakubali kabisa umuhimu wa kuanzisha *SSRA,* huyu mdhibiti atakayehakikisha Mifuko hii inafanya kazi kwa ulinganifu, hicho kilikuwa ni kitu cha muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini haya yanayokuja kujitokeza baada ya sheria mbalimbali kutungwa na kutaka kutumika, kama maeneo tunaona yana upungufu, hii si hoja ya kuendelea kusikitika bali ni hoja ya sisi Wabunge kuchukua nafasi yetu kwa mujibu wa Katiba na kuangalia ni nini kifanyike kwa maslahi ya Watanzania. Kwa hiyo, hapo wala hakuna hoja ya kusema kwamba hakuna mwenye dhamira ya dhati wala nini, wote tupo pamoja na nikushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa maamuzi yako na pia niishukuru sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuona namna ya kulitazama suala hili kwa manufaa ya wafanyakazi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye tatizo la ajira. Ripoti ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2011 inaonyesha takribani watu milioni 205 hawana kazi duniani lakini ripoti hiyo inasema takribani vijana milioni 77 hawana ajira duniani lakini ripoti hiyo inaendelea kusema kwamba vijana ambao hawana ajira ni wale

wenye wastani wa umri kati ya miaka 15-24. Shida kubwa katika nchi yetu ya Tanzania, idadi kubwa ya Watanzania ni idadi ya Watanzania ambao wana umri kuanzia miaka 24 kushuka chini, kwa hiyo unapata picha kwamba katika nchi yetu ya Tanzania tatizo la ajira ni kubwa sana na hasa kwa vijana. Sasa kama taarifa hizi zipo kwenye Ripoti ya Umoja wa Mataifa, ni lazima sisi tuitafsiri ripoti ile kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumza vigezo viwili katika tatizo hili kubwa la ajira. Kwanza kabisa nataka kuzungumzia suala la tatizo la ajira kwa maana ya ajira zilizo rasmi lakini tatizo la ajira kwa maana ya ajira zisizo rasmi. Shida tunayoipata ni kipindi cha mpito na mimi niseme ni ile *transition period*, tumewekeza, mifuko imewekeza kwenye vyuo vikuu vingi, *graduates* ni wengi sana katika nchi yetu ya Tanzania kwa sasa lakini ni nani anajua *graduates* wetu toka wanapomaliza chuo wanakwenda kufanya nini baada ya kusomeshwa na fedha ya Serikali ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, wakati tunapitisha bajeti ya fedha, tumeona tunakwenda kufungua miradi mikubwa sana ya kilimo, tena kilimo cha umwagiliaji na tumeyataja mabonde kama sita. Mimi hapo ndiyo nimeanza kujiuliza kwamba miradi mikubwa itakayosimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Fedha itatumia *billions of shillings* za Tanzania na hata kama ni za mkopo lakini tunasema kwamba watakaokwenda kuwekeza kwenye ile miradi ni wawekezaji kitu ambacho ni kizuri na sina matatizo nacho lakini sheria zetu za kazi zitawalindaje *graduates* wetu ili waweze

kuajiriwa kwenye miradi mikubwa tunayokwenda kuifungua kwa fedha za mwaka huu kwenye bajeti zetu? Hebu nijiulize, kule tunakoanza kwenda kufanya kilimo cha umwagiliaji yaani Malagalasi, atakapokuja huyo, hivi tumemwambia kwamba tuna *graduates* wetu wa kilimo kutoka *SUA* wako 200 na kabla ya kufungua uwekezaji wake achukue *graduates* wetu 50 waingie kwenye mradi huo? Mimi nadhani hayo ndiyo mambo ambayo tunatakiwa kujadili sasa, ile *connection* ya hii mipango mizuri tunayoifanya na tatizo la ajira kama nilivyosema la shilingi bilioni 77 wakiwa ni vijana na tumesema *problem* ni *transition period* wanapotoka kwenye vyuo vikuu na wengine kwenda kwenye ajira, tunafanya nini hapo? Ndiyo tatizo lipo!

Mheshimiwa Spika, nikimuuliza Waziri leo, hivi nani anayewajua vijana hawa waliomaliza, wamepata elimu katika nchi yetu, wako wapi, wanafanya nini, wanahitaji nini na wana uwezo gani wa kusaidia nchi hii? Kwa nini tumeendelea kuacha mlango wazi? Wawekezaji wanakuja, kweli kwa sera nzuri za nchi yetu lakini wanakuja na wafanyakazi wao, ina maana sisi hawa tunaowasomesha si bora? Mimi haya ndiyo maswali ambayo najiuliza na ninadhani hapo ndiyo Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ione, ninaiomba Serikali yangu katika mradi mikubwa yote tuliyoitengea fedha kwenye bajeti ya mwaka huu, ninaomba robo tatu ya watumishi kwenye miradi hiyo wawe ni vijana wa Kitanzania na wawe vijana wa Kitanzania kwenye kazi zenye staha waliosomeshwa kwa fedha ya Watanzania. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumeweza kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pensheni kwa wazee. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba suala la pensheni kwa wazee nimeliuliza ndani ya Bunge siyo chini ya mara sita na ninashukuru juzi nimeuliza tena na Waziri ametoa *commitment* ya Serikali kwamba mwakani wazee wataanza kulipwa pensheni.

Mheshimiwa Spika, asilimia 58% ya watoto yatima wanalelewa na wazee katika nchi ya Tanzania. Wazee hawa hawana nyumba, hawana mali yoyote na matokeo yake watoto yatima wanashindwa kuendelea na masomo, wanageuka kuwa watoto ombaomba na watoto wa mitaani na ni watoto ambao wanakuwa ni wazazi katika umri mdogo na tatizo la vifo vya akina mama na watoto linaendelea kuongezeka. Kwa hiyo, tuone kwamba kuwalipa pensheni wazee faida zake ni mara tatu au tano au kumi kuliko tunavyofikiri. Naomba sana Serikali ijitahidi kuchukua hatua ya kutoa pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, *CMA* yaani Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Nasikitika sana katika hali tuliyonayo sasa, migororo mahali pa kazi imekuwa ikienda mbele, *CMA* wanapewa bajeti ndogo sana, sasa tunategemea nini? Hebu tuongeze fedha *CMA* watusaidie kutatua migogoro ya wafanyakazi kabla haijashika kasi. Vyama vya Wafanyakazi na Serikali yetu kama *CMA* watapata nafasi ya kuelimishana huko basi migogoro ya wafanyakazi itapungua.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kuunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwanza nashukuru kwamba tumeweza kujadili vizuri na tukirudi jioni tutakuwa na watu watatu tu, ataanza Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Esther Bulaya na Mawaziri mtawasiliana namna mtakavyogawana muda uliobaki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.10 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunamalizia, niliwataja wafuatao wataendelea kuchangia, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Esther Bulaya na Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MBUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Kwa nini unashangaa kwa nguvu hivyo? Haya Mheshimiwa Martha Umbulla!

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia

uzima na kutuwezesha kufanya yote kwa kuwa katika yeye yote yawezekana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwapongeze na kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Manyara walioniwezesha kuwa Mbunge. Niko pamoja nao na nawatakia uchaguzi mwema unaoendelea ndani ya jumuiya yao.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Makongoro Mahanga, kwa umahiri na juhudi kubwa za kutekeleza majukumu yao katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa za kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika dhamira ya dhati ya kuleta maisha bora kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, hebu tujiulize kwa nini ajira na kazi ni muhimu kwa wanadamu? Pamoja na majibu mengine ni ili kujiletea maisha bora na maendeleo endelevu. Kwa hivyo, naomba sote tupige picha nyuma, tuangalie Serikali iliyoko madarakani imetimiza haya kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, vigezo muhimu ni elimu, afya na mengineyo. Katika elimu, hakuna atakayebisha tumepiga hatua kubwa ya kuboresha elimu yetu nchini. Hii hakuna atakayekataa kwamba Serikali

imefanya kazi kubwa katika elimu ya nchi yetu kwa watu wake.

Mheshimiwa Spika, katika afya, sote tunaelewa tumepigana na maradhi mbalimbali; Malaria, Ukimwi na kadhalika. Hakuna atakayebisha kuhusiana na hatua tuliyopiga katika sekta ya afya. Halikadhalika kwenye miundombinu, barabara zetu tunaziona. Masuala ya kuendeleza reli, bandari zetu, juhudi kubwa inayowekwa na Serikali tunaijua.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya kilimo, hatutarajii tena kuomba kutoka nje hata chakula cha njaa. Viwanda na biashara, masuala mengi ya kuongeza thamani katika bidhaa zetu kwanza za viwandani na za kilimo hatuna wasiwasi ni kipaumbele cha kitaifa. Sasa najiuliza hivi wanaobeza hatua zote hizi wana maana gani kwa sababu mwenzangu alisema mwenye macho haambiwi tazama, nadhani wanaobeza haya mambo wamuogope Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hii kubwa ya Serikali, nchi yetu bado inakabiliwa na umaskini uliokithiri kwa baadhi ya maeneo. Pamoja na sababu nyingine, umaskini huu unachangiwa kwa kiwango fulani kwa kutofanya kazi yenye tija na kukosekana kwa ajira. Tumeelezwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kuwa, watu wapatao milioni 205 duniani hawana ajira na hasa wale walioko katika umri wa nguvu kazi. Hii ni changamoto kubwa lakini bado Serikali yetu imeunda Wizara hii ya Ajira na Kazi ili kupambana na changamoto hii ya kuhakikisha

kwamba inaboresha ajira kwa wananchi wetu na kutafuta fursa za kufanya kazi kwa ajili ya wananchi wetu ambao hawako katika ajira.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amebainisha mikakati mbalimbali ya kuboresha viwango vya kazi, kazi zenye staha na kuwekeza katika kutafuta fursa za ajira. Hii ni hatua kubwa ya Serikali yetu ambayo sote hatuna budi kuipongeza. Lakini mimi naamini kwamba tukiunga mkono juhudi za Wizara hii hatimaye tunaweza tukaondokana na changamoto hii, tukapunguza umaskini unaokaikabili nchi yetu na hatimaye tukaendeleza wananchi wetu wakapata maisha bora.

Mheshimiwa Spika, hapa naiomba Wizara iweze kufikiria, pamoja na majukumu yake ya msingi ihakikishe inawajengea vijana wetu uwezo wangali wadogo, wakafanye kazi za kuzalisha mali kuliko kuwalea katika namna ambayo wanadhani kazi ni ile ya kufanya ofisini na kupata mshahara. Kutokana na mwelekeo wa kidunia sasa hivi, wananchi wanapaswa kuelewa kwamba kazi ya kujiajiri ndiyo ambayo italeta maisha ya maendeleo endelevu. Kwa hivyo, ninaiomba Wizara iweze kuangalia jukumu hili la kimsingi kabisa, watoto wawezeshwe kufanya kazi nyumbani, si kwamba wakitoka shuleni wahimizwe kusoma tu *tuition* na mambo mengine, bali wahimizwe kufanya kazi ndogondogo kama za kulima bustani au kufuga kuku. Hiyo itawajengea fikra ya kuweza kufanya kazi na kujiajiri katika maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, mengi ambayo nilitarajia niyazungumze, yamesemwa lakini naomba hapa nizungumzie migogoro katika sehemu za kazi au kwenye ajira. Nchi yetu hivi karibuni imekumbwa na migogoro na migomo katika ajira na sote tunaelewa kwamba mahali penye migogoro na migomo hakuna kupiga hatua mbele, zaidi sana tutapiga hatua kwenda nyuma. Mwaka jana bajeti ya Wizara hii ilikuwa shilingi bilioni 18.5 na naona mwaka huu wameomba bilioni 15.9 lakini ningependa fedha hizi za Serikali zitakapotolewa zisiende kufanya kazi nyingine ya kutatua migogoro na kusuluhisha migomo na kuweza kufidia zile hasara ambazo zimetokana na migomo kama vile ya kuchoma moto shule na vitu kama hivyo, bali ziende kufanya kazi ya Serikali ya kuweza kukamilisha mikakati ambayo tumejiwekea. Ndiyo maana hata naweza nikavilaumu sana vyombo vile ambavyo vinatumika kuhamasisha watu kugoma. Kwa mfano, vyama vile ambavyo vimeundwa sehemu za kazi kama Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kwa namna moja au nyingine vimeweza kuhamasisha migomo isiyo ya lazima katika nchi yetu. Kwa hivyo, nadhani ni kurudi nyuma na kuwaelekeza kwamba warudi katika misingi ya wajibu wao kama vyombo ambavyo vinapaswa kuleta hamasa na maelewano kati ya wafanyakazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tujiulize na hivyo vyama viweze kutafakari, je, wajibu wao ni kuhamasisha migomo na migogoro baina yao na Serikali? Je, kwa nini waelekeze athari ya migomo yao kwa wale wanaowategemea? Kwa sababu Daktari

anamtegemea mgonjwa na Mwalimu anamtegemea mwanafunzi la sivyo hana kazi ya maana, kwa nini wasiilenge Serikali moja kwa moja? Kwa sababu migomo na migogoro yao imeleta athari kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba vyombo hivi vitafakari majukumu yao ya msingi. Kwanza kabisa viweze kuangalia misingi ya kuanzishwa kwake na vijiulize vimewasaidiaje wanachama wao kuwajibika ipasavyo, kwa kuwa kuna baadhi ya Walimu ambao hawatimizi wajibu wao katika kazi na vilevile kuna malalamiko mengi ya wananchi kwamba Madaktari wengine hawafanyi kazi inavyotakiwa? Kwa hiyo, nilidhani jukumu la msingi la vyama hivi ni kuhakikisha wanachama wao wanawajibika ipasavyo badala ya kuhamasisha migogoro ambayo inasababisha athari isiyo ya lazima na hasa migomo ambayo haifuati sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya faida ya kuruhusu vyombo hivi kuhamasisha vurugu na kuleta majanga na hasara isiyo ya lazima kwa wananchi. Serikali yetu isiruhusu vyama hivi kuvuruga amani na utulivu tulionao katika nchi yetu. Madhara makubwa yaliyotokana na mgomo na mgogoro wa Madaktari sijajua Serikali itakavyofidia kwa sababu sijui atakayepaswa kufidia kama ni Serikali au ni vyombo hivi? Je, vijana wetu waliokosa masomo na haki yao ya msingi ya kupata elimu na hasa wale wanaotakiwa kufanya mtihani wa darasa la saba wataweza kufidiwa kwa kiwango gani? Nilikuwa nashauri hasara yoyote itakayotokana na mgomo usio halali na usiofuata

sheria, vyombo hivyo vilivyohamasisha vichukue jukumu la kulipa fidia kwa madhara yote ambayo yatakuwa yametokana na matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii nawapongeza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, umeishiwa muda.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Bulaya!

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo inagusa Watanzania wengi, lakini pia inagusa vijana wengi wa taifa hili ambao wamenituma nije niwawakilishe hapa Bungeni. Ukiwauliza vijana wa Tanzania kipaumbele chao cha kwanza ni nini, watakwambia ni ajira, cha pili watakwambia ajira na cha tatu watakwambia ajira, ajira, ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mama yangu ambaye namheshimu sana, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka pamoja na Mheshimiwa Makongoro Mahanga. Natambua jitihada zao ambazo wanazifanya mbali na Wizara yao kukabiliwa na changamoto nyingi. Wakati naingia

hapa Bungeni, wanawake wa mkoa Wa Mara wamesema nimfikishie salamu Mheshimiwa Waziri, wanatambua mchango wake na wamesikiliza hotuba yake na wana imani naye sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nianze kuchangia. Nitajielekeza kwenye mambo mawili au matatu ya msingi. Kwanza kabisa na mimi naungana na Wabunge wenzangu kuitaka Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii na hasa hicho kipengele ambacho kinamtaka mtu kuchukua fedha zake baada ya kufikisha miaka 55.

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki si rafiki kwa wafanyakazi wa Tanzania na hasa wengi ambao wanafanya kazi migodini ambao ni vijana wenzangu. Leo hii ukiniambia nitafikisha miaka 55 sijui maana ni kudra za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, kwa kweli kuna haja ya kufanya marekebisho kwenye hiki kipengele. Pia kipengele hiki hakimpi uhuru mfanyakazi pale ambapo anaamua kuachana na mfumo huo wa ajira kwenda kwenye mfumo mwingine kwani hawezi kupata mafao yake mpaka afikishe miaka 55. Nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba hilo halikubaliki na kuna haja ya kuleta marekebisho haraka na Bunge hili tuweze kutunga sheria kwa sababu sheria siyo Msaafu. Najua wote mnafahamu tuliitunga hapa sheria kuhusiana na jinsi gani tutaweza kuendesha mchakato huu wa Katiba mpya, lakini watu waliruhusiwa kuleta *amendment*. Nadhani kwa *speed* ileile na katika kifungu hiki ni hivyohivyo ambavyo tunapaswa kufanya marekebisho ili wafanyakazi wa Tanzania waendelee kufanya kazi kwa amani na

utulivu kwa sababu sasa hivi wengi sana wameingiwa na *shock*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuzungumzia suala zima la michango. Kumekuwa na malalamiko sana kwa wafanyakazi hasa ambao ajira zao ni za mkataba wa muda mfupi. Waajiri wamekuwa na tabia moja, wanamuajiri mtu kwa mkataba wa muda mfupi lakini wanamlazimisha kuendelea na mfumo wa pensheni. Tunajua kabisa mfumo wa pensheni una faida kubwa kwa mwajiriwa ambaye yuko katika ajira ya muda mrefu, lakini mfumo wa pensheni hauna faida kabisa na mtu ambaye anaajiriwa katika ajira ya mkataba na wengi ndiyo wako migodini, wengi ndiyo vijana wenzangu ambao wanakosa fursa za kuajiriwa, wako kwenye ajira za mkataba. Kwa hiyo, napenda hilo na lenyewe Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi wa kutosha. Waajiri wamekuwa wakitumia fursa ya kuwanyonya wafanyakazi ambao wako katika ajira za mikataba kwa kutumia kipengele hicho. Hili limekuwa likizungumziwa sanasana na wafanyakazi wengi wamekuwa wakililalamikia sana hasa ambao wako migodini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii kutokana na kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali. Ni jambo zuri sana na kati ya vitu ambavyo vimenifurahisha ni kuwekeza kwenye elimu hasa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM).* Hilo ni jambo zuri sana lakini kuna haja ya Serikali kulipa madeni ili fedha hizi ziweze kwenda kuwekezwa kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 800 na mifuko mbalimbali imechangia pale, lakini kwa masikitiko makubwa bado Serikali haijaanza kulipa deni. Tunatambua mchango wenu wa kuwekeza kwenye elimu, tunatambua mchango wa Mifuko hii ya Hifadhi ya kuwekeza katika sekta mbalimbali, lakini Serikali lazima ilipe madeni. Hii inachangia kuleta hofu kwa wanachama ambao wanachangia fedha zao kwenye hii Mifuko kwamba kuna uwezekano wa Mifuko ika-*collapse* kwa sababu fedha zinawekezwa lakini *speed* ya kurudisha imekuwa ndogo sana. Tunatambua *NSSF* inaidai pia hata Serikali katika ujenzi wa ukumbi wetu huu wa Bunge lakini pia Wizara ya Usalama wa Raia ambayo sasa hivi ni Wizara ya Mambo ya Ndani, ujenzi wa nyumba za Polisi tangu mwaka 2007 bado Serikali haijalipa. Tunajua pia kule Kiwira wanadai, wanadai maeneo mengi sana. Ni vyema hizi fedha zikarudishwa ili Mifuko hii iweze kwenda ku-*invest* katika maeneo mengine. Ni jambo la busara kuwekeza lakini pia vilevile ni muhimu zikalipwa ili wanachama waone kwamba fedha zao zipo na zinaendelea kufanya kazi na watakapozihitaji zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, ku-*invest* kwenye maeneo ambayo yanalipa kirahisi na lenyewe pia ni jambo zuri sana. Kuna uwekezaji umefanyika wa Machinga *Complex*, lakini pia hata Mheshimiwa Rais wakati anafungua Bunge letu alisema kuna haja ya kutanua huo uwekezaji kwa kujenga majengo mengine kwa ajili

ya kusaidia vijana kwenye kanda mbalimbali kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilizungumzia tatizo kubwa ambalo linaikabili nchi yetu la wimbi la wageni kuingia kwa wingi na kufanya kazi za wazawa. Hilo ni tatizo kubwa sana na mimi niliishatoa ushirikiano sana kwa mama yangu Mheshimiwa Kabaka kwa kumwambia kuhusiana na Kampuni ya Simu ya Zantel na hata kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Shamsi Nahodha na nilimpa nchi mpaka na majina. Kwa hiyo, napenda kupata ufafanuzi suala hili limefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia ripoti ya utekelezaji wa Serikali kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, imeonesha Wizara imefanya ukaguzi kwenye makampuni na viwanda 78 katika Mikoa mbalimbali ikiwemo ya Mara, Kilimanjaro, Arusha na Dar es Salaam. Sasa ningependa kujua wamegundua nini katika ukaguzi huo wa vibali vya kazi na wamechukua hatua gani kukabiliana na tatizo la wageni kuja kufanya kazi za Watanzania huku vijana wenzangu wakihangaika na tatizo la ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawaishii hapo tu, wamekuwa wakiingia kinyume na taratibu na hata kuwatesa Watanzania wenzetu. Hilo naomba Mheshimiwa Waziri alijibu kwa ufasaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri amezungumzia vijana kupata kazi za staha. Tumepitisha hapa Mkataba wa Vijana na

moja ya maazimio ni kuhakikisha nchi wanachama wanawasaidia vijana kufanya kazi za staha.

Mheshimiwa Spika, bado vijana wa Tanzania hawafanyi kazi za staha. Hii leo ukienda kwenye hoteli kazi yao kubwa ni kutandika vitanda, kufungua vizibo vya soda na kuosha vyombo lakini huwezi ukamkuta ni Meneja hata siku moja. Tofauti na wenzetu wa Kenya, mgeni akienda kuwekeza akitoka mzawa atachukua nafasi ya yule mgeni. Sasa kwa hapa kwetu naona tatizo hili lipo. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe vijana wa taifa hili wanaweza kunufaika na ajira za staha katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kujua hivi vituo vya kazi vinatoa mchango gani katika kumsaidia kijana wa Tanzania katika kupata ajira? Hizi *Labor Exchange Bureau* zipo lakini hatujui zinafanya kazi gani? Tunaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama zikiboreshwa zikaweza kutoa *training* kama ilivyo moja ya vigezo vya kazi ni kijana kuwa na uzoefu, hakuna sehemu yoyote ambayo kijana anaweza kupata uzoefu zaidi ya *field*, hilo wote tunajua. Sasa hivi vituo vikiboreshwa na kuwezeshwa vitasaidia kutoa *training* ili kuweza ku-*penetrate* kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, naomba na hili Waziri alifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atupe ripoti ya ziara zake kwenye kukagua vibali vya kazi na pia tunahitaji takwimu za kutosha, vijana wangapi ambao wamejiajiri wenyewe na kujiajiri wenyewe siyo mtaji wa viberiti 10, kuuza maji barabarani ambao hata

haumwezeshi kupata kima chini cha mshahara kwa mwezi. Kwa hiyo, napenda kupata takwimu sahihi za vijana ambao wamejiajiri wenyewe kwa mitaji ya kutosha na hilo napenda Mheshimiwa Waziri na lenyewe alitolee ufafanuzi sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Richard Ndassa!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi hii na mimi nichangie machache pamoja na kwamba mengi yamekwishasemwa.

Mheshimiwa Spika, lakini awali ya yote nitamke kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa sababu kazi nyingi zimefanywa. Lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri ya asubuhi ya utangulizi hasa alipozungumzia hii Mifuko kwa sababu Mifuko hii imepotoshwa, hata leo hapa asubuhi tumesikia wachangiaji wengi wanasema Mifuko hii haina maana lakini nawashukuru sana wenzangu wameizungumzia vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, Mifuko hii ina faida nyingi, ni vizuri sisi kama Wabunge kwa kweli tuwashukuru wanaosimamia Mifuko hii *NSSF, PPF* na Mifuko mingine

ili tuwape moyo kuliko kuwadhalilisha na kusema kwamba hawafai, Mifuko inatumika vibaya, tunakuwa hatuwatendei haki lakini na sisi wenyewe hatujitendei haki kwa sababu na sisi tumo humu ndani kwenye jumba hili ambalo matunda yake ni Mifuko ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kidogo naomba niwapongeze sana, siyo kidogo, niwapongeze sana Walimu wote nchini wale ambao hawakugoma. Sisemi niwalaani lakini nawasikitikia sanasana Walimu ambao waliogoma kwa sababu kwa kitendo hicho hawakuwatendea haki watoto wetu na watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba za Vyama na Sheria za Ajira na Mahusiano Kazini, Na.6 ya mwaka 2004 zimeainisha namna ya fedha za chama zitakavyotumika na zitakavyonufaisha wanachama wake. Mimi hoja yangu ya msingi hapa nataka niwaulize hasa Waziri, hii michango ya asilimia mbili kwa kila mshahara wa Mwalimu Tanzania nzima ni ya hiari au ni ya lazima? Matumizi yake nani anayaangalia? Nijiulize Mheshimiwa, hivi yule Mwalimu aliyeko Sumve, aliyeko Njombe, aliyeko Peramiho ananufaika vipi na hizi fedha?

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ambazo ninazo ni kwamba fedha hizo zinaishi Makao Makuu. Mfano, mwaka 2010, Chama cha Walimu Tanzania kilikusanya shilingi bilioni 16,491,000,000/= kikatumia shilingi bilioni 13.2 ambapo shilingi bilioni 7.8 zilitumika Makao Makuu pekee yake lakini Mikoani ambako ndiko kuna Walimu

wengi, kwenye Ofisi za Mikoa za Walimu zikapelekwa shilingi milioni 944 tu, ukigawa kwa Mikoa iliyokuwepo wakati huo kwa wale wanaojua mahesabu zaidi sitaki niwarahisishie, lakini Mheshimiwa Maige yupo pale anaweza kugawa, lakini Wilayani kati ya shilingi bilioni 13, Ofisi za Wilaya wakati ule zipo 104 walipeleka shilingi bilioni 2.6 gawa kwa Wilaya 104 utajua walipeleka ngapi? Najiuliza hivi shilingi bilioni zote hizi ni kwa nini zitumike Makao Makuu pekee yake, shilingi bilioni 7.8, kuna nini kama siyo watu hawa wanajilipa posho wao wenyewe na kuna maslahi mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tukijiuliza, lile jengo la *Mwalimu House*, lipo pale Ilala, kuna Benki imepanga pale, Wachina wamepanga pale, hizo fedha zake nani anaziratibu, nani anazitumia? Hivi tukiulizana humu ndani Waheshimiwa Wabunge kwenye Wilaya zetu ni wapi ambapo pana *SACCOs* kupitia hii michango ya asilimia mbili ya Walimu ambapo zinawanufaisha Walimu wetu? Kazi yao ni kusema Serikali iongeze mishahara ili wapate fedha nyingi zaidi ili waweze kuzitumia wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka 2011 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 20.2 na matumizi yalikuwa shilingi bilioni 15.7, kati ya fedha hizo, Makao Makuu yaliyopo Dar es Salaam yalitumia shilingi bilioni 8.4 kwa kazi gani sijui lakini kwenye Ofisi za Mikoa wakapeleka shilingi bilioni 1.2 tu, kwenye ofisi za Wilaya wakapeleka shilingi bilioni tatu, tugawe kwenye Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kipo kichekesho kingine ambacho itabidi tumwombe *CAG* labda aende akasaidie kukagua. Kwa sababu idadi ya Walimu na kwa sababu wanaingizwa bila kufuata utaratibu, Mfuko huu nao ni vizuri ukakaguliwa isije ikawa sehemu ya kichaka cha watu kujifichia kujipatia fedha na kunufaika, lakini ukienda kule ukimuuliza Mwalimu hebu niambie Mwalimu katika huu mchango wa asilimia mbili unaochanga, hivi wewe unanufaika nini? Tofauti na Mifuko mengine, ukichanga kwenye mifuko baada ya muda fulani miaka 55, miaka 60 unapata mafao yako lakini Mfuko huu, hivi kweli unamnufaisha namna gani Mwalimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Walimu wanatumika sana tu, Walimu wetu wanatumika, watu wamekaa wamejilundika kule wanajilipa posho, wanajilipa marupurupu kibao, nendeni mkahangaike halafu fedha sisi tuchukue tule. Kwa sababu ukiangalia shilingi bilioni saba (7) Makao Makuu, shilingi bilioni nane (8) Makao Makuu zinafanya nini kama siyo za kula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tukijiuliza lile jengo la Mwalimu *House,* mapato yake yote yanatokana na wapangaji waliopo humu ndani yanakwenda wapi? Tujiulize! Ndiyo maana nimesema ipo haja kubwa ukimchunguza mwenzako basi na wewe uchunguzwe. Kwa sababu hawa kila siku Serikali wanaisema ni mbaya kumbe wapo watu wanataka kujinufaisha wao wenyewe. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili hebu alisimamie kwa sababu sioni sababu na ninajua

na bahati nzuri nimetokea JUWATA, baada ya JUWATA ikaja *OTTU* na baadaye ikaja TUCTA... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taratibu za migomo zinajulikana lakini Serikali ina utaratibu wake, anakaa mwajiri hapa, *TUCTA* inakaa hapa, *ATE* inakaa hapa wanakaa wanazungumza kwa pamoja wanakubaliana. Wakishindana wanarudi wanakaa tena wanakwenda kuzungumza mpaka wanafikia muafaka lakini leo ukiwauliza hata huu mgomo wa Walimu sina uhakika kama *TUCTA* walishirikishwa kama Chama Shirikishi ambacho ndiyo Chama Kikuu cha Vyama vingine hivi kama 14. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Vyama hivi havijaanza leo, vina historia yake na migomo hii haijaanza leo ina historia yake lakini migomo siyo suluhisho ya ufumbuzi wa matatizo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namsihi sana Mheshimiwa Waziri vyombo vitatu hivi viwe na utaratibu wa kukaa kama ambavyo vilikuwa vinakaa zamani. Ulikuwa unaitwa utatu; Mwajiri, *ATE* na *TUCTA*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Serikali na Wizara chini ya uongozi

wa Mheshimiwa Waziri G. Kabaka, Naibu wake Mheshimiwa Makongoro, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, wakuu wa taasisi na watendaji kwa kazi wanazofanya ingawa ni katika hali ngumu ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nina mchango kwa hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ingawa tumerekebisha Sheria ya Hifadhi za Jamii mwezi Aprili 2012 lakini nataka ufafanuzi kuhusu formula zinazotumika kukokotoa mafao ya wastaafu nchini kwa sababu yaelekea kuna wastaafu waliopunjwa mafao yao kwa kutumia formula ya mwaka 1990s badala ya ile iliyorekebishwa 2001. Kwa msingi huo, yafaa Waziri katika majumuisho yake awaelimishe wafanyakazi wote nchini kuhusu hali hii kwani nina mfano wa Ndugu Mendile ambaye bado anahangaika kudai haki yake *PSPF,* naamini wako wengi wanaohangaika pia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu ajira kwa watu wenye ulemavu nchini. Pamoja na jitihada za Wizara kuratibu ukuzaji wa ajira kwa makundi yote nchini lakini kwa upande wa vijana wenye ulemavu waliosoma vyuo vikuu huwawia vigumu kupata ajira hata Serikalini au wakibahatika kupata ajira ni baada ya mateso sana. Sasa, je, Wizara inaweza kutoa maagizo kwa Tume ya Ajira na TaESA (*Tanzania Employment Service Agency*) ili taasisi hizi ziweke vigezo maalum vya kuwezesha wenye ulemavu kuweza kuajiriwa? Pia inaelekea wenye ulemavu wanaopatiwa mafunzo hayo wengi wao wanatoka

mijini tu. Sasa wale wa vijijini utaratibu ukoje kwa vile hizo *NGOs* na makampuni husika hawafikishi huduma hizo vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefafanua kuwa mwaka 2011, Mkutano Mkuu wa *ILO* ulipitisha mkataba namba 189 na pendekezo namba 201 kuhusu kazi za staha na haki za msingi kwa wafanyakazi wa majumbani na naamini Tanzania ilishiriki kikamilifu katika hili. Kwa msingi huo, nataka kufahamu ni lini mkataba huu utafikishwa Bungeni ili uridhiwe? Nashauri Wizara iharakishe suala hili kwa vile kwa kiasi kikubwa kumekuwa na malalamiko ya ukiukwaji wa haki toka kwa waajiri wa wafanyakazi hao wa majumbani.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kusikia kwamba Tanzania na Qatar zimefanya makubaliano ya Watanzania wenye sifa kwenda kufanya kazi katika nchi hiyo tajiri. Hata hivyo, naomba ufafanuzi kazi hizo ni katika sekta zipi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya wafanyakazi nchini, nashauri Wizara kushughulikia haraka kila migogoro hiyo inapotokea badala ya kusubiri kukomaa kwa vile athari za migogoro hiyo kitaifa ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kukubali kuleta marekebisho ya Sheria ya *SSRA* hapo Oktoba 2012, kutokana na malalamiko mengi yaliyojitokeza toka kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali nchini. Uamuzi huo ni wa kizalendo na ukomavu wa kiutendaji kwa Wizara. Hongera sana

Wizara haikupuuza malalamiko hayo na kusubiri mgogoro kupanuka.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja ingawa bajeti bado ni ndogo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa sekta binafsi na mashirika ya binafsi wamekuwa wanalalamikia mikataba mibovu isiyoangalia maslahi yao na haki zao kazini. Pamoja na Serikali kutangaza kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi hapa nchini, sekta binafsi wamekuwa wanajipangia kiasi cha kutoa mishahara wanayoona wao na siyo kufuata sheria na taratibu zilizopo. Hii leo wafanyakazi wengi wanalipwa kima cha chini shilingi 70,000 mpaka 100,000 kwa mwezi. Kumekuwepo na kutotendewa haki maeneo ya kazi na hata kunyanyaswa na waajiri wao. Mfanyakazi akiumia kazini anatelekezwa hospitali na baadaye anaachishwa kazi akiwa mgonjwa, anateseka yeye na familia yake na hana tena uwezo na nguvu za kufanya kazi. Tunaiomba Serikali kuweka taratibu na mikakati ya kuwabana waajiri wote wafuate sheria za nchi na kulipa mishahara inayotamkwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa kampuni ya *Security* iliyopo pale uwanja wa ndege wa Dar es salaam wanafanya kazi masaa kumi na mbili. Kuna *shift* za usiku na mchana. Wale wa asubuhi wanatoka

makwao saa 9.00 usiku wanatumia *taxi* au pikipiki, hawapatiwi chakula wala maji ya kunywa wanalipwa 70,000, huu si unyonyaji?

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni michango ya wafanyakazi hivyo ni mifuko ya wanachama. Wanachama wa mifuko hii wanashirikishwaje kwenye matumizi ya mifuko hii? Ni utaratibu gani uliowekwa na Serikali kuhakikisha taarifa zote zinazohusu mipango na matumizi zinawafikia wanachama wote?

Mheshimiwa Spika, mifuko hii imekuwa inatumika kuwekeza kwenye miradi mbalimbali mikubwa na miradi mingine ni ya kuzalisha pesa. Ni kwa utaratibu upi wanachama wananufaika na uwekezaji huo? Kuna utaratibu gani wa mifuko hii kukopesha wanachama kwa riba nafuu ili waweze kujikwamua na hali ngumu ya maisha kwa kuanzisha miradi ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, kuna mfuko wa kujenga *skills* za wafanyakazi (*skills development levy*) unaochangiwa na mashirika na makampuni yote ya sekta binafsi. Makampuni na mashirika yote yanatoa kisheria kiasi cha asilimia 6% kila mwezi kuchangia mfuko huu. Lengo kubwa ni kujengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia stadi za kazi na ujuzi kazini na hivyo waweze kufanya kazi kwa ufanisi. Kiasi cha asilimia 2% zinakwenda kuendeleza vyuo vya *VETA,* tungependa kujua kiasi cha 4% fedha zilizobaki zinatumika wapi na kuwa ajili ya nini?

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema siku hii ya leo ambaye ndiye iliyeniwezesha kufika hapa katika Bunge lako Tukufu na kupata fursa hii ya kuchangia ijapokuwa kwa uchache kupitia njia hii ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira kwa kuwasilisha vyema hotuba yake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kwa kuangalia zaidi ajira kwenye kundi la vijana wetu ambapo kila siku tatizo la ajira kwa vijana linazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kila kunapopambazuka vijana wengi waliomaliza darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita hadi chuo kikuu huwa wapo mitaani wanazurura kwa kukosa kazi za kufanya huku wakisubiri kuajiriwa na taasisi mbalimbali au Serikali. Wahitimu hawa wanaomaliza vyuo na shule za sekondari hubaki mitaani wakihangaika kutafuta ajira Serikalini kwa miaka nenda miaka rudi bila kufanikiwa. Sio kwamba hawana uelewa juu ya kubuni vitu mbalimbali vya kufanya hapana vijana hawa wanauelewa ila wanapuuzia na kudhani kuwa hawana hadhi ya kufanya vitu hivyo mfano kama vile kulima bustani za mbogamboga, kuuza nyanya, ndizi, ufugaji wa kuku na vitu vingine ambavyo vipo maeneo wanayoishi ambavyo vingeweza kuwaingizia kipato. Tafsiri ambayo imeganda miongoni mwa vijana wengi ni kwamba wanadhani ukisoma sana basi huwezi kulima

wala kufanya biashara ndogondogo ambazo zingeweza kuwapatia kipato wakati ambapo wanasubiri ajira zao. Dhana hii potofu ndiyo inawapelekea vijana wengi kujiingiza katika makundi mabaya ya ujambazi na utapeli na hatimaye wengi wao wakiishia gerezani wakiwa na elimu yao vichwani.

Mheshimiwa Spika, tatizo linaloonekana hapa ni kutokujitambua kwa vijana wetu kuwa wao ndio Taifa la kesho ambalo linahitajika katika kujenga Taifa lenye nguvu. Taifa lenye nguvu linahitaji vijana ambao wapo tayari kupambana ili waweze kuikomboa nchi yao hususan katika hali ya umakini uliotawala na kuathiri maisha ya wengi lakini vijana wengi wanaohitimu masomo yao hawajitambui kuwa wao ni akina nani katika nchi yao na laiti kama wangejitambua wangekuwa na uthubutu wa kufanya mabadiliko. Leo hii ukimwambia kijana aliyemaliza kidato cha sita aanzishe hata mradi wa kulima bustani ya mbogamboga katika eneo lake analoishi ataona kuwa unamdharau akidhani kuwa yeye hana hadhi ya kufanya kazi hiyo kumbe kupitia kazi hiyo ingeweza kumpatia kipato cha kujikimu katika hali yake ya ujana badala ya kutegemea familia. Nchi yetu ya Tanzania tumejaliwa kuwa na vyanzo vingi sana ambavyo kama hawa wahitimu wa elimu mbalimbali wangekuwa na uthubutu wa kujaribu kuvitumia vyanzo hivyo, kilio cha tatizo la ajira lisingesikika kwani kila mhitimu angekuwa anajishughulisha na kazi yake akisubiri kuajiriwa na Serikali au taasisi binafsi ambayo anaihitaji lakini kwa wakati wote ambao anasubiri kuajiriwa angekuwa na mradi wake badala ya kukaa bila kazi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango wangu katika maeneo machache nilyochagua kuyawekea mkazo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuungana na wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi kuwatakia Waislam swaumu njema.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nijielekeze katika kutoa mchango wangu katika maneno machache ambayo nimeyachagua kuyatilia mkazo. Pongezi kwa Waziri na timu yote ya Wizara ya Kazi na Ajira, kwa kuandaa maelezo ya bajeti yenye ufafanuzi wa kina. Naunga mkono hoja na bajeti asilimia mia kwa mia kwa sababu katika kipindi cha 2012/2013 taasisi zilizo chini ya Wizara hii zimefanya kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani. Ujenzi wa Chuo cha Dodoma ni matunda ya mfuko wetu wa *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, ushauri kuhusu kuongeza ajira. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ya kuongeza ajira hapa nchini, bado Serikali inayo kazi kubwa sana ya kufanya jitihada za makusudi kutunga sheria zitakazopiga marufuku makandarasi wakubwa ku-*supply* kila kitu kwenye *project* zao. Kwa mfano matofali, mchanga, mbao, nondo na kadhalika. Waachiwe wajasiriamali wadogowadogo wanawake

na vijana ili waweze kujiajiri wenyewe na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ajira kupitia viwanda. Kwa kuwa sekta ya kilimo ndio inayotoa ajira kwa watu wengi hasa kwa wanawake na vijana hapa nchini, napenda kuishauri Serikali ihamasishe Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwekeze katika kujenga viwanda vya kusindika mazao vya korosho, pamba na mazao ya chakula na kuzalisha *grey cloth*.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha nguvu kazi ya Taifa. Pamoja na jitihada za Serikali za kuwahimiza watu wapende kuifanya kazi kwa bidii na maarifa, bado Watanzania walio wengi hawafanyi kazi kwa bidii na maarifa. Naishauri Serikali iandae mkakati maalum utakaowezesha watu kufanya kazi, mifano ipo mingi. Wakati nchi yetu inakabiliwa na misukosuko mingi ya kuyumba kwa uchumi tulianzisha Kilimo cha Kufa na Kupona, kila mtu alilima na chakula kilipatikana. Mheshimiwa Hayati Moringe Sokoine alituletea Nguvukazi, kila mtu alifanya kazi hasa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi hapa nchini, naishauri Serikali iendelee kuboresha zaidi mazingira ya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na maslahi yao hasa wafanyakazi wa kada ya mwanzo na ya kati.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* kuwekeza katika maeneo yalio nyuma. Naipongeza *NSSF* kuwekeza miradi mikubwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwa ni utekelezaji kwa ahadi yake hapa Bungeni kwa kujenga daraja la Kigamboni, kukopesha wanachama kupitia SACCOS na ujenzi wa Chuo cha Sayansi cha Nelson Mandela baada ya *UDOM* na kufungua ofisi katika Mikoa mipya ya Njombe na Geita. Naomba Waziri atakapokuwa akifanya majumuisho anipe majibu ya kuridhisha, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza katika Mikoa iliyoko nyuma kwa maendeleo mfano Lindi, Mara, Kagera, Singida na Tabora? Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga ofisi za *NSSF* katika Mikoa ya Katavi na Simiyu?

Mheshimiwa Spika, Waziri anipatie majibu na Watanzania waishio vijijini wasikie, je, Serikali ina mpango gani wa kupanua wigo wa hifadhi ya jamii katika sekta isiyo rasmi na sasa vijijini? Je, Shirika la *NSSF* lina mpango gani kutekeleza jukumu hili?

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira mbaya ya watoto. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali na asasi mbalimbali za kijamii ikiwemo na UWT bado tatizo la ajira mbaya za watoto ni kubwa. Naomba Serikali iweke mkakati wa kuzuia ajira mbaya kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE.ANNA MARYSTELLA J. MALLACK:** Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya ajira ya watoto na mazingira hatarishi ya kazi. Pamoja na Serikali kupitia Wizara yake

kuratibu juhudi mbalimbali za kukomesha utumikishwaji na ajira mbaya ya mtoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Serikali za Mitaa, naipongeza Wizara kwa hatua hii ya kuhakikisha watoto wanaokombolewa katika unyanyasaji huu na udhalilishwaji wa watoto kwa kuwapatia mafunzo ya fani mbalimbali ikiwemo elimu ya msingi watoto 8,402, elimu ya MEMKWA watoto 1,428 na elimu ya ufundi watoto 12,413. Pamoja na mpango huu, bado naiomba Serikali kupitia Wizara iongeze juhudi kwani katika Taifa letu bado kuna wimbi kubwa la watoto wanaozagaa hovyo na kuombaomba, kulala hovyo vichochoroni, kuokoteza majalalani na kwa watoto wa kike kubakwa hovyo hasa nyakati za usiku na kuwasababishia magonjwa ya maambukizi na mimba za utotoni na kuzaa watoto wasio na baba wa kuwatunza. Naiomba Wizara kuendelea kuwabaini watoto hawa kwa kufanya ukaguzi sehemu mbalimbali kama mashamba ya tumbaku, kahawa, chai, mkonge, korosho na kadhalika. Pia katika vituo vya mabasi kwa ajili ya ubebaji mizigo, migodini na *station* za treni. Watoto bado wanatumikishwa sana sehemu kama hizi mpaka sasa, ni hatari.

Mheshimiwa Spika, hata hapa Dodoma ukitembea usiku utakuta watoto wamelala mbele ya maduka ya wafanyabiashara wakiwa wametandika mifuko ya simenti. Serikali iwakamate na kuwahoji endapo wana mzazi hata moja au mlezi ili walezi wao au mzazi hata mmoja wahojiwe ni kwa nini watoto wanazagaa hovyo na kuajiriwa katika ajira hatarishi?

Mheshimiwa Spika, ajira kwa watu wenye ulemavu, pamoja na Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 inayosisitiza kukuza usawa wa fursa za ajira na mapato kwa makundi yote wakiwamo walemavu, Wizara ijaribu kushauri Wizara nyingine kama Wizara ya Afya wanapojenga majengo kwa ajili ya kutolea huduma za afya walenge na makundi haya ya walemavu kwani mlemavu anapojengewa ghorofa kwenda kupata matibabu, je, huko ni kuzingatia usawa?

Mheshimiwa Spika, mafao ya wazee. Serikali ingeboresha mafao ya wazee kwani wazee ni hazina, kundi bila wazee ni sawa na kukosa kwani wazee wetu ni washauri wetu wakubwa. Naiomba Serikali kuimarisha Sera ya Wazee kama vile matibabu bure. Wasinyanyaswe kama ilivyo sasa, ukosefu wa dawa, vipimo na kadhalika. Ni aibu kwa Taifa na ni laana kutokana na manung'uniko yao. Naomba Serikali inijibu kupitia Waziri wa Wizara hii, je, kwa nini Serikali hii isianzishe ajira kwa wazee kwa kuwatengea miradi ya wazee kila Mkoa na Wilaya zake ili kuwakwamua na maisha magumu waliyonayo?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kabaka, Naibu Waziri Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kuwasilisha hotuba hii inayoonyesha hali ya kazi na ajira nchini, changamoto

na vipaumbele vya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa ajira kwa vijana. Ukosefu wa ajira hasa kwa vijana umeendelea kuwa changamoto kubwa sana katika nchi yetu. Ninatambua kazi na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kukuza ajira nchini na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008. Tatizo la ukosefu wa ajira, kwa kiasi kikubwa linatokana na ukosefu wa taarifa za ajira na pia uelewa mdogo wa vijana juu ya fursa za ajira zilizopo ambazo si za kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa Wizara kuhakikisha kuwa kuna mfumo bora wa kuhakikisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za ajira kwa vijana katika Mikoa na Wilaya zote hapa nchini. Pia ni lazima Wizara iwe na mikakati na mipango ya kuwajengea uwezo vijana ili waweze kujiajiri na au kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kwa ufanisi. Je, Wizara ina mipango na mikakati gani mahsusi ya kutatua changamoto hizi?

Mheshimiwa Spika, ajira kwa watoto. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (*Tanzania Employment and Labour Relations Act* 2004) inazuia ajira kwa watoto chini ya umri wa miaka 14. Hata hivyo, bado watoto wengi wa chini ya umri huu wamekuwa wakitumikishwa katika kazi mbalimbali ambazo zinaweza kuleta madhara kwa afya zao, ukuaji wao na pia kuwanyima fursa za kwenda shule.

Mheshimiwa Spika, nipatiwe majibu ni watoto wangapi wameshatambuliwa kuwa wapo katika ajira mbaya, ni wangapi wamefikiwa au wamepatiwa msaada na Wizara na hivyo kurudishwa shuleni? Je, Wizara inatoa kauli gani juu ya tatizo lililoko katika miji mikubwa kama Dar es Salaam ambapo wazazi na walezi wamekuwa wanawatumia watoto wadogo kuomba (ili wazazi na walezi hao wajipatie kipato) badala ya kuwaacha watoto hawa waende shule?

Mheshimiwa Spika, hali hii ya wazazi kutumia watoto kuomba ni ajira mbaya kwa watoto hivyo Wizara hii inajukumu la kushirikiana na Wizara nyingine kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ili kupunguza na hata kutokomeza kabisa tatizo hili. Je, Wizara inatoa kauli gani juu ya hili? Ni kwa nini wasiwakamate wazazi na walezi wanaotumia watoto kuomba na kuwafikisha katika vyombo vya sheria?

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya njema. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Waziri kwa kuchapakazi na kwa hotuba nzuri, vilevile nampongeza Naibu Waziri kwa ufanisi wa kazi zake.

Mheshimiwa Spika, naanza mchango wangu kwa kuzungumzia vibali vya ajira ya wageni. Utaratibu wa kutoa vibali vya ajira kwa wageni vimekuwa vikitolewa holela na kupelekea kuwepo wageni wengi ambao wanafanya kazi ambazo Watanzania wana uwezo wa kuzifanya. Athari ya jambo hili ni kuwanyima

Watanzania wazawa ajira na wengi kubakia wachuuzi. Naomba utaratibu huu uangaliwe kwa makini sana kwa maslahi ya Taifa. Kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya wafanye Watanzania. Katika hili, wapo wageni ambao wanaomba vibali kwa kazi maalum (ya kitaalamu) lakini utamkuta anafanya biashara za mkononi sawasawa na machinga.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia ajira za wageni hasa mahoteli ya kitalii, madukani na makampuni, katika sehemu hizi ambazo nimezitaja inatia wasiwasi kwa sababu utakuta wanachukua ndugu zao, wajomba zao kutoka nje na sijui vibali kama hivi wanavipata wapi, vya kuchukuana na kuajiri kwa ukoo? Kwa mfumo huu, inatia wasiwasi wa kupata vibali kwa rushwa. Naomba Serikali iangalie vyema utaratibu huu wa utoaji vibali. Vilevile ukiangalia makampuni ya ujenzi wa barabara hasa wa Kichina, wanachukuana wenyewe yaani ndugu zao ndio wanaofanya kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya. Ushauri wangu, makampuni yakiingia Tanzania wao wawe wasimamizi wa shughuli muhimu. Shughuli zote ambazo si za kitaalam basi waajiriwe Watanzania na zile za kitaalam ambazo wapo Watanzania wanao utalaam basi ni lazima wapewe Watanzania na kusiwe na ulazima wa kuajiri watu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimshukuru Mungu kwa upendo wake kwangu kwa kunilinda hadi kuifikia siku hii. Pia

napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri ikiwa ni pamoja na jopo lake linalomsaidia katika kufanikisha azma ya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, katika Maandiko Matakatifu ya Mungu, katika Biblia yanasema, ‘asiyefanya kazi na asile’. Maneno haya yanaonyesha umuhimu wa kazi iwe kazi za maofisini, mashambani, viwandani na kadhalika ili mradi kazi hiyo ilete manufaa kwa mtendaji. Kuna kazi za kuajiriwa na za kujiajiri, kwa zile kazi za kuajiriwa mwajiri anatakiwa ahakikishe kwamba wafanyakazi wake anawapa mambo yote ya lazima. Mambo hayo ni pamoja na haki, maslahi stahiki, heshima na kadhalika. Waajiri wakiwa wanawajali wafanyakazi wao ipasavyo, wafanyakazi watafanya kazi kwa moyo na kwa juhudi maana watakuwa wanaipenda kinyume cha hayo hakuna maelewano na hatima yake ni kutokea kwa mawimbi ya migomo katika sehemu za kazi. Tumeshuhudia migomo mbalimbali kama vile ya wanafunzi wa vyuo vikuu, Madaktari, Walimu na kadhalika. Migomo iliyo mingi huwa ni kwa upande wa maslahi. Ni juu ya waajiri kukaa na wafanyakazi wao na kupatana nao mara matatizo au dalili zinapoonekana kuliko kungoja mambo yaharibike.

Mheshimiwa Spika, inafahamika wazi katika nchi zote duniani waajiriwa ni wachache ukilinganisha na wanaojiajiri. Naiomba Serikali iwaangalie kwa namna ya pekee ili nao waweze kujipatia vipato ili wajikwamue kiuchumi ili waweze kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Wazee. Kwanza niwazungumzie wazee wastaafu. Kwa kweli wazee hawa Serikali imewaweka nyuma wakati hawa walifanya kazi nzuri Serikalini lakini baada ya kustaafu hawafikiriwi vizuri kwa kuwashukuru kwa kazi njema walizozifanya. Kumekuwa na malalamiko mengi juu ya *pension* wanazopata kulingana na ugumu wa maisha na hali ya bei zinazopanda kila kukicha. Kile kima cha shilingi 20,000 kwa mwezi hakitoshi kabisa. Kulikuwa na taarifa za kuongezwa kiwango hicho kwa kipindi kirefu sasa bila kufikia utekelezaji. Naiomba Serikali iwafikirie vilivyo vilevile wazee kwa ujumla iwatazame kwa macho ya huruma pale iliposema watatibiwa bure hadi leo bado ni kitendawili. Tukumbuke ya kwamba wazee ni dawa na kwamba wana mchango mkubwa katika nchi.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Msumbiji ambako wamepata uhuru kwa msaada wa Serikali yetu yaani nyuma yetu na karibuni wao wanawajali wazee kwa kuwapa posho. Naiomba Serikali itimize ahadi yake kwa wazee.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana na kigezo cha uzoefu. Nashauri kigezo cha uzoefu wa zaidi ya miaka 5 - 10 kisizingatiwe katika kuwapa ajira vijana. Hiki kigezo cha uzoefu kinawakosesha ajira vijana wa Kitanzania. Kigezo hicho kiondolewe ili wapate kazi *then* wapate hiyo *experience*. Lakini kwa kazi zenye kuhitaji ujuzi maalum, uwepo utaratibu wa kutoa mafunzo hata ya miezi mitatu baada ya kuwaajiri vijana, mafunzo yatolewe

ndani ya miezi mitatu ile ya *probation months,* akifuzu vizuri aendelee na kazi.

Mheshimiwa Spika, ili vijana wengi waweze kujiajiri, Serikali ihamasishe vijana wasomi wa kada tofautitofauti kwa mfano Wanasheria, Mainjinia na kadhalika kujiunga katika makundi *then* wapewe mikopo ya kujiajiri kwa kuanzisha *firms* zao. Hii itasaidia kupunguza utegemezi wa kuajiriwa. Wataweza kujitegemea kwa ajira. Serikali iniambie inalichukuliaje suala hilo?

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ikiwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwekeza kwenye majengo ya kukodisha ya kibiashara, Watanzania wapewe faida inayotokana na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipe pesa zilizotumika kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama mikopo ilipwe haraka mfano fedha zilizojenga Chuo Kikuu cha Dodoma ili mifuko iwe na fedha za kulipa mafao kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, nashauri mifuko yote inayojenga nyumba itoe elimu ya kutosha kwa wanachama wake ili waelewe jinsi gani wanaweza kufaidika katika mikopo na ununuzi wa nyumba hizo ili wawe wa kwanza kufaidika na mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, usalama mahali pa kazi. Serikali iangalie au isimamie uwepo wa vifaa vya usalama kama *fire extinguisher,* milango ya dharura, lazima

iwepo katika ofisi za Serikali lakini pia ofisi za *private*. Vifaa vikaguliwe mara kwa mara kama ni vizima. Pia maeneo ya *workshops* na ujenzi wapewe vifaa stahili vya kuvaa mfano *helmet, boots, gloves* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kazi kwa watu wenye ulemavu. Mazingira ya kazi kwa watu wenye ulemavu bado si rafiki. Ofisi nyingi tukianzia na jengo la utawala la Bunge letu na hata jengo la Ukumbi wa Msekwa, sio majengo yaliyo rafiki kwa wafanyakazi na Wabunge wenye ulemavu. Iletwe sheria itakayosaidia kujali watu wenye ulemavu ili ijali mazingira yao ya kazi ili wasijione wanatengwa kwa maana ya miundombinu iliyopo katika ofisi nyingi zilizopo Tanzania, nao wana haki.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na mpango wa kazi, naomba taasisi za umma zilizo chini ya Wizara zizingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA). Kwa kuzingatia aya ya 70 juu ya malengo ya kufanya ukaguzi wa kawaida na maalum kuhusu usalama mahali pa kazi, naomba katika orodha ya maeneo ya kufanyiwa ukaguzi tajwa kwa mwaka 2012/2013 liwepo pia Jimbo la Ubungo Manispaa ya Kinondoni hususan kwenye viwanda vya kufua chuma (*steel mill)* vilivyopo Mabibo na Kigogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania, *(TaESA),* aya ya 71, kuwaunganisha

watafuta kazi na waajiri na kufanya utafiti katika nyanja za upatikanaji wa ajira. *TaESA* iweke mfumo wa kuwaunganisha watafuta kazi katika Jiji la Dar es Salaam na fursa za ajira katika zabuni na kandarasi za mikataba mikubwa ya ujenzi na huduma. Aidha *TaESA* ifanye utafiti maalum kuhusu upatikanaji wa fursa za ajira katika mikataba ya ujenzi na huduma ambayo ina mfumo tofauti na matangazo yanayotolewa kwa ajira za kudumu kwenye sekta binafsi na sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*, aya ya 72, katika mwaka wa fedha 2011/2012 niliomba maelezo kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali ya Apollo unaofanyika katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hivyo katika mwaka wa fedha 2012/2013, *NSSF* na vyombo vingine vya Serikali vihusishe wadau ili kuwa na uelewa na mwelekeo wa pamoja kuanzia katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Jengo la Maadili Dar es Salaam, *NSSF* ieleze iwapo mazungumzo ya ujenzi huo yanahusu kiwanja ambacho kwa sasa kina ofisi ya Sekretariati ya Maadili ya Umma. Kama ni kiwanja hicho, Serikali iingilie kati kuwezesha mgogoro kwenye kiwanja hicho unaoihusisha pia kampuni ya Uwakili ya Mkono umalizwe kwa mamlaka ya Rais na Waziri wa Ardhi ili Sekretarieti ya Umma ikiendeleza kiwanja husika kwa ubia na vyombo vingine vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Tija la Taifa *(NIP)*, aya ya 73, katika kuendesha mafunzo na

huduma za ushauri katika sekta ya umma, naomba katika mwaka wa fedha 2012/2013, *NIP* iingize pia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika orodha ya walengwa. Hii ni kwa sababu, Halmashauri ina vitega uchumi vingi mathalani Shirika la Maendeleo Dar es Salaam *(DDC),* Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA), Machinga Compex,* Shirika la Masoko Kariakoo na hisa katika vitega uchumi vingine lakini hakuna tija wala faida katika vitega uchumi husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)*, aya ya 74, naomba Mamlaka itoe tangazo la kutengua taarifa yake kwa umma ya kusitisha Fao la Kujitoa. Aidha, Wizara ieleze wazi vifungu vingine vya sheria vya kabla ya tarehe 13 April 2012 vilivyochangia katika mgogoro unaoendelea kuhusu Fao la Kujitoa ili pamoja na kulinda pensheni ya uzeeni Fao la Kujitoa liwe sehemu ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ina wajibu muhimu katika uchumi wa nchi na maisha ya wananchi kwa kuweka mazingira bora ya kisera, kisheria, kimkakati na kiutekelezaji kuhakikisha ujira na ajira bora. Katika kutekeleza mpango wa kazi kutokana na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba Wizara na taasisi zake kuzingatia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu aya ya 59, pamoja na kukamilisha utafiti wa vima vya chini vya mishahara katika sekta 12 na kuweka vima vya chini vya sekta

hizo kwa mwaka 2012/2013, naomba Serikali itoe maelezo kuhusu kutozingatiwa kwa viwango vya mishahara vilivyotangazwa miaka iliyopita. Mathalani wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, wafanyakazi wa hoteli ya Blue Pearl na wafanyakazi wengine wa sekta binafsi nchini ikiwemo ya makampuni ya ulinzi, wamekuwa na malalamiko kuhusu kulipwa viwango vya mishahara tofauti na tangazo la Serikali.

Mheshimiwa Spika, utafiti kuhusu mfumo bora na endelevu wa kutoa pensheni kwa wazee kwa mujibu wa ahadi ya Serikali Bungeni mwaka 2011, ulipaswa kuwa umekamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Hivyo Wizara ieleze ni kwavnini muda unazidi kusogezwa mbele na iwapo pensheni husika zitaanza kulipwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu aya ya 60, kiwango cha fursa za ajira kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kimetajwa kwa upande wa Halmashauri za Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, imeelezwa kuwa ajira zipatazo 6,885 zitazalishwa. Hata hivyo, kiwango hicho ni kidogo ukilinganisha na fursa zinazoweza kupatikana na ukubwa wa tatizo la ukosefu wa ajira hususan kwa vijana. Kazi ya utambuzi wa fursa za ajira katika mipango na programu za maendeleo haikushirikisha wadau na hata mimi kama Mbunge na Diwani sikuhusika katika mchakato huo muhimu. Hivyo lengo lipandishwe na liongezwe na kuweka mfumo wa kuhakikisha zabuni na mikataba yote ya kandarasi za ujenzi na huduma inawekewa mfumo thabiti juu ya fursa za ajira katika maeneo ya utekelezaji. Aidha,

pamoja na Halmashauri za Serikali za Mikoa kutakiwa kuweka wazi mikataba yote ya ujenzi na huduma inayotekelezwa, ni muhimu mikataba yote mikubwa ya ujenzi inayosimamiwa na Serikali Kuu katika Manispaa za Dar es Salaam nayo ikawekwa wazi na fursa za ajira kutumika mathalani Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi *(DARTS),* ujenzi wa miradi ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini pamoja na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu aya ya 64, Wizara ishirikiane na Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha kwamba eneo la wazalishaji wadogo na viwanda vidogovidogo linatengwa kutoka mojawapo ya viwanja vya viwanda vilivyodidimia baada ya ubinafsishaji katika eneo la viwanda vya Ubungo (*Ubungo Industrial Area*). Aidha, Wizara ishirikiane na Manispaa kutenga eneo la wafanyabiashara wadogo Ubungo kwa kuzingatia ahadi ya Rais ya kujenga *Machinga Complex* kila Jimbo la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2011/2012, aya ya 22, kumeelezwa utekelezaji wa mpango wa kuimarisha na kuendeleza hifadhi ya jamii nchini. Kama sehemu ya utekelezaji huo, Wizara imeeleza kuwa imekamilisha marekebisho ya sheria za taasisi sita za hifadhi ya jamii nchini na kupitishwa na Bunge tarehe 13 April 2012. Wizara ilieleze Bunge ni kwa nini yamekuwepo malalamiko ya wafanyakazi na wadau kadhaa wa hifadhi ya jamii kuwa hawakushirikishwa kwenye kuridhia kuondolewa kwa mafao ya kujitoa tofauti na maelezo yaliyotolewa Bungeni tarehe 13 April 2012 kuwa marekebisho yote

yaliridhiwa na wadau. Aidha, nakubaliana na maoni yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani, katika sehemu ya 4.0 ya hotuba ya Msemaji, kuanzia ukurasa wa 16 - 20 na naomba Wizara itoe majibu.

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru kwa kauli ya Wizara iliyotolewa na Waziri Bungeni ya kuletwa Muswada wa Marekebisho kwa Hati ya Dharura kwenye Mkutano wa Tisa wa Bunge kufuatia Maelezo Binafsi yaliyowasilishwa Bungeni tarehe 6 Agosti 2012 na Mbunge wa Kisarawe na pia kwa sehemu Mwongozo niliomba Bungeni tarehe 2 Agosti 2012. Hata hivyo, katika majumuisho, naomba Waziri wa Kazi na Ajira atoe kauli ya ziada iwapo Serikali imekubaliana na Mwongozo niliomba tarehe 2/08/2012 ambapo umejitokeza pia katika Maelezo Binafsi yaliyowasilishwa na Mbunge wa Kisarawe tarehe 06/08/2012 wa kutengua maagizo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na taarifa iliyotolewa kwa umma kwamba kufuatia kuanza kutumika kwa marekebishao ya sheria yaliyofanyika tarehe 13 April 2012 kuwa maombi mapya ya kujitoa yamesitishwa kwa kipindi cha miezi sita. Hatua hii itawezesha mafao ya kujitoa kuendelea kutolewa kwa wafanyakazi kwa mfumo uliokuwepo kabla mpaka pale marekebisho yatakapofanyika kuweka mfumo bora zaidi wa mafao ya kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kuzingatia pia umuhimu wa kuwa na pensheni wakati wa uzeeni.

Mheshimiwa Spika, aidha, naunga mkono sehemu ya mapendekezo ya Kamati kwenye kipengele cha 5.1.1 cha taarifa, ukurasa wa 9 - 11 na maoni ya Kambi Rasmi, kipengele cha 4.0, ukurasa wa 21 - 22 na iwapo

Serikali haitazingatia na kutoa majibu, nitaendelea na kusudio la kuwasilisha Muswada Binafsi kama nilivyoeleza tarehe 2 Agosti 2012.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuzungumzia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA).* Kuna malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi mfano kukosekana kwa haki katika maamuzi ya Tume ambapo ni kutokana na waajiri wengi kuwa na nguvu ya fedha. Takwimu zinaonyesha migogoro katika sekta ya afya imeongezeka kwa asilimia 23, huu ni ukiukwaji wa haki za wafanyakazi kunakopelekea migogoro hiyo. Nashauri watendaji wa Tume hii kuzingatia weledi katika kutekeleza majukumu yao hii ni pamoja na kutoa haki kwa wakati na kuwachukulia hatua kwa wakati waamuzi ambao hawazingatii taratibu za kazi pamoja na kutoa haki pale inapostahili.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi *(OSHA).* Wafanyakazi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu yasiyozingatia usalama wa afya zao. Taasisi hii haijafanya kazi vya kutosha ili kulinda usalama wa afya za wafanyakazi kazini. Wizara iweke utaratibu wa kuhakikisha mashirika, taasisi na makampuni yote nchini yanatekeleza matakwa ya *OSHA* na kuongeza adhabu kwa taasisi ambazo hazizingatii taratibu hizo.

Mheshimiwa Spika, ajira hatarishi kwa watoto. Takwimu zinaonyesha 18.7% ya watoto wanaotumikishwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni kufanya kazi katika migodi, mashamba makubwa, majumbani

na shughuli za uvuvi. Wizara iwe na mkakati endelevu ambayo inatatua tatizo la kutokulindwa kwa haki za watoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga hoja mkono na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hasa *PSPF* imekuwa inachelewa sana kuwalipa mafao watumishi wanapostaafu kwa maeneo mengi tu, watumishi wamekatishwa tamaa na hasa watumishi wanapofariki kabla ya kustaafu. Naomba sana Wizara hii itatue tatizo hili. Hivi nini mantiki ya *PSPF* kuuliza barua ya kuajiriwa wakati mtumishi ameshachangia Mfuko kwa miaka thelathini au zaidi na katika kipindi hiki cha TEKNOHAMA? Wastaafu wengi wamekosa kulipwa mafao yao tu kwa sababu hawana kumbukumbu za barua za kuajiriwa au kupandishwa cheo.

Mheshimiwa Spika, namna ya kuwapima wafanyakazi kuwa na tija ya ufanyaji kazi lazima itafutwe kama nchi hii tunataka kusonga mbele. Wafanyakazi wengi wako tu kwa kutaka kupewa mishahara kwa hiyo hujituma kwa kiwango kidogo sana. Lazima tuwe gari moja waajiri na waajiriwa kama nchi hii tunataka kuigeuza nchi iliyoendelea.

**MHE. JASSON S. RWEKIZA:** Mheshimiwa Spika, niishauri Wizara ya Kazi na Ajira isimamie vizuri Mifuko ya Hifadhi ili iache kunyanyasa wanachama wake.

Uamuzi wa kukataa kuwalipa wanachama wanaoacha kazi au wanaoachishwa kazi hadi wawe na au hadi wafikie miaka 55 ni kitendo cha kunyanyasa wanachama hawa. Malipo hayo tajwa hutolewa kutokana na michango ya wanachama na waajiri wao. Hata kama ni sheria iliyopitishwa na Bunge hili, sheria ina mahali ambako inaanzia. Bila shaka ni kwa mifuko hii yenyewe kwa maslahi fulani.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa baadhi ya Mifuko hii haiko chini ya Wizara hii lakini Wizara ikiwa ni sehemu ya Serikali ina wajibu wa moja kwa moja wa kuishauri Serikali vizuri kuhusu jambo hili. Hivyo ni muhimu sheria hizi zifanyiwe marekebisho kabla ya hoja binafsi za Wabunge kufikia hatua ya kuletwa kama Miswada Binafsi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ahadi za Serikali na utekelezaji wake. Taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 185 ilibainisha kwamba Wizara ya Kazi imekamilisha Rasimu ya Muswada wa Sheria Mpya ya Ajira na kuwasilisha Bungeni. Mpaka sasa hakuna Muswada wa Sheria Mpya ya Ajira uliowasilishwa Bungeni. Naomba maelezo toka kwa Waziri, ni lini Muswada huu muhimu unatarajiwa kuletwa Bungeni na kwa sasa uko katika hatua gani? Muswada huu ni muhimu sana katika kipindi hiki ambacho nchi inakabiliwa na changamoto kubwa sana ya tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, taarifa husika imebanisha kwamba Serikali ilikuwa inaratibu

uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Mafunzo kuhusu Masuala ya Ajira (*National Centre of Employment Studies*) ambacho kitasaidia kutoa elimu na taarifa kuhusu masuala ya ajira kwa wadau mbalimbali. Ningependa Mheshimiwa Waziri alipatie taarifa Bunge hili Tukufu mchakato huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, tatizo la wageni kufanya kazi nchini. Sheria ya Uwekezaji, Na.26 ya 2007, Sura ya 38, kifungu 24, kinatamka kwamba mwekezaji anatakiwa kuleta wataalam wasiozidi watano (5) toka nje ya nchi na iwapo haja ya kuongeza ipo, atapaswa kuwasilisha ombi maalum kuongeza wataalam toka nje kwa kituo cha Taifa cha Uwekezaji ambacho kitaruhusu iwapo itathibitika hakuna Watanzania/Mtanzania hata mmoja mwenye utaalam husika.

Mheshimiwa Spika, kinyume na matakwa ya sheria, kumekuwa na wimbi kubwa sana la wageni, wengi wao wakitoka Bara la Asia. Wengi wa watu hawa wameingia nchini kinyemela, hawana vibali vya kufanya kazi na ushahidi upo na baadhi ya majina yameshawakilishwa kwenye mamlaka mbalimbali za Serikali bila hatua zozote kuchukuliwa. Binafsi nimeshatoa taarifa kwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, juu ya tatizo la wafanyakazi wa Kihindi waliojazana katika kampuni ya Zantel ambao wamekuwa wakifichwa pale ambapo vyombo vya dola vinakwenda kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa *NSSF*. Naungana na hoja ya Kambi ya Upinzani na Wabunge mbalimbali

walivyoonyesha hofu juu ya matumizi ya fedha za wanachama. Natambua kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali za uchumi kama ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo na menginenyo. Hata hivyo, fedha za Mifuko hiyo ni za wanachama, hivyo umakini unatakiwa kuhakikisha kwamba uwekezaji unafanywa katika biashara zenye manufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna sintofahamu nyingi sana juu ya fedha za wanachama ambazo zimewekezwa au kukopeshwa, naomba Mheshimiwa Waziri alipatie Bunge hili Tukufu taarifa ya fedha zote ambazo *NSSF* imekopesha kwa Serikali, watu na makampuni binafsi na kutoa taarifa juu ya marejesho ya mkopo husika na kuliarifu Bunge hili Tukufu juu ya wakopeshwaji sugu na hatua ambazo Wizara inapanga kuzichukua.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Walimu kimekuwa kikilalamikiwa sana na wanachama wake. Mchango wa 2% ya mshahara wa Walimu kwa mwezi kama sehemu ya mchango wao kwa CWT, imekuwa ni kero kubwa sana. Wengi wao hawaoni umuhimu wa kutoa kiasi kikubwa cha fedha. Kero hii nimeikuta katika shule zote za Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua nafasi ya Wizara katika kushugulikia kero hii. Ni muhimu Wizara ikaingilia kati kutokana na ukweli kwamba Walimu wanalalamika sana kutokuona faida ya uwekezaji ambao umefanywa kutokana na fedha zao. Kwa kuzingatia kwamba CWT imeshawekeza vya kutosha

na tayari ina vitega uchumi vya kujiendesha, ni muhimu mzigo wa mchango kwa Walimu ukapunguzwa hasa ikizingatiwa kwamba wana makato mengi sana yanayoathiri mapato yao.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, kumekuwa na ombi maalum toka kwa Walimu juu ya kupunguziwa mzigo wa kodi *(PAYE).* Ni muhimu Serikali ikaangalia ni kwa namna gani itaweza kutumia mamlaka yake kupunguza kodi kwa Walimu hasa ikizingatiwa kwamba Serikali imekuwa ikitoa visingizio vya kutokuwa na uwezo wa kuongeza mshahara na marupurupu ya wafanyakazi.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Kazi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya ajira na usimamizi wa kazi nchini.

Mheshimiwa Spika, muda wa kazi, napenda kushauri Serikali tena kuwa kitendo cha kutokuwepo na utaratibu wa namna ya watu kuwajibika kazini kikamilifu, kimezorotesha uchumi sana wa nchi yetu. Sasa ni wakati wa Serikali kuja na utaratibu wa kufanya watu kuwepo kazini na kulipwa kulingana na kazi iliyofanywa. Hivyo nashauri utaratibu wa kuwa na vitambulisho vyenye kuweza kuthibitisha kuwepo kwa mtu kazini na kutoka kazini na hivyo kulipwa sawasawa na masaa aliyofanya kazi. Hii itaongeza ufanisi kazini na tutazalisha zaidi na uchumi utapanda, mwajiri hatampunja mwajiriwa na mwajiriwa hatampunja mwajiri kwa kulipwa zaidi ya alichofanyia kazi.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, liko tatizo kubwa la ajira nchini. Idadi ya vijana inazidi kuongezeka nchini baada ya shule za kata na vyuo vikuu vingi kujengwa, wasomi nao wameongezeka. Baada ya kuanzishwa Shirikisho la Afrika Mashariki na kufungua milango ya soko la ajira, ajira zimezidi kuwa adimu. Kuna haja Wizara hii iliseme tatizo la ajira katika kikao cha Mawaziri *(Cabinet)* ili uwepo mkakati wa kuanzisha viwanda vya nguo vingi vyenye (*labour intensive*) viweze kuajiri idadi kubwa ya vijana.

Mheshimiwa Spika, iko haja ya Serikali kuweka mkakati wa kina katika Kilimo Kwanza ambacho sera yake inaonekana kufeli. Kilimo kikiwa kizuri, vijana wanaweza kufaidika sana hasa kwa vile soko la chakula ni kubwa Afrika Mashariki yote. Kilimo kinaweza kuwa cha mazao ya nafaka, mbogamboga, maua na kadhalika. Miundombinu ikiwekwa katika maeneo hayo na mbolea ikipatikana inawezekana kabisa kilimo kikawafaidisha vijana na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mkakati wa kutangaza nafasi zilizoko nje ya nchi, ajira, kwa ajili ya Watanzania. Mfano mashirika ya ndege (*Emirates, Qatar Airline)* na kadhalika. Kuna haja kufanya mikataba na mashirika yaliyo tayari ili kuajiri Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Jamii *(NSSF, PPF)* na kadhalika inafanya kazi nzuri kwa kuwekeza katika miradi inayotunisha Mifuko. Nashauri Serikali iwe makini ile miradi iwe inatoa tija (faida) ili mikopo iweze kulipwa

kwa mifuko hii mfano *UDOM* isipolipwa kwa wakati, kuna hatari ya Mifuko kuporomoka.

Mheshimiwa Spika, *recruiting agency* ya Serikali iwepo na ifanye kazi ya kuandaa wanaoomba kazi ili waweze kuwa katika ushindani na wanaoomba kazi wa nchi za jirani za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ziko ajira ambazo zinawezwa kufanywa na Watanzania ambazo raia wengi wa nchi za kigeni wanafanya. Mfano eneo la Kariakoo, eneo la *Slip Way, Restaurant* za Kichina mfano the *Great Wall Restaurant,* mtaa wa *Haileselasie, Restaurant* iliyopo *Old Bagamoyo Road* karibu na *K-net House* ziko nyingi ambazo wanaenda kuchukua wafanyakazi katika nchi zao badala ya kuchukua Watanzania. Nashauri Serikali ipitie maeneo haya, kazi hizo zichukuliwe na Watanzania itakuwa ni njia mojawapo pia ya kuwapa *training* Watanzania in *different skills*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri na Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, Naibu Waziri, Bwana Shitindi, Katibu Mkuu, Kamishna wa Kazi na Wakurugenzi wa idara, wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za kazi na ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *NSSF* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa

nyumba kwa ajili ya wanachama wake. Nimefurahishwa sana na mradi wa nyumba za Kijichi Dar es Salam. Naamini kabisa kuwa chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Dau, shirika hili litaendelea kutunza fedha za wafanyakazi na kuwawezesha kupata huduma mbalimbali zikiwemo zile za afya, likizo, ugonjwa na kadhalika. Nawahakikishia ushirikiano wangu na ofisi yangu ili watimize malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, vibali vya ajira. Mkoani Arusha, hoteli zilizo nyingi zinaongozwa na wageni zaidi ya hayo wapo wafanyakazi wa kawaida ambao hushika nafasi zinazoweza kushikwa na Watanzania wenye elimu ya kawaida. Nashauri Wizara iwe na utaratibu wa kuchuja maombi ya vibali vya kazi ili kulinda maslahi ya Watanzania ili kubaini wafanyakazi wasio na vibali vya kufanya kazi nchini. Nashauri kuwa kila Mkoa uwe na timu ya ukaguzi wa kazi itakayojumuisha Afisa wa Kazi, Afisa Uhamiaji na Polisi.

Mheshimiwa Spika, pensheni ya wazee. Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 imeelekeza Serikali kuwa ipitie upya sera na sheria ya Hifadhi ya Jamii ili kuwezesha wazee ambao hawajawahi kuajiriwa kwenye sekta rasmi wapatiwe mafao ya uzeeni. Nashauri kuwa Wizara iharakishe maandalizi ya utekelezaji wa maelekezo hayo na kwa kutumia takwimu za sensa ya watu na makazi ya 2012 iandae orodha kamili ya wanufaika na kuomba idhini ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuthibitisha kuwa naunga mkono hoja, nawasilsiha.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Idara kwa kazi nzuri. Nampongeza Dkt. Dau wa *NSSF* kwa kazi kubwa ya kuimarisha *NSSF* na mchango mkubwa wa *NSSF* kwa kuchangia kwa kasi katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, *OSHA* waongeze kasi katika kusimamia usalama mahala pa kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Uyui haina Chuo chochote cha ufundi mchundo, fundi stadi au ufundi wowote kama kichocheo cha kuajiriwa au kujiajiri. Wana Igalula, wanaomba Wizara watujengee Wilayani vyuo vya ufundi ili vijana wajiajiri na kuajiriwa baada ya kufuzu ufundi.

Mheshimiwa Spika, mkongo wa Taifa utasaidia vijana walifuzu *ICT* kuajiriwa wakiwa Tanzania kwa kuingia mikataba na makampuni makubwa ya Ulaya na Marekani katika nyanja za *business processing*. Jamaika inafaidika na ushirikiano na Marekani kwa kuchenjua kuponi za biashara. Ziko kampuni Sillicon Valley, California, za *ICT* zinaweza kuajiri vijana wakiishi Tanzania. Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kufanikisha jitihada hizi.

Mheshimiwa Spika, mikopo mingi ya ujenzi wa viwanda na miundombinu kutoka China, inatoa ajira nyingi kwa wageni kuliko Watanzania. Uwepo utaratibu wa asilimia hamsini kwa hamsini ili nao Watanzania wafaidike kwa ajira hizi. Hivi sasa China takriban Watanzania mia moja wako kwenye orodha ya wafungwa wa kunyongwa kwa makosa ya kusafirisha madawa ya kulevya. Haya ni makosa ya jinai, hakuna mjadala, ila uwepo uwiano wa ajira kwa wananchi wa nchi mbili hizi ili kusiwe na ukosefu wa ajira upande mmoja na kusababisha vishawishi vya kujiingiza katika biashara ambazo si halali.

Mheshimiwa Spika, sheria ya pensheni ipitiwe upya ili haki wapate wastaafu bila kujali umri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu wa kusema ndani ya Bunge mchana nikiwa mchangiaji wa tatu, naomba nichukue fursa hii kuongeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Shirika la Hifadhi la Jamii *(NSSF)* kwa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa mwaka 2012/2013 ambazo nina uhakika zitaleta tija na kutengeneza ajira zaidi. Mfano *NSSF* imejipanga kukamilisha ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Kahama, Shinyanga, Mbeya, Moshi, Mara, Mwanza na Ilala. Naomba nishauri *NSSF* iwekeze pia katika maeneo yaliyoduni ili

kuharakisha maendeleo ya sehemu hizo mfano katika Mkoa wetu wa Pwani (Kisarawe, Rufiji, Mafia na Bagamoyo) hakuna uwekezaji wowote uliofanyika. Pia matumizi ya vitega uchumi vinavyojengwa na Mifuko hii yatazamwe upya ili kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *NSSF* kwa kujenga *Machinga Complex* pale Ilala lakini nasikitika Serikali na Jiji wameshindwa kusimamia utekelezaji wa mradi huu. Naiomba Serikali ipige marufuku biashara ya barabarani ili jengo hili likidhi madhumuni yake na hatimaye *NSSF* na mifuko mingine iweze kujenga *Machinga Complex* zingine kama ilivyoahidiwa na Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2010 - 2015.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuiomba Serikali kubadilisha sheria ili mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii iwe chini ya Wizara hii ya Kazi na Ajira na sio utaratibu uliopo kwa vile itatoa fursa nzuri kutathmini mafanikio na changamoto za mifuko hii kwa pamoja mfano leo tumepokea taarifa ya utekelezaji wa *NSSF* tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kuunga mkono hoja ya Waziri wa Kazi na Ajira. Pili naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii na taasisi zake kwa juhudi kubwa wanazofanya kuendeleza gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hi kuelezea suala la ajira ambalo Serikali kupitia Wizara hii inalifanyia kazi. Nashauri Wizara iendelee kutoa elimu vyuoni kabla hawajaingia katika mfumo wa ajira ili waweze kupata elimu ya kujiajiri katika mfumo usiokuwa rasmi kwani vijana wengi wakimaliza vyuo wana mategemeo kuajiriwa Serikalini pale wanapokosa wanapata msongo wa mawazo na kuchukia Serikali yao. Pia Wizara ishirikiane na kuhamasisha taasisi mbalimbali katika kutoa elimu ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, napongeza Shirika la *NSSF* chini ya Mkurugenzi Mkuu Dkt. Dau, kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa katika uanzishaji wa miradi mbalimbali ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kushiriki ujenzi na Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na daraja la Kigamboni ambalo litakuwa ni kiungo kikubwa cha wananchi na kuleta maendeleo. Pia napongeza mfuko wa *PPF* kazi kubwa wanayofanya katika kushiriki katika ujenzi wa nchi yetu. Nawapongeza pia kwa kujali watoto yatima kwa kuwapa elimu na kuwahakikishia matumaini katika maisha yao. Mifuko yote iinge mfano wa *PPF* kuhudumia watoto wa wanachama wao waliofariki.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira ya watoto bado ni tatizo kubwa hapa nchini. Wizara iendelee kushirikiana na Halmashauri ili kutokomeza ajira kwa watoto. Tatizo la wafanyakazi wa majumbani nalo linatakiwa kuangaliwa upya ili kabla hawajaingia katika ajira hii wapate mafunzo. Hivyo Wizara ishirikiane na wadau wengine ili kuboresha maslahi na hata

kuifanya huduma hii kama kazi nyingine, kuondoa manyanyaso wanayopata na ukizingatia wengi ni wasichana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa letu hivyo ni vema ikachukua nafasi yake vema katika kutoa elimu kwa jamii ili kujua kwanza wajibu wao na elimu hii iwafikie vizuri watumishi wanaofanya kazi vijijini. Kutokana na kukosa elimu hiyo kuna wafanyakazi wananyanyaswa sana na waajiri wao ikiwa ni pamoja na kuwafukuza hovyo bila kufuata sheria za utumishi na kulipa ujira mdogo kwa watumishi na hasa katika sekta za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji mdogo wa watumishi katika utumishi wa Serikali. Watumishi wa Serikali ya Tanzania sehemu kubwa wanalipwa ujira wao bila kuwajibika sawasawa katika ufanyaji wa kazi, mara nyingi maofisi yametawaliwa na *story,* kusoma magazeti, visingizio vya kutofika kazini kwa kufiwa, kuugua, sherehe za harusi na kadhalika. Hivyo, Watanzania waandaliwe katika kuwajibika kwa kazi, waache kulalamikalalamika, kulaumu Serikali bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara isimamie ipasavyo ili ajira za Watanzania zilindwe. Bado ziko *institutions* mbalimbali ambazo zinaajiri watu toka nje kwa nafasi ambazo

Watanzania wanao uwezo wa kuzifanya (*professionally).*

Mheshimiwa Spika, wako wageni toka nje ya nchi ambao uwekezaji wao ni uuzaji maduka ya viatu, maua, mapazia na kadhalika. Nao huleta ndugu zao toka nje, wamejaa sana Kariakoo, wanafanya kazi za Watanzania, hii haipendezi. Kwenye meli, ndege ndogondogo nyingi, kazi zinafanywa na wageni wakati watanzania wapo?

Mheshimiwa Spika, afya kazini, *occupational health (OSHA).* Kutokana na kufumuka kwa viwanda vingi vya *size* tofauti na ongezeko la shughuli za ujenzi nchini, ipo haja ya kufuatilia kwa karibu juu ya afya za wafanyakazi wakiwa kazini ili wapate vifaa vya kinga kwa ajili ya afya zao.

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Hifadhi (Mifuko). Hongera kwa kazi nzuri inayofanywa na uwekezaji mzuri ila ni vyema faida inayopatikana basi itiririke hadi kwa wana mifuko ili waone faida ya uwekezaji wao. Aidha, Serikali ijitahidi kupunguza deni lake la *NSSF* ili waweze kuendelea kuwekeza zaidi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, naelekeza mchango wangu kwenye suala la *CMA* na vyombo vingine vilivyoundwa kwa ajili ya kutetea wafanyakazi lakini *unfortunately* vyombo hivi vinatumika na waajiri kukandamiza waajiriwa (wafanyakazi). Kuna malalamiko mengi yanayoashiria mazingira ya rushwa katika utendaji wa *CMA* na hata Maafisa Kazi. Mfano ni hujuma iliyofanywa na

aliyekuwa Afisa Kazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bwana Mushi ambaye baada ya madhambi yake kubainika ikiwemo hujuma aliyowafanyia wafanyakazi wa *Jambo Plastic* kwa kumsaidia mwajiri kuwakandamiza, ambapo baada ya madhambi yake kujulikana amerudishwa Makao Makuu, Wizarani badala ya kuchukuliwa hatua zinazostahili ikiwemo kufukuzwa kazi. Naomba Waziri aliambie Bunge na Taifa ni kwa nini mtu kama huyu Bwana Mushi hajachukuliwa hatua zinazostahili? Analindwa na nani?

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kima cha chini cha mishahara, bado makampuni mengi yanalipa kima cha chini shilingi 80,000/= tu au chini ya hapo tofauti na agizo la Serikali. Mfano wa makampuni haya yanayokiuka agizo la Serikali ni pamoja na *Jambo Plastic* na kiwanda cha Marmo-Mbeya. Nataka kauli ya Serikali, ni kiasi gani makampuni yanatakiwa kulipa kima cha chini kwa mujibu wa sheria za nchi?

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la Sheria Mpya ya Pensheni kwamba wafanyakazi sasa hawataruhusiwa kuchukua mafao yao mpaka wafikishe umri wa kustaafu yaani miaka 55 hadi 60. Wote sisi ni mashahidi kuwa Taifa na wafanyakazi wote nchini wamelipinga na sababu za wafanyakazi kuligomea hili ziko wazi kabisa ikiwemo ukweli kuwa Sheria zetu za Kazi sasa zimefuta usalama wa ajira. Kwa maana hiyo Mtanzania anaweza kupata kazi na kufanya kwa miaka 3 - 5 na kazi hiyo ikaisha sasa iweje mfanyakazi asipewe mafao yake kwa muda aliofanya kazi ili aweze kuendelea na maisha yake kwa hata kuwa na kimtaji cha kufanya biashara ndogondogo?

Kwa kuwa Serikali inatakiwa iwe kwa niaba ya watu na wafanyakazi ndio watu wenyewe, natumaini Serikali italiangalia upya suala hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Serikali iache kutumia Mahakama kuzuia migomo ya wafanyakazi nchini. Kwa kuwa kwa kufanya hivyo Serikali inatengeneza migomo baridi makazini ikiwemo kwa Walimu, Madaktari na kada nyingine. Vinginevyo migomo hii baridi ni hatari zaidi kwa ustawi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji na watumishi wote wa Wizara hii. Napenda kushauri Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana wetu ni changamoto kubwa inayotokana na misingi na miongozo ya mifumo yetu ya elimu inayomwandaa mwanadamu na wanafunzi kwa misingi ya kuajiriwa ofisini. Mifumo ya elimu imwandae mwanafunzi kwenye fikira pana hasa ya ajira binafsi (kujiajiri wenyewe hasa sekta ya kilimo).

Mheshimiwa Spika, Sheria zetu za Ajira na hasa za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zijielekeze kwenye mazingira ya kitanzania ya mifumo ya ajira zisizo endelevu hasa ajira katika sekta binafsi mpaka umri wa kustaafu. Sheria za nchi nyingine zenye mifumo ya uhakika ya hifadhi ya jamii na ajira mpaka umri wa kustaafu haziwezi kufanya kazi katika mazingira yetu.

Wanachama wanapojiunga na mifuko hii ni pale wapatapo matatizo waweze kurudishiwa/kupata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, haki bila wajibu siyo stahiki ya mwanadamu. Tanzania inabidi tuelezane kwa uwazi umuhimu wa kufanya kazi kwa saa zinazokubalika kwa mujibu wa sheria na mkataba na upimaji wa tija kwa kila mfanyakazi hasa katika sekta za umma. Umuhimu wa vigezo vya maadili, uadilifu, uwajibikaji, kuheshimu sheria, haki za binadamu, kupenda kufanya kazi na kutawala muda vipewe kipaumbele kwa kila mfanyakazi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu suala zima la Vyama vya Wafanyakazi. Vyama vya Wafanyakazi vitekeleze majukumu yake kama malengo ya vyama yanavyowaelekeza, wasiingie kwenye mambo ya kisiasa kwa kuwashinikiza wafanyakazi wagome. Migomo sio suluhisho ya matatizo ya wafanyakazi na haswa sekta muhimu zinazohusu maisha ya binadamu kama vile afya (Madaktari na Wauguzi), Walimu ni vyema waangalie jinsi ya kutatua matatizo ya wafanyakazi kwa njia ya amani si kwa migomo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pensheni za wazee, naipongeza Serikali kwa kuwa na matamko mbalimbali

yanayoelekeza kutoa huduma muhimu kwa wazee kama vile matibabu, nyumba, pensheni zao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu, kwa kuwa walemavu, wanawake, vijana wana uwakilishi Bungeni, kwa nini wazee hawana uwakilishi Bungeni? Lini sheria italetwa? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Serikali, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 18, inaeleza idadi ya vijana ambao walielimishwa ni 76241 na ambao waliweza kujiajiri ni 1741 tu. Kutokana na takwimu hizo, inaniweka pahala kuona kwamba bado Serikali haijajiandaa ipasavyo kwa kutoa uelewa wa vijana hawa wafanye nini baada ya elimu waliyoipata.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri nilionao ni kwamba laiti kama Serikali itakuwa karibu na wahitimu hawa wangalisema wanataka nini kama vile viwanda, ardhi, mikopo na kadhalika lakini Serikali inatoa elimu tu na hakuna anayewafuatilia. Ushauri wangu mwingine ni kutoa elimu baada ya elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, *Machinga Complex,* itajengwa lini Mwanza? Hii ni kwa ajili ya vijana machinga Mwanza - Mlango mmoja.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia machache katika hotuba hii ya Wizara ya Kazi na Ajira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana linaongezeka kwa kasi japokuwa Serikali kila siku inaleta hotuba nzuri zenye maelezo yanayowatia moyo vijana wetu waliobahatika kupata elimu na wale wasiobahatika kupata elimu ya juu. Kwa mfano, Serikali inaelekeza kuwa kila Halmashauri ichangie asilimia 5% ya mapato yake ya ndani kwenye mfuko wa vijana ili waweze kupata mikopo katika maeneo yetu ya vijijini. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze katika mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012, ni Halmashauri ngapi za Wilaya zilitenga hiyo asilimia 5% kwenye mfuko wa vijana?

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ni muhimu sana kwa maslahi ya wafanyakazi kwa kuwa wanapostaafu ama kujitoa kazini wanapata fedha ya kuanzia maisha. Je, fedha zinazokopeshwa na Mifuko hii ya Hifadhi kama *NSSF, PSPF* kwa Serikali na taasisi kwa ajili ya uwekezaji ni kwa kiasi gani mchangaji (mfanyakazi) naye ananufaika?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tabia ya baadhi ya waajiri kutopeleka fedha za wafanyakazi wao katika Mifuko ya Hifadhi kama inavyotakiwa. Je, Mheshimiwa Waziri na timu yake wamejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili la waajiri hawa ambao hawapeleki fedha za wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi kwani hii ni dhuluma kwa wafanyakazi wanyonge.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia katika hoja iliyombele yetu. Kwanza naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu lipo kwenye suala la vibali vinavyotolewa nchini kwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini (*work permit*). Mashaka yangu hapa ni kuwepo kwa idara nyingi za Serikali mfano Wizara ya Kazi, Mambo ya Ndani na kadhalika. Nadhani upo umuhimu wa kuwepo kwa Idara moja tu inayotoa vibali vya kufanya kazi nchini kama ilivyo Uingereza. Kuwepo kwa idara tofauti zinazotoa vibali kwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini, inakuwa vigumu kwa Wizara ya Kazi kufuatilia nani mwenye kibali na nani asiye nacho.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, ajira za wazawa kuchukuliwa na wageni hata wasio na sifa stahiki. Licha ya kuwepo sheria mbalimbali, bado jambo hili linaendelea. Wizara ya Kazi iimarishe ushirikiano baina yake na Wizara ya Mambo ya Ndani, vyombo/vyama/taasisi za kitaalauma kama vile bodi na mabaraza ya taaluma (Uhandisi, Uhasibu, Udaktari, Walimu na kadhalika ili kuimarisha utekelezaji wa sheria ikibidi Wizara itie saini *MoU* na wadau hao wawili. Wizara zishirikiane katika kuzuia/kudhibiti uingiaji na kufanya kaguzi kubaini waliojipenyeza na kuchukua hatua wakiwemo wale wanaofanya udanganyifu kwa kuwasilisha taarifa zisizo sahihi wakati wa kuingia.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kazi na Ajira pamoja na wasaidizi wake na watendaji wote kwa hotuba nzuri na kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni vyema wakatambua changamoto zilizopo katika sekta ya ajira hasa yale maeneo ya wawekezaji. Ile sheria inayoruhusu kuingiza wafanyakazi nyeti watano katika kampuni husika lakini makampuni mengi hasa yanayomilikiwa na watu wa asili ya India wamekuwa wakiajiri hadi walinzi na makarani toka nje. Naomba Wizara ilifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mikataba ya muda mfupi katika sekta ya mahoteli ambayo inalenga wafanyakazi wenye uzoefu maalum. Lakini unakuta *waiter,* mlinzi na kadhalika wanaajiriwa kwa mkataba wa miezi mitatu, mitatu halafu anatakiwa aombe ajira upya, kwa kufanya hivi wanalenga wasipate mafao.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi Maeneo ya Kazi inapaswa ifanye kazi vyema kwa sababu maeneo mengi ya kazi yako chini ya viwango vya usalama na afya. Kule *Speke Bay Lodge* - Busega wafanyakazi wanatumikishwa kwa kusomba kinyesi kwa kutumia toroli bila mavazi rasmi. Hii inafanyika kwa sababu hoteli haitaki kutumia fedha kuagiza gari la kunyonya mavi. Huu ni unyama wa hali ya juu, naomba Wizara ifuatilie.

Mheshimiwa Spika, waajiri wengi wanawatisha wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi kwa kuwatisha kuwafukuza kazi au kuanzisha umoja unaosimamiwa na menejimenti. Hii ni njia ya kuua vyama vya wafanyakazi, kuviziba midomo na kuvihujumu na pia ni kuvunja sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna wanavyoiongoza Wizara hii ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kwani bila ya kuwa na kundi la wafanyakazi kamwe hatuwezi kufikiria malengo yetu tuliyo nayo kama nchi. Aidha, napenda kumpongeza pia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Mwisho lakini si kwa muhimu, nawapogeza wafanyakazi wote nchini kwa namna wanavyoitumikia nchi yao katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuiomba Wizara iipitie upya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika sheria hii mwezi wa nne mwaka huu. Mamlaka hii ni muhimu lakini ifikie wakati sasa maslahi ya mtumishi na mfanyakazi yawe ni kipaumbele. Matakwa ya sheria kwamba mtumishi hawezi kulipwa pensheni yake kabla hajatimiza miaka 55 na 60 si sahihi kabisa. *SSRA* iangalie mazingira yetu ya Tanzania kuhusu fao la kujitoa. Kitendo cha kutoruhusu mtu kuchukua pensheni ili kuitumia kwa

mahitaji na vipaumbele vyake ni vyema ikarekebishwa. Watumishi wanatofautiana vipaumbele vya maisha. Michango ya pensheni ni michango ya mtumishi na ni haki ya mtumishi kuamua ni wakati gani achukue pensheni yake na ni kwa ajili ya shughuli zipi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Sheria ya *SSRA* inatambua na kuruhusu Mashirika, Mwajiri na Taasisi zingine za Ajira kuanzisha '*supplementary schemes*' kwa ajili ya kuongezea marupurupu/mafao ya pensheni pindi mtumishi atakapostaafu. Mfano wa taasisi ambazo tayari zimeanzisha *schemes* za aina hii ni *TBL, TANESCO* na nyinginezo. Ni vyema sasa Wizara itoe orodha ya waajiri ambao wanatekeleza *schemes* za aina hii. Naomba Wizara ilitajie Bunge lako Tukufu orodha ya makampuni/waajiri ambao wanatekeleza mfumo huu. Aidha, ni muhimu pia kwa *SSRA* kuwahamasisha/kuwaelimisha waajiri wengi zaidi ili waweze kutekeleza mfumo huu japo ni wa hiari.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, ni nzuri ila ina upungufu mwingi unaohitaji kurekebishwa. Ni vyema sasa Wizara ikalieleza Bunge lako Tukufu ni lini itazifanyia mapitio sheria zote zinazohusu Kazi na Ajira ili ziweze kuendana na wakati. Nitawasilisha Wizarani baadaye mapendekezo halisi ambayo ninayaona ni muhimu na kwa kushirikiana na *TUCTA*.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya mifano ya maeneo ambayo yanahitaji kurekebishwa ni suala zima la udalali katika sekta ya ajira au *labour broking.* Ni muhimu kuweka udhibiti katika uendeshaji wa huduma

za ajira za muda ‘*temporary employment services’* na namna watoa huduma hii au madalali watakavyodhibitiwa kwani hivi sasa mtumishi amekuwa akinyonywa haki na jasho lake na kukosa mafao muhimu anayostahili. Madalali wamefikia hatua wao ndiyo watumishi, wanapokea hela nyingine halafu wanawalipa watumishi ujira mdogo. Wizara isimamie hili, dalali anatakiwa kulipwa ‘*commission*’ tu kwa udalali/kwa ajira atakayokuwa amemtafutia mtumishi. Tena inatakiwa afaidike mara moja tu na si kila mwezi dalali anafaidika na mtumishi aachwe aendelee na ajira bila ya kukatwa na dalali tena dalali ndio anapata faida kubwa. Dhana nzima ya udalali inakuwa haipo tena. Tugeuze hii hali si haki hata kidogo na ikiwezekana basi watumishi waajiriwe moja kwa moja na mwajiri maana kwa mfumo wa madalali wamekuwa wakinyanyasika sana na kunyimwa mafao wanayostahili kisheria. Lakini pia madalali wengine wamekuwa wakilipwa kila mwezi na cha kushangaza anakaa na hela ya mtumishi na anachelewa kumlipa mtumishi kwa makusudi kabisa. Hili si la kufumbiwa macho, wakaguzi wafanye kaguzi sehemu mbalimbali za kazi ili kuyabaini haya na kuchukua hatua kali dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia tatizo la ukosefu wa ajira limekuwa likiongozeka siku hadi siku, ni muhimu na naishauri Serikali ifikirie kuanzisha Mfuko wa Bima kwa ajili ya watu wasio na ajira (*Unemployment Insurance Fund).* Mfuko huo utasaidia kila wananchi kupata maisha bora. Mfuko huu utasaidia watu wasio na ajira kupata mafunzo ili waweze kupata ajira nyingine na kuwatengenezea ajira.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fidia kwa walioumia kazini imepitishwa muda mrefu sasa. Ningependa kufahamu hadi kufikia sasa ni watumishi wangapi walioumia wakiwa kazini wamelipwa? Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika kuwalipa watumishi hao katika mwaka wa fedha unaomalizika?

Mheshimiwa Spika, yako makundi maalum ya watumishi ambayo siku zote mishahara yao ni midogo na inakuwa ngumu kwao kuwa na akiba ya kukatwa. Kitendo cha mifuko mbalimbali kama *GEPF* na mengine kuwafikiria kwa kuwapa uhuru wa kuchangia haiwasaidii. Serikali i-*determine* njia bora itakayowasaidia wafanyakazi wanyonge wa makundi maalum kama wafanyakazi wa majumbani, walinzi, madereva, wafanyakazi katika baa, hoteli, migahawa na nyumba mbalimbali za kufikia wageni. Hii itawasaidia kupata mafao mbalimbali wakiwa kwenye ajira na pindi watakapostaafu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa namna anayozingatia maslahi ya wafanyakazi. Napenda kuishukuru na kuipongeza Wizara kwa namna ilivyoshiriki katika mchakato mzima wa kuweka saini katika Mkataba wa Kimataifa unaohusu Wafanyakazi wa Majumbani mnamo mwezi Juni 2011. Hongereni sana na kwa niaba ya wafanyakazi wa majumbani popote walipo, nashukuru Serikali kwa niaba yao. Hata hivyo nchi hupewa mwaka moja tangu iliposaini kama muda wa ahueni ‘*grace period’* kwa ajili ya kujiandaa na maandalizi ya

Kuridhia Mkataba wa Kimataifa. Napenda kufahamu mchakato huu umefikia wapi? Je, Azimio la kuridhia litawasilishwa lini Bungeni kwa ajili ya kuridhia? Sambamba na hili ningependa kufahamu idadi ya mikutano ya wadau ambayo imefanyika hadi sasa, ni muhimu sana Azimio hili likaletwa mapema.

Mheshimiwa Spika, taasisi ya *OSHA* ni taasisi muhimu sana. Taasisi hii inatakiwa kuongezewa uwezo wa kibajeti, kiutumishi, elimu na utalaamu lakini pia *OSHA* siku zote imekuwa ikitengewa bajeti ndogo sana wakati mwingine tumekuwa tukishuhudia ikitengewa shilingi milioni 60, ili ikazifanyie nini? Itawezaje kutekeleza majukumu yake ya kisera na kisheria kwa hali hii? Eneo lenyewe lilipo *OSHA* na ingekuwa inajikagua yenyewe ingefungwa. Jengo ni bovu, limechakaa na halifai hata kidogo. Watumishi wanastahili kulipwa vizuri na kupewa vivutio na motisha ili waweze kuwasimamia vizuri waajiri na sehemu za kazi na ili wawe na utendaji mzuri, wanaohitaji kuwa na vitendea kazi vya kutosha ili waweze kufanya kazi itakayoleta matokeo. Ningependa pia Bunge lako lielezwe ni sehemu ngapi za kazi zimesajiliwa na *OSHA* na ambao hawajasajiliwa wamechukuliwa hatua gani? Ni muhimu pia kujua ni sehemu ngapi za kazi zimechukuliwa hatua kwa kutotekeleza vyema Sheria ya Afya na Usalama Sehemu za Kazi na wamechukuliwa hatua gani, ambao hawajatekeleza wamefanywa nini?

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia ukaguzi wa utoaji wa vibali kwa ajira kwa wageni vikatizamwa kwa makini.

Mheshimiwa Spika, ni vyema katika mwaka 2012/2013, msisitizo zaidi ukawekwa kwenye ukaguzi na ufuatiliaji marekebisho ya sheria mbalimbali, ukaguzi wa afya na usalama kazini na katika kuhakikisha kunakuwa ajira zenye staha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza haya, kwa mara nyingine tena nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri. Naunga mkono hoja.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote kwa hotuba nzuri waliyoiandaa.

Mheshimiwa Spika, binafsi ninalo swali dogo na ningependa nipatiwe majibu ya kina.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* limetajwa kwenye hotuba ukurasa 52 lakini nilitegemea mengi yangeongelewa katika hotuba kuhusiana na shirika hili kwa ujumla. Lakini hotuba hii haikugusia changamoto kubwa ambayo inalikumba shirika hili na changamoto hiyo si nyingine bali ni ile ya shirika kujiendesha lenyewe bila ya kuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa takribani miaka mitatu sasa jambo ambalo limepelekea shirika kutotekeleza majukumu yake ipasavyo. Maamuzi makubwa kama yale ya kujenga *NIP Tower* kwa kushirikiana na *NSSF* yamebakia

kuwa ndoto. Natumai yatakuwepo maamuzi mengi ambayo yanakwama katika kipindi hichi ambapo shirika halina Bodi. Je, ni sababu zipi zimepelekea shirika hili kujiendesha lenyewe kwa takribani miaka mitatu bila Bodi ya Wakurugenzi? Je, ni lini hasa Waziri ataona umuhimu na uharaka wa kuunda Bodi hiyo? Napenda Waziri alieleze Bunge lako Tukufu katika miaka yote hiyo mitatu (ukiachilia mbali kutokujengwa kwa *NIP Tower*) ni upungufu gani mwingine umejitokeza kutokana na shirika hili kujiendesha bila Bodi ya Wakurugenzi? Ni matumaini yangu maswali haya yote yatajibiwa ili kuwaondolea wafanyakazi wa shirika na wananchi kwa ujumla utata huu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie licha ya kuwepo sheria kadhaa zinazosimamia masuala ya kazi na ajira nchini, Sheria Namba 6 na 7 za mwaka 2004 bado kumekuwepo migogoro mingi ambayo imekuwa ikijitokeza kwenye sehemu za kazi, wafanyakazi wakidai mishahara na stahili zao nyingine na matatizo haya yapo karibu kwenye sehemu zote za kazi hasa kwenye migodi/na mashamba makubwa. Nashauri Serikali/Wizara husika itoe elimu ya kutosha kwa waajiriwa ili wajue haki zao, pia kwa waajiri ili wafahamu haki na majukumu yao kwa waajiriwa wao kuliko hivi sasa wanavyoteseka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la ajira kuwa gumu, nashauri vijana wapatiwe elimu ya ujasiriamali kuliko watu wote kuendelea kukaa kusubiri kuajiriwa. Lakini lipo tatizo kubwa la waajiri wengi hivi sasa kuajiri wafanyakazi wageni toka nje ya nchi ambao huwalipa zaidi na nafasi hiyo au ujuzi huo wa kazi unaweza ukafanywa na Watanzania. Nashauri Serikali ipitie tena sheria ya ajira kwa wageni.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa utendaji wao wa kazi pamoja na mikakati yao. Pamoja na pongezi nilizozitoa, nina maswali ambayo naomba Wizara hii inipatie majibu.

Mheshimiwa Spika, taratibu zinazotumika kufanya ukaguzi katika sehemu za kazi na haswa viwandani kwani nimesikitishwa sana na jinsi waajiri wasivyojali afya ya wafanyakazi kwa kutoa au kutokutoa vitendea kazi. Haya nimejionea katika viwanda kama *Steel Industry* kilichopo Dar es Salaam na *Urafiki Textile Limited* kilichopo Dar es Salaam. Napenda kujua hatua zinazochukuliwa na Wizara punde inapogundua upungufu niliotaja hapo juu kwani wanaoumia na kupata matatizo ni Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana katika ajira ya watoto na haswa katika mazingira hatarishi ya kazi, hili tusiliangalie kwenye viwanda tu bali tuliangalie hadi kwenye ajira za majumbani huku ndiko watoto wengi wadogo wanapatiwa ajira mbaya na ambazo hazina tija. Ni vyema Serikali ikatoa tamko katika eneo

hili ambalo linawagusa hata watumishi wengi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, usalama na afya mahali pa kazi ni muhimu sana, lakini kwa masikitiko makubwa sana hili halifanyiki. Watumishi wengi hawajui haki zao za msingi ikiwemo kufanya kazi bila bima ambazo ni muhimu sana kwao pindi panapotokea ajali. Ni vyema Serikali ikatueleza mkakati wake ili tuweze kujua waajiri wamejipanga vipi kuwakatia bima watumishi wao.

Mheshimiwa Spika, ajira ni tatizo kubwa sana hapa nchini. Zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania hawana ajira za uhakika na haswa vijana, vijana wengi wana elimu bora lakini ajira hazipo. Eneo hili ni *very sensitive* kwa uhai na mstakabali wa nchi yetu lakini Wizara hii haijatueleza imejipanga vipi kuhakikisha vijana walio wengi ambao wameanza kupoteza imani na Serikali yao wanapata ajira za uhakika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii, hasa kwa kujikita katika suala zima la ajira na hasa ajira kwa vijana. Licha ya Waziri kutoa takwimu za ajira zilizotolewa au zilizopatikana hapa nchini, Waziri ameshindwa kutueleza ni kazi za aina gani zilizotolewa na kwa ujira upi na wanufaika ni Watanzania wenye ujuzi na utaalam wa kiwango gani isije ikawa ni ajira ambazo ni za kutumia nguvu nyingi sana na ujira mdogo sana ambao hauwezi kumkomboa Mtanzania kwa kasi ya maisha yanavyokuwa magumu kila kukicha. Waziri pia

kagusia juu ya kazi iliyofanywa na *TaESA* kwani fursa za ajira zilizopewa Watanzania ndani na nje ya nchi bila kunyambulisha.

Mheshimiwa Spika, suluhisho si kuainisha ni ajira ngapi tumetoa kwa Watanzania bali ni kuainisha kuna vijana au Watanzania wangapi ambao hawana ajira na hapa ni kwa wale wenye ujuzi na wasomi na wale ambao hawana ujuzi wa kutosha au elimu. Utatuzi wa hili ni Wizara kuwa na *database* yenye *CVS* za Watanzania wasomi na wale wenye elimu ya kawaida, ili iweze kujua ni kiasi gani cha Watanzania wana ajira na wasio na ajira ambapo mara fursa itakapopatikana wataweza kuwa-*consult* watu hawa na kusaidia kuhakikisha wanapata ajira.

Mheshimiwa Spika, kuna fursa nyingi za ajira zinajitokeza ndani na nje ya nchi ambazo Watanzania walio wengi hasa wale waishio Mikoani wanakuwa hawazipati taarifa husika ambapo wanapoteza *opportunity.* Hii Wizara ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje itaweza kusaidia ajira nje ya nchi na kwenye mashirika ya kitaifa ambapo itachangia sana kukuza pato la Taifa. Kuna fursa nyingi sana nje ya nchi mfano kwenye nchi ya Sudan Kusini ambalo ni Taifa jipya na linahitaji ujenzi wa Taifa hili. Wizara ilitakiwa kutumia fursa hii na kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje kupeleka Watanzania wenye sifa mbalimbali katika sekta mbalimbali Sudan Kusini ambayo kwa sasa haina wataalam wa kutosha. Hili linaweza kufanikishwa tu pale ambapo tutakuwa na *database* itakayotu-*guide* kwenye kujua Watanzania

wenye fursa, ni wakati sasa wa kudhamiria tuyafanyayo.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuzungunzia suala zima la usalama na afya mahala pa kazi. Hili ni tatizo kubwa sana ambapo unakuta makampuni mengi na migodini hawafuati na wala kuzingatia usalama maeneo ya kazi . Pia katika maeneo ya ujenzi, kuna malalamiko mengi sana yanayotolewa na wafanyakazi kufuatia kufanya kazi kwenye mazingira hatarishi. Viwandani kunalalamikiwa, watu wanafanya kazi bila vifaa vya kufanyia kazi mfano watu wenye viwanda vidogovidogo unakuta wanachomelea bila hata kifaa cha kujikingia. Utakuta Watanzania wanazibua maji taka bila hata vifaa maalum. Wafanyakazi wa viwanda vya ngozi, korosho, mkonge/katani pia wanafanya kazi kwenye mazingira hatarishi na hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafanyakazi wa migodini ambao hulalamika juu ya *scanning* ambayo hufanyiwa mfano mgodi wa *North* Mara, *GGM* na kwingineko ambapo wanadai kuwa *scanner* hizo zina madhara kwao. Mathlani mtu anakuwa *scanned* kwenye kichwa huku kanyoa kipara kabisa. Pia mazingira ya kazi kwa kemikali wanazotumia hasa wa *section ya plant*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kuhusu wimbi kubwa la wageni kuwepo Tanzania na wanafanya kazi ambazo Watanzania wa kawaida kabisa kielimu na kitaaluma wanaweza kuzifanya. Mfano wa *drilling,*

*driving*, *guarding/watchman* na zingine, unakuta hawa wageni wanategemea msaada wa wenyeji ili wao wafanye kazi hiyo na unakuta wanapewa ujira mkubwa sana kuliko hata wazawa, nimekuwa nikizungumzia hili muda wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata takwimu ni kwa kiasi gani Wizara imejipanga kuondoa kabisa wimbi hili la wageni kupora kazi za Watanzania. Nchi za wenzetu wana-*monitor* kwa kiasi kikubwa kwenye sekta hii. Nchi yetu imetawaliwa sana na rushwa ambazo zinapelekea wageni kuhodhi nchi yetu na kupora uchumi wa nchi yetu kwani pato kubwa limeenda kujenga kwao na mchango katika Taifa ni kama hakuna. Tunataka kuona wageni wanaokuja ni wale *expertise* tu na baada ya muda nadhani (miaka mitatu) Watanzania wanarithi kazi hizi. Naomba kupata mkakati wa Serikali juu ya janga hili.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kuhusu bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka huu wa fedha imeomba kutengewa Sh.2,835,880,000/= kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Kiwango hicho cha fedha hakiwezi kukidhi matakwa ya utekelezaji wa miradi ya maendelo kwa ufanisi. Ninasema hivyo kwa sababu kwa mfano mradi wa *"Child protection and participation"* kwa miaka miwili mfululizo haujatengewa fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wake. Bado Serikali imeendelea kutegemea ufadhili wa *UNCEF* jambo ambalo halileti matumaini

sana kwa mradi huo kufanikiwa. Serikali iangalie jinsi ya kuhakikisha kwamba tunajitegemea katika miradi yetu hata kama ni kwa kiwango kidogo kuliko kuachia wafadhili kwa asilimia mia kwa mia kwani tumesikia kwamba kudorora kwa kiuchumi kumeathiri sana wafadhali jambo ambalo linaashiria kupungua kwa misaada kwa nchi zinazoendelea ikiwemo nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *"Support Employment Creation Program"*, ni mradi muhimu sana hasa kwa wakati huu ambapo vijana wengi hawana ajira. Fedha iliyotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012, ni fedha za wahisani Sh.146,985,000 wakati kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa/kuomba fedha za wahisani Sh.350,880,000/=.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa 38/39, kuna maelezo kwamba katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 kutakuwa na upatikanaji wa fursa za ajira zaidi ya 800,000. Je, upatikanaji huo wa fursa za ajira utafanikiwaje wakati mradi umetegemea wafadhili kwa miaka miwili mfululizo? Nirejee nilivyosema hapa awali kwamba uchumi katika nchi za wafadhili umedorora hivyo hatuna uhakika wa kupokea fedha hizo ili kufanikisha mradi huu na miradi mingine ya maendeleo inayotegemea asilimia mia moja kutoka nchi wafadhili. Serikali itenge kiasi cha fedha za kutosha kuendesha mradi huu uliopo *vote 65*, *subvote 2002, 6243, "Support Employment Creation program".*

Mheshimiwa Spika, kuna wageni wanaofanya kazi hapa nchini katika nafasi ambazo wataalam wazawa wangeweza kabisa kufanya kazi hizo. Serikali ifuatilie jambo hili ili Watanzania wasio na ajira na wenye uchu mkubwa wa kufanya kazi waweze kupata nafasi ambazo zimeshikiliwa na wageni kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALUM K. BARWANY**: Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kusema siungi mkono hoja. Hii ni kutokana na kushindwa kwa Wizara kusimamia haki za wafanyakazi na kusababisha migogoro mahala pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ameelezea Wizara yake ilivyoshiriki katika utatuzi wa migogoro. Ni matarajio yangu kuwa umefika wakati wa kujiuzulu kwa kushindwa kulishughulikia suala la mgogoro kama alivyodai jambo ambalo limesababisha migogoro ya mara kwa mara ya wafanyakazi kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tumeshuhudia migomo ya Madaktari na Walimu wa shule za Serikali. Pamoja na kujitokeza kadhia hiyo, hatujaona jududi za Wizara kulimaliza tatizo hili kwa maafikiano, kilichojitokeza ni ubabe na vitisho na pengine kwa kuitumia Mahakama ya Kazi. Wizara ndio msimamizi wa maslahi ya wafanyakazi ili kila mfanyakazi alipwe kwa mujibu wa hali ya maisha ilivyo. Ni vyema Wizara ikazingatia kuwa kipato cha Mwalimu ni cha chini na

hali ya maisha imepanda. Hivyo, ni jukumu la Wizara kuwatetea wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba amezungumzia mafunzo ya kuwawezesha wajasiriamali kujiajiri. Kwenye Jimbo langu la Lindi Mjini hutokea mafunzo kama hayo lakini kutokana na umaskini wa Lindi Mjini (wa kutengenezwa), vijana wengi wanashindwa kujiajiri. Je, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine ina mpango gani wa kuinua hali ya maisha ya vijana hawa ambao wako nyuma kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba amezungumzia viwango vya kazi vya Kimataifa lakini ndani ya nchi yetu kumetokea matukio mengi ya unyanyasaji kwa wafanyakazi wa Kitanzania kunyanyaswa na baadhi ya waajiri wa kigeni, wafanyakazi kunyanyaswa migodini bila wahusika kuchukuliwa hatua zozote, watoto kufanyishwa kazi hatarishi bila ya Wizara kuongeza kasi ya kukomesha manyanyaso hayo kwa watoto, mfano halisi ni hapa Dodoma watoto wengi wako mitaani wakikosa elimu kwa kuuza miwa, mayai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wafanyakazi wenye madai kwenye sekta mbalimbali, hali ni mbaya zaidi. Wafanyakazi wanaodai mafao yao bila mafanikio ni wengi kama wafanyakazi wa viwanda vya korodho, wafanyakazi wa yaliyokuwa mashamba ya mkonge, kwenye Jimbo langu kuna wafanyakazi wa shamba la *TASCO*, *Kikwetu Sisal Estate* na *Kitunda Sisal Estate*. Wafanyakazi hawa ambao wengi wao wana maisha duni na wachache wao wameshafariki bila

hata kujua hatma ya malipo yao, ni jukumu la Wizara kuchukua hatua za haraka ili wale wote wenye jukumu la kuwalipa wafanyakazi hao waadae malipo hayo tena kwa thamani ya shilingi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kuchangia kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya wakishirikiana na watendaji wao wa Wizara ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kwa kutaka ufafanuzi kuhusiana na suala zima la ajira kwa vijana wanaomaliza vyuo vikuu ambao wanakutana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzoefu mkubwa unaotakiwa katika nafasi za kazi zinapotangazwa. Je, Wizara hii inachukua nafasi gani katika kuhakikisha vijana hawa ambao wanatoka *fresh from university* na wana *qualify* katika kazi hizo upande wa kigezo cha elimu lakini suala la uzoefu ambao huwa miaka 5 -10 ni kikwazo kwa vijana hawa kupata kazi? Je, Wizara inawasaidia vipi vijana hawa?

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia suala la wafanyakazi wa ndani (*house girls).* Hawa vijana hawana mshahara unaofanana, wengi wanalipwa elfu tano na wengine laki moja, ukiachilia mbali suala la mishahara ambalo ni sugu, je, Wizara imejipanga vipi kurekebisha tatizo hili? Je, *security* ya wafanyakazi hawa wa ndani Wizara imejipanga vipi maana wengi wanaonewa, mishahara hawalipwi na mateso mengi, haki zao kimsingi wanakosa, Wizara

inashirikiana vipi na Wizara nyingine katika kuhakikisha wanapata haki zao?

Mheshimiwa Spika, mafao yetu ya *NSSF* ni tatizo pindi tunapotaka kupewa pesa zetu. Aidha, mtu kaacha kazi au kastaafu kuna mlolongo mkubwa wa malipo ambao unakatisha watu tamaa kwa pesa ambayo ni yao.

Mheshimimimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina hazina kubwa ya kuweza kupata ajira duniani nayo ni lugha ya Kiswahili. Hivi sasa nchi mbalimbali duniani zimefanya hima ya kuweza kujifunza Kiswahili. Katika hali hiyo, ni dhahiri mahitaji ya Walimu wa kufundisha Kiswahili yatakuwa yameongezeka. Wizara imejipanga au itajipanga vipi ili Walimu wa Kiswahili waweze kuajiriwa katika nchi mbalimbali? Hii ni fursa kwetu sisi na kama hakutakuwa na mkakati maalum ajira zinaweza kwenda kwenye nchi ambazo sisi tumewafunza Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 11, amezungumzia juu ya fidia kwa wafanyakazi waliokatika utumishi wa umma. Kuna malalamiko kuwa fidia ni ndogo na wakati wengine huchukua muda mrefu kupata fidia hiyo. Je, Wizara ina mipango gani ya kuboresha fidia na pale inapotokea watumishi kupata ajali, fidia iweze kutolewa haraka kadri inavyowezekana?

Mheshimiwa Spika, ukurasa 12,13 mpaka 14 unazungumzia suala zima la ajira kwa watoto. Serikali imewatoa watoto 22,243 katika utumikishwaji na kupatiwa mafunzo. Ni jambo lisiloelekea na kukatisha tamaa kuwa kipindi cha mwaka mmoja 2011/2012, ni kesi tatu tu ziko katika hatua ya kufikishwa Mahakamani. Hii inadhihirisha kuwa ufuatiliaji wa ajira haramu kwa watoto ni mdogo mno kwani idadi ya kesi tatu kwa nchi nzima na kwa mwaka mzima haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira na hasa kwa vijana. Kwetu sisi sehemu kubwa inayoweza kuchukua ajira kubwa kwa vijana ni kilimo, kilimo chenye mtizamo wa kisasa na sio tu jembe la mkono. Wizara hii imesaidia vipi katika kufikia lengo la kuweza kuwa na kilimo cha kisasa? Ni vijana wangapi wamesaidiwa ili waweze kujiajiri kwenye kilimo na sio ajira ya biashara ndogondogo ambazo sio wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara hii sasa ijielekeze kwa kushirikiana na vyombo vingine, yawepo mazingira ili vijana waweze kushiriki kikamilifu katika kilimo, Kilimo Kwanza kiwaangalie vijana.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi ni moja kati ya mihimili mikuu ya kuboresha maisha ya wananchi. Kwa njia moja au nyingine, kada zote za umri wowote, wawe vijana, wazee hata rika la kati mwelekeo wao ni Wizara ya Kazi, wawe wa jinsia zote. Suala kubwa linaloikabili

nchi, ni ajira kwa vijana, ajira kwa wanawake, ajira isiyostahiki lakini hufanywa kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, ajira ina nyanja nyingi, kuna ya Serikali, sekta binafsi na ile ya kujiajiri mwenyewe. Vijana wengi wanaomaliza shule hataraji kupata ajira kutoka Serikalini na hawana nadharia ya kutaka kujiajiri wenyewe. Shughuli hii yote inatokana na elimu wanayoipata wanapokuwa shuleni, kwani elimu inayotolewa si ya kumfanya mtu ajiajiri mwenyewe. Mfumo wa elimu Tanzania haumlengi wala kumpa dira mwanafunzi kuwa mkakamavu, mbunifu, mdadisi ili impelekee kujiajiri mwenyewe. Ni vyema Wizara ya Kazi, ikishirikiana na Wizara ya Elimu, Kilimo na Viwanda wakae pamoja na kujaribu kufanya mtaala utakaoweza kuwasaidia wanafunzi wawe wa *primary*, sekondari hadi chuo ili watakapomaliza kiwango chochote cha elimu waweze kujiajiri wenyewe. Hii itawapa nafuu kwa upande wao na Serikali nayo itakuwa ina nafuu kwa kuangalia mengine ya kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi nayo ina mchango mkubwa wa kusaidia wananchi na vijana wa Kitanzania lakini kuna baadhi ya sekta hizi huwa na fursa ya kuwaajiri watu kutoka nje ya nchi au pengine kutoka kwao, ambayo inaleta tatizo kwa vijana wetu kukosa kazi na nafasi hizo kuchukuliwa na watu ambao si raia, eti tu kwa sababu hawana uzoefu, wavivu na kadhalika. Wizara iwe macho kwa mtindo huu unaojitokeza hasa katika sekta za hoteli, kuna vijana wengi kutoka Kenya na Zambia.

Mheshimiwa Spika, kuna unyanyasaji katika sekta hizi ama kwa upande wa mishahara au dhamana "*post".* Kuna vijana wenye viwango bora vya kazi, elimu lakini utakuta wazawa hawapewi dhamana na kama wakipewa huwa ni msaidizi na yule kutoka nje ndio huwa bosi. Pili, wanaweza wote wakawa na kiwango kimoja cha elimu lakini anayetoka nje mshahara huwa mkubwa kuliko kijana wa Kitanzania, huu ni unyanyasaji wa kisaikolojia ili kumfanya kijana kuichukia kazi na nchi yake, hili liangaliwe kwani lipo katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa ajira, katika taarifa ya Wizara, vijana walioajiriwa ni 9,056,217 sawa na 86.6 % na wasioajiriwa ni 1,398,677 ni sawa na 13.4%. Je, hawa vijana walioajiriwa ni pamoja na wale machinga wanaoranda mchana kutwa kwa kuuza karanga, vibiriti, kahawa na nguo mkononi ambao hata chakula chake kwa siku hakipati? Naomba Waziri atakapokuja kujibu hoja, atufafanulie, wameajiriwa katika kada gani?

Mheshimiwa Spika, jumla ya watoto 22,243 wametolewa katika utumikishwaji na kupatiwa mafunzo ya fani mbalimbali. Ni vizuri lakini "*what next*", watoto hawa hivi sasa wanafanya nini? Wamejiajiri wenyewe au Serikali wamewaajiri? Waziri hukutueleza faida iliyopatikana kwa vijana hawa *at least* wananchi wakaelewa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA), ni jambo la kutia moyo kuona vijana wetu sasa wanaweza kupata ajira nchi za nje, hili ni jambo la

kuleta faraja. Lakini naomba Waziri aangalie ni aina gani za kazi, kuna ushahidi tosha kwa baadhi ya mawakala hupeleka vijana wetu nje kwa kufanya kazi za nyumbani na hupata taabu kwanza hawana mapumziko, mshahara hawapati, pasi zao za kusafiria hunyang'anywa, mwisho hufanyiwa mambo ya uchafu. Waziri ni vyema akaliangalia hili kwani limewakuta hata vijana wa jirani zetu hapo Kenya na kufanya Serikali kuzuia vijana wake wasiende kufanya kazi huko hasa za nyumbani.

Mheshimiwa Spika, pensheni kwa wanaoacha kazi ni jambo la busara, haipendezi kuona wananchi waliofanya kazi toka utoto, ujana na hata kuwa watu wazima, wakateswa na Serikali yao wakati hivi sasa hawana nguvu hata ya kumpiga mtu seuze kumtupia maneno. Waziri, wazee hawa wanahitaji mafao yao na wapewe kulingana na uchumi uliopo sasa na sio uliopita kwa kumpa mtu fedha ambayo haimtoshi hata kwa siku tano seuze akawa mzee huyu ana familia kubwa, anahitaji fedha ya usafiri ya kwenda na kurudi ofisini kuchukua fao lake!

Mheshimiwa Spika, nashauri vijana wapatiwe mikopo nafuu kutoka benki ili waweze kujiajir; vijana wahamasishwe kwa kujiweka pamoja na kuanzisha *SACCOS*; vijana wapewe elimu ya kuwasaidia katika maisha yao na vijana waelimishwe wasichague kazi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia na kutoa ushauri kwenye Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, napenda kutoa ushauri kwamba Tume hii ibadilishwe na kuwa "Baraza la Usuluhishi". Aidha, Tume ifungue ofisi zake Mikoani na hata Wilayani.

Mheshimiwa Spika, pili, Tume ya Usuluhishi iajiri watumishi ambao wamesoma Sheria *(LLB)* ili kuepusha usumbufu ambao umekuwa unajitokeza kwani baadhi ya Wasuluhishi wamekuwa wanafanya usuluhishi na Mahakama Kuu inaagiza usuluhishi huo urudiwe upya.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kushauri Sheria ya Taasisi za Kazi, Na.7 na 6 ya mwaka 2004 ifanyiwe marekebisho ili mlalamikaji au mlalamikiwa asiporidhika kwenye Tume akate rufaa (*appeal*) isiwe *review* pekee.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Napenda kutoa ushauri kwamba duniani kote mifuko hii pia inahusisha sekta zisizo rasmi yaani *informal sector.* Hii hujumuisha waendesha bodaboda, wavuvi, wakulima na kadhalika nao wanajiwekea kipato na kunufaika uzeeni. Mfano mzuri ni Ibara ya 27, Katiba ya Afrika Kusini pia Katiba ya India inatambua *informal sectors* kwenye hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, usumbufu wa *PSPF* – Kigoma. Napenda kupata majibu kutoka kwa Serikali dhidi ya *PSPF*-Kigoma ambao wamekuwa wakishindwa kutatua matatizo ya wastaafu, hata mimi Mbunge nikituma *emails* hamna jibu. Pia *PSPF* wamekuwa wakichelewesha malipo kwa waliokuwa wanachama wake. Napenda kupata majibu kwa nini mfuko huu umekuwa na usumbufu mkubwa kwa wazee na

usumbufu huu utaisha lini? Pia napenda kupata majibu ya Serikali wanachama wa *PSPF* wa Wilaya ya Kibondo wamechoka kusumbuliwa muda mrefu, je, usumbufu huo utaisha lini?

Mheshimiwa Spika, ukosefu na tatizo la ajira. Kumekuwa na tatizo kubwa la ajira na kwa mujibu wa kitabu cha Serikali cha Taarifa ya Hali ya Uchumi mwaka 2011, takwimu zinazotumika ni za mwaka 2006. Napenda kutoa ushauri kwa Serikali ifanye utafiti kwa miaka hii ili kuweza kubaini idadi sahihi ya Watanzania wasio na ajira.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa ushauri kwa Serikali kuwa na mfumo wa kuwatambua wanafunzi wote waliomaliza na wanaoendelea kumaliza vyuo vikuu na Serikali ijue wako wapi, wanafanya nini na wanalipwa nini. Hii itasaidia kuwatafutia fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, migogoro na migomo ya wafanyakazi. Napenda kutoa ushauri kwa Serikali kujitahidi kutatua migogoro kabla ya migomo na usuluhishi. Serikali iwalipe wafanyakazi fedha zao kabla ya migomo aidha taasisi za Usalama wa Taifa na kadhalika, zifanye kazi yake na kushauri ili wafanyakazi walipwe kabla ya migomo. Serikali inayotatua migogoro kwa migomo au maandamano ni kuhatarisha ustawi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa kigeni wanaoajiriwa nchini – Wilayani Kibondo. Napenda kupata majibu juu ya raia wawili wa Kenya walioajiriwa

kwenye Idara ya Afya Wilayani Kibondo. Je, utaratibu gani ulitumika na waliajiriwa kwa sheria zipi? Kwani wamefika Kibondo – Kigoma lakini hawajui hatma yao na pia hawajui *payment* zao zitakuwaje kwani hawapo kwenye orodha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Wafanyakazi, ni mali ya wafanyakazi wenyewe lakini kwa kuwa Mifuko hii inafanya biashara mbalimbali, ni vyema ofisi ya sasa chini ya Mkurugenzi wa *SSRA* ikawa wazi katika kueleza kwa usahihi ni vipi fedha za Mifuko hiyo inafanya biashara na namna inavyopaswa kutoa gawio litokanalo na biashara kwa fedha zinazokusanywa na Mifuko husika ili kila mfanyakazi mwanachama katika mifuko hiyo aelewe kwani kila baada ya muda fulani au atakapostaafu ajue kwamba anastahili kupata asilimia ngapi ya fedha aliyochanga kwa muda alioanza uanachama huo.

Mheshimiwa Spika, usalama pahali pa kazi. Suala la usalama kwa mfanyakazi hasa pahala pa kazi na hata mazingira ya eneo la kazi, ni jambo la msingi na hasa ukizingatia kwamba gharama za matibabu kwa sasa katika nchi yetu ni ghali sana lakini pia mfanyakazi hasa katika maeneo ya viwanda kwa kweli wanafanya kazi za ku-*risk* kwani wanacheza na vitu vyote ambavyo ni vya hatari kwa usalama na maisha yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, usalama migodini. Watanzania wanaofanya kazi katika migodi nao wana mazingira magumu sana na wanapaswa waangaliwe, kwani mazingira wanayofanyia kazi ni magumu na ni ya kubahatisha lakini  pia manyanyaso wanayopata ni makubwa toka kwa wamiliki wa migodi. Hivyo basi, ni vyema *OSHA* wafike katika maeneo hayo ili kujionea hali halisi ili waweze kutoa ushauri kwa usalama wa wafanyakazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana, *ILO* kwa kila mwaka hutoa fedha kwa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania ili kusaidia vijana kuweza kujiajiri au kuwajengea mazingira mazuri ya kuweza kujiajiri.
Utaratibu huu wa *ILO* kusaidia nchi yetu umeanza lini na hadi leo hii ni miaka mingapi Tanzania tumekuwa tukifaidika na mpango huu? Lakini sio hilo tu, je, ni vijana wangapi wa Tanzania Bara na Zanzibar ambao wamefaidika na fedha hizo lakini pia ni mtindo upi unaotumika katika kupata hao vijana ili kuweza kufaidika na msaada huu wenye lengo la kuwakwamua vijana wetu ili wajiajiri wenyewe?

Mheshimiwa Spika, suala la mwanachama wa mfuko kupata mafao yake kwa utaratibu wa kutimiza umri wa miaka 50-60, jambo hili ni tatizo na mfanyakazi ni vigumu kustaafu halafu asubiri kutimiza miaka hiyo ndipo apate mafao yake. Jambo hili linaleta manyanyaso na hata dhara inaweza ikawa ni kuwaibia au kuwakosesha haki zao wafanyakazi wetu hasa ukilinganisha sababu mbalimbali zitolewazo na Serikali kwamba kumbukumbu za wastaafu zimepotea

na ndio miongoni mwa sababu za Serikalii za kuchelewesha ama kutolipa mafao kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Gaudentia M. Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira kwa hotuba nzuri na ambayo imejaa uchambuzi wa kina ambayo imetolewa asubuhi hii. Naomba bila kuchelewa nitamke kwamba ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimpongeze sana Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, Mbunge wa Segerea kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu. Hongera sana Dkt. Milton Makongoro Mahanga.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM imetuelekeza kwamba, Serikali yake ikiingia madarakani kazi yake kubwa itakuwa ni kuweka mazingira ambayo yatamwezesha mwananchi hasa vijana na wanawake waweze kujiajiri. Jambo hili ni lazima lisisitizwe, kuweka mazingira ni kupeleka umeme vijijini, kupeleka maji vijijini, kutengeneza barabara za vijijini ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao na kuyapeleka katika magulio na katika masoko. Kufikiri kuwa Serikali inaweza kuleta ajira bila ya kuwa na miradi ni kuibebesha Serikali mzigo usiobebeka. Ajira ni miradi bila miradi hatuwezi kuwaajiri watu wetu. Katika hili ipo haja ya kuwaunganisha wananchi katika vikundi

vya uzalishaji mali kupitia ushirika *SACCOS*, vikundi vya vijana wa akinamama na kuhakikisha wanapatiwa mikopo kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu pia hakina budi kusisitize huduma za ugani na matumizi ya teknolojia ya kisasa na kuachana na utaratibu wa kutegemea mvua na badala yake tusisitize kilimo cha umwagiliaji. Ajira kubwa katika nchi yetu ipo katika kilimo. Watanzania takribani asilimia 80% wanategemea kilimo *spill over effect* ya kilimo ni kubwa na ambayo itatuondolea tatizo la ajira nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu liwe ni kumpatia Mtanzania chakula, mavazi, malazi, makazi na upatikanaji wa huduma za afya, elimu, maji, huduma za kiuchumi na kijamii kwa bei nafuu kadri iwezekanavyo. Aidha, litakuwa ni jambo jema kuwa na vyuo vya *VETA* ambavyo vitaimarisha stadi za vijana wetu, hakuna mtu atakayemwajiri kijana kama hana hakika kwamba mhusika ana ujuzi. Ujuzi hapa ni pamoja na utaalamu kama vile, useremala, uashi, ufundi umeme, fundi bomba, uhunzi, kushona viatu, ufundi nywele, upishi, ulinzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja hii.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayoifanya katika kusimamia mambo yote yanayohusu ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nina maoni yafuatayo:-

(i) Kuzingatia na kuyafanyia kazi kwa utekelezaji Maazimio yote yaliyoainishwa katika Maelezo Binafsi yaliyotolewa na Mheshimiwa Selemani Jafo.

(ii) Naiomba Serikali isimamie vyema usalama wa wafanyakazi mahala pa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya busara kwa kuwajali wazee na kuwapatia pensheni, hilo ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wengi wanaopata mafunzo *VETA* na *SIDO* bado wapo mitaani kwa kukosa mitaji ya kuweza kuanza shughuli za kujiajiri. Naomba sana Waziri apange mkakati endelevu wa kuwasaidia vijana hao kwa kuwachukulia dhamana ya mikopo kwa vikundi na baadaye wajipatie ajira wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Waziri asimamie sekta binafsi wanapotaka kuajiri vijana kama kwenye hoteli na viwanda vidogovidogo, waombe *VETA* wawapatiwe vijana hao kulingana na elimu walizozipata pale chuoni. Hii itawezesha vijana wengi kujiunga na masomo *VETA* badala ya kuzurura ovyo kwa kuwa na uhakika wa ajira baada ya kuhitimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, ahsante.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote kwa kazi wanazofanya. Ninapenda kuchangia yafuatayo:-

(i) Elimu itolewe zaidi kwa wafanyakazi ili watumie vyama vyao vya wafanyakazi kudai haki zao, waajiri nao wapewe elimu kuhusu kufuata sheria za kazi.

(ii) Vyombo vya usuluhishi wa migogoro viwezeshwe kufanya kazi kikamilifu kwa mujibu wa sheria. Wawezeshwe kifedha ili vikao vifanyike kufuatana na kanuni na sheria.

(iii) Mifuko ya Hifadhi inapowekeza faida inayopatikana ielekezwe katika kuongeza mafao ya wafanyakazi.

(iv) Kuwe na jitihada ya makusudi ya kuwa na ajira kwa ajili ya walemavu.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, sehemu nyingi za kazi hawaelewi utaratibu na Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini (*Employment and Labour Relations Act, 2004*) kwa nini Serikali haitoi elimu ya kina juu ya sheria hii pamoja na kuhusu migomo kazini ambayo imeonekana kukithiri mwaka huu na miaka ya hivi karibuni? Ibara ya 20 na 84 zilizopo zinapingana, *CMA* haifahamiki katika sehemu nyingi nchini.

Mheshimiwa Spika, malipo kidogo na unyanyasaji watumishi katika hoteli zilizopo katika Hifadhi za Taifa, Wizara au Serikali ina mpango gani wa kufuatilia tatizo hili sugu? Watumishi hao wanalipwa mishahara na mafao hafifu. Kwa watumishi hawa ziara za mara kwa mara zifanyike.

Mheshimiwa Spika, kupanua ajira nchini, kwa nini ajira zinaendelea kuwa finyu kwa wahitimu wetu nchini? Ni vizuri Wizara hii iandae maelezo kwa Wizara nyingine ili ziweze kupanua ajira kwa Watanzania suala hili ni muhimu ni vyema litafutiwe utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuweka mfumo wa aina moja wa mafao ya hifadhi ya jamii kwa vile watumishi wote nchini wanajalisha kulingana kuwa wanaitumika Serikali hii moja, mafao yao na kanuni virekebishwe.

Mheshimiwa Spika, uanzishwe utaratibu wa kulipa posho kwa wazee na wasomi wote wasio na ajira, ni vyema kuanza kutoa posho kwa wale wote waliofikia maiaka 60. Pia ni vyema kutoa posho (*social support system*) kwa wasomi wote nchini ambao hawakupata bahati ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahoteli mengi nchini na sehemu nyingine kuajiri wageni, Watanzania wengi wanakosa ajira kwa kuwaajiri wageni, suala hili liangaliwe upya na kwa makini.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti. Pia nampongeza Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara. Waziri naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Ukurasa 27(c) panapozungumzia *NSSF,* narejea tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri inayofanywa na *NSSF* chini ya Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe wake, Mkurugenzi Mkuu Dkt. Ramadhani K. Dau pamoja na timu yake yote ya menejimenti.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana *NSSF* kwa daraja la Kigamboni, ni kilio cha siku nyingi cha wananchi wa Dar es Salaam. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie jambo moja pale Kurasini linapoanzia daraja, tunadaiwa fidia na kampuni mbili; moja, *Alifu Sttom Company Limited* pili *Miembe Saba Company Limited* naomba Serikali na *NSSF* walipe wadai hao kabla ya kuanza ujenzi wa daraja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Waziri kwa namna ilivyochambua masuala mbalimbali ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ni Wizara mama katika kuipatia nchi watumishi pamoja na usimamizi wa rasilimali watu. Naipongeza Wizara kwa namna ya pekee kwa namna inavyoendelea kuisimamia migogoro mbalimbali kati ya wafanyakazi

na waajiri, kwa mfano, migomo iliyokuwa imeandaliwa na Madaktari pamoja na Walimu.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa sheria mbalimbali hapa nchini umeepushia mbali uwezekano wa kuzuka kwa migogoro ambayo ingeathiri kwa kiasi kikubwa ukuzaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Wizara kwa namna ya pekee kwa jinsi inavyosaidia ukuzaji wa ajira nchini. Sekta ya umma na sekta binafsi zimeshirikishwa kikamilifu katika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la mtazamo hasa kuhusiana na uchaguzi wa ajira miongoni mwa Watanzania ni changamoto nyingine inayopaswa kushughulikiwa ipasavyo kwani vijana wengi hawataki kufanya kazi, badala yake tunakuwa na kundi kubwa la vijana walalamishi na watu wasiokuwa na maadili na uzalendo kwa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa namna Wizara inavyolisimamia vema Shirika la *NSSF,* shirika ambalo limejengea Taifa heshima ndani na nje ya nchi miradi inayosimamiwa na shirika hili imeleta mageuzi makubwa katika Mashirika ya Umma na kuwa kielelezo kwamba kumbe Watanzania tukiamua tunaweza.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Mashirika mengine ya Umma kuiga mfano mzuri wa Shirika la Mfuko wa Hifadhi za Jamii *(NSSF)*. Hongera kwa kazi

nzuri, Watanzania tunajivunia kazi zuri za shirika hili kwa kuleta mapinduzi nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kuyaelekeza Mashirika mengine kama Shirika la Bima la Taifa na kadhalika nayo yaoneshe michango yake kama *NSSF* ilivyoleta mageuzi makubwa katika utendaji kazi wa taasisi za umma. Natoa rai kwa waajiri mbalimbali nchini kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuboresha mafao ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mipango yote iliyopangwa kwa lengo la kutekelezwa katika bajeti hii ni vema ikatekelezwa kama ilivyopangwa. Naishauri Serikali iiongezee fedha Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hotuba nzuri ya Waziri na naunga mkono hoja hii. Sasa napenda niishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *NSSF/Pension Funds*, napongeza juhudi ambazo Mifuko ya Hifadhi wamefanya katika uwekezaji katika nchi hii hasa katika miradi mikubwa ya majengo/madaraja na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, tunashauri NSSF itumike pia kutekeleza miradi ya ngazi za chini mfano, ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu, zahanati, madawati ili kupunguza upungufu

uliopo katika jamii zetu, Watanzania walio wengi hawaoni faida za Mifuko hii kwa sababu miradi inayotekelezwa iko mijini na iko kwenye majengo makubwa/vyuo vya juu. Serikali ikope pesa hizo toka kwenye Mifuko hiyo ili mipango iweze kwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, huduma za ajira kwa vijana wetu zifanyike katika hatua zote za Kitaifa na Kiwilaya kwani fursa hizi za ajira zinatangazwa katika ngazi za Wilaya na Taifa, na kuacha kufika ngazi za Tarafa, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, mafao ya kujitoa, Mifuko ya Jamii iridhie maombi ya wafanyakazi wanaotaka sheria ya kujitoa ya mafao irekebishwe.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudensia M. Kabaka; Naibu Waziri, Dkt. Makongoro Mahanga; Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii. Nashindwa kujizuia kuwa bajeti hii ni nzuri sana kwani imeainisha vipaumbele vizuri kwa maslahi ya Watanzania hususani vijana.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza uamuzi wa Serikali wa kuunda Baraza la Vijana la Taifa kwani itawasaidia sana kuwaunganisha vijana bila kujali itikadi zao wala dini zao. Chombo hiki kikianzishwa kitawasaidia sana kujadili mambo au kero mbalimbali zinazowakabili kuliko ilivyo sasa hadi inafikia kugombana wao kwa wao bila sababu zozote za

msingi, napenda kujua Muswada huu utaletwa Bungeni lini kujadiliwa na kupata baraka za Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kuwa mpango wa Serikali wa kutaka kila Halmashauri kutenga asilimia tano na Serikali kuchangia ni mpango mzuri sana na una lengo zuri la kuwakomboa vijana kuondokana na umaskini. Tatizo linalojitokeza hapa ni pale Halmashauri zinaposhindwa kutenga kwa kisingizio cha makusanyo duni.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe kauli ya Halmashauri iweze kutenga bila kukosa na vile vile Serikali kuongeza kiwango cha kuchangia Mfuko huu ili uweze kuwa na tija kwa vijana kwa kuwawezesha kukopa kwa ajili ya kutunisha mitaji yao. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya ujasiriamali kwa vijana, vijana wengi wanapoanzisha miradi ya ujasiriamali hushindwa kuendelea na wale waliokopa hushindwa kurudisha mikopo yao kwani wengi huwa hawana elimu ya kuendesha miradi au biashara zao. Naiomba Serikali kutoa elimu kwa vijana kwanza ya namna ya kuendesha miradi yao kabla ya kuwapa mikopo. Napenda kujua fedha kiasi gani zimetengwa za kutoa elimu kwa wajasiriamali kwenye bajeti hii ya 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Idara ya Kazi Mikoani, napenda kukiri kuwa Ofisi za Idara ya Kazi zilizoko Mikoani ikiwemo Ofisi ya Kazi ya Mkoa wa Singida zinafanya kazi kwa mazingira magumu sana

kwani bajeti wanayotengewa ni ndogo sana ukilinganisha na majukumu waliyonayo. Hali hii inawavunja moyo pia inaweza kuwa kishawishi cha watumishi kupokea rushwa. Napenda kujua bajeti hii imeongeza mgao kwenye sekta hii kwa asilimia ngapi. Naomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wanipe majibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zawadi za wafanyakazi bora kwenye taasisi za Serikali; napenda kuipongeza Serikali kwa kutenga siku ya wafanyakazi yaani Mei Mosi kila mwaka. Nayapongeza Mashirika yote ya Umma na yale ambayo siyo ya Serikali kwa jinsi yanavyowathamini wafanyakazi bora kwani huwapatia zawadi nono ambazo hutoa changamoto kubwa kwa wafanyakazi wengine ili na wao waweze kupata tuzo hizo vipindi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lipo kwenye taasisi ambazo ziko chini ya Serikali hupata zawadi ndogo sana tofauti na Mashirika ya sekta binafsi. Napenda kujua ni mkakati gani wa kutunisha zawadi hizi za wafanyakazi bora wanaoteuliwa toka Serikalini. Naomba maelezo ya Waziri au Babu yangu Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Alhaj Ramadhani Dau na watumishi wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusaidia Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia Mfuko wa NSSF mfano chuo kikuu cha Dodoma. Naomba Serikali iendelee kuwatumia pamoja na

kuwaunga mkono ili waendelee kusaidia Serikali yetu kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ombi, kwa kuwa Mfuko huu unazalisha sana na fedha hizi zinatokana na wafanyakazi wakiwemo wastaafu, naomba malipo ya Pensheni kupitia Mfuko huu yaongezwe kwa wastaafu ili waendelee kufaidi matunda yao. Vile vile, manufaa wanayopata wastaafu yaainishwe na kuwekwa wazi ili kila mwanachama anapostaafu awe anajua haki zake.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalize kwa kuunga mkono hoja hii, Mungu awatangulie walioshiriki kuandaa utekelezaji uwe wenye tija.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira ya mwaka 2012/2013 naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali wakati wa kutoa ajira, Serikali itoe kipaumbele kwa vijana na akinamama kwa mujibu wa elimu zao, aidha Serikali iweke mkakati wa ajira hizo zipitie JKT iwe ni lazima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusimamia maslahi ya wafanyakazi, naishauri Wizara kusimamia ipasavyo maslahi halali yatolewe kwa wakati na yamfikie mhusika aliyekusudiwa, Wizara iwe macho na maafisa maslahi katika taasisi husika.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza

napenda kumpongeza Mheshimiwa Gaudencia Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara yake akisaidiana na Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, nawapongeza pia kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa pensheni ya wazee, je, suala hili litatekelezwa lini? Napenda kuijulisha Wizara kwamba wapo wazee wengi wastaafu waliolipwa kwa mkupuo wakati wao wa kustaafu lakini wanajaribu sana kufuatilia waingizwe kwenye utaratibu wa *Pension* imeshindikana kwa madai kwamba hawana vielelezo ingawa wanazo hati zinazoonesha kuwa ni wastaafu, je, Wizara inawasaidiaje wazee hawa?

Mheshimiwa Spika, wapo walemavu wengi hapa nchini, tatizo kubwa ni ukosefu wa ajira jambo linalopelekea kuwa ombaomba ingawa wanao uwezo wa kufanya kazi, Naiomba Wizara ianzishe Mfuko Maalum wa kusaidia ajira kwa walemavu aidha, kwa njia ya kuwapatia mikopo na elimu ya ujasiriamali au kuanzisha vituo vya uzalishaji wa bidhaa fulani au yote mawili kwa pamoja. *Caritas German* wanao utaratibu mzuri wa kuwapa ajira walemavu hata wale wenye mtindio wa ubongo, naomba Waziri atembelee huko Ujerumani aonane na *Caritas* na wabadilishane uzoefu.

Mheshimiwa Spika, vijana na akinamama wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira kwa upande wa vijana, wapo wengi wasiopenda kujituma

na hata wanapopatiwa ajira wanashindwa kufanyakazi kwa bidii. Ni ushauri wangu kuwa, Wizara iwapatie vijana elimu ya kujitambua msisitizo ukiwa katika "Mtu ni kazi" wapewe pia elimu ya ujasiriamali. Kimsingi vijana walio tayari wafanyakazi kwa kujiajiri wanakabiliwa na tatizo la kukosa mitaji na hasa kukosa dhamana kwa ajili ya kupata mikopo. Naomba Wizara ifuatilie suala la MKURABITA kama linaweza kuchangia kuongeza ajira kwa akinamama na vijana, lakini pia kwa wale wasio na kitu kabisa basi wafanyiwe utaratibu wa kudhaminiwa ili wakopesheke hasa wale wenye kuonesha bidii ya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kazi inayoendelea kufanya. Wizara ya Kazi na Ajira ni Wizara inayosimamia sera ya kazi na ajira, sera inayoingiliana na Wizara na sekta zote. Ajira na kazi ndio kusudio mojawapo kuu na msingi mkuu wa miradi mbalimbali ya kiuchumi na mipango yote ipangwayo na aidha, Serikali au sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa la ukosefu wa ajira na kazi katika nchi yetu. Serikali haina uwezo mkubwa wa kuajiri sekta binafsi nayo bado haijaweza kukabili tatizo la ajira ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tunao vijana wengi ambao wanamaliza shule za msingi, sekondari, vyuo na hata wachache hawajasoma kabisa, njia pekee ya kuondokana na tatizo hili kubwa ni Wizara sasa

kushirikiana kikamilifu na Wizara na sekta mbalimbali kwa kutambua idadi ya vijana wasio na ajira, sifa zao na mahali waishipo yaani *Database* ya wasio na ajira na wanaozalishwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia itambue njia kuu za kuanzisha au kutoa ajira. Kwanza iwe na takwimu za waajiri wa sasa iwatambue, itambue sekta zote rasmi zinazotoa ajira na kushirikiana nazo kwa kuweka sera ya ushirikiano kiutendaji kati ya Wizara na sekta hizo. Bado hakuna ushirikiana bayana na rasmi kati ya sekta binafsi na Wizara katika kukuza ajira. Wapo waajiri wengi katika sekta binafsi ambao ndio tegemeo kubwa sana ambao hakuna utaratibu wa kusaidiwa na Wizara hata kwa kutambuliwa, kusikilizwa matatizo na changamoto zao ili kuboresha uwezo wao wa kuajiri. Yapo makampuni binafsi yenye ajira zaidi ya wafanyakazi 1,000 lakini wala hawajatambuliwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara sasa itambue kundi kubwa la vijana wanaojiajiri katika sekta zisizo rasmi angalau yafuatayo yafanyike: Wapewe maeneo maalum ya kufanya shughuli zao, wapewe mafunzo maalum kulingana na mazingira ya kazi au shughuli wanazozifanya, uangaliwe uwezekano wa kuwasaidia na njia mbalimbali za kuwapatia mitaji.

Mheshimiwa Spika, haya yote hayatawezekana, Wizara ikiyabeba yenyewe, hapa ni mtambuka yaani Wizara iweke utaratibu maalum wa mawasiliano kati yake na Wizara nyingine husika kama TAMISEMI, Wizara ya Ardhi na kadhalika ili sera hii iweze kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana kabisa maana katika Jimbo langu la Kibaha, tayari tumekuwa na programu ya kambi za vijana wajasiriamali na tumeshirikiana na Mkoa, Wilaya, Halmashauri zote na taasisi mbalimbali tumefanikiwa sana katika zoezi hilo maana vijana wengi ambao hawakuwa na ajira wamepata mafunzo ya ufundi, ujenzi na wafadhili walijitokeza kuwapa mitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kambi hizi zimefanyika kule Msonga na nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa ufadhili na msaada wake, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa usimamizi na kuhakikisha hili linafanyika, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Wenyeviti wa Halmashauri kwa ushirikiano walioonesha.

Mheshimiwa Spika, hakika kambi hizi kama zitachukuliwa Kitaifa zitaleta mwamko mkubwa katika suala la ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ameonesha dhahiri kuwa Serikali ipo makini kuhakikisha kuwa matatizo ya ajira kwa Watanzania yanapatiwa ufumbuzi kwa kuzingatia fursa zilizopo. Lakini lipo tatizo kubwa sana kwa makampuni mengi nchini kuajiri wageni kufanya kazi ambazo hata Watanzania wana uwezo mkubwa wa kuzifanya. Wizara imekuwa haichukui tahadhari ya kutosha, lakini pia inatoa vibali bila ya kuthibitisha vigezo kwa wageni kuja kufanya kazi kwa maana ya vyeti vyao, ujuzi na uzoefu. Ikiwa Mtanzania aliyesoma nje anatakiwa vyeti vyake vipate ithibati kutoka *TCU*, kwa nini wageni waruhusiwe bila ya kuthibitishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ifanye jitihada za kutosha kulinda ajira kwa Watanzania katika sekta zote ikiwemo biashara kwa maana sasa wageni wamefika hata vijijini na kunyima fursa wazawa ambao hawahimili ushindani kwa ufinyu wa mitaji na uzoefu wa biashara tabia hii ikomeshwe mara moja kwa kuwazuia kufika na kuishia mijini tu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba Waziri amezungumzia suala la ajira kwa vijana kuwa ni changamoto kubwa, naishauri Wizara ishirikiane na Wizara ya ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kutumia Jeshi hili ili kutatua tatizo la ajira kwa vijana kwa kuanzisha kambi maalum kuwajengea vijana uwezo wa kujituma, kujiamini na uadilifu. Lakini pia kambi hizi vijana watapata mafunzo ya aina mbalimbali kama ufundi, ufugaji na kilimo. Serikali iharakishe kutatua tatizo hili maana sasa limekuwa kama ni la kisiasa. Wizara

itangaze fursa zilizopo kujiajiri na kujenga uwezo wa vijana kujitambua na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana katika ulipaji mishahara na maslahi ya watumishi katika sekta mbalimbali hasa binafsi. Wageni wengi wanalipwa mishahara mikubwa zaidi ya Watanzania bila kuangalia uzito wa kazi wanazofanya. Hii si sahihi kwa kujenga ustawi na mazingira bora kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwa mafao ya wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, nawashauri kuwa suala hili si la kisiasa. Elimu ya kutosha itolewe ili kukomesha tabia hii kwa maana uhai wa Taifa kiuchumi, lakini pia uhai wa Mifuko unategemea sana michango ya wanachama. Suala la wanachama kutaka kujitoa kabla ya umri wa kustaafu (*withdraws*) si sahihi na ni hatari sana. Hii ieleweke kuwa pale ambapo mtu amejitoa na kufikia umri wa kustaafu baada ya kutumia vibaya mafao yake, jukumu linarudi kwa Serikali na jamii nzima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, wastaafu wa miaka ya 90 na 2000 mwanzoni mafao yao ni kidogo mno. Kuna watu wanapata *Pension* ya sh. 2000/= au 5000/= kwa mwezi, kwa kuwa Mifuko ya *Pension* inawekeza kwenye miradi mbalimbali, nashauri Serikali itunge sheria ya kuongeza *Pension* kwa wastaafu hawa na kuongeza kiwango kutoka kwenye faida ya miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mifuko ya *Pension* ya mwaka ina kasoro kubwa ambayo wananchi wengi wana manung'uniko makubwa hasa kwenye kipengele cha kupata mafao ya waajiri mpaka wanapofikisha umri wa miaka 60 hata kama waliacha au kuachishwa kazi mapema maishani. Naiomba Serikali ilete Muswada wa kurekebisha kasoro hii haraka sana.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Walimu Tanzania kinapewa michango kutoka kwenye mishahara ya Walimu nchi nzima. Michango hiyo imekiwezesha chama hicho kuwekeza kwa mfano mradi wa jengo la Walimu pale Ilala, Dar es Salaam. Je, mradi kama huo unawafaidishaje Walimu nchini? Au ni wa manufaa kwa viongozi tu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, suala zima la ajira, takribani karibia wanafunzi 600,000 wanaotafuta kazi lakini cha kusikitisha mpaka sasa hivi bado kuna vigezo vinavyotumika haswa kuhusu uzoefu katika kazi. Hivi Serikali inasaidiaje hawa vijana unakuta ni wasomi wazuri, lakini kigezo hiki kinawashinda. Je, ni kwa nini mikataba mingine ya wastafu wanairudia (*extend)* kwa kazi ambazo siyo za kitaalam sana, kwa mfano, Wakurugenzi wa Halmashauri? Ni kweli kazi hii haiwezi kufanywa na kijana aliyemaliza kozi? Ni kwa nini kabla ya kustaafu vijana wasifanye kazi kwa vitendo ili muda

wa Mkurugenzi kustaafu ukifika wakute tayari yule kijana ameshaelewa kazi hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa wageni, ni kwa kiasi gani Serikali inafanya ili iweze kulinda ajira kwa ajili ya wananchi wake? Pamoja na utandawazi kuwepo lakini bado kila nchi kuna baadhi ya ajira huwa ni kwa ajili ya wananchi wake. Kwa mfano, hapa kwetu kazi kama za ulinzi, kazi za magereji, kukwangua magari rangi, kuosha magari, kazi za viwandani unakuta kwa kiasi kikubwa kazi hizi zinafanywa na raia wa kigeni hasa raia wa kutoka Bara la Asia (Wachina na Wahindi). Kwa mtindo huu mwisho wa siku vijana wetu wanakosa kazi wanaishia kuwa wezi au kujiingiza katika biashara haramu za dawa za kulevya na hatimaye kupunguza nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, je, sheria inasemaje kuhusu kuwapa vibali vya kazi kwa wageni ambao kazi hizo zinapaswa kufanywa na wazawa? Je, Serikali ipo tayari kufanya msako kwa kuanzia katika viwanda, magereji ya Wachina, *super market ya shopaz Plaza* iliyopo Old Bagamoyo *road* na kuwafutia vibali kwa wale wote watakaobainika wanafanya kazi ambazo kisheria zinatakiwa kufanywa na wazawa?

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Jamii *(NSSF)* ni jambo zuri kuwa na Mifuko lakini ni kwa jinsi gani wanachama wanafaidika na michango yao zaidi ya kupata wakishaacha kazi? *NSSF* imekuwa ikijenga majengo mengi sana ya kifahari na ya kati. Je, kwa nini *NSSF* isijenge nyumba za bei nafuu ili iweze kuwakopesha

wanachama wake kwa riba nafuu? Ili nao waweze kuonja uzuri wa michango yao?

Mheshimiwa Spika, *NSSF* imewekeza sana katika miradi mingi, ni lini Serikali itaweza kulipa muda ya kukijenga chuo kikuu cha Dodoma sababu tayari chuo hiki *school fees* zinalipwa hivyo wanao wajibu wa kuanza kulipa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI na Virusi vya UKIMWI mahali pa kazi, kuna njia ya kupambana na gonjwa hili naipongeza Wizara kwa kutimiza pendekezo hili lakini ningependa kujua je, ina idadi, ni wafanyakazi wangapi walioathirika na ugonjwa huu ili waweze kuwasaidia?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *NSSF* na mafao kwa wastaafu ni ukweli usiopingika kwamba Mashirika mengi ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini, ikiwepo *NSSF* yamekuwa yanapata faida kubwa sana kutokana na kuwekeza katika miradi mingi sana. Ni muhimu ikumbukwe kwamba chanzo cha fedha hizo ni michango ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwamba imefika wakati sasa Mashirika yote ya Hifadhi ya Jamii ikiwepo *NSSF* yatazamwe viwango vinavyolipwa kwa wastaafu na wale wote ambao mikataba yao ya kazi itafikia mwisho. Ni busara ya

kawaida kumlipa vizuri mtumishi anayechangia vizuri na kwa muda mrefu baada ya kustaafu. Kinyume na hivyo Mifuko hiyo ya Hifadhi ya Jamii haitakuwa na maana yoyote.

Mheshimiwa Spika, *OSHA* ni wakala wa usalama na afya mahali pa kazi. Huu ni wakala muhimu sana kwa usalama na afya za wafanyakazi. Ni muhimu basi wakala huu uwezeshwe ili uweze kufanya ukaguzi wa usalama na afya za wafanyakazi. Yako baadhi ya Mashirika ya Umma na watu binafsi, viko pia baadhi ya viwanda ambako afya na usalama wa wafanyakazi haviangaliwi vizuri. Katika hali na mazingira hayo ni lazima Wakala huu ufanye kazi yake vizuri ili kufikia mashirika na viwanda vyote kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba usalama na afya za wafanyakazi vinazingatiwa. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kwamba Wakala huu unatengewa pesa ya kutosha ili uweze kufanya kazi hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa wageni, bado upo udhaifu mkubwa sana katika suala la ajira kwa wageni ukitembelea viwanda vingi na baadhi ya taasisi hasa za binafsi zinazoendeshwa na wawekezaji wa kigeni, utakuta waajiriwa kutoka nje wakiwa wengi sana kinyume na sera na Sheria ya Ajira kwa wageni. Naomba nishauri, Wizara hii ili isimamie sana suala hili. Ziko kazi ambazo Watanzania wanaziweza kama vile Uhasibu, Uhandisi, Ukarani na kadhalika. Lakini cha kushangaza kabisa utakuta kazi za namna hiyo zinafanywa na wageni.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*, ni chombo muhimu sana katika kusuluhisha na kuamua migogoro ya kikazi kwa bahati mbaya sana. Chombo hiki kimekuwa kikilalamikiwa sana katika kufanya maamuzi, moja hulalamikiwa kufanya maamuzi kwa upendeleo. Pili, ni kulalamikiwa kuchelewesha kutoa maamuzi ya migogoro ya kikazi. Kuna tatizo ni watumishi wachache, basi Wizara iongeze watumishi katika chombo hicho. Ni vizuri Serikali pale inapoweza basi ijitahidi kupunguza malalamiko ya watumishi katika maeneo kama haya.

Mheshimiwa Spika, bado lipo tatizo la ajira kwa watoto katika nchi hii, watoto hawa wengi huajiriwa kwenye ajira za mazingira mabaya na magumu. Aidha, watoto hawa kuanzia wale wa majumbani, nyumba za wageni, viwandani, mashambani na kadhalika, hulipwa mishahara midogo sana. Nashauri Wizara kutumia vyombo vyake ifanye kazi ya ziada ili kuwaokoa watoto hawa na wale wote watakaobainika kuwatumia vibaya basi wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kazi, Mheshimiwa Kabaka, Naibu Waziri Mheshimiwa Makongoro, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ni kiungo muhimu sana baina ya waajiri na waajiriwa.

Hata hivyo, zipo changamoto kubwa sana wanazozipata wafanyakazi kutokana na sheria za kazi zilizopo, pengine zimepitwa na wakati na zinahitaji marekebisho, kumekuwa na malalamiko sana hasa wafanyakazi wa migodini inaonesha wanazo changamoto sana ambazo zinahitaji mkono wa Serikali. Wafanyakazi wa migodi wanalalamikia utofauti wa mishahara baina ya Watanzania na wageni wenye ujuzi sawa na kazi ile ile unakuta mgeni analipwa milioni ishirini na mtanzania kulipwa laki tano. Huo ni ubaguzi wa hali ya juu sana kiasi kwamba Serikali inatakiwa ilifanyie utafiti na utatuzi wa suala hili. Vile vile Sheria ya Fidia ya mwaka 2008 ni vema ikafanyiwa kazi, Watanzania wengi wafanyakazi wa migodini wanapata ulemavu kazini kutokana na *nature* ya kazi zenyewe. Wengi wanalalamikia sheria hii kwa sababu wengi wanapopata ulemavu kazini hawapati fidia stahiki, Serikali iangalie upya sheria hii na vile vile iangalie namna ya kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Jamii, kuna tofauti kubwa sana ya mafao kati ya mfuko mmoja na mfuko mwingine mfano *PPF* inalipa mafao kidogo sana ukilinganisha na *PSPR, NSSF* na *LAPF* mtumishi anayechangia *PPF* mwenye cheo sawa na mtumishi mwingine aliyejiunga na Mfuko mwingine malipo yao yanatofautiana sana. Hivyo, Serikali inayo haja ya kuangalia upya Mifuko hii na namna ya kupata mafao haya.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni upatikanaji wa mafao kwa wastaafu, ni tatizo kubwa sana, Serikali

iangalie utaratibu mzuri zaidi wa namna ya utoaji mafao kwa wastaafu hasa wazee walio vijijini, wanahangaika sana kupata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi hotuba imezungumzia namna ambayo Wizara imeendelea kufuatilia. Naomba Wizara pia iangalie usalama na afya hasa katika shughuli za uchimbaji madini. Madawa yanayotumika ni makali sana pengine athari za madawa haya yanayotumika migodini na sehemu za wachimbaji wadogo yana athari kwa afya za wafanyakazi hao. Serikali ifanye utafiti katika suala hili, wafanyakazi wengi wanahofia usalama wao, kutokana na kazi wanazofanya migodini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa maandishi, pia sina budi nimshukuru Waziri jinsi alivyowakilisha hotuba yake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Taifa lolote linategemea zaidi kuwa na sera za uhakika za ajira kwa walio wengi nchini. Kwa maana hiyo, naiomba Wizara kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ubunifu wa ajira (*creation of jobs*) vijana wengi hivi sasa hawana kazi jambo ambalo linadhoofisha ustawi wa jamii na kukosa kuwa

na malengo ya kimaisha, kwa hiyo, ni vyema Wizara hii kuwa bunifu kwa kuanzisha vyanzo vya ajira.

Mheshimiwa Spika, haki za waajiriwa (*employees Rights*) bado Wizara hii haijakuwa makini kusimamia haki za wafanyakazi wa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu ziko ajira za sekta binafsi kama zile za mahotelini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa sekta binafsi wanakuwa hawatekelezewi haki zao za ajira, wako wafanyakazi mahotelini wanafanya kazi kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 2.00 usiku. Huu ni wastani wa masaa 14 ya kazi lakini malipo wanayolipwa hayalingani na kazi wanayofanya pia na uzito wa kazi wanayoifanya. Lakini jambo la kusikitisha Wizara hii haifuatilii kujionea wengine jinsi Watanzania wanavyonyanyaswa na waajiri hao wa *sector* binafsi.

Mheshimiwa Spika, mishahara kwa wafanyakazi, ni jambo lisilopingika kuwa maisha kwa Mtanzania wa kawaida yamepanda sana, na hivyo hayalingani na malipo (mshahara) wanayolipwa. Kuna haja kuangalia kwa makini kuhusu malipo mbalimbali ya wafanyakazi ili yaweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kama hili halikuangaliwa linaweza kuleta madhara makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, malipo ya *Pension* ni madogo sana, hayalingani na mahitaji ya kujikimu kwa wafanyakazi waliostaafu, hivyo napendekeza *Pension* ziangaliwe upya ili kubadili maisha ya wastaafu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana ni muhimu sana namwomba Waziri awasaidie vijana kwa kuwapatia udhamini kwa wale waliopata mafunzo *SIDO* ili waweze kukopa fedha na kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAMIA HASSAN SULUHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa hotuba yenye maelezo mazuri kwa mwaka ujao wa fedha 2012/2013. Nawapongeza pia kwa utekelezaji mzuri wa malengo ya mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hoja ya utenganishi kwa utoaji wa *Work Permits na Resident Permits* ruhusa za kuweza kufanya kazi nchini zitolewazo na Wizara ya Kazi kupitia Kamishna wa Kazi, kwa aina zozote za kazi kwa wageni. Idara ya Uhamiaji iweze kutoa ruhusa za kukaa nchini bila kuwa na vipengele vya kutoa ruhusa ya kufanya kazi nchini. Hali hii ya Idara ya Uhamiaji kutoa pia ruhusa ya kufanya kazi kulingana na aina ya ruhusa ya ukaazi (*resident*

*permit*) inatoa mwanya wa kuwepo kwa watu wengi wageni wanaofanya kazi ndogo ndogo hapa nchini, hasa wale wanaoomba ruhusa ya ukaazi kupitia Ofisi za Mikoani. Katika sura nyingine, hali hii inasababisha kuwepo kwa vitendo vya rushwa hasa kwa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuoanisha mipango ya maendeleo ya nchi na utengenezaji wa nafasi za ajira upewe kipaumbele inavyostahili ili kupunguza tatizo la ajira nchini, pamoja na kutunza amani na kupunguza uhalifu.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kuweza kutufikisha hapa tukiwa na hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hotuba hii kwa upande wa ajira. Tanzania bado ina tatizo la ajira na tatizo hilo limekuwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ije na mpango mkakati juu ya kuliondoa tatizo hilo, naomba nishauri kwamba, vijana wapatiwe elimu ya ufundi ili wanapohitimu waweze kujiajiri wenyewe na pia Serikali iwapatie mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kurejesha mkopo huo, wapate kupewa wenzao.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nijikite katika sekta ya usalama mahali pa kazi, wafanyakazi hususani wa viwandani bado afya zao ni mgogoro na baadhi ya viwanda havina usalama mzuri kwa wafanyakazi wao. Hali hii inapelekea wafanyakazi hao baada ya muda

mdogo hali zao zinazoofika na kupelekea ugonjwa na maisha yao kuzidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza viwanda vyote vifanyiwe ukaguzi upya kabla havijafanya kazi na pia kuwekewa masharti maalum ambayo yatazingatia Sheria za Usalama Mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kufika kumi la pili (kumi la *maghfira*) la mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tunaomba azidi kutupa amani na utulivu nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio, lakini bado kuna matatizo ya ajira za watu wazima, juhudi ziongezwe kwani vyuo vinaendelea kuzalisha wahitimu wa fani mbalimbali. Pamoja na hilo, kuna tatizo la ajira za watoto, hii inatokana na baadhi ya watoto kuajiriwa. Tafiti zinaonesha watoto wa umri kati ya miaka mitano (5) hadi 17. Hivyo basi, mkakati wa Tanzania mwaka 2015 wa kukomesha umaskini ni mzuri lakini, je, Serikali imejipangaje katika hilo?

Mheshimiwa Spika, tafiti za mwaka 2005-2006 zinaonesha watoto wengi wanafanya kazi za biashara ndogo ndogo, madini, kilimo (chai, tumbaku) na hata ombaomba mitaani.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kusaidia wakulima wadogo wadogo na hata sekta binafsi utaleta tija kwao na familia zao. Napenda niipongeze *NSSF* kwani wao wanafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana kwani kuweka/kuwezesha hata ajira binafsi kujiunga na Mfuko wao. Mbali na hayo Mifuko ya Jamii ina tija kubwa sana kwa Taifa letu sote ni mashahidi. *NSSF* ina miradi mingi ambayo pia inaleta maendeleo na kutoa ajira kwa wingi, *UDOM*, Nelson Mandela pia kuna miradi ya kilimo (Kagera *Sugar*) hii ni baadhi tu

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutoa kibali cha ujenzi wa daraja la Kigamboni kwani kuna ajira zaidi ya 1,000 na pia daraja lile ni ukombozi kwa wananchi wanaoishi Kigamboni na maeneo jirani, linaongeza na kuinua uchumi wa wanaoishi Kigamboni kwani naweza kusema kwa madaha kabisa kwamba, kwa daraja la Kigamboni maendeleo yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kupata nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, natoa masikitiko yangu makubwa kabisa kwa Serikali kwa jinsi ambavyo watoto wetu au vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu na kufaulu vizuri kabisa masomo yao wanavyokosa ajira na kuwa vijana wa kukaa vijiweni na kujifunza

mambo yasiyofaa kwa jamii. Hii inasikitisha sana na ni aibu pia kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ilione hili katika uzito wake na Serikali itafute namna ambayo itaweza kuwasaidia watoto hawa. Naunga mkono hoja iliyotolewa ya kurudisha Jeshi la Kujenga Taifa, hii pia ni nzuri kwani itapunguza watoto wengi kuzagaa bure mara tu wanapomaliza shule.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niiombe Serikali iweze kuanzisha *Short course* kwa vijana wetu wanapomaliza vyuo vikuu angalau miezi 3-6 ili angalau waweze kufundishwa namna ambayo wataweza kukabiliana nazo baada ya masomo yao hata kama watakuwa hawajapata ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba sana waajiri kupunguza masharti ya ajira kama wanavyotoa kwa vijana ambao wanatoka vyuoni, masharti magumu kama, uzoefu wa miaka 3-5, hii inanyima haki ya vijana wetu. Hawa vijana wanapotoka vyuoni wanakuwa wamekamilika kabisa wafayiwe *interview,* wajiriwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara hii kwa kuongelea masuala mawili muhimu ya Wafanyakazi wa Kiwanda cha Mtibwa *Sugar*. Niliwahi kuomba hapa Bungeni kuwa Wizara iangalie ajira za wiki tatu tatu kuwa si nzuri

badala yake pawepo na ajira za kuanzia miezi sita ili wafanyakazi hawa wapate mafao ya *NSSF*. Watumishi wengi wa msimu walibadilishwa na kuwa watumishi wa wiki tatu tatu, kuna dalili za kiwanda kuweza kuchukua hatua za kuelewa hoja yangu na niliongea na *NSSF,* Mkoa wa Morogoro waanze kurekebisha suala hili, naomba msukumo wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, madai ya wastaafu wa Kiwanda cha Mtibwa baada ya kubinafsishwa mwaka 1997 kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu na suala hili nimeliongelea hapa zaidi ya mara mbili na Mheshimiwa Waziri aliniahidi atafika Mtibwa. Juzi nilimwandikia barua na tumeongea, naomba sana tukae na wastaafu wote, *PPF* uongozi wa Mtibwa, mimi kama Mbunge na Mheshimiwa Waziri, tuwasikilize wastaafu hawa hii itasaidia mambo yafuatayo:-

- Tutapata kwa pamoja kujua ukweli wa malalamiko yao;

- Wastaafu watapata majibu ya moja kwa moja na kuelewa hatima yao;

- Kwa wale wenye kesi na kiwanda kitatoa fursa kubwa pande mbili kumaliza madai yao nje ya Mahakama na kuwapunguzia usumbufu wastaafu; na

- Matatizo ya wastaafu tutakuwa tunayamaliza na tutadumisha umoja na mshikamano kwa wananchi, Kiwanda na Serikali.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi tu kama yupo tayari kuja Mtibwa kuongea na wastaafu na wafanyakazi kama nilivyoomba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji kwa uandaaji wa bajeti nzuri, lakini hasa kwa uendeshaji mzuri wa Wizara yenye changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, ajira nyingi za Watanzania ambazo wanaziweza zinachukuliwa, napendekeza uhamiaji na mamlaka nyingine wawe macho zaidi na watende kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubaguzi kazini, bado kuna makampuni ambayo yanapanga mishahaara siyo kufuatana na uwezo bali kufuatana na rangi na pia *race,* napendekeza hili lisiendelee kuruhusiwa au kuvumiliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwajiri mkuu hapa Tanzania ni sekta binafsi, Serikali lazima isimamie sheria zote za kazi ili kuhakikisha wafanyakazi wanapata haki zao za:-

- Malipo halali (*minimum living wage);*

- *Pension scheme;*

- Bima kazini na sehemu ya kazi iwe imesajiliwa *OSHA;* na

- Likizo ya *maternity* na ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, nimesema hayo kwa sababu wafanyakazi wengi hasa wale walioajiriwa na Kampuni za Wahindi na ndugu zetu Watanzania wananyanyaswa kwa kutokuwa na elimu kuhusu haki zao, Serikali itoe haki hizo. Aidha, nashauri Serikali ijenge vituo vya *CMA* katika Wilaya zote nchini au zile Wilaya zenye migogoro mingi ya kazi. Nashauri Serikali ihakikishe Sheria yetu ya Hifadhi ya Jamii inatungwa kwa kufuata mikataba ya *Internarional Labour Organization (ILO),* hatuwezi kuishi tofauti na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, sababu ya kuwa na *unemployment* kubwa ni kwa sababu ya sera mbovu ya uwekezaji, wawekezaji hawawekezi Tanzania, hakuna viwanda kama *incentives to invest,* hazitoshi kuwaita wawekezaji, nashauri sera hizo zirekebishwe.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu moja kwa moja katika suala zima la ajira ambalo waathirika wakubwa wa tatizo hili ni vijana.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali ijipange kuanzisha ajira mpya, vijana wengi hawajui mustakabali wa maisha yao kwa sababu hawana

kipato chochote hali inayopelekea kipato cha uchumi wa nchi kukua kwa kasi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, vijana lazima wawezeshwe waweze kujiajiri na kuajiriwa, nashauri Serikali ianzishe Mfuko Maalum kwa ajili ya vijana itakayowahudumia vijana vijijini na mijini kwa ajili ya kutoa mikopo ya riba ya chini, vijana waelimishwe katika sekta husika kulingana na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, vijana wawezeshwe mikopo kulingana na maeneo yao kama eneo hilo ni zuri kwa kilimo wasaidiwe katika kilimo kama uvuvi wawezeshwe kwenye mifugo na sekta nyingine kulingana na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ijipange vizuri kuhakikisha inasadia vijana, tusipowasaidia vijana sasa hivi tutakuwa tumewaharibia vijana maisha yao yote hawatakuwa wametumia nguvu zao kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu kukaimisha watumishi kwa muda mrefu, kuna baadhi ya mashirika likiwemo Shirika la Tija la Taifa hukaimisha watumishi wake kwa muda mrefu jambo ambalo husababisha kushuka kwa ufanisi, Mkurugenzi anapokaimishwa kwa muda mrefu hawezi kufanya maamuzi ikiwemo kutoa *promotion* kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, hivi Taifa letu halina watu wanao-*qualify* nafasi husika mpaka watu wanakaimishwa kwa muda mrefu namna hiyo? Naomba kauli ya Serikali kuhusu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa naunga mkono hotuba au hoja ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa asilimia mia moja. Sasa napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tatizo la ajira limekuwa kubwa sana kwa vijana wetu wa Tanzania. Je, Wizara wana mpango gani wa kuhakikisha suala hili linaangaliwa kwa umakini? Kwani hivi sasa taratibu za ajira katika sehemu nyingi zimegeukwa na Wizara hii, kwa mfano, katika Makampuni ya Simu kuna wageni wengi ambao wamepewa ajira za kufanya ambazo Watanzania wengi wanaweza kama vile Idara za Masoko, Uhasibu hata Maafisa Uhusiano, hivi kweli kazi hizi lazima zifanywe na wageni?

Mheshimiwa Spika, sera za CCM mwaka 2010-2015 zimeahidi kutoa kadi maalum zenye picha za wazee wasiojiweza ili waweze kupata nafuu ya kutopata usumbufu ambao kwa kweli ni kero kubwa. Nina imani Wizara hii italisimamia suala hili kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya Wizara ya Kazi na Ajira.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake kwa hotuba nzuri na mikakati mizuri ya kuwapatia ajira vijana wetu. Pamoja na pongezi hizo, naiomba Wizara iangalie upya Sheria ya Mafao ya Uzeeni ili iendane na mabadiliko ya maisha kwa nchi yetu ambayo yanatokea kwa kasi sana. Nia ya mabadiliko ya Sheria iwe ni kutoa nafasi kwa Mifuko ya Jamii kupewa nafasi ya kutengeneza *products* mbalimbali zinazolenga makundi mbalimbali bila kuhatarisha uwepo wa Mifuko hiyo. Hii itaondoa malalamiko yaliyopo sasa juu ya kulazimisha umri wa kustaafu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, natoa hongera kwa Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri uanzishwe Mfuko wa Mikopo ya Uwekezaji wa Vijana kwenye kilimo na viwanda vyenye *backward linkage* kwenye kilimo. Tukitaka kuongeza ajira kwa vijana ni lazima tuwe na mipango ya muda mrefu ya kuwekeza kwa vijana wetu wasomi na wale wa vijijini. Tufanye jitihada za makusudi za kuanzisha na kutenga eneo maalum la kuwekezaji kwenye kilimo na viwanda husika. Ukimpa Kijana mmoja mkopo awekeze kwenye kiwanda unahakikisha unamtaka awekeze kwenye kilimo kikubwa na awezeshe *outgrowers*, unampa masharti nafuu, unapeleka miundombinu na hapo utakuwa umetatua matatizo mengi kwa mpigo! Kuanzia lile la masoko, tija na uzalishaji na umepunguza utegemezi

wa wananchi kwa chakula cha misaada kutoka Serikalini ama soko la mazao ya chakula toka Serikali na umetengeneza ajira kwa makundi tofauti ya vijana wasomi na wale wasiosoma! Zaidi umekuza *GDP* yetu.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi itumike kukopea pesa kwa ajili ya nyumba. Mashirika haya yanaweza yakajenga nyumba na kuwataka wanachama wanaopenda kununua nyumba wakope *against* akiba yao, pia wanachama wa Mifuko hii waruhusiwe kukopa pesa na kununua bima za afya na maisha yao, pia waruhusiwe kukopa fedha kwa ajili ya kulipia ada za masomo. Kuwe tu na mgawanyo wa asilimia (kiwango) anachoweza mtu fulani kukopa na kiwepo kiwango fulani cha lazima ambacho ni lazima kibaki kwenye *account* yake. Watu wakiziona faida hizi, wengi zaidi wataingia kutokea *informal sectors* ili wafaidike na Mifuko itapata fedha nyingi zaidi ya sasa na hata huu wasiwasi unatufanya kuzuia fao la kujitoa hautakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, nilisema kwamba kilimo ni biashara kama zilivyo biashara nyingine, kinaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, kina nafasi ya kupunguza umaskini katika yote, mtaji wa nguvukazi ni vijana.

Mheshimiwa Spika, nimepanga katika mwaka 2012/2013, kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira, Vyuo Vikuu, Wizara ya Ardhi na Vyuo vya Kilimo kuandaa mpango utakaowezesha wahitimu wa vyuo hivyo kupata mitaji ya kuendeleza kilimo ikiwemo ardhi, zana za kilimo na umwagiliaji na pembejeo ili waweze kujiajiri katika sekta ya kilimo, aidha tutahusisha sana Taasisi za fedha yakiwemo mabenki ili kwa pamoja tuangalie uwezekano wa kuwawezesha wahitimu, hasa wa kilimo waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuandaa mpango kama huo ni kuwavutia vijana ambao ndio nguvukazi kukipenda kilimo, njia pekee ya kuwavutia vijana ni kupunguza harubu za kilimo kwa kutumia zana za kisasa ili waweze kutumia ujuzi wao vizuri, wabaki vijijini na kutoa ajira kwa wananchi wengine walioko vijijini. Aidha, mpango huu utasaidia sana kupunguza kasi ya vijana kukimbilia mijini. Naomba ushirikiano katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa na takwimu za ajira katika sekta ya kilimo inazalisha ajira nyingi ambazo siyo rasmi na hazijulikani, natoa mifano michache ifuatayo:-

(i) Katika mashamba makubwa ya miwa wako wananchi wengi ambao wameajiriwa kama madereva wa matrekta *operators* wa mashine na mafundi mbalimbali. Wako pia vibarua wa muda mrefu (kila msimu) wanaotayarisha mashamba, kupanda, kupalilia, kuvuna na kadhalika.

(ii) Katika ujenzi wa miradi ya umwagiliaji mikubwa kuna ajira za mikataba ya *professionals* kupitia Makampuni ya Ushauri (*consultants*) na Makampuni ya Ujenzi (*contractors*). Makundi haya mara nyingi yanajulikana kama yanazalisha ajira.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Wizara ya Kazi na Ajira kushirikiana na Wizara yangu kuweka utaratibu wa kudumu wa kupata takwimu sahihi za ajira.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika sekta ya kilimo, nimefanya mazungumzo na *NSSF* na *PSPF* ambao wameonesha nia ya kusaidiana na wawekezaji wa ndani ili kuanzisha viwanda vya kusindika mazao kama Viwanda vya Korosho na Viwanda vya Nguo (pamba). Mpango huu ukifanikiwa tutaongeza Viwanda vya Korosho na Nguo, hivyo kuongeza thamani, mapato na ajira. Tafadhali tusaidieni tushirikiane katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao kuendelea kuiongoza Wizara hii adhimu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mfupi wa leo utalenga kwenye eneo moja la ajira/fursa za kufanya kazi kwa wageni nchini. Wapo watu kutoka nje ambao wapo nchini kwa muda mrefu na kwa kutolea mfano, tu (*sample*) ni raia hawa wawili wa India ambao wapo nchini kwa takribani miaka mitano bila kuwa na *permits*

za kuwaruhusu kuwepo nchini, kwa muda huo huku wakitumia mpaka *visitors pass*, vile vile Kampuni ya *Hotels and Lodges (*Tanzania *Limited)* ina wafanyakazi wengi kutoka nje ambapo mchakato mzima wa kupitia *TIC* ili kuongeza idadi ya *expatriates* haujafuatwa wala kuzingatiwa, *wame-exeed limit* kinyume na sheria.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hizi *visitors pass* zimegeuzwa *CTA* na ili kuidanganya mamlaka husika wamekuwa wakitaka hizi *pass* Namanga, wakati mwingine Dar es Salaam hata Kilimanjaro kwa miaka mitano. Kuna Watanzania wengi wenye uwezo na hawana ajira, halafu raia hawa wa kigeni nitakaowataja wanafanya kazi za kupaka rangi mbao kwenye hoteli hizi za kitalii. Kazi hizi zinaweza kufanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tafadhali wakati wa kuhitimisha tupate maelezo ya watu hawa na ufafanuzi wa *visitors pass* kutumika kufanya kazi (kama *permit*) lakini pia ufafanuzi wa *visitors pass* kugeuzwa *CTA*. Majina ya raia hao ni Mahaveer Prasod na Jay Kishan Jangir (hawana kabisa *permit* yoyote).

Mheshimiwa Spika, mwisho niwatakie kila la kheri kwenye kazi nzito za Wizara hii katika kuwahudumia Watanzania.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini nomba ufafanuzi wa haya yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa tatizo la ajira ni kubwa sana hapa nchini, kwa nini wahitimu/wasomi wa vyuo vikuu wanaomba kazi/ajira wawekewe sharti la uzoefu (*experience*) na waajiri wawe watu binafsi au Serikali. Kwa nini wasiajiriwe wakapata uzoefu kazini?

Pili, je, Serikali inafahamu kuwa kutangaza nafasi za kazi kwenye magazeti inayofanywa na Serikali, Mashirika ya Umma na sekta binafsi, kuwa ni namna tu ya kutimiza wajibu kwa vile wahusika wameshawaleta ndugu/jamaa zao ili wapate ajira hizo?

Tatu, naiomba Serikali wapate nafasi hizo hususan katika Mahoteli, migodi na sekta ya utalii.

Nne, ni kwa nini wastaafu ambao kazi zao hazikuwa za *rare professional* waongezewe mikataba ya utumishi wakati ambapo ajira ni tatizo kubwa nchini?

Tano, wakati mwingine mamlaka za uteuzi zinampa mtu mmoja kazi mbili, kwa mfano, Mbunge kuwa *DC/RC* na kadhalika kwa nini hali iwe hivyo, wakati kuna upungufu mkubwa wa ajira? Wizara ishauri Mamlaka za uteuzi kama Rais na wengine juu ya hili.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Kazi na Ajira. Kumekuwa na tatizo kubwa la ajira, vijana wengi wamekuwa wakikimbilia mijini, Serikali na Wizara ni kwa nini wasiwawezeshe vijana ambao wapo vijijini kwa mfano, kutoa mikopo midogo midogo ili

waweze kujikita kwenye sekta ya kilimo. Ukiangalia vijana hawa wanapokimbilia mijini, wanajiunga kwenye vitendo viovu kama vile kutumia madawa ya kulevya hatimaye kujiingiza kwenye ujambazi (wizi).

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kwa wawekezaji ambao wanakuja kuwekeza Tanzania, wamekuwa hawawachukui wazawa wa hapa Tanzania, kwa mfano, Hoteli za kitalii wawekezaji wengi wamewachukua wafanyakazi kutoka Kenya, Uganda hata zile kazi za kufanywa na Watanzania zinafanywa na wageni kutoka nje. Wawekezaji hawa wanapowapatia Watanzania nafasi za ajira pia wamekuwa wakiwanyanyasa, hawawalipi mishahara kwa wakati muafaka, mishahara midogo, hata wanapoumia kazini hawapati huduma za matibabu. Wawekezaji hao wanakuwa wanawasimamisha kazi mpaka watakapopona kuhusu matibabu wanajihudumia wenyewe wafanya kazi hao. Kwa kuwa Watanzania wengi hawajui sheria za kazi (sheria ya mwajiriwa na yule anayemwajiri) hivyo, kuingia mikataba mibovu bila kujua sheria za kazi. Je, Serikali na Wizara mtahakikishaje wananchi wengi wanapatiwa elimu elekezi?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro mingi katika sehemu za kazi, wajiriwa wengi wanafanyishwa kazi kinyume na sheria, wanafanyishwa kazi muda mwingi, ni tofauti kabisa na malipo wanayolipwa kwa kuwa sheria hawazijui. Kwa mfano, nilitembelea shamba la maua na *Star times* ambayo ipo chini ya *TBC*. Huko nilikuta malalamiko matupu watu wanafanya kazi bila mikataba kwa zaidi ya miaka

mitatu, mishahara midogo, wananyanyaswa, wengine wamefukuzwa kwa kudai haki zao ili kuwatisha wanaobaki wafanye kazi katika mazingira ya uoga.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali na Wizara haioni kuwa sasa hivi ni wakati muafaka wa kuwasimamia wananchi kupata haki zao kwa kutembelea sehemu zote ambazo zinalalamikiwa mara kwa mara? Je, ni kwa nini pindi wanapopata malalamiko kutoka kwa wafanyakazi hawafuatilii ipasavyo au kutoa misaada kwa wanaoleta malalamiko ili wapate haki zao?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutoka kwa wanachama wa mifuko hii, wamekuwa wakikatwa fedha zao na kuingizwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Pesa hizo wanazokatwa zimekuwa zikitumika bila idhini ya wanachama. Kwa mfano, kuna malalamiko kwa wanachama ambao wamejiunga na Mfuko wa *NSSF* wanachangia Mfuko huo katika upande wa matibabu na hospitali wanazopewa hazilingani na michango wanayotoa, wanapangiwa hospitali zisizokuwa na dawa, hazina vifaa vya kutosha vya uchunguzi wa maradhi, pia Madaktari ni wachache.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri haoni *NSSF* inaingia migogoro na wanachama wake ambao wanachangia Mfuko huu bila kunufaika na huduma za afya kama walivyokubaliana na wanachama wake? Je, *NSSF* haioni sasa kuna umuhimu wa kuhakiki

hospitali walizowapangia wanachama wao ili wapate matibabu yanayoendana na michango wanayotoa?

**MHE. DKT. DAVID M. MALOLE:** Mheshimiwa Spika, Mahakama za Kazi *(Labour Tribunals*), zimeendelea kuleta utata mkubwa sasa hivi na zinakatisha tamaa, waajiri wengi hasa wa sekta binafsi, pale mtumishi anapokwenda kwenye Vyama vya Wafanyakazi, mfano *CHODAWU* na vinginevyo na baadaye kwenye Mahakama za Kazi na wote wakiwa wanampendelea mtumishi na kumgandamiza mwajiri. Utata mkubwa umejitokeza katika mambo haya yafuatayo:-

Chama cha Wafanyakazi au Mahakama ya Kazi kudai kuwa mtumishi alikuwa analipwa kidogo, eti kinyume cha sheria, wakati mkataba ni maelewano au makubaliano kati ya mtumishi na mwajiri, kama mshahara ni kidogo kwa nini mtumishi alisaini mkataba? Kwa nini asikatae kusaini mkataba na kukataa ajira? Kwa nini pia mtumishi afanye kazi kwa muda mrefu wa miaka miwili au zaidi. Akishamaliza mkataba ndipo aende *CHODAWU* kulalamika na wajiri kutakiwa kulipa pesa nyingi na faini?

Mheshimiwa Spika, madai ya marupurupu kwa mwajiri ambayo hayapo kwenye mkataba, je, marupurupu ni haki ya mtumishi? Ninavyofahamu mimi ni kuwa marupurupu (*allowances*), ni mapenzi ya mwajiri (*discreation*) na wala si haki ya kisheria. Haki ya kisheria ipo kwenye mshahara tu (*salary*) na wala si katika marupurupu! Iwaje sasa mwajiri alazimishwe kulipa marupurupu ambayo yapo nje ya mkataba wa kazi? Je, haya siyo manyanyaso kwa mwajiri?

Mheshimiwa Spika, kama mkataba unaeleza kuwa mtumishi akishindwa kutekeleza wajibu wake wa kazi, kwa kuwa mvivu (*laziness*), kutoonekana kazini (*absenteeism*), utovu wa nidhamu (*misconduct*), kisha mtu akaonywa mara ya kwanza, ya pili na ya tatu (kimaandishi), kwa nini Vyama vya Wafanyakazi na Mahakama ya Kazi watetee maovu ya mtumishi? Je, tutamudu kweli Soko la Ajira la Afrika ya Mashariki, kwa mtindo huu wa kutetea watumishi wabovu katika vituo vyetu vya kazi. Je, nchi inaweza kuendelea kwa kulinda wavivu, watoro na watumishi wenye nidhamu mbovu katika vituo vyetu vya kazi?

Mheshimiwa Spika, mwisho, napendekeza yafuatayo:-

(1) Kutokana na kesi nyingi katika Mahakama zetu za kazi basi watumishi wote nchi nzima wajaze fomu za mikataba za kazi zitakazotolewa na Wizara ya Kazi ili kuepuka manyanyaso kwa waajiri ambao wamewekeza kwa moyo mweupe na kuajiri kwa moyo mweupe, lakini mwisho kuishia kwenye adhabu kwa kulazimisha waajiri kulipa fedha nyingi kwa watumishi kinyume kabisa na makubaliano yaliyosainiwa kati ya mtumishi na mwajiri!

(2) Sheria za kumlinda mtumishi mvivu, mtoro na mwenye tabia mbovu zifutwe ili kuimarisha utendaji kazi na kuleta tija katika kazi za maendeleo ya Taifa letu.

(3) Mheshimiwa Spika, vipeperushi vya sheria za kazi vitengenezwe kwa wingi na kusambazwa nchi nzima, hasa kwa sekta binafsi ili waajiri wajue nini kinatakiwa kuliko kuwasomea sheria ngeni na wasizozijua, baada ya mtumishi mwenye shukrani za punda, kukimbilia Mahakama za Kazi, ndipo Mwajiri kuanza kusomewa sheria ambazo hajapata kuzisikia tangu azaliwe! Sekta binafsi ni wadau, si adui katika maendeleo ya Taifa. Haki ni wadau si adui katika maendeleo ya Taifa. Haki itendeke pande zote mbili, mtumishi na mwajiri bila upendeleo.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwenye Wizara hii katika mambo mawili ama matatu. Wizara hii imekuwa ni kiungo muhimu kati ya mfanyakazi na mwajiri wake pale haki inapokuwa haitendeki kwa upande wowote kati ya pande hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuongelea suala la wafanyakazi walioko migodini, kuna unyanyasaji mkubwa sana unaofanywa na migodi iliyopo hapa nchini na hasa migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu na Mwadui.

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana na kuwapo kwa unyanyasaji huu kwa wafanyakazi wanaopata matatizo wakiwepo kazini, nimebahatika kuwaona baadhi ya wafanyakazi hao ambao migodi hiyo imetelekezwa baada ya kupata matatizo ya afya zao yanayotokana na kazi walizokuwa wanafanya migodini.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi hawa wako katika hoteli inayoitwa Durban iliyoko karibu na mnara wa saa Dar es Salaam, huku wakila na kulala bila kutibiwa kikamilifu na wengine wanatakiwa waende India kwa matibabu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi wafanyakazi hao waliandikiwa barua za uthibitisho kuwa maradhi yao ni kutokana na shughuli walizokuwa wanafanya mgodini, lakini makampuni hayo yakaunda *Medical Board* wanayoijua wenyewe na kubadilisha *statement* za Daktari aliyeandika ripoti na kuonekana na maradhi waliyokuja nayo kazini.

Mheshimiwa Spika, nauliza haya Makampuni ya kuchimba rasilimali zetu yamepewa kibali cha kuchimba na kunyanyasa Watanzania wanaofanya kazi? Migodi hii imeshindwa kuwalipa fidia, pesa za kuhudumia familia zao, kinachofanyika sasa hivi ni kupoteza pesa nyingi kuendelea kuwalipia hoteli za kifahari huku afya zao zikiendelea kudhoofu?

Mheshimiwa Spika, nimeguswa sana na habari hii na niliweza kuwatembelea vijana hawa katika hoteli hiyo, ni mambo ambayo yanatia uchungu sana, vijana bado wana umri mdogo, lakini ndoto zao zinataka kuzima kama mishumaa huku Serikali yao imeshindwa kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada walizofanya wamekwenda mpaka Wizara ya Kazi na Ajira na barua ya wito kuwaita wenye migodi hiyo

kuandikwa mpaka leo hakuna aliyeitikia wito huo! Ni nani anayeyapa jeuri haya makampuni?

Mheshimiwa Spika, hata pesa walizokuwa wanajitibia wenye mgodi huo (*Barrick, Old* Bulyanhulu) hawajarudishiwa. Naomba majibu toka kwa Serikali wafanyakazi hawa wa *Barrick Gold* Bulyanhulu watapatiwa matibabu stahiki na kulipwa madai yao halali?

Mheshimiwa Spika, ninavyo vielelezo vyote vinavyohusu afya zao na barua ambazo Wizara ya kazi iliandika kwa mwajiri huyo.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Mwadui *(PETRA)* umekuwa ukilalamikiwa na wafanyakazi wake kuwa umekuwa ukifanya ambayo yanadhalilisha wafanyakazi wake, kwanza kumekuwa na tabia ya wafanyakazi kubambikiwa kesi za wizi ili mradi tu wafukuzwe ili kukwepa kuwalipa kwani wana mpango wa kupunguza wafanyakazi. Ili kukwepa kuwalipa wanawasingizia wizi na atakayewezesha kusingizia mwenzie wizi anapewa Sh. 1,000,000/=. Naomba sana Serikali iangalie kwa nini wafanyakazi hawa wemekuwa wakinyanyaswa katika nchi yao?

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni Mifuko ya Jamii. Suala hili limeibuka hivi karibuni na maeneo ya migodini yaliathirika mpaka kupelekea migodi kufungwa wafanyakazi hawa wanaochangia Mifuko hii wamekuwa wakikatwa kila mwezi, lakini Mifuko hii imekuwa ikitumia pesa hizo kwa ajili ya miradi mingi

sana. Cha kusikitisha hakuna anayepata gawio hata kwa senti moja.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kujua, je, Serikali ina mkakati gani sasa kuwafanya wachangiaji wa Mifuko hiyo kufaidika katika gawio kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri sana kwa kuteuliwa kwa nafasi hiyo, Mheshimiwa Rais amekuona wewe ndiye unafaa kushika dhamana hiyo, hongera sana!

Mheshimiwa Spika, kazi na ajira ni watoto mapacha na tabu kuwatenganisha, hivyo basi kazi zipo nyingi tu au niseme vyanzo vya kazi vipo vingi na kutoka hapo ndipo inapozaliwa ajira. Kwa kuwa ajira ni haki ya kila Mtanzania na kwa kuwa Watanzania wajibu wao ni kufanya kazi kwa faida na maisha yao na maslahi ya Tanzania. Hivyo, Serikali kwa upande wake ni kuibua vichocheo vya kazi kwa wananchi wake, ili nao waweze kupeleka mbele maisha yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya Watanzania themanini kwa kila mia moja ambao ni asilimia 80 ya watu wetu wanatengemea kilimo, mifugo na uvuvi na asilimia iliyobaki ni waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kazi za maofisini zimepungua na zitaendelea kupungua kila mwaka kutokana na ongezeko la Sayansi na Teknolojia, hivyo sehemu

kubwa ya kazi hubebwa na mashine zinazoibuliwa na maendeleo ya kisayansi. Kama hivyo ndivyo ni kwa kiasi gani basi Serikali yetu imejipanga vyema kuitumia rasilimali watu, ardhi na vile vilivyomo kwenye ardhi na hata baharini kuhakikisha kwamba rasilimali hizo zinatumika kwa tija?

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu bado kinadai kwa kuandamwa na changamoto kadhaa na hasa umaskini uliokithiri nchini na mipango mibovu inayoendelea ya matumizi ya ardhi. Nakumbuka sana kauli ya mwalimu pale aliposema: "Ili tuendelee tunahitaji mambo manne (4), watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora."

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri anisaidie kwa kunijulisha ni wapi tulijikwaa? Kundi kubwa linalokua siku hadi siku na ni lile lenye mahitaji makubwa, ni vijana, ila mimi naamini ajira ni ya watu wetu wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na rasilimali maji kwa maoni yangu tukijipanga vizuri na kuweka uzalendo mbele naamini wananchi wetu watapata ajira na kwa vijana kamwe tusitegemee kuwapeleka mashambani, ama mbugani au kwenye uvuvi hata kidogo! Ila vijana wengi tutawapata kwenye viwanda pale tutakaposindika mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na matumizi mazuri ya maji.

Mheshimiwa Spika, kilimo ili kiwe na tija na kujitosheleza kwa chakula ni kuboresha uzalishaji kwa kutumia zana bora na pembejeo nyingine za kilimo. Mazao ya mifugo na uvuvi ni muhimu sana kwa lishe hasa kwa mama wajawazito, wanaonyonyesha na watoto! Kuyasindika viwandani mazao hayo, hizo ndizo ajira *locally available employment* ukiacha kutokuwa na vijana wasiokuwa na sifa kwa zile kazi chache za kiofisi zinapotokea. Mheshimiwa Waziri kwa makusudi Serikali sasa ilichukue suala la ardhi kuwa ni *issue* na kamwe isipuuzwe hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ardhi itumike ipasavyo, na mipango safi iliyoandaliwa kusudi umilikishwaji ardhi kwa wananchi uweze kutumika kupatia mikopo ya kuendeleza kilimo. Pia zitafutwe zana za kisasa za uvuvi endelevu na wenye tija kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai na pia kwa maendeleo ya watu na viumbe vyote hai na kwa kilimo na maendeleo ya viwanda. Maji ni muhimu na yanakabiliwa na changamoto kubwa za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na kadhalika. Hivyo, naomba sana umahiri na nia njema ya watendaji wa maeneo husika kutanguliza uzalendo mbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitotumia nafasi hii ambayo ni fursa adhimu kuwapa pongezi

Mawaziri; Mheshimiwa Kabaka na Mheshimiwa Mahanga pamoja na watendaji wao kwa jinsi wanavyojitahidi kutenda kazi zao hasa ukizingatia ufinyu wa bajeti ambayo haitoshelezi katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira ni suala mtambuka ambalo linagusa kila sekta/Taasisi na asasi mbalimbali za kijamii na kiraia. Suala la vibali vitolewavyo kwa ajira ya wageni inaonekana kuwa ni tatizo kubwa kwani Wizara haijaonesha ni kwa namna gani wamewekeza kudhibiti ajira kwa wageni hususan kwa kazi ambazo si za kitaalam kufanywa na wageni. Mifano ya wingi wa wageni katika ajira za Watanzania kama vile katika Mahoteli ya Kitalii, Makandarasi wa Ujenzi, viwandani na hata katika sekta za biashara za madukani mfano, *super markets*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuachiwa vibali vya ajira kutolewa kiholela, leo hii tumesababisha vijana wetu walio wengi kuwa ni wachuuzi badala ya kuwa wazalishaji na hii imesababisha kuongezeka hata kwa ajira za watoto kwani ni wageni hao hao hususan wenye asili ya Kiasia kuwatumia sana watoto kuchuuza bidhaa zao. Ni vyema Wizara kufuatia Vyama vyake vya Kazi, kufanya sensa maalum katika maeneo ya ajira na kuona ni kwa namna gani, ukubwa wa tatizo hili unavyoathiri ajira ya wazawa katika viwanda, ofisi binafsi, makampuni ya ujenzi na hata madukani.

Mheshimiwa Spika, usalama wa wafanyakazi maeneo ya kazi bado sio mzuri katika maeneo ya kazi hasa pale waajiri/wamiliki wanapokuwa hawajali wafanyakazi wao. Wafanyakazi wengi wanaathirika

na wengine kupoteza maisha yao wakiwa kazini kutokana na maeneo yao ya kazi kutokuwa na usalama. Mfano halisi, ni vitendo vinavyofanyika katika Kampuni ya Jambo *Plastic*, Viwanda vya Kubangua Korosho, Viwanda vya Chuma na kadhalika. Baya zaidi ni usimamizi mbaya wa afya katika maeneo ya kazi kama vile utumiaji wa kemikali katika viwanda na maeneo ya migodini. Naiomba Wizara kwa kufuatia Taasisi yake ya *OSHA* ikae pamoja na Vyama vya Wafanyakazi husika kuangalia upya sheria zetu na kanuni ili kama tayari zimepitwa na wakati ni vyema kuboreshwa.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye matumaini na hasa kwa upande wa ajira. Kutokana na ukweli kwamba idadi ya Watanzania inazidi kuongezeka na hususan vijana, tatizo la ajira litazidi kuwa kubwa. Ili kupambana na tatizo hili, Wizara na wadau wengine wanashauriwa kuandaa mikakati ifuatayo:-

(i) Masomo ya ujasiliamali yaanzishwe kutoka elimu ya msingi ili wahitimu wa elimu ya msingi waweze kuwa wabunifu zaidi na kujiajiri.

(ii) Serikali iongeze kazi ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi ili wahitimu wengi wa elimu ya msingi na sekondari waweze kupata fursa ya mafunzo hayo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

(iii) Serikali ione uwezekano wa wahitimu wa elimu ya juu kujiunga katika vikundi, wakiwemo wataalam wa fani mbalimbali ili kuwapatia mikopo na kuanzisha uzalishaji kama ilivyo katika nchi za Misri (Egypt) na Botswana. Uanzishwaji wa Benki ya Kilimo utasaidia sana katika azima hii.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa wageni sasa hivi limekuwa ni jambo la kawaida, wageni kuajiriwa katika kazi ambazo Watanzania wangeweza kufanya. Ajira katika sekta isiyo rasmi imevamiwa sana na wageni na hususan Wachina! Haita chukua muda kuanzishwa kwa China *City* katika baadhi ya Majiji yetu kama vile Dar es Salaam. Serikali iangalie upya jambo hili na hasa vibali vya kazi vinavyotolewa.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na Ajira kwa hotuba nzuri na yenye matumaini kwa Watanzania kwa jumla. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyoshughulikia changamoto za Wizara yake na masuala ya ajira na kazi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa itambulike kuwa ajira na kazi ni suala mtambuka na kwa hali hiyo ni suala ambalo haliwezi kuachiwa Wizara ama Serikali peke yake. Kwa hiyo, Serikali ina jukumu kubwa la kutunga sheria, kuweka sera, mikakati na miongozo itakayowezesha sekta hii kukua kuendelea na kujenga mazingira mazuri ya Watanzania kufanya kazi kwa tija, amani na heshima inayostahili. Kwa sasa hivi tuna tatizo kubwa kwa waajiri wengi

wananyanyasa wafanyakazi kwa kutowapa mikataba, kutowalipa mishahara stahiki, kutowapa stahili zao, kutowalipia michango yao ya pensheni na hata kuwadhalilisha. Wizara na Idara za Wizara hususan Maafisa kazi wamekuwa wakichangia kwenye kukuza tatizo kuwatetea waajiri na kuwanyima haki wafanyakazi. Hii inawakosesha haki zao za msingi, kuondoa motisha ya kazi kupunguza tija na kurudisha nyuma Taifa. Kwa hivyo, tunamwomba Waziri na Wizara yake kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Sheria za Kazi na taratibu zake kuhakikisha kuwa wajiri wanatimiza wajibu wao na waajiriwa hali kadhalika vile vile kurejea usimamizi wa Mahakama za Kazi kuhakikisha haki inatendeka.

Mheshimiwa Spika, nirejee kwenye suala la mtambuka wa sekta hii ya ajira na kazi na kuishauri Wizara kuweka mkakati wa kuhakikisha kuwa kila Wizara inazalisha kazi, kwa kuweka malengo ya ajira watakazozalisha na kwa muda mfupi. Hii itawezesha kuhakikisha majukumu ya kuzalisha ajira na kazi nchini yanagawanywa kwa kila mmoja kuwasimamia Taasisi chini yao, lakini vile vile hii itafanya kila Wizara isimamie na kutenga bajeti ya kujenga ajira na ufanisi wa kazi chini ya Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa maendeleo ya nchi yoyote hupimwa kwa uwezo wake kuzalisha na kuwapa ajira wananchi wake, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri kushirikiana na sekta binafsi na ile isiyokuwa ya Kiserikali kuhakikisha kuwa uwezo wa wananchi unaongezeka ili waweze kukidhi ushindani katika soko la ajira. Hii ina maana kuhakikisha kuwa

Watanzania wanapata taarifa zote zinazohusu fursa za ajira Tanzania na Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla. Aidha vijana kuwapatia mafunzo na semina jinsi ya kutengeneza *CV*, kuhudhuria *interview* za kazi, mafunzo ya jinsi ya kuji-*present* kuvaa na kadhalika. Hivi vyote vinasaidia sana katika kushindana katika soko. Kuna haja sana ya kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Vijana, Maendeleo ya Jamii, Utumishi, Elimu, Sayansi na Teknolojia kuandaa mafunzo nchi nzima ya kuwawezesha vijana na wananchi kwa ujumla kufahamu mambo ya jinsi ya kujikita na ushindani wa ajira.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtia moyo Mheshimiwa Waziri na kumwahidi ushirikiano wa hali na mali kutoka Wizara yangu katika kutimiza malengo ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa masikitiko yangu makubwa juu ya kesi za matukio mengi ya udhalilishaji wa wafanyakazi wa ngazi za chini, vijana wetu kwenye sekta ya utalii hususani Mahoteli ya Kitalii. Wafanyakazi hawa hawana mikataba ya ajira, wanafukuzwa ovyo, wanakatwa mishahara bila kufuata utaratibu, wanafanya kazi masaa mengi kwa malipo duni. Hawana wa kuwatetea kwa sababu hawaruhusiwi kujiunga na Vyama vyovyote vya Wafanyakazi na matokeo yake hata wakishtaki Maofisa wa Kazi wanahongwa na kuwatetea wajiri. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri awasaidie hawa vijana ambao wamekata tamaa, wanafanya kazi kwa shida na unyonge katika nchi yao huku wakiona

wafanyakazi toka nje wakipewa nafasi na upendeleo kwenye maslahi. Hii inawavunja moyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumtia moyo na kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Wizara yake nikimwahidi ushirikiano wa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia fursa hii ya kuchangia hoja hii ya ajira na kazi iliyopo mbele yetu. Naomba nianze na suala la mafao ya wafanyakazi ambao Mifuko ya Hifadhi imekuwa ikikusanya, lakini shida inakuwa ni jinsi gani ya kuyatoa wakati muafaka mwanachama huyo au mstaafu anapoyahitaji. Aidha, suala la Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kutokuwa na ushirikiano wa moja kwa moja na wanachama wake katika kutoa maoni na ushauri, miundo ya Mamlaka ya Bodi husika haimhusishi mchangiaji huyu au mwanachama katika kupata maoni au mawazo yake katika uboreshaji au uendelezaji wa Mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la *NSSF*, ni Mfuko ambao kimsingi unatoa mafao mazuri, lakini mafao hayo hayafiki kwa muda muafaka! Utaratibu unakuwa wa kusuasua ambao muda wa kutekelezwa unakuwa haueleweki. Mfuko huu una wanachama wa kutosha na unajishughulisha sana na miradi mingi ya kukuza kipato cha Mfuko pamoja na ubunifu wa mafao mbalimbali, jambo kubwa na la msingi ni jinsi gani mapato yanayotokana na kazi

mbalimbali zinazofanywa na Mfuko huu yamegawanywa kwa wanachama wake kama sehemu ya gawio linalotokana na michango ya pesa zao kama mtaji anzia wa kufanya kazi hizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri na kweli kwamba Mfuko huu umejenga Chuo Kikuu cha Dodoma, sasa hivi wapo kwenye mchakato wa kujenga daraja la Kigamboni. Lakini mwanachama huyu hana taarifa ya Mfuko wake umepata kiasi gani cha fedha, yeye kama mwanachama anapata gawio kiasi gani kuliko kutegemea kile tu ambacho ameweka kama akiba yake na mwajiri kuongezea. Nashauri Mfuko huu wa Hifadhi uwe unaendesha Mfuko wake kama kampuni, wanachama wawe na hisa, wapate gawio na wakiamua wauze hisa zao ili waweze kunufaika na fedha zao au mafao yao wakiwa bado hai na nguvu za uzalishaji mali pale watakapohitaji kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la SSRA *(Social Security Regulatory Authority*) kuzuia fao la kujitoa au kuacha kazi. Sheria hii inakuwa kandamizi kwa kutompa fursa huyu mchangiaji kufaidi jasho lake. *SSRA* inapaswa kurudisha sheria hii ijadiliwe upya hapa Bungeni na pia kuwepo na sehemu ya wananchi au wanachama katika sehemu mbalimbali za kazi kutoa maoni yao! Utaratibu huu uhusishe nchi nzima na siyo sehemu kadhaa kama uwakilishi wa wananchi wote. Sheria ya Mfuko wa mafao ya kazi iangaliwe upya na nafasi itolewe ya kukusanya maoni na maoni hayo yawe huru.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inapaswa kufanya kazi na Wizara nyingine nyingi, hii ni Wizara mtambuka, ili kulinda na kutoa takwimu sahihi za ajira, Wizara inapaswa kufuatilia masuala mbalimbali ya wafanyazi na waajiri. Tunahitaji Wizara iwe inatoa taarifa za ajira zilizotolewa na Serikali katika sekta na Taasisi mbalimbali. Pia Wizara itengeneze mfumo au utaratibu wa kutoa mafunzo ya kujengea uwezo vijana wetu wawe na uhakika wa kujiajiri na siyo zaidi kutegemea kuajiriwa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Gaudensia Kabaka; Naibu Waziri, Dkt. Mahanga; Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina changamoto kubwa sana ya ajira, kwa sababu asilimia kubwa sana ya vijana wetu wasomi bado Serikali haijawa na mpango mkakati wa ajira kwa vijana hao. Pengine Serikali ingetueleza ni vipi suala hili linaweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba Serikali itueleze ni kwa nini bado zile ajira zisizo rasmi mpaka leo hazijarasimishwa?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hasa kazi za ndani, mpaka leo bado wanapata mateso, hakuna mikataba, kila mwajiri anajipangia mshahara anaotaka kumlipa. Ni vema sasa Serikali ikaweka kiwango cha mshahara kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali haijaweza kusimamia mikataba ya wafanyakazi wa migodini kuna malalamiko makubwa sana ya unyanyasaji kwa raia wetu, raia wageni wanapata vibali vya kufanya kazi ambazo hata raia wa Tanzania wana utaalam nazo na hata ikitokea raia wa Tanzania akapata kazi hiyo bado mshahara anaolipwa unakuwa haulingani na nafasi ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia suala la baadhi ya Taasisi zinazotangaza nafasi za ajira bado wamekuwa wakitaka uzoefu wa kazi hiyo. Tatizo hilo linawanyima haki vijana waliomaliza kazi kupata nafasi za kazi hizo na huku wakiwa na vigezo vyote vinavyotakiwa, ningeomba pia jambo hili Serikali ingeliangalia kwa sababu kama Taasisi zote zitahitaji uzoefu vijana wanaotoka *fresh from school* hawatapata kazi.

Mheshimiwa Spika, pia walemavu bado hawapewi kipaumbele katika ajira nchini, pamoja na kuwa walemavu wa aina zote kuhitimu katika Vyuo Vikuu, lakini bado Serikali haijawaweka mpango mzuri sana wa kuhakikisha nao wanatendewa haki katika zoezi zima kuanzia kujua matangazo yenyewe, mahojiano na kupata kazi hizo.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, maisha ya binadamu yanategemea kazi na ajira katika kupata mahitaji ya kila siku, kwa hiyo, Wizara hii ni ya muhimu sana kwa jamii ya Kitanzania. Kwa umuhimu wake napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Wizara kuwa na bajeti ambayo inatosheleza mahitaji ya Wizara.

(ii) Kuangalia maslahi ya wafanyakazi na kuwatetea wafanyakazi ili kulinda haki zao katika maeneo ya kazi.

(iii) Vijana wengi wanaomaliza elimu ya sekondari na vyuo vikuu walio wengi hawana kazi, Serikali iweke mipango mikakati iliyo wazi kwa vijana wetu ili kila kijana anapomaliza masomo yake anajua atafanya nini ili kuyamudu maisha yake.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inatoa matangazo ya ajira kwa vijana, lakini inachukua muda mrefu sana wa kuwaajiri mpaka walioomba nafasi hizo wanajisahau na wengine ambao sio mazuri kwa vijana kama vile kujihusisha na madawa ya kulevya na kuvuta bangi. Sasa naiomba Serikali ikitangaza nafasi za kazi basi, ratiba ya kuajiri iwe inatolewa mapema ili vijana hao waweze kuajiriwa. Kuna unyanyasaji sana wa ajira hasa katika makampuni ya watu binafsi (*private company*) sasa ni vizuri sheria za ajira na kazi ziwekwe wazi kwa wafanyakzi wa makampuni ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, mishahara ambayo inatolewa na makampuni ya watu binafsi ni midogo sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke sera ya mishahara ya wawekezaji ili waweze kuwalipa wafanyakazi wao mishahara ambayo inaweza kuwasaidia katika kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, pia masharti ya ajira kwa vijana yaangaliwe upya hasa kwa vijana ambao hawana uzoefu wa muda mrefu kwa sababu katika kutangaza nafasi za kazi wanaweka kipengele cha uzoefu wa kazi kwa muda, kwa mfano, miaka 2-5 ambayo inawabana sana vijana ambao wanatoka mashuleni/vyuoni.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWAGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Kabaka na Naibu Waziri Mahanga kwa kuteuliwa na Rais kuongoza Wizara hii, hasa yenye changamoto nyingi hasa kwa wale wanaofanya kazi kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, ni bora tukasema wazi kuwa, ni vema sasa kama nchi tukawa tayari kupitia Wizara yako kuleta Muswada wa kuwabana wale ambao wanajiita wawekezaji ili kukawa na haki za wafanyakazi wa viwanda au makampuni ya wawekezaji ili kutoa haki kwa wafanyakazi wa sekta hizo. Kumekuwa na manyanyaso hasa kwa wafanyakazi wa viwanda vya samaki, wafanyakazi hao hufanya kazi zaidi ya saa kumi na mbili, pia hulipwa posho isiyolingana na kazi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi hufanya kazi hadi miaka kumi, mtu huyo akiwa kibarua tu, haajiriwi kwa kutambua kama atamwajiri, itamlazimu amlipe kiinua mgongo ndani ya miaka kumi na hupata

kiinua mgongo kama si laki mbili basi ni laki mbili na nusu tu ndani ya kazi miaka kumi au zaidi. Huu ni uonezi. Kama haitoshi wafanyakazi hawa hufanya kazi baadhi katika vyumba vya barafu, bila vifaa vya kuzuia hali ya baridi iliyoko ndani humo, halafu tunasema kuna *OSHA, OSHA* hasa kazi yao nini? *OSHA* wana bajeti ya kutekeleza kazi yao kwenye maeneo hasa yenye viwanda vingi? Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho naomba tamko lake la haya niliyochangia hapo juu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia kuna manyanyaso ambayo baadhi ya wafanyakazi wanaofanya kazi katika makampuni ya watu binafsi hukamatwa na pesa na kupelekwa katika Mifuko ya Hifadhi. Lakini matajiri hawa huwafukuza wafanyakazi wao na kuwanyima barua ambazo zitawasaidia kupata akiba zao walizoweka. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani kwa waajiri wenye tabia kama hii (hili linanigusa) si haki kuweza kumfanyia haya mfanyakazi ambaye anaweza kuwa amefanya kazi miaka mingi kwa tajiri huyo. Nahitaji kauli ya Mheshimiwa Waziri ili watanzania wenye matatizo kama haya waweze kujua nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kujua kuna kazi ngapi mpya katika mwaka huu ambazo zitatoka Serikalini na ni bora sasa kwa wale wazee wanaostaafu wasiajiriwe kwa mkataba, kwani vijana wengi wasomi wapo mitaani na kazi hawana. Kila miaka Vyuo Vikuu na vya Ufundi vinatoa vijana wengi, pia kuhusu uzoefu kipengele hiki ni vema kikalegezwa na uwezo wa vijana hawa ukaangaliwa wakati wanapotoka vyuoni

mwaka wa pili ambapo huenda kufanya kazi kwa vitendo, namna gani alivyofaulu wakati huo. Pia ni muhimu katika mitaala ya shule za msingi toka darasa la tano hadi la saba kukawa na masomo mepesi ya ujasiriamali ili vijana wetu waweze kuelewa kuwa kuna uwezo wa kujifunza katika kukabiliana na wimbi la ukosefu wa ajira. Tukianzia hapo tutaendelea sekondari hadi vyuo vikuu. Nina imani tutapunguza vijana wazururaji na tutaongeza walipa kodi katika nchi yetu. Tusiwe na wahitimu ambao wanategemea kuajiriwa tu.

Mheshimiwa Spika, naamini tutaokoka tu na maendeleo tutapata, ajira au kujiajiri ni muhimu. Ahsante.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabilioni ya Kikwete na Mikopo kwa vijana; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiona tatizo kubwa la ajira kwa vijana na kwa nia yake njema aliamua kutoa fedha zilizojulikana kama mabilioni ya Kikwete kwa kila Mkoa ili ziwanufaishe wananchi hususani vijana ili waweze kukopa na kunasuka kutoka kundi la umaskini na kuachana na wimbi la kukimbilia mijini kwenda kufanya ajira zisizokuwa na staha kama kupiga debe kwenye vituo vya daladala na kukokota chupa za maji kama vichaa na kwa watoto wa kike kuuza miili yao. Lakini nia hii njema ya Rais haikuweza kuwanufaisha vijana wengi hasa wa vijijini kwa sababu fedha hizi zimedakwa na kundi dogo la wajanja na wamekopeshana wao kwa visingizio kwamba vijana

hawana uwezo wa kukopa. Pamoja na ukweli kwamba vijana wengi hawajapewa elimu ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara, pia kumekuwa na urasimu mkubwa wa kupata fedha hizo kwa wale wachache ambao wana uwezo wa kufanya biashara ndogo ndogo . Ni vizuri sasa Wizara ikapitia upya fedha hizi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuona ni kwa namna gani zinaweza kuwanufaisha vijana wote wa Tanzania pamoja na wale wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kuwa kumekuwa na migogoro kati ya wafanyakazi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusu *formula* ya kukokotoa mafao yao ya uzeeni. Mifuko mingine ikilalamikiwa ikitumia *formula* vizuri zaidi na hivyo kutoa mafao manono na mengine, kutoa mafao hafifu na hivyo kumfanya mstaafu kuishi kwa shida na hivyo kupelekea Mifuko kuanza kushindana kunyang'anyana watumishi na mingine kama *PPF* kuanza kukimbiwa na watumishi. Ni vema sasa Serikali ikaona umuhimu wa kuwa na Mifuko miwili tu ya kujiunga kwa lazima, mmoja ukishughulika na sekta ya umma na mwingine kwa ajili ya sekta binafsi. Huu wa sekta binafsi unatakiwa uwe *flexible* kuliko wa sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna Mfuko wa *GEPF* ambao unaweza kukidhi matakwa ya wafanyakazi wenye mkataba hasa wale wanaoajiriwa kutoka sekta binafsi na hata Wabunge pia maana mkataba wao ni miaka mitano tu. Ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara ni vema sasa Serikali ikawaelimisha wafanyakazi wenye ajira za muda mfupi na kuwahamishia *GEPF*, lakini pia huyu *regulator SSRA*,

kwa maoni yangu ingawa ameanzishwa na Serikali, kwa hali ilivyo sasa, ameonekana kama bado hana umuhimu kwa vile bado hatujawa na *voluntary schemes*, hivyo kimsingi bado hatakiwi kufanya kazi sasa. Wizara itakapoanzisha *voluntary schemes* tunaweza kuwa na *regulator*.

Mheshimiwa Spika, ajira za mikataba baada ya umri wa kustaafu, kwa nchi ilivyo sasa kuna vijana wengi sana wanaomaliza vyuo tena wengi wakiwa wamefaulu kwa kiwango kizuri, lakini wamekuwa hawapati kazi kwanza kwa kigezo kwamba hawana uzoefu na pili kwa kuwa ajira zao zinazibwa na wazee ambao wamefikia umri wa kustaafu na wanaongezewa muda wa kufanya kazi kwa mkataba wa miaka miwili miwili. Ni kwa nini wazee hawa ambao wamemaliza muda wao wa utumishi waache kupumzika na kuendelea kula pensheni zao na kuwaachia vijana nao walitumikie Taifa baada ya kusomeshwa kwa kodi za wananchi. Mzee au mstaafu apewe ajira ya mkataba pale itakapoonekana ni kweli kwamba katika nafasi ile hakuna mtu anayeweza kufanya kazi ile baada ya Tangazo kutolewa na Watanzania wote wakaonekana hawawezi ila yeye tu na hiki ni kitu ambacho sidhani kama kipo. Huu utaratibu unatakiwa uachwe ili kutoa nafasi ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya, pongezi za kipekee kwa Mheshimiwa

Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango utakuwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ajira kwa vijana;
(ii) Mifuko ya Jamii; na
(iii) Masharti ya ajira.

Mheshimiwa Spika, nianze na ajira kwa vijana, imekuwa tatizo kubwa sana na hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam, idadi kubwa ya wahitimu wa vyuo wako mijini. Naishauri Serikali yangu sikivu sasa kuungana na Wahadhiri wa vyuo kuweka katika mitaala somo la ujasiriamali ambalo litawaandaa wanafunzi kujiajiri mara wamalizapo masomo. Ajira za Serikali ni chache sana haziwezi kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali idhibiti vijana wanaotoka nje kuja kufanya kazi Tanzania, nchi zinazoleta watu wengi ni India, Kenya na Uganda. Naomba Serikali ifanye uchunguzi kutambua mwingiliano wa ajira uliopo.

Mheshimiwa Spika, pili, nizungumzie Mifuko ya Jamii; *NSSF, PSPF*, Bima ya Afya na kadhalika, Mifuko yetu inafanya kazi nzuri sana, lakini shukrani za kipekee ziwaendee *NSSF* kwa kazi nzuri wanazofanya, ni nyingi mno na tunaziona. Ushauri wangu, Serikali iangalie uwezekano wa kufanya marejesho ya fedha zinazotumika katika miradi ya Serikali ili ziweze kufanya kazi nyingine na kuwawezesha wastaafu walipwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni urasimu wakati wa kulipwa mafao, milolongo imezidi pale unapohitaji mafao yako, barua za ajira na mambo mengine mengi tu kwa nini haviwekwi katika *system* kama benki? Ukienda na kitambulisho wakulipe? Mfuko wa watumishi wa umma unasumbua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niongelee masharti ya ajira kwa vijana, tunaomba kipengele cha uzoefu wa kuanzia miaka miwili watoe kabisa watu wote wana uwezo wa kufanya kazi miezi mitatu tu ya majaribio inatosha mtu kufanya kazi popote.

Mheshimiwa Spika,naunga mkono hoja.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, ajira ni tatizo kubwa sana, si Tanzania peke yake bali duniani kote, hii imesababishwa zaidi na mtikisiko wa uchumi wa mara kwa mara unaotokana na vita vya Kimataifa unaoathiri bei ya mafuta katika Soko la Dunia. Serikali yetu imekuwa ikijitahidi sana kupambana na hali hii na kiasi fulani naisifu kwa jitihada. Ili ajira zipatikane ni lazima uchumi imara ujengwe ambao utaruhusu fursa za ajira kuwepo. Niishauri Serikali na Wizara, tutumie fursa ya gesi iliyopatikana kujenga uchumi na kutengeneza ajira kwa ajili ya watu wetu hasa vijana, rasilimali hii ya gesi imeshaongelewa sana na naamini hii ni nafasi yetu nzuri ya kupunguza tatizo la ajira lakini tukijipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hitaji linalojirudia kila wakati toka kwa wafanyakazi la kuhusu ujira/mshahara mdogo. Hali hii imesababisha kuwepo

kwa migogoro isiyokwisha baina ya Serikali na wafanyakazi. Naomba niishauri Serikali iweke utaratibu wa kukaa meza moja kila mara angalau mara nne kila mwaka yaani kila baada ya miezi mitatu ili kuwapa hali halisi ya uchumi, uwezo na nia safi ya Serikali katika kuwatumikia. Hili lifanyike kupitia sekta mbalimbali au Idara na Taasisi za Serikali, yapo maeneo mengi ambayo waajiri hawana desturi ya kuonana na wafanyakazi wao kitu ambacho husababisha manunguniko yasiyokwisha miongoni mwa wafanyakazi na kufikiri Serikali haiko pamoja nao. Waajiri, Idara, Taasisi na vingine ziagizwe kupanga utaratibu wa kukutana na wafanyakazi kila mara.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Wafanyakazi na Mabaraza ya Wafanyakazi ni vyombo muhimu vya kuleta ufanisi mahali pa kazi, vikitumika vizuri. Kwa bahati mbaya, vyombo hivi vimekuwa vikichukuliwa na waajiri na Serikali kama maadui. Ni ukweli usiopingika kuwa vyombo hivi vikishirikishwa kikamilifu katika masuala mbalimbali naamini vyombo hivi vitasaidia Serikali kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwa sababu vyombo hivi viko katika Taasisi na Idara zote mahali pa kazi. Ni lazima Taasisi na Idara husika ziweke mikakati ya kuwa na mahusiano mazuri baina yake na vyombo hivi ili kutengeneza utamaduni sisi/yetu badala ya mimi/yeye, sisi/wao. Wapo baadhi ya waajiri na wasimamizi wa wafanyakazi wanatengeneza mifumo kandamizi kwa wafanyakazi, mfano, upendeleo, udikteta, dhuluma, uonevu na kadhalika. Mambo kama haya hayatasaidia kuleta utulivu na ufanisi katika maeneo ya kazi. Wapo waajiri na wasimamizi wanaofukuza waajiri pasipo kufuata taratibu za kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la usuluhishi wa migogoro kazini nalo liangaliwe upya, chombo kilichoundwa kushughulikia suala hili ni Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* ili kupunguza urasimu na pia mlundikano wa kesi Mahakamani. Cha ajabu chombo hiki nacho kimekuwa kikwazo na urasimu kama ule wa Mahakamani. Badala ya kesi kusikilizwa kwa muda mfupi, shauri linachukua muda mrefu kiasi cha kupoteza ile maana/mantiki ya kuanzishwa kwake. Nimepewa taarifa na baadhi ya wafanyakazi kuhusu ucheleweshaji mkubwa wa mashauri yao. Chombo hiki kiagizwe kifanye/kitimize ile maana ya kuanzishwa kwake ili wafanyakazi watendewe haki zao.

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri mabadiliko ya kipengele cha fao la kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, naiomba Wizara na Serikali kwa ujumla isikilize kilio cha wafanyakazi. Kilio chao ni kuendelea na ule utaratibu wa mwanzo wa kupata fao la kujitoa (*withdraw benefits*) ili kuwatendea haki wafanyakazi wetu. Naomba tusipuuze kilio cha wafanyakazi kwani hata katika Jimbo langu sitapenda kuwaona watumishi wakikosa raha na kunung'unikia Serikali yao kwa jambo ambalo liko ndani ya uwezo wetu. Linalowezekana leo lisingoje kesho.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali na sera wachukue hatua mahsusi kuelimisha umma kuhusu mfumo wa hifadhi ya jamii, changamoto iliyopo kwenye suala la fao la kukotoa inatokana na Mfuko wa *Social Security* kutoeleweka. Kwa vyovyote vile ni lazima kuendelea kuruhusu wanachama kujitoa, lakini

lazima umma uelezwe madhara ya kujitoa kwenye maisha ya huzuni. Ni jukumu la dola kuhakikisha pensheni kwa wazee. Serikali isisite kuchukua uamuzi muhimu na yasiyopendwa kuhusu *pension*. Nakubaliana na ushauri wa Kambi ya Upinzani kwamba *withdrawal* iwe *partial (only 7.5 out of 20*) iruhusiwe. Au michango ile tu iliyotolewa na wanachama ndio uruhusiwe kutolewa na michango ya waajiri ibakie kwenye Mifuko mpaka kustaafu. Serikali lazima ilinde mfumo wa hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, narejea pendekezo langu kwamba Mifuko ya Kitaifa iunganishwe na kubakia na mifuko miwili tu *NSSF* na *PPF* iunganishwe na kuwa Mfuko mmoja kwa ajli ya sekta binafsi na *PPF* na *LAPF* na *GEPF* iunganishwe kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya sekta ya umma. Mifuko yote iwe chini ya Wizara ya kazi na ajira kwa ajili ya uratibu bora, suala hili liamuliwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za *actual* kuhusu Mifuko ya Pensheni ziwekwe wazi ili kuepusha maneno ya uzushi kwamba mifuko imefilisiwa. Tusiruhusu watu wachache kuweka hofu kwa wananchi kuhusu pensheni zao. *NSSF* iangalie namna ya kuwalipa pensheni wazee kupita *M-Pesa*, hii itapelekea wazee kupata mafao yao kwa haraka na mahali walipo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, kwanza nomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Kazi na Ajira kwa hotuba nzuri waliyoitoa hapa Bungeni. Pia nawapongeza kwa kuendelea

kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005-2010. Pamoja na pongezi hizi ninayo machache ya kuchangia ili kuongezea pale Mheshimiwa Waziri alipoishia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kulipa pensheni ya wazee wote nchini jambo ambalo lilipokelewa kwa shangwe na wazee wote nchini na pia kwa kuzingatia majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira Bungeni wakati akijibu swali namba 327 amelieleza Bunge kuwa Serikali inakusudia kuanzisha malipo ya pensheni kwa wazee wote nchini kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Naipongeza hatua hii na tunasubiri utekelezaji wake na ni vizuri tukaelezwa utaratibu utakuwaje.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kati ya Wizara nyeti sana katika nchi yetu, lakini ni kati ya Wizara zinazopewa bajeti ndogo sana ambayo haikidhi mahitaji/hali. Je, ni kwa nini Wizara hii isipewe bajeti halisi. Mahakama Kuu, Kitengo cha Kazi wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani watumishi wa Wizara hii hawatoshi hasa Waheshimiwa Majaji kitendo kinachochelewesha uamuzi wa mashauri yanayowahusu wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina utaratibu mzuri wa kuweza kutoa taarifa za hali ya ajira na ukosefu wa ajira nchini, taarifa zinazotolewa kwa sasa ni za tafiti zilizofanyika mwaka 2006 yaani miaka sita iliyopita, hivyo taarifa hizi haziendi na hali halisi ya sasa. Nashauri Serikali ije na mfumo kabambe utakaowezesha kutoa taarifa sahihi kwa kila mwaka kuhusu ajira na ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisoma kwenye vyombo vya habari hasa magazeti na televisheni kuwa wafanyakazi wanapinga Sheria ya Mifuko ya Jamii kuhusu kupokea pensheni zao hadi watakapostaafu! Watumishi wengi wanataka sheria ibadilishwe ili watumishi waruhusiwe kujitoa kwenye pensheni muda wowote kabla ya kufikia umri wa kustaafu. Naona kuna mikanganyiko ya uelewa kati ya mafao yanayoruhusu kujitoa (*provident schemes*). Napenda kuishauri Serikali hasa Wizara ya Kazi na Ajira itoe elimu ya kutosha kwa wafanyakazi wote na hata kupitia vyama vyao. Taarifa pia zitolewe kwenye magazeti, redio, luninga, mikutano ya hadhara na kadhalika. Pia Waziri atoe tamko kwenye vyombo vya habari kuhusu hali hii, pia kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi kuhusu sakata hili ili nao waende kuelimisha wananchi wanaowaongoza. Naamini kwa kufanya hivyo kutaondoa matatizo yanayoendelea nchi nzima. Hakuna sababu ya Serikali kuendelea kukaa kimya wakati hali halisi iko wazi.

Mheshimiwa Spika, migogoro kazini ni tatizo kubwa, hivyo, ni vizuri Serikali iiwezeshe Wizara kifedha ili ifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo ya kazi hasa Mikoani ili waendelee kutoa elimu katika maeneo ya kazi, jambo ambalo litapunguza hata ikibidi kumaliza migomo kazini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti. Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu ina kazi nyeti ya kusimamia ajira nchini. Ajira ni tatizo kubwa sana (*it is a time bomb*). Vijana wengi hawana kazi na kwa sababu hiyo wengi wanakuwa *frustrated* na kuamua kujiingiza katika masuala ya uhalifu. Baadhi ya uhalifu katika biashara ya madawa ya kulevya na wengine kuamua kuwa majambazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira ni kubwa sana Wilayani Ngara, vijana wengi waliomaliza darasa la saba la 12 na hata wale waliomaliza *form* VI wako vijiweni. Kunahitajika mkakati wa Kitaifa wa kuwawezesha hawa vijana waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Ufundi; vijana wengi wanahitaji kupewa mafunzo ya ufundi stadi pamoja na elimu ya ujasiriamali ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo**;** Wizara ya Kazi na Ajira ikishirikiana na Waziri wa Uwezeshaji na ile ya Maendeleo ya Jamii mnatakiwa kuwatafutia vijana mikopo nafuu ambayo watakopa kama vikundi na kuanzisha miradi midogo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mpango wa MKURABITA ni fursa muhimu sana katika kuongeza ajira, Serikali inatakiwa kuongeza bajeti ya MKURABITA ili mpango wa kurasimisha mali na biashara za wanyonge ufanikiwe. Vijiji vyote vikipimwa na Wizara ya Ardhi na

kuwa na matumizi bora ya ardhi, vijana watahamasishwa kuwa na mashamba yaliyopimwa na kwa kutumia mashamba hayo kuweza kupata hati miliki za kimila ambazo watazitumia kujipatia mikopo nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *SACCOS*, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya maendeleo ya Jamii na Wizara inayohusika na vijana kuwa na mikakati madhubuti ya kuunda vikundi vya ujasiriamali, vikundi vya *SACCOS* na kisha kuwatafutia mikopo.

Mheshimiwa Spika, ajira ya wageni Tanzania imekuwa *a plastic society* wageni wanaingia na kutoka bila udhibiti wowote, wageni hao wanaingia na kupewa *Resident permits* na hapo hapo *work permits,* vibali vyote viwili vinatolewa na *Immigration*. Wizara ya Kazi inatakiwa kudhibiti ajira ya wageni. Sera ya ajira inatakiwa kutamka kinaganaga kwamba wageni watapewa kazi ambazo wananchi hawana uwezo nazo au Wataalam Wazalendo wapo kwa ajili ya kazi za aina hiyo. Kwa hiyo, ni muhimu kutenganisha *resident permit* na *work permit*. *Resident permit* itolewe na *Immigration* na *work permit* itolewe na Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la *Foreign Contractors* na hasa wa miundombinu ya barabara kama vile Wachina kuleta vibarua wengi wa kichina pindi wanapopewa mikataba ya kujenga barabara. Kwa nini iwe hivyo wakati wangeweza kutumia vibarua wetu.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba Serikali isimaie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, usalama wa ajira migodini, wafanyakazi wanafukuzwa kazi kila siku, hivi sasa kuna wafanyakazi saba wa Mgodi wa Bulyanhulu wameandikiwa barua ya kusimamishwa kazi eti kwa kushiriki kwenye mgomo haramu kuhusu suala la mafao ya kujitoa *NSSF/PPF*. Kama Waziri wa Kazi alivyokwishaagiza kwamba warudishwe kazini bila masharti, naomba alisimamie hilo, pia wameomba aende Bulyanhulu kuzungumza na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu athari za kiafya kwa wafanyakazi migodini; wafanyakazi wengi wanaathirika kiafya wakiwa kazini hawatibiwi hadi mwisho na wengi wanakufa ovyo na mwajiri kukataa kuwahudumia kwa madai kuwa, hakuna uthibitisho kuwa maradhi yao yanatokana na kazi. Naomba Serikali ifanye yafuatayo:-

(a) Kuwabana waajiri watoe huduma bora za afya kwa wafanyakazi; na

(b) Kuwabana waajiri kuwawekea Bima za maisha wafanyakazi walio katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni suala la mafao ya kujitoa kwa wafanyakazi. Suala hili limeleta mgogoro mkubwa, naomba wafanyakazi waruhusiwe kuendelea kujitoa na kupewa mafao yao pindi wanapopoteza ajira zao.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu Vyuo vya Ufundi Kahama; pamoja na Wilaya ya Kahama kuwa na migodi miwili mikubwa, hakuna Chuo cha Ufundi Stadi kwa ajili ya vijana ili wapate kazi migodini. Naomba sasa Serikali itekeleze ahadi yake ya kujenga Chuo cha Ufundi eneo la Bugarama Jimboni Msalala. Ni ahadi aliyoitoa Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa Kampeni mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya nyongeza hiyo, sasa naomba kuhitimisha mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, pale asubuhi wakati ninatambulisha wageni wetu hapa, bahati mbaya Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi niliwataja kwa jumla tu, sikuwataja kwa sababu nilikuwa sijapata majina. Sasa nimepata majina. Vyama vya Wafanyakazi, vinaongozwa na Katibu Mkuu *TUCTA*, yeye ni Kaimu Kiongozi wa Msafara, anaitwa Heziron Kaaya, naomba asimame alipo. Ahsante sana Bwana Kaaya. Halafu ndugu Baraka Hussein Igagula, Mwenyekiti wa *TAMICO*, mahali popote alipo asimame. Viongozi wangekaa kule bwana. Kuna Hassan Ameir, Katibu wa *TAMICO*. Viongozi wote nitakaowataja wahamie kule kwenye *Speakers Gallery*. *(Makofi)*

Halafu kuna Katibu Mkuu TUICO, anaitwa ndugu Mkakatisi Boniface, naomba popote alipo asimame.

Katibu Mkuu *TUGHE*, anaitwa Ali Kiwenge, naomba asimame alipo, ahsante. Mwenyekiti wa *TUGHE* anaitwa Dkt. Mrutu, naomba asimame alipo, ahsante. Lakini viongozi wote hawa naomba wakae *Speakers Gallery*. *(Makofi)*

Halafu kuna Rais wa CWT, Ndugu Mkoba Gratian, ahsante sana. Kaimu Katibu Mkuu wa CWT, Ndugu Olochi Ezekiel, ahsante. Naomba mhamie kule wote. Kuna Kaimu Katibu, TIPAU anaitwa ndugu Kabegwe Kabegwe, naomba asimame mahali alipo. Halafu kuna Katibu Mkuu wa TEUTA, anaitwa ndugu Yunusu Mdalo. Kwa hiyo, naomba viongozi wote wa Vyama vya Wafanyakazi wahamie katika *Speakers Gallery* pale. Karibuni sana. Ujenzi wa Taifa letu ni pamoja na sisi wote tuweze kufanya vizuri katika shughuli zetu.

Sasa naomba nimwite *AG* kwa dakika chache.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kunipa nafasi hii, lakini pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga kwa kazi nzuri waliyofanya na kwa ushirikiano wao na Ofisi yangu.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa ajili ya kuzungumzia neno moja tu ili kuweka kumbukumbu zetu sahihi kusudi tuonekane kama ni chombo makini.

Mheshimiwa Spika, asubuhi kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani kuanzia ukurasa wa 16 mpaka

ukurasa 20, yamesemwa maneno mazito ambayo yanaonyesha kwamba Serikali ililipenyeza kinyemela kwa maana kwamba kwa kuvunja haki za Bunge katika Muswada huu ambao Mheshimiwa Waziri nafurahi amesema ni Mfuko wa Pensheni.

Mheshimiwa Spika, katika *record* zetu, ukiona *Bill* yaani Muswada uliochapishwa tarehe 27 Julai, 2012 pamoja na Muswada mwingine ambao ulikuwa umechapishwa kabla ya wakati huohuo, utaona kwamba kwenye Ibara 107 inasema hivi, kwenye huu Muswada wa tarehe 27 Julai, 2012, ni ukurasa wa 65, Ibara ya 107 inasema, *the Principal Act is amended by repealing sections 37 and 44.*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulichapishwa pia kwenye *record* za Bunge yaani *Hansard* na ukiangalia ukurasa wa 317 wa *Hansard* katika Mkutano wa Saba, Kikao cha Nne, tarehe 13 Aprili, 2012, Ibara ya 107 ni sawasawa na Ibara niliyorejea kwenye Muswada halisi. Wanasema, *the Principal Act is amended by repealing sections 37 and 44.*

Mheshimiwa Spika, *sections* hizo zinazorejewa ni zile za Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma yaani Sheria inaitwa Sura Namba 372 au kama unapenda Kiingereza *PPF*. Sasa vifungu hivyo vilikuwa vinasemaje, maana vilirekebishwa kwa kufutwa. Naomba tuelewane na wale ambao wanafanya marejeo waangalie ninachosema na wasiangalie *lips* zangu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 44 cha Sheria hiyo kinasomeka, nanukuu kwa ruhusa yako:-

*"44(1):- Where a member ceases to be benefits employed in circumstances in which he is not eligible for any pension, gratuity or any other benefit under the provisions of this Act, he shall be refunded the amount of his own contributions and that of his employer to the Fund.*

*(2) Where a member has been employed for a period of not less than five years and the cessation of such employment is not due to dismissal for misconduct the amount of his own contribution and that of his employer together with a simple interest at that rate to be determined by the Board of Trustees shall be paid to him".*

Mheshimiwa Spika, vifungu hivyo ndio mapendekezo yaliyoletwa kwenu Waheshimiwa Wabunge na hakuna mtu atakayesema kwamba Wabunge hawakuwa makini, mkasema vifutwe na vikafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri si vizuri hapa, nasema si kweli na niliposikia maneno haya mimi nilifanya utafiti kwa sababu aidha mimi niache kukalia kiti hiki niondoke au mtu awe amefukuzwa kazi. Hakuna kosa kubwa, hakuna *contempt* ya *Parliament* kama kuingiza maneno ambayo Bunge halikuyasema.

Mheshimiwa Spika, sasa tunachofanya ni nini? Tunachofanya ni kwamba ni vizuri na sisi tuelewe

kwamba hii *section* ni *exception* lakini msingi wa pensheni ni kwa ajili ya uzee, ujanja si sifa na uzee siyo kashfa, fainali uzeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa inaonekana kuna msukumo, wafanyakazi wengine wanaona kwamba mtu anafanya kazi anafika miaka 35 anaacha, hawezi kungojea mpaka afike miaka 55. Kwa hiyo, kwa ajili hiyo tutarudisha, lakini tunajua ni *exception.* Kwa sababu na sisi tumeingia kwenye mahusiano na wenzetu wa Kimataifa kwenye eneo hili, naomba Waheshimiwa Wabunge kabisa waone kwamba kwa kweli hakuna kitu cha hila kilichoingizwa hapa na sasa tumepata akili timamu, akili iliyotukuka, tunaona turejee na Bunge haliwezi kunyimwa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tutaleta marekebisho hapa na ninyi mtarudisha maneno hayo kwenye sheria. Nilikuwa nafikiria kuyafanya kwa njia ya kitaalam lakini nikafikiri ni kosa kwani haitakuwa ni kazi ya Bunge kwamba unafanya kama ni *rectification of printing errors* kwa sababu hii sio *error*. Hili ni kama Bunge liliamua na Mheshimiwa Spika nina ushahidi katika *Hansard,* ukurasa wa 224, kifungu cha 106, 107 mpaka 117 inasema Ibara zote zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuwahakikishia Wabunge lakini hasa Watanzania kwamba Serikali haikufanya hila isipokuwa hili ni jambo ambalo lilifanyika hapa Bunge na halikufanyika kwa sababu Wabunge walikuwa wamelala, hapana! Wakati ule tulifikiri hivyo, ila hawa waliolalamika ndio

wametuonesha kwamba sio sawasawa na hakuna haja ya kuona aibu, turudi tufanye marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea, tuna muda mfupi Mheshimiwa Naibu Waziri. Kila mtu anapewa muda wake wa kuchangia, mimi muda wangu ni *very scarce,* ninafanya mahesabu muda hautoshi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie kidogo kwenye hoja hii ya Waziri wa Kazi na Ajira. Nitangulie kutamka kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika wako, Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa ufanisi na umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu kwa miongozo yake ndani ya Bunge na ndani ya Serikali inayosaidia sana Serikali kutimiza majukumu yake kama inavyotarajiwa na Bunge na kama inavyotarajiwa na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wenzangu na Watanzania wote kutoa salamu za rambirambi na pole nyingi kwa misiba iliyowakuta baadhi yetu na ajali zilizotokea hapa nchini ikiwemo ajali ya *M.V. Skagit* iliyowaua Watanzania wengi.

Mwenyezi Mungu awarehemu wote waliopoteza maisha na kuwapa nguvu na imani wafiwa wote.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake thabiti na kuendelea kuniamini katika nafasi yangu. Nimshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, kwa ushirikiano na uongozi wake. Napenda pia kumshukuru mke wangu mpendwa Florence ambaye leo yuko hapa pamoja na watoto wetu na familia yetu kwa ujumla kwa kuendelea kunivumilia, kunisaidia na kunipa moyo katika kutimiza majukumu yangu ya kifamilia, ya Kibunge na ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda niwashukuru sana wananchi na wapiga kura wangu na viongozi wenzangu wote wa Jimbo la Segerea kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano mkubwa katika kutimiza wajibu wangu wa kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Segerea. Nataka niwahakikishie kwamba yote yale ambayo tuliahidi kuyatekeleza katika Jimbo letu hadi mwaka 2015 na hasa kero za maji, barabara na wananchi kujiletea maendeleo kupitia ushirika na vikundi, tutayatekeleza tukishirikiana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hisia kali ya upendo, napenda niwashukuru sana wapiga kura wangu na Watanzania wote wanaonipenda kwa namna walivyonifariji, kunisaidia na kuniombea wakati nilipokuwa nakabiliwa na kesi ya uchaguzi katika Jimbo letu la Segerea. Namshukuru Mungu kwamba haki

iliweza kutendeka Mahakamani na kesi ile ya kipuuzi kabisa ikatupiliwa mbali na kama nilivyosema siku ya hukumu pale Mahakamani, wananchi wote bila ya kujali itikadi zetu sasa tuache malumbano, tushirikiane kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Segerea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi, napenda sasa nichangie hoja ya Waziri wa Kazi na Ajira kwa kutoa ufafanuzi kwenye baadhi ya hoja zilizotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri wangu atakuja kutoa ufafanuzi kwa hoja zingine. Kutokana na hoja kuwa nyingi na muda kuwa mdogo, mimi na Mheshimiwa Waziri huenda tusiweze kujibu hoja zote hapa leo, lakini tunaahidi baadaye kuleta majibu ya hoja zote zilizotolewa na Wabunge kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitachangia zaidi katika suala la ajira na ukosefu wa ajira hapa nchini. Wabunge wengi sana wamechangia suala la ukosefu wa ajira hapa Tanzania na nitachangia machache na Waziri wangu atakuja kuongezea mengine. Lakini nianze kwa kusema kwamba tafsiri ya ajira ni nini? Nataka tukubaliane na Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba kwa kweli ajira ina *characteristics* tatu muhimu ukiacha zingine. Kwanza, ajira lazima iwe ajira ambayo inakubalika kisheria, ukiuza bhangi sio ajira, lakini pili, ajira iwe ya staha kama alivyosema Mheshimiwa Bulaya, yaani iwe ambayo unaonekana kwamba unafanya kazi ya staha isiyokuwa ya kuonewa, kudhulumiwa, kulazimishwa na ya kuumizwa, lakini tatu, ajira angalau uweze kupata kipato ambacho si chini ya kiwango cha chini cha kima cha chini. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Bulaya kama wanauza viberiti na wanaweza mwisho wa mwezi wakapiga hesabu kwamba viberiti vile vimewapatia kima cha chini, ni ajira inayohesabika katika maana hii.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukosefu wa ajira imeelezwa vizuri sana na Wabunge wengi na siwezi kuwataja wote hapa, lakini niseme kwamba suala hili kwanza sio tatizo la Tanzania peke yake, tumeelezwa duniani kote watu milioni 205 hawana kazi. Lakini ukiangalia takwimu za kiwango cha ukosefu wa ajira sasa hivi ni asilimia 6.2 kwa maana ya wastani kidunia na sisi tuko kule kwenye 12 lakini wenzetu wengi tu hata nchi zilizoendelea wako kwenye 8, 9, 10, 11 hata ukichukua Uingereza, Marekani ambao wako kwenye 8.3 mwezi huu, wote wako kwenye *level* hiyohiyo. Kwa hiyo, unakuta kwa kweli tatizo hili ni kwa nchi zilizoendelea na nchi zetu ambazo hazijaendelea, Tanzania ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia masuala ya takwimu, Mheshimiwa Engineer Chiza, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwamba hatuna takwimu, ni kweli. Suala la takwimu vilevile si la Tanzania peke yake ni la nchi nyingi za Afrika. Ndiyo maana hata ukitaka kuangalia takwimu za ajira kwenye nchi za Afrika utakuta 2005, 2006 kama ambavyo ilivyo Tanzania na hii inatokana na sababu za wazi kwamba nchi zetu hizi kwanza hatukuwa kwa mfano na *ID* au utambulisho wa Taifa halafu uchumi wetu ni *informal* ku-*capture data* inakuwa ni ngumu sana lakini vilevile hatujaendelea sana katika mtandao wa kisasa. Kwa hiyo, mambo haya na mengine ya

kuweza ku-*capture* mambo ya kiuchumi kama *unemployment* inakuwa ni vigumu sana na ndiyo maana bado tuko nyuma, lakini sio sisi peke yetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukosefu wa ajira ambayo imechangiwa sana na Wabunge wengi ni mbaya katika nchi yetu na kama ambavyo imezungumzwa tunayo nguvukazi sasa hivi Tanzania ya watu karibuni milioni 25 kati yao asilimia 70 ni vijana. Kwa maana kwamba wale watu 25,000,000 ambao ni nguvukazi kati ya miaka 15 mpaka 34 ambayo ni asilimia 70 watu milioni 17.5 ni vijana, lakini wanaokosa kazi, nguvukazi hii ya watu milioni 25, milioni tatu hawana kazi ni asilimia kama 12. Kwa vijana ni mbaya zaidi asilimia 30 hawana kazi kwa wale milioni 17.5, milioni mbili hawana kazi kwa upande wa vijana na wanaendelea kuingia kwenye soko la ajira. Walikuwa wanazungumzia laki nane wanaingia hawa vijana kati ya miaka 15 na 24 wanaomaliza elimu ya msingi, sekondari na vyuo sasa hivi tukipitia takwimu vizuri ni milioni moja vijana wanaomaliza masomo yao wanaingia kwenye soko la ajira. Kati yao ni asilimia tano tu kama 50,000 ndio wanapata kazi kwenye sekta rasmi, sio kwamba ndio wanaokuwa na ajira tu, maana yake kuna dhana kwamba ni vijana 40,000 tu au 50,000 ndio wanakuwa na ajira wengine wote hawana ajira, hapana. Wale wanaoingia kwenye sekta iliyo rasmi ni asilimia tano lakini asilimia 35 kati ya wale bado wanakwenda kwenye kilimo na asilimia 30 nyingine wanakwenda kwenye sekta isiyo rasmi, ile asilimia 30 ya vijana kwa kweli waliobaki sasa ndio hawana kazi. Sasa tatizo ni kubwa, kilimo bado kinatoa ajira lakini

vijana bado kwa kweli wanapata tabu kama mlivyosema.

Mheshimiwa Spika, sababu zimetolewa na nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwa nini ajira ni shida katika nchi yetu. Uchumi wetu ni mdogo kuweza kuhimili watu wengi hao wanaoingia kwenye soko la ajira. Hatuna uchumi, hatuna *industrial economy* bado tuko na uchumi ule ambao ni wa kilimo zaidi, viwanda havijaendelea sana na biashara kubwakubwa, wawekezaji hawajaingia kwa wingi sana kwa hiyo tunalo tatizo hilo. Vilevile vijana wetu wanaomaliza elimu ya juu wengine wanakuwa hawana ujuzi unaotakiwa kwenye maeneo ya kazi. Lakini tunajua vilevile kwamba kuna mitaala ambayo haina tija sana ndani ya soko la ajira na vijana wanatangatanga hawa wengine wana digrii ukiacha wale Madaktari, Wahandisi ambao wanapata kazi, Wafamasia au wataalamu wa Kilimo, lakini wengine hawa wanapata shida sana mitaani. Lakini vilevile elimu ya ujasiriamali ni shida, vijana kupenda kazi, kuwa wabunifu, kuingia kwenye sekta zingine ambazo zinaweza zikawafanya wakapata ajira imekuwa ni tatizo kubwa. Ukosefu wa mitaji ni tatizo kubwa na mmelisema sana hapa na ndiyo maana Serikali imekuwa ikiendelea kuhamasisha suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo na sababu ziko nyingi, sasa tunafanya nini? Wengi mmetoa hapa njia mbalimbali na mimi nakubaliana na ninyi mikakati ambayo mmeisema ndiyo hiyohiyo ambayo kwa kweli Serikali tumekuwa tukiiendeleza na nianze kwa kusema tu kwamba kwa kweli katika kutafuta mikakati ya

kukuza ajira hapa nchini lazima tuelewe kwamba suala hili ni mtambuka. Si Wizara ya Kazi inayotegemewa kutoa ajira, lakini ni uchumi mzima unaotakiwa kuleta ajira. Mimi nataka kukubaliana kabisa na Dkt. Mbassa, Mheshimiwa Kigola na hata Mheshimiwa Janet Mbene na wengine ambao mmesema jamani suala hili ni mtambuka. Katika mikakati hii kuna mikakati ya kukuza ajira kupitia ukuaji wa uchumi na uwekezaji na uzalishaji pamoja na Serikali kupanuka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizo ajira zinaletwa na Serikali na zinaletwa na sekta binafsi. Katika Serikali, kuna ile ajira ambayo wanaajiriwa katika nafasi za Walimu, Wafamasia, Madaktari na kadhalika lakini Serikali hiyohiyo ukiacha wale wanaoajiriwa ndani ya Serikali, Serikali inawawezesha wananchi wengine wengi kuajiriwa kwa kuweka bajeti yake kubwa katika mwaka huu wa fedha, mkiangalia ule mpango wetu wa maendeleo karibu zaidi ya shilingi trilioni 4.5 zinakwenda kwenye sekta mbalimbali za uchumi na miundombinu na huduma za jamii. Zile fedha watakaotekeleza miradi ile wale Makandarasi wataajiri watu, kwa hiyo tumepeleka kwenye barabara, nishati, mawasiliano, kilimo tumepeleka fedha nyingi kule ajira zinatoka, afya, maji, ujenzi wa shule na kadhalika. Kwa hiyo, ukiacha sekta hii ya kuajiri watu moja kwa moja bajeti ya Serikali inayokwenda kwenye hizi sekta inazalisha ajira kule.

Mheshimiwa Spika, lakini mlemle ndani kwenye sekta za uzalishaji kuna sekta binafsi, wawekezaji tunaowaleta ndani ndio maana tunajitahidi jamani tuendelee kuwaita wawekezaji waje nchini

wanawekeza kwenye kilimo, mawasiliano, hizi simu zetu zote hizi, hawa wenzangu wanywa bia tunafurahia Makampuni ya Bia yanapokuja kwa sababu ajira inatoka kule, mawasiliano, madini, utalii, hoteli zinazojengwa na watu binafsi na wawekezaji kutoka nje na ndani zinaleta ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiacha mikakati hii ambayo tunaendelea nayo ya kukuza ajira kupitia ukuaji wa uchumi na uzalishaji ndani ya uchumi wetu sasa ndio unakuja kwenye ile ambayo ni ngumu sana mikakati ya moja kwa moja ya kukuza ajira, ile hasahasa kwa zile ajira ambazo ni kwa sekta isiyo rasmi. Wale ambao wameshindwa kuajiriwa moja kwa moja ile sekta ya kujiajiri ni sekta nyingine. Sasa hii tunafanya nini, ndiyo hiyo sasa mafunzo ya ujasiriamali ili hao waweze kujiajiri ndiyo tunayo *SIDO, VETA* tunafundisha, tuna Mifuko mbalimbali, Mifuko ya JK, Mifuko ambayo iko chini ya Baraza la Uchumi, Mabenki mbalimbali, *TIB*, Benki ya Akinamama, zote hizo zitoe mitaji ili watu wakope wafanye ujasiriamali waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema tukiendelea kuwekeza kwenye mambo haya ambayo Serikali inaendelea kufanya, nina hakika kwamba ajira zitaendelea kuzalishwa. Sasa sisi kama Wizara ya Kazi, kama nilivyosema mwanzoni sisi kazi yetu kwa kweli sio kuleta ajira ni kuweza ku-*coordinate* haya yanayofanyika ili tujue ajira zinavyotoka na tuweze kushauri namna ya kukuza ajira kwa kusimamia sera na programu za kuleta ajira ambazo tunazisimamia. Nakubaliana na Profesa Kahigi, Mheshimiwa Kigola na

hata Mheshimiwa Umbulla. Sasa nasema bajeti yetu ni ndogo, sisi si kwamba tunataka bajeti kubwa sana, sisi ukipeleka bajeti kubwa kwenye kilimo watu wakaajiriwa kule furaha yetu sisi watu waajiriwe. Ukiweka bajeti kwenye viwanda, madini kwa wingi, kwenye umeme watu wakaajiriwa huko sisi tunachukua takwimu tunafurahi. Hatuna haja sisi tupate fedha kama anavyopata Mheshimiwa Magufuli, hata kidogo lakini ni kweli kwamba katika hii *coordination,* ufuatiliaji ku-programu hizi tunahitaji fedha sio nyingi, sisi tukiweza kupata shilingi bilioni tano (5) na mwaka kesho nadhani tutapata shilingi bilioni tano (5) zaidi tunaweza tukafanya mambo makubwa sana katika hii *coordination* kwa sababu sisi hatuzalishi ajira, hatuhitaji mabilioni, haya mabilioni yaende huko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasimamia hizi sera, tunayo *TaESA* ambayo wanasaidia vilevile kuonyesha fursa za ajira zilipo, tunashirikiana na watu kama *ILO* katika kufundisha wajasiriamali, tuna hizi program kama ajira nje nje ambazo mmezitaja Waheshimiwa hapa na mipango mingine. Lakini kwa sasa tumezamia sana katika kutengeneza mfumo wa kuweza ku-*capture* takwimu za ajira, *labour market information system* ambayo tukiikamilisha, tutakuwa na uwezo mzuri sana wa kujua ajira ngapi tunazalisha na kadhalika. Lakini vilevile tunahuisha sasa masuala ya ajira kwenye program mbalimbali na *plans* za kila Wizara yaani *mainstreaming of the employment issues* katika *plans* na bajeti za Serikali. Tukifanya hivyo, tutakuwa na uwezo wa kujua ajira zinazalishwaje kila mahali. Lakini vilevile tunaanza ku-*coordinate* kujua watu wasiokuwa na ajira wako wangapi, wako wapi,

namna gani tuweze kuwasaidia kwenye elimu, mafunzo kwenye mitaji na kadhalika na kazi hiyo tutaendelea nayo kwa bajeti hii ndogo lakini tukiongezewa mwaka ujao tutafanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, wanasema nyie mmezalisha ajira ngapi? Tumesema mwaka jana tu tulizalisha karibu ajira laki mbili na nusu na tumetaja pale. Mwaka huu unaokuja na ni mifano, kwa kweli hii ni mifano midogo sana. Hii ajira laki nane tunasema ambazo tutazalisha mwaka kesho kwenye maeneo mbalimbali, Serikalini, biashara, ujenzi, kilimo, ni mifano midogo nina hakika tutafanya kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, jamani ajira za wageni, nisipomaliza Mheshimiwa Waziri ataongezea, ni suala zito na mimi nimefanya ukaguzi na nikuhakikishie Mheshimiwa Bulaya nimekwenda kwenye hoteli za kule Arusha na Mheshimiwa Nassari nikwambie nimefika pale *Hotel and Lodges* na huyo mtu uliyemtaja nilimfukuza mimi na iliandikwa kwenye magazeti baada ya siku chache amekwenda India kumbe amerudi, sasa nataka kusema hapa tukimaliza hapa asiwepo hapa nchini. Maana yangu ni kwamba lazima tutunze ajira za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuna Sheria ya mwaka 1999 ya Ajira, tuna Sheria ya Uhamiaji tunajaribu kuzioanisha, tutaleta hapa Bungeni ili anayetakiwa kutoa kibali cha ajira ajulikane kwamba ni Wizara ya Kazi na Ajira na wala sio *Immigration.* Hilo tutalibadilisha kwa sababu ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, *TaESA* wameendelea kufanya kazi nzuri, ajira za watoto na walemavu ni mambo ambayo tunayakazania sana kwa kufuata zile Sheria. Sheria za Mtoto lakini na Sheria ya Ajira hasa ile Sheria ambayo inataka kila mwajiri aajiri angalau asilimia tatu lakini katika maeneo niliyopita hata asilimia moja haijafika, bado iko chini, hatujawaajiri watu wenye ulemavu kama inavyotakiwa lakini yote haya tutayafanya.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya migogoro ya kazi, atakuja Mheshimiwa Waziri atayaelezea vizuri na mengine yale ya pensheni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mambo ni mengi lakini tutaleta tena kwenye maandishi kila kitu ambacho tumekisema. Niseme tu kwamba mtuachie mimi na dada yangu tufanye kazi hizi ambazo mmezisema ili mwakani tukifika hapa tuwe na hakika hata na takwimu zetu zisiwe za kubabaisha, tuwe mbele sio kama nchi nyingine za Afrika ambazo zinatoa taarifa za mwaka 2005, tuwe *more current* lakini tunahitaji tuwezeshwe ili tuweze kufanya kazi hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga tena mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA**: Asante, Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA**: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunialika tena kuja hapa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi na kujibu hoja ambazo Mheshimiwa

Naibu Waziri, kaka yangu amejaribu kuziongelea lakini nyingine zimebaki na zile zinazohusu masuala ya sera hasa masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza, naomba nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wengi sana ambao wamechangia hasa kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza ni 12 ambao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakusya, Mheshimiwa Zainab R. Kawawa, Mheshimiwa Subira K. Mgalu, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema na Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi wa kwanza ni Mheshimiwa Cecilia D. Pareso, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Amos G. Makala, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Asaa Othaman Hamad, Mheshimiwa Augustino M. Masele,

Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Antony G. Mbassa, Mheshimiwa Dkt. David Malole, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa Ester N. Matiko, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abuu H. Jumaa, Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mhesimiwa Jadi Simai Jadi, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mheshimiwa Jason Rweikiza, Mheshimiwa Josephine Chagula, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Juma Athuman Ali, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Kaika S. Talele. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mahamoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Namelok E. Sokoine, Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Rachel

Mashishanga Robert, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Rajab Haji Salehe, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Samia Sururu Hassan, Mheshimiwa Selemani S. Jafo, Mheshimiwa Sylvester Koka, Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhamed, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Subira K. Mgalu na Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Ramo Makani, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Said Mtanda, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Assumpter Mshama na Mheshimiwa Halima J. Mdee. Jumla ya waliochangia kwa maandishi ni wachangiaji 97.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa maelezo kama nilivyosema kwa kweli wachangiaji ni wengi, hatutaweza kujibu yote. Mheshimiwa Naibu Waziri amejitahidi sana kuongelea hasa hili suala la ajira ambalo katika Wazira yetu ndiyo *core subject* lakini pia tuna *labour issues*.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kwanza kwa kuelezea suala hili ambalo limezungumzwa na Kambi ya Upinzani katika maoni yao kuhusu uwekezaji usiokuwa na tija au uwekezaji katika maeneo ambayo si muhimu kwa kutumia Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii. Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii miwili au mitatu kwa pamoja imechangia katika maeneo kadhaa. Mengi yamezungumzwa asubuhi lakini nisingependa kuyarudia lakini nitaje machache kwa umuhimu zaidi: Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kimechangiwa na mifuko karibu yote. Chuo hiki na wote tunafahamu ni chuo ambacho Serikali ya CCM iliahidi na ni chuo ambacho kwa kweli kitachukua idadi kubwa ya vijana wetu wanaomaliza kidato cha sita na tuna-*plan* kwamba kitakapokuwa *full fredged* maana bado kinajengwa kitachukua zaidi ya wanafunzi 40,000. Ni chuo kikubwa ndani ya Afrika Mashariki na Kati, kwa sasa hivi kina wanafunzi 18,000 wa kozi mbalimbali lakini chuo hiki pia kimeweza kutengeneza ajira. Kwa harakaharaka kuna ajira zaidi ya 1000 ukiacha wale wanaotoa huduma mbalimbali pale chuoni hasa wakati wa ujenzi kuna huduma nyingi na ajira nyingi. Sasa sielewi kama huu ni uwekezaji ambao sio muhimu kwa Tanzania. Nafikiri Watanzania wengi watakapokuwa wanasikia hili kwa kweli watasikitika na nafikiri wenzetu hawakuwa na maana hiyo. Kwa hiyo, ningekuwa Spika ningesema waondoe maneno yao kwenye hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna uwekezaji kutumia Mifuko hii katika Shirika la *Kagera Sugar* kule Bukoba. Kama tunavyofahamu siku za nyuma kampuni hii iliwekeza kwa kutumia mvua ya Mwenyezi Mungu na

ilianza kutetereka kwa mashamba kukauka kwa sababu mvua zenyewe hazina uhakika na kiwanda kile kilianza kufa kwa wale ambao tunajua historia ya kiwanda kile. Lakini kwa kutumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *NSSF* na *PSPF* sasa hivi ukiingia *Kagera Sugar* kama hutajua umepitia Kagera hauwezi kujua kama uko Tanzania kwa maana ya uwekezaji mkubwa ulioko pale. Wana mashine kubwa za kumwagilia na kazi kubwa inayofanyika pale ni ajira kwa Watanzania na wameajiri zaidi ya watu 3,500 na *concept* nzima ya Kilimo Kwanza iko pale. Nashauri kwa wenzetu ambao wanafikiri na huu pia sio uwekezaji muhimu watuambie uwekezaji muhimu ni wa namna gani wakati tunatengeneza ajira; lakini pia kiwanda hicho kinatengeneza sukari ambayo ni bidhaa muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kigamboni kutakuwa na daraja kubwa ambalo litaondoa adha kubwa kwa Watanzania na haswa wanaoishi Dar es Salaam, lakini ajira zitakazopatikana pale za kudumu zitakuwa zaidi ya 1000 na ajira za muda mfupi ni karibu 3,000 na karibu zinaanza.

Mheshimiwa Spika, tukiacha maeneo hayo, kwa ujumla tuseme, mimi sikusomea Kiswahili lakini kuna msemo unaosema akutukanaye sijui anafanyaje; lakini tuishie hapo. Kwa hiyo, mimi nafikiri wakati tunashauri na wakati tunazungumza, kwa kweli tuangalie zile *national interest,* tuzizungumze *very positively* na kama hakuna kitu basi tusizungumze kwa njia hiyo. Wengi wanafahamu kwamba huu ndiyo ukweli kwa hiyo sikujua kwa nini hii sehemu iliandikwa namna hii.

Mheshimiwa Spika, niseme hivi, anayesema kwamba mashirika haya katika kuwekeza yanakufa, kigezo kizuri cha kupima uwezo wa Shirika hasa haya ya Hifadhi ya Jamii, ni kutumia *actuarial valuation*. Nikiangalia kwa mfano Shirika la *NSSF* lilifanyiwa *actuarial valuation* mwaka 2009 na hii haikufanywa na Mtanzania sababu Tanzania hatuna *actuary* wa kufanya kazi hii. Mtaalam George Langis ambaye alitoka Canada ndiyo aliyefanya kazi hiyo na aliletwa na *ILO*. Katika *actuarial valuation* hiyo alisema tathmini ya Shirika la *NSSF* matokeo yanaonyesha kwamba *reserve ratio* ni 6.8. *Reserve ration* kuwa 6.8 ina maana gani? Ina maana kwamba Shirika la *NSSF*, nimechukua Shirika hili kwa sababu ndiyo lipo chini ya Wizara yangu *directly* na ndiyo ninaweza kupata hizo takwimu lakini hili Shirika linaweza kumudu kulipa mafao yote kwa wanachama na kulipa gharama zote za uendeshaji wa Shirika kwa muda wa miaka sita na miezi minane bila kuingiza hata senti moja kwa maana ya ukusanyaji wa michango au mapato kutoka kwa vitega uchumi vyake bila vingine kutetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaweza kufanya mambo ya *administrative cost* lakini na kuwalipa wadau wake mafao bila kuchangisha kwa muda wa miaka sita. Sasa Shirika linalofilisika haliwezi kufanya haya. Lakini mashirika mengi ya hifadhi ya jamii yameshafanyiwa *actuarial valuation* na zote zinaonyesha kwamba hayana matatizo kama ambavyo yanahisiwa. Ndiyo maana tunasema *no research no right to speak.* Mimi nafikiri tukubaliane hilo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba *NSSF* pia imewekeza katika maeneo ambayo yapo nyuma kimaendeleo. Mimi nafikiri nirudie kusema kwamba uwekezaji wa *NSSF* unazingatia uwezo wa mradi wa kuweza kurudisha mtaji wa fedha lakini pia Shirika linafanya upembuzi yakinifu ili kubaini maeneo mazuri ya kuwekeza kulingana na Sera ya Uwekezaji wa shirika lenyewe. Shirika litaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio, televisheni na vipeperushi na semina nchi nzima kupitia ofisi zake za Mikoa lakini pia mikutano ya wadau ambapo mkutano wa mwisho ulikuwa Februari na niliwaalika Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Zitto Kabwe alihudhuria na aliona jinsi wanachama walivyokuwa wanashukuru kwa kuwa sehemu ya *NSSF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilizungumzwa kuhusu *NSSF* ni hili suala la ukaguzi wa *CAG*. Taarifa hii kwanza naomba niseme imekabidhiwa kwa Spika ili iweze kujadiliwa na Kamati ya *POAC* ambayo Mwenyekiti wake anatoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa hiyo, tulikuwa hatuna haraka ya kuzungumzia hili kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(b) lakini hiyo ripoti itawekwa Mezani na itajadiliwa. Hata hivyo, kwa kuwa shutuma hii imetolewa na ni nzito, basi naomba niijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *CAG* inaonesha uchambuzi wa miradi ambayo tayari ilikwishafanywa

na sio ile ambayo inatarajiwa kufanywa na jambo lingine ni kwamba miradi yote na vitega uchumi vya *NSSF* vinafanywa kwa utashi na maamuzi ya Bodi ya Udhamini ya *NSSF* na sio kwa maagizo ya Serikali kwamba Serikali imeamua kuchukua pesa za wanachama wa mifuko imewekeza kwenye vitega uchumi na nimeshaeleza faida zake kwa ajili ya Watanzania wote lakini nimesema Mifuko hii haifilisiki kwa sababu hiyo na sio Serikali inayoagiza Mfuko wa *NSSF* au Mfuko wa Hifadhi wa Jamii wowote kwamba lete pesa tuwekeze. Bodi ndiyo inayokaa na kuweka mikakati lakini baada ya Serikali kuzungumza na ku-*negotiate* kuhusu mradi unaombewa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na Sera ya Uwekezaji, miradi yote mitano ilyotajwa kwa mfano huo wa Mchikichini, Daraja la Kigamboni, Jengo la Maadili, umeme Mkuranga, ni miradi ya kibiashara na itarudisha fedha za uwekezaji na faida yake. Kwa hiyo, miradi isiyoweza kukidhi kanuni, haiwezi kutekelezwa na *NSSF*. Kwa maana wanao wataalam, wana watu ambao wanaweza kuwashauri na wana Mainjinia ambao wanaweza kufanya kazi hiyo. Kwa mfano, ilibidi Serikali itoe ruzuku ya asilimia 40 ya gharama ili kuwezesha Shirika kuwekeza katika mradi wa Daraja la Kigamboni. Kwa hiyo, hii ni *PPP arrangement* kati ya Serikali na *NSSF* ili tuweze kujenga lile daraja kwa maendeleo ya nchi lakini pia kwa faida ya Watanzania wote na hasa wale wanaoishi Dar es Salaam na wale waliopata viwanja huko Kigamboni hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kuna hili la *Machinga Complex*, hili pia Halmashauri ya Jiji inafahamu kabisa hili deni

lazima lilipwe na tumefanya juhudi kubwa sana, Serikali, Halmashauri ya Jiji pamoja na shirika lenyewe kwa kweli jiji wakaanza kulipa pesa za jengo lile. Kwa sababu nia ilikuwa nzuri na *NSSF* ilikuwa tayari kwenda kujenga majengo mengine ya namna hii katika Mikoa mingine ili kusaidia vijana wetu ambao wanifanya ujasiliamali wasizagae mitaani lakini wapate sehemu moja ya kuweza kukaa na kufanya biashara. Kwa hiyo, mikataba imewekwa vizuri na vitega uchumi vyote hivi kuna mikataba halali ambayo imesainiwa.

Mheshimiwa Spika, nimeshaeleza juu ya mashaka ya kifedha yanayohusu mifuko hii. Kipimo pekee ni umahiri wa kuchagua mradi kifedha lakini pia *actuarial valuation.*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo kwamba Serikali isitishe miradi ya *NSSF,* nafikiri sasa baada ya maelezo haya jambo hili limeeleweka, Serikali haishughuliki kabisa kuielekeza *NSSF* au mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii uwekeze wapi.

Mheshimiwa Spika, Mbunge mmoja alichangia kwamba Rais awawajibishe watendaji wote wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Siwezi kumshauri Rais kwa sababu siyo kazi yake hii, wana Bodi zao na kama kuna matatizo yanashughulikiwa kibodi, kwa hiyo, Serikali haiingiliani na masuala haya.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Diana Mkumbo kwa pongezi zake kwa *NSSF,* kwa Dkt. Dau na watendaji, lakini ombi lake ni kwamba Mifuko iongeze viwango vya *pension*. Ni kweli

*NSSF* inaboresha *pension* mara kwa mara na kwa mfano mwaka 2006 *pension* iliboreshwa kwa kati ya asilimia 14 mpaka asilimia 80. Hilo ni ongezeko kubwa sana la *pension* na mwaka 2010 pensheni hiyo iliboreshwa kwa asilimia 52, kwa hiyo ilizidi hiyo asilimia 80. Kwa marekebisho ya sheria hii mpya, sasa hivi kupitia *SSRA,* Mifuko hii itaanza pamoja na fomula zao lakini ifanye *indexation*. Maana yake ni kwamba kila mara mafao yaendane na thamani ya pesa ya wakati huo. Kwa hiyo, pensheni hizo zitaboreshwa na ninawashauri mjiunge ingawa sisi hatuwezi kuingia kwenye *pension* kwa sababu ni *supplementary scheme* lakini hata hivyo Wabunge wengi naona wamechangamkia kujiunga na *NSSF*, nawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine la Mheshimiwa Diana ni kwamba *NSSF* iwekeze kwenye ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu. Kufuatana na Sera ya Uwekezaji wa Shirika, mradi wowote unaoweza kufanywa ni lazima uonekane unakidhi vigezo vya kuwekeza na kuweza kurejesha pesa za wanachama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgalu alitoa pongezi na akaomba kwamba *NSSF* wawekeze zaidi hasa Mkoa wa Pwani, naamini wamesikia na wataweza kufanya hivyo watakapokuwa wame-*study* hali halisi ya mradi na kuona kama utarudisha pesa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika amesema ujenzi wa Apolo *Hospital* kwenye viwanja vya Chuo Kikuu uhusishe wadau wote ili kuwa na uelewa na mwelekeo wa pamoja tokea hatua za

awali. Pia Mheshimiwa Mnyika, amesema ujenzi wa Jengo la Maadili, kiwanja kina mgogoro hivyo Serikali iingilie kati ili kiwanja hicho kisiendelezwe na Sekretariati ya Maadili ya Umma. *Well*, mradi wa ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Apolo ni suala la kitaalam linalowahusu zaidi wamiliki, washauri na wajenzi. Tutajitahidi kuwahusisha wadau wengine kwa kadri inavyoonekana kwamba inafaa na ushauri kuhusu kiwanja pia tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Mdee amesema uwekezaji wa *NSSF* ufanywe kwenye maeneo ya biashara zenye manufaa, tunakubali, inafanywa hivyo kwa sababu ni uwekezaji wa kibiashara. Aidha, anasema Waziri atoe taarifa Bungeni fedha zote ambazo Serikali na kampuni binafsi ilizokopa na marejesho yake. Sawa, nitatoa, nafikiri walimaanisha *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, *in fact* pesa ambazo Serikali wamewekeana mikataba kwa mfano *UDOM,* nyingi zimeanza kulipwa. Suala la mkataba lilikuwa na utata lakini kupitia ofisi ya *AG,* utata ule umeondolewa. Kwa hiyo, sasa hivi Serikali na *NSSF* wana mawasiliano mazuri kuhusu kulipa pesa ya ujenzi wa majengo ya *UDOM*.

Mheshimiwa Spika, sina uhakiki na hili swali la Waziri atoe taarifa ya wakopeshwaji sugu na hatua ambazo Wizara imechukua, wakopeshwaji sugu wengi wamepelekwa Mahakamani, kwa mfano kuna *Continental Venture* na kadhalika. Hawa wamepelekwa Mahakamani, nafikiri taarifa hiyo inatosheleza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya ameuliza kwamba wanachama wananufaika vipi na uwekezaji wa *NSSF*. Kwa jinsi Mfuko ulivyoundwa una mafao saba na ni mazuri. Hayawezi kutolewa kwa kutumia michango tu bali kwa kutumia michango na mapato kutoka vitega uchumi na ndiyo maana ya hivi vitega uchumi kwa kweli. Pamoja na kuweka *fast lifting* ya miji yetu lakini nenda Ghana uone, Mheshimiwa Jenista Mhagama amezungumzia Malyasia, mimi sijafika Malyasia lakini nimeenda Ghana, majengo yote mazuri, vitega uchumi, *conference halls* za Serikali na kadhalika yamejengwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tena Ghana wana Mfuko wa mmoja tu na ndiyo umefanya kazi zote hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Augustino Masele anatoa pongezi kwa *NSSF*, pia Mheshimiwa Abbas Mtemvu, tunashukuru sana kwa pongezi hizi. Fidia kwa kampuni ya *Oilcom* na Miembesaba *Limited* ilipwe mapema ili kupisha ujenzi wa daraja la Kigamboni. Wizara ya Ardhi inafanya tathmini ya fidia hii kwa wale wote wenye viwanja katika eneo la mradi huu. Mara tu zoezi hilo litakapokuwa limekamilika basi *NSSF* italipa. Swali hili lilitoka kwa Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mbunge wa Temeke na ana sababu ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zabein Muhaji, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, anatoa pongezi, tunashukuru na amesema *NSSF* isaidie kuchimba visima Jimbo la Kondoa Kaskazini na ombi litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum anasema huduma za afya kwa mafao ya *NSSF* ni hafifu, hospitali walizoingia nazo mikataba hazina vifaa na madawa. *NSSF* imeingia mikataba na hospitali zaidi ya mia tatu nchi nzima, hospitali hizo zinatakiwa zifanye kazi kwa mujibu wa mikataba maana wamewekeana mikataba na zile ambazo zinakiuka mikataba basi huduma huwa zinasitishwa mara moja. Kwa hiyo, kama wewe ni mdau umeona jambo hilo, tunaomba utupe taarifa ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji usiokuwa na tija umezungumziwa na watu wengi kwa mfano Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, wa Kambi pia ya Upinzani ilizungumzia kuhusu suala la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umetumia shilingi bilioni 13.403 katika uwekezaji huu ambao hauna tija na walitaja uwekezaji katika *Medical Care Centre* ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Lakini tunasema hili eneo pia linalenga kuhakikisha kwamba kuna huduma nzuri za rufaa hapa nchini. Angalia Dodoma, Mbunge wa Dodoma alikuwa anazungumza kuhusu Hospitali ya *General* inavyokuwa *congested* hasa tunapokuwepo hapa. Kwa hiyo, hiki kituo cha Chuo Kikuu kitakapokuwa kimekuwa tayari ambacho pia kitakuwa ni *referral hospital* na *teaching hospital* kitasaidia sana. Kwa hiyo, hivi ni vitega uchumi ambavyo hata havina sababu ya kuvi-*doubt* lakini kinachotakiwa ni kwamba uwekezaji uende kwa masharti na Bodi inavyoshauri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sasa suala la Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA).*

Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, anasema Tume ifungue pia ofisi nyingine Wilayani. Ushauri umepokelewa, Serikali itafanya hivyo tutakapokuwa tumepata pesa kwa sababu huduma za *CMA* zinatakiwa kuwa karibu na watu kwa sababu kila mahali kuna wafanyakazi na kila mahali pa kazi kuna migogoro na migogoro hiyo haiwezi kusubiri mpaka iende Mikoani. Kwa hiyo, hilo ni ombi zuri lakini katika nchi nzima tuna Wilaya tano ukiacha Mikoa maana kila Mkoa kuna ofisi ya *CMA* lakini pia tuna Wilaya tano ambazo ni Muheza, Korogwe, Mufindi na Njombe kwa hiyo kama ni Wilaya ya kwako basi tutaona hali halisi.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya ucheleweshaji wa kusikiliza mashauri, *well*, *CMA* inasikiliza mashauri kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Na.6 ya mwaka 2004 na kanuni zake. Kwa mujibu wa sheria hii, mashauri huanza kusikilizwa kwa njia ya usuluhishi ndani ya siku thelathini na baada ya hapo ushauri hupelekwa hatua za uamuz. Lakini tatizo linakuja, huwa kunatokea *preliminary objections* nyingi sana mara mmojawapo katika zile *parties* hataki labda huyu asikilize, kwa hiyo hizo ndiyo zinachelewesha. Lakini wamejiwekea mikakati ya kusikiliza kesi zao haraka sana ndani ya siku thelathini.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi iwezeshwe bajeti ili kufanya kazi zake, hiyo ni kweli Mheshimiwa Margaret Sitta aliliongelea hili.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba *CMA* haifahamiki sehemu nyingi, hilo alizungumzia Dkt

Kebwe. Tume inajitahidi kujitangaza, imefungua ofisi kila Mkoa…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tupo ndani ya Bunge acheni mazungumzo.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, lakini tutajitahidi pia kutayarisha vipeperushi vingi ili *CMA* iweze kufahamika zaidi.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni kengele ya kwanza na nafikiri kengele ya pili inakuja, naomba nizungumzie kidogo hili suala la Vyama vya Wafanyakazi ambalo amelizungumzia pia Mheshimiwa Ndassa. Ukweli ni kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mahusiano Kazini, kifungu cha 51 na 52, Vyama vya Wafanyakazi vilivyosajiliwa vinawajibika kuwasaidia wafanyakazi wao kwa kutumia michango ya asilimia mbili. Baadhi ya kazi hizo, ni kuwasaidia kutatua migogoro kwa kuweka Mawakili au vyama vyenyewe kuwasaidia katika hilo. Kama mlivyoona juzi Chama cha Wafanyakazi cha Walimu kilikuwa bega kwa bega na Walimu wetu katika kuhakikisha kwamba wanapata maslahi yao. Kwa hiyo, pesa zinatumika hivyo na wanakaguliwa. Kwa mfano Chama cha Walimu kinakaguliwa na *Logical Accountant and Business Advisers* wa Dar es Salaam. Nitaleta majibu mengine kwa ufasaha kulingana na maswali mengine aliyoyauliza ambayo majibu yake siwezi kuwa nayo hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Haji alichangia kuhusu chama cha *TUICO* Makao Makuu na

kuuliza kimekufa? Naomba kumpa taarifa tu kwamba alipozungumzia suala la wafanyakazi wa majumbani, chama kinachohusika ni Chama cha *CHODAWU* na siyo chama cha *TUICO*. *TUICO* haijakufa na Katibu Mkuu wake ni Ndugu Mkakatisi yupo pale juu na amesikitika sana kusikia Chama chake kimekufa au kiko *ICU*. Ni chama kikubwa sana kinashughulika na masuala ya taasisi za kibenki na nafikiri ni chama cha pili ukiacha chama cha Walimu kuwa na wafanyakazi wengi. Kwa hiyo, naomba Katibu Mkuu hili lisikusikitishe ni kwa sababu tu Mheshimiwa Haji kama alivyosema mwenyewe alikuwa hana uhakika ni chama gani kinashughulikia wafanyakazi wa majumbani.

Mheshimiwa Spika, katika migogoro hii na unyanyasaji wa wafanyakazi majumbani, tumeshausaini mkataba lakini tutauleta Bungeni kuuridhia na baada ya kuridhia ule mkataba sasa itabidi sheria ifuate mkondo wake kwa waajiri wanaowanyanyasa wafanyakazi wa majumbani ikiwemo kuwanyima chakula, kuwalaza chini na kuwafanya kama nyumba ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, sina muda wa kutosha, naomba nikiri kwamba haitawezekana kujibu hoja zote lakini naomba niwashukuru sana Wabunge, inaonesha kwamba mnaifahamu Wizara yangu ya Kazi na Ajira na kazi zake na mngependa tufanye mambo mazuri zaidi. Kama alivyosema Naibu Waziri, kaka yangu, sisi tunafanya kazi na wabia, masuala ya ajira sisi ni *coordinators* na masuala ya kazi na *labor standards* tunashirikiana pia na waajiri wengine ikiwemo chama chetu cha Shirikisho la Chama cha

Waajiri *ATE* kwa ajili ya kuboresha na tunashirikiana nao vizuri sana pamoja na Vyama vyote vya Wafanyakazi ndiyo maana wamejaa hapa, tuna ushirikiano mzuri na tunaunda huo utatu ambao mpaka sasa unaendelea. Mheshimiwa Ndassa, utatu haujafa tangu enzi za JUWATA mpaka leo na ndiyo maana unaona wote tupo hapa tunashirikiana. Tuna Baraza letu *LESCO*, Upinzani wamesema *LESCO* ife, haiwezi kufa kwa sababu hatutakuwa na mahali pa kuongelea wafanyakazi, waajiri na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia ndugu zangu waliotoka Musoma kuja kunishuhudia hapa nawasilisha, ni njia ndefu lakini Mwalimu Mgini na Mwalimu Longino na Madereva na wengine wameamua kusafiri na kuja Dodoma. Nawashukuru sana kwa kuniunga mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja liamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, hatua inayofuata, Katibu!

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kif.1001 *Administration & HR Management……*...................Shs. 2,131,329,000/=

**MWENYEKITI:** Hii ni *Commission,* siyo mshahara wa Waziri, hili ni Baraza la Usuluhishi tu, *Commission* haina ugomvi na ninyi, tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 - Wizara ya Kazi na Ajira**

Kif.1001 *Administration & HR Management……*...........Shs.2,780,306,000/=

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri, ameshawaambia yeye hana hela, ninyi bado mnataka kuchukua?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilisikitishwa sana hotuba ya Waziri lakini vilevile hotuba ya Kambi ya Upinzani kutokuzungumzia suala lolote kuhusiana na sensa ambayo inakuja mwezi huu hasa tukizingatia kwamba Wizara hii ni lazima iwe na takwimu, takwimu ambazo itazipata katika sensa inayokuja. Je, Mheshimiwa Waziri, hivi ni kweli Wizara yako pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wako, Vyama vya Wafanyakazi Tanzania havikubaliana na sensa inayokuja mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Naomba msisikitike, umepata nafasi sema, sasa ukisikitika sisi hatuwezi kuona.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sensa liko chini ya Wizara ya Fedha na halihusiani *direct* na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba wafanyakazi hawakubaliani na sensa hii, wanakubaliana nayo kwa sababu wameshahamasishwa na hamna tatizo. Sijapata mgogoro wowote, Vyama vya Wafanyakazi havijaniambia kwamba wafanyakazi hawatahusika na sensa. Kwa hiyo, haikuwa *issue* ya kuzungumzia kwenye bajeti. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilipenda kupata ufafanuzi kuhusiana na Mfuko wa *Skill Development Levy* ambapo mashirika yote ya *private* pamoja na makampuni yanatoa asilimia sita (6) ya *payroll* zao kwa ajili ya Mfuko huu, asilimia mbili (2) ya Mfuko huu inakwenda kuimarisha vyuo vya *VETA*. Ningependa kujua asilimia nne (4) ya Mfuko huu inakwenda wapi na inafanya kazi gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoamua hapa wenyewe, asilimia nne (4) inakwenda kwenye elimu ya juu ambapo vijana wetu wanakopeshwa ili waweze kwenda shule, hiyo nyingine inakwenda kwenye *VETA*, lakini nyingine tuliamua kwamba iende kwenye elimu ya juu. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu utaratibu ambao unatumika kuajiri raia wa kigeni nikitoa mfano wa Wilaya ya Kibondo kuna Wakenya wawili ambao wameajiriwa kwenye Idara ya Afya na wamekaa pale, hawajui kinachoendelea ni nini, *payroll* za watu wengine zimetoka. Sasa nilitaka nipate ufafanuzi, mnatumia vigezo gani kuwaajiri watu hawa na kwa nini wanakaa muda mrefu bila kulipwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya wageni inatawaliwa na Sheria ya Ajira na inatawaliwa vilevile na Sheria ya Uhamiaji. Sasa kama nilivyotoa maelezo, inawezekana kuna matatizo katika mawasiliano kati ya Idara ya Kazi na watu wa *Immigration* kitu ambacho tutakuja kukirekebisha. Lakini mimi naamini kabisa kwamba kama ambavyo sheria zile zinasema wanatakiwa watu wa nje waajiriwe ambapo Watanzania wamekosekana wanaoweza kufanya kazi ile. Sasa kama kuna *specific issue,* watu wameajiriwa unadhani ni kinyume cha sheria hizo nilizozitaja basi nadhani tuwasiliane ili tufuatilie wao wameajiriwaje na wako Tanzania kwa namna gani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka ufafanuzi wa kisera wa Serikali pamoja na uamuzi wa kuahidi kwamba kwenye mkutano wa Bunge ujao italeta Muswada wa dharura kuhusiana na Fao la Kujitoa, nilitaka kauli ya Serikali juu ya agizo

lilitolewa na *SSRA* la kusitisha utoaji wa mafao ya kujitoa katika kipindi hiki cha miezi sita (6) na kuhusiana na wafanyakazi waliosimamishwa katika hatua ya kudai hayo mafao. Sasa iwapo Wizara inatoa kauli ya kutengua sitisho hilo na vilevile inatoa kauli ya kutaka kurejeshwa kwa wafanyakazi waliosimamishwa katika hatua ya madai ya fao hili la kujitoa, ningeomba kauli ya Wizara.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hiyo sheria imeshapita, imeshasainiwa na sisi tunakwenda kuleta marekebisho kwa ajili ya kurekebisha hilo suala la Fao la Kujitoa. Sasa hii anayosema agizo la *SSRA* halikuagizwa kama sera nafikiri ilikuwa tu ni katika utekelezaji wa sheria hiyo. Kwa hiyo, mimi nafikiri tutalifanyia kazi agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi labda niongezee tu kusema kwamba kwenye ile migodi ambayo imefanya fujo, wafanyakazi wamekuwa na fujo ndani ya mgodi kutokana na agizo hilo, mimi nafikiri wafanyakazi wawe na utulivu. Kama tulivyoagiza, sisi tutaleta marekebisho Bunge lijalo ni mwezi wa 11, ni mwezi mmoja na nusu au miwili, kwa hiyo, mimi nafikiri waendelee na maisha yao kama walivyokuwa wanafanya halafu tutaleta marekebisho. Baada ya marekebisho kazi nyingine zitaendelea. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu raia wa kigeni ambao ni Waindia ambao wako nchini na

wamekuwa wakifanya kazi kwenye hoteli za kitalii kwa kutumia *visitors pass* ambazo zimebadilishwa na kufanywa kuwa *CTA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati wa Hotuba ya Mambo ya Ndani niliuliza nikaambiwa wapo nchini kihalali, leo nimeleta ile *document* nime-*attach* kwenye mchango wangu na Mheshimiwa Naibu Waziri ameniambia kwamba yeye mwenyewe alimfukuza huyu mtu lakini amerudi nchini kinyume na sheria. Lakini napenda nimwambie kwamba huyo ni mmoja nimemtolea maelezo lakini wako watatu na ni zaidi ya hao, hiyo ni *sample* nimeileta. Vilevile napenda kumfahamisha kwamba huyo mtu alipomfukuza nchini hakuondoka nchini walimpeleka Zanzibar kwenye hoteli yao nyingine akajificha huko na baadaye wakamrudisha, yupo porini sasa anaendelea kufanya kazi. Sasa napenda kupata kauli ya Serikali kwamba hawa watu watafanyiwa kitu gani kwa sababu mwekezaji analeta watu wanafanya kazi kinyume na sheria, Waziri amewafukuza nchini hawajaondoka nchini wamekwenda Zanzibar wamerudishwa tena wanaendelea kufanya kazi. Nini kauli ya Serikali kwa watu hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Watu wa aina hiyo, hao mnaojuana mtakwenda pamoja.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumjibu Mheshimiwa Nassari pale mbele, akaniletea vikaratasi viwili nilidhani sasa ananiachia tu utekelezaji kwa maana ya ufuatiliaji lakini najua anataka kuzungumza vilevile ndani hapa,

nimhakikishie tu kwamba nitafuatilia. Lile jina moja ambalo amelileta tayari ninalo na kama nilivyosema huyu mtu nilimwondoa na nilizungumza na bosi mwenyewe wa hoteli zile za *Hotels and Lodgers* za kule Manyara na aliahidi kwa simu kwamba anamwondoa na nikathibitisha amemwondoa. Kwa hiyo, uliponiletea hii nikashangaa kidogo ndio maana nilisema tayari nimeshapeleka *message* kwa Afisa Kazi wa Mkoa wa Arusha alifuatilie aone kwamba huyu amerudi kwa njia gani? Ni kweli kwamba kuna huo ujanja wa kutumia hizo *visitors passes* wanasema kwamba ndio *CTA* lakini ni kuvunja sheria. Sasa sisi tuahidi kwamba tutaendelea kufuatilia. Naomba kwa sababu ya *capacity* mliyonayo, mnapopata hizi taarifa moja moja mkituletea hata kwa *message,* mimi watu wangu wanajua sana ninavyotumia *message* zinazokuja kwa malalamiko kwenye maeneo hayo, tutaendelea kufuatilia. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachotaka kusema ni kwamba tunaona kabisa katika nchi yetu kwa sasa suala la mwingiliano wa ajira kati ya Watanzania na wageni limeanza kuleta mgogoro mkubwa na wakati mwingine unapokwenda hata kwenye viwanda vya wageni vilivyopo hapa nchini kumekuwa na tabia ya wageni kutumia hata maeneo hayo ya viwanda kuwa ni nyumba za makazi za kuwaficha wafanyakazi ambao wanafanyakazi kwenye viwanda hivyo. Shida hii inazidi kukua kwenye nchi yetu. Sasa naomba ili kuwatendea haki wawekezaji wetu, lakini vilevile kuwatendea haki vijana wa Tanzania, wasomi waliosoma na wanaohitaji kupata ajira katika sekta

mbalimbali kwenye nchi yetu, kwa nini Mheshimiwa Waziri na Serikali isituletee sheria hiyo hapa Bungeni ili sasa tuweze kuwa na umakini wa kusimamia suala hili na atakayekiuka aweze kuchukuliwa sheria na hatua kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati na tuahidi kwamba huo mchakato utaendelea, tutaleta sheria hiyo.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba katika mahoteli mengi ya wawekezaji kuna wafanyakazi wa daraja la kawaida tu siyo kazi maalum lakini wanaajiriwa kwa mikataba ya muda mfupi, kitu ambacho kinawanyima fursa yao ya mafao ya uzeeni. Sasa Serikali ina kauli gani kuhusiana na hili? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hatuna vibarua, kuna mikataba ya muda mfupi, kuna mikataba ya muda mrefu na muda maalum. Kwa hiyo, inawezekana hawa wanaajiriwa kwa mkataba huu wa muda mfupi. Wanachotakiwa ni kutimiza masharti yote ya kazi ya staha ikiwemo kuwawekea hayo mafao yao ya Hifadhi ya Jamii. Kwa wale wanakiuka, kwa kweli kaguzi zetu zikigundua tunawachukulia hatua. Sasa hivi kwa kweli vijana wetu wamekuwa *trained* kuchukua hatua kali ikiwemo kuwapa hiyo *compliance order* kwa kuwa ni ukiukaji wa sheria. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Katika kuchangia kwangu, nikiungana na michango ya wenzangu inaelekea suala la ukosefu wa ajira ni gumu lakini mimi nilikuwa naomba watu wenye ulemavu nimeelezwa hapo kwamba kuna taasisi zimejaribu kuwafundisha ili waweze kujiajiri, lakini najua taasisi hizo ziko mijini. Serikali ina mikakati gani ya kuwaelimisha watu wenye ulemavu katika maeneo mbalimbali ili nao wakaweza kujiajiri kivyao huko?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimjibu kifupi tu Mheshimiwa Margareth Mkanga kwamba kwa kweli suala hili kama nilivyosema ni suala ambalo sisi kama jamii kwa ujumla tunatakiwa tusaidie. Kwa hiyo, kama hiyo taasisi na mimi nataka nishukuru sana wenzetu wa *CCBRT* na wengine ambao wamesaidia sana katika kuwaelimisha wenzetu wenye ulemavu ili wapate ajira. Sasa pale ambapo hata taasisi za kijamii, *NGO*, zikajitokeza kusaidiana na Serikali basi zifanye hivyo. Sisi tutafanya kwa uwezo ule ambao utakuwepo wa Serikali.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati nachangia kwa maandishi nilizungumzia kuhusu mazingira magumu hasa yanayohatarisha afya za wafanyakazi migodini na nikaeleza kwamba hivi tunavyozungumza kuna wafanyakazi wengi wanaofanyakazi Mgodi wa Bulyanhulu hasa kule *underground* ambao wako hospitali, lakini mwajiri hawatazami. Mara nyingine wanapokuwa wagonjwa kwa muda mrefu anawa-

*terminate* na anakana kwamba magonjwa waliyonayo ni *work related*. Nilitaka kujua Serikali inachukua hatua gani kusaidia hawa wafanyakazi wa aina hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo tunalifahamu na tayari tunayo taarifa ya wagonjwa kutoka Mgodi wa Bulyanhulu ambao wako Dar es Salaam. *OSHA* wanajitahidi sasa hivi kwa kweli kwenda kufanya hizi kaguzi za usalama na afya maeneo ya kazi na tunapokuwa tumegundua matatizo kama haya tunachukua hatua stahiki na tunawaomba wale waajiri waweze kulipa fidia. Kwa migodi hii ambayo kuna wagonjwa tayari kwa kweli tuna- *sympathise* lakini mimi niahidi tu kwamba tutaendelea kutumia kitengo hiki cha *OSHA* kutumia sheria yao ambayo inahakikisha kwamba waajiri hawa wanawahudumia wale wafanyakazi wao ambao wanaumia kutokana na athari za kazi.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa *NSSF* imeendelea kufanya vizuri kwenye uwekezaji na kwa kuwa Serikali inapaswa iendelee kukopa fedha nyingi kutoka hivi vyombo, nilikuwa nafikiria kwamba sasa ni muda muafaka kwa *NSSF* kuja kujenga mfano nyumba za Walimu Tanzania nzima ili Serikali iwalipe kidogo kidogo kwa sababu wana-*reserve* kubwa, je, Serikali inasema vipi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* wamesikia watawasiliana na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu wa maandishi niliandika kuhusiana na malalamiko ya vyombo kama *CMA* na vyombo vingine vya kutetea wafanyakazi kama Ofisi za Kazi za Mikoa kutumika badala ya kuwatetea wafanyakazi vimekuwa vikitumika kwa namna fulani kuwakandamiza wafanyakazi aidha, kwa kutumia udhaifu wao wa uelewa wa Sheria za Kazi na kadhalika. Hii ilijitokeza mfano kwa Afisa Kazi wa Dar es Salaam mwaka jana Kamati yetu ilipokwenda kutembelea Kiwanda cha *Jambo Plastic,* ilidhihirika wazi kwamba Afisa Kazi wa Mkoa wa Dar es Salaam alitumika na kile kiwanda kuwapotosha wafanyakazi na hatimaye wafanyakazi zaidi ya 400 wakapoteza haki zao na mpaka sasa wako nje wanalalamika kila siku wanatuma *message*. Mbaya zaidi ni kwamba yule mtu ilipobainika kwamba kafanya makosa badala ya kuchukuliwa hatua akarudishwa Wizarani. Nataka kauli ya Serikali kuhusu watu kama hawa ambao wanatumia vyombo hivi kama *CMA* na vingine kwa namna ya rushwa kukandamiza wafanyakazi badala ya kuwasaidia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbilinyi anajua kabisa kwamba *CMA* inasaidia sana kutatua migogoro na kutoa haki mahali pa kazi. Suala la Walimu limepitia *CMA* limeishia Mahakama ya Kazi na hawakunyanyaswa. Lakini inaweza ikatokea hatua ambayo inafikia kutoelewana kati ya mfakanyakazi na *CMA*. Mara nyingi ni kutokana na kutofuata taratibu za migomo na mambo ya kufanya katika sehemu za kazi.

Kwa hiyo, hapo sasa kama mfanyakazi haelewi *CMA* itampa tuzo yule mwajiri. Suala la *Jambo Plastic* liko Mahakamani na huyu Afisa tuliyemhamisha kuja Wizarani, hatujahakikisha kwamba alipewa rushwa, lakini kutokana na tuhuma zilizokuwepo tumeona arudi Wizarani kusudi tuweke mtu mwingine pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (2) zimebakia dakika tano, kwanza nimefanya kinyume, tunaendelea na *guillotine*.

**Fungu 65 - Wizara ya Kazi na Ajira**

Kif.1001 *Administration & HR Management*……….............Shs.2,780,306,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts ......*Shs. 337,060,000/=
Kif. 1003- *Policy and Planning.......*Shs. 356,027,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit .......*Shs. 128,676,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Management Unit .........*Shs………………… 187,251,000/=
Kif.1006 –*Government Communication Unit......*Shs……………………132,430,000/=
Kif.1007–*Information and Communication Tech Unit.....*Shs. 107,880,000/=
Kif. 2001 – *Labour*................................Shs. 7,210,126,000/=
Kif. 2002 – *Employment Division* Shs. 1,750,951,000/=
Kif. 2003 – *Registrar of Trade Union.* Shs. 118,791,000/=
Kif.5001–*Youth Development*...................Shs.0/=

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 65 - Wizara ya Kazi na Ajira**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.............Shs.0/=
Kif.1003- *Policy and Planning*..Shs. 1,276,925,000/=
Kif.2001 – *Labour*............Shs. 708,425,000/=
Kif.2002 – *Employment Division*.. Shs.850,450,000/=
Kif.500 – *Youth Development* ........Shs. 0/=

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira na Taasisi, zake kwa mwaka wa 2012/2013, Mafungu kwa Mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na Watalaam wake wote na Vyama vyote vya Wafanyakazi kwa kazi nzuri wanazozifanya. Sehemu ya kazi na ajira ni muhimu sana katika nchi yetu, tujaribu kwenda kiutawala wa kisheria kusudi tuweze kwenda mbele. Kwa sababu mambo yote yasiyokuwa mazuri hayana faida kwa mtu yeyote. Pale panapokuwa na kasoro basi tutumie vyombo vinavyohusika kuweza kutatua migogoro yetu. Tunawatakia kazi njema katika kipindi kinachokuja.

Waheshimiwa Wabunge, pia nina matangazo machache hapa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, anaomba niwatangazie Wabunge kwamba kesho tarehe 8 wataendelea na kazi waliyoanza saa tatu na nusu asubuhi katika ukumbi namba 231. Kwa hiyo, Kamati ya Fedha na Uchumi, kesho mtaendelea na kazi kuanzia saa tatu. Kesho ni *public holiday* lakini mnalazimia kufanya kazi hiyo, kwa hiyo, mnahitajika kufika bila kukosa.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Amos Makalla, anawatangazia Wabunge wote kusheherekea Sikukuu ya Nanenane hapa Dodoma kesho tarehe 8/8/2012. Timu ya *Bunge Sports Club* ya Mpira wa Miguu na Netball itacheza na timu ya *Mwananchi Communication Limited* kutoka Dar es Salaam katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa tisa na nusu alasiri. Wote mnaomba kuhudhuria mkaishangilie timu yenu. *(Makofi)*

Lakini vile vile tuna habari njema kwamba Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Idd Azzan pamoja na kwamba jana alinusurika kwenye ajali lakini Mwenyezi Mungu amewajalia na mke wake wamepata watoto mapacha. Siyo mapacha tu watatu kwa mpigo. Sasa hapo Mungu akupe nini. Kwa hiyo, amepata watoto watatu jamani tumshukuru Mungu kwa hilo na kwamba pia alinusurika jana kwenye ajali. *(Makofi)*

Pia ninapenda kuwatangazieni kwamba jioni Mheshimiwa Alhaji Missanga na wenzie wametukaribisha kwenye futari hapo kwenye *bassment* saa 12.30.

Lakini kesho tarehe 8/8/2012 saa 12.15 jioni, Mheshimiwa John Tendwa, Msajili wa Vyama vya Siasa ameleta mwaliko kwa Wabunge wote kwa ajili ya kufuturu. Tarehe 8/8/2012 saa 12.15 jioni katika mgahawa wa Sanjai Park, ipo uwanja wa Nanenane karibu na banda la JKT na Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, mnakwenda kusherehekea kulekule na kufuturu kulekule. Kwa hiyo, mnakaribishwa wote.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, ninapenda pia kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Abdallah Juma Saadala alikuwa anaelekea Dar es Salaam amepata ajali ambayo imetokea katika eneo la Maembesaba Kibaha. Mheshimiwa Waziri anaendelea vizuri na amepelekwa Hospitali ya Tumbi Kibaha kwa msaada wa Mheshimiwa Membe nadhani walikuwa wameongozana kwa uchunguzi wa awali wa

matibabu. Katika gari hilo alikuwa na watoto na msichana wa kazi. Watoto pia wanaendelea vizuri. Dereva na wasichana wa kazi wamepata michubuko wamekimbizwa hospitalini kwa uchunguzi wa awali kwa ajili ya matibabu. Kwa hiyo, hii ni taarifa nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa kazi mliyofanya mpaka leo, mmefanyakazi kwa nidhamu nzuri kabisa na wananchi wanatutegemea, hivyo wanataka tutumie muda wao vizuri zaidi kuliko tulivyokuwa tunafanya. Mimi katika maisha yangu habari ya Miongozo nimesikia safari hii lakini siku zote nilikuwa sisikii. Kwa hiyo, busara inawaambia Kanuni ile ya Mwongozo siyo kila kitu unasimama ukifurahi tu, kwa sababu tuna ratiba, tuna *Order Paper* na Kanuni zinasisitiza kwamba mtakwenda kwa mujibu wa *Order Paper* kama mtu atakuwa na Mwongozo basi mnamwandikia Spika kwamba unataka kusema kitu gani kusudi akuweke sawa. Vinginevyo tunakuambia kaa chini, ukisimama tu hivihivi, kila mtu anasimama si kweli wananchi hawapendi.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge Tundu Lissu alikuwa amesimama kutaka Kiti kimsikilize)*

**SPIKA:** Tuangalie Kanuni, siyo Mahakamani hapa. Mheshimiwa Tundu Lissu na wewe ndio unayeongoza kwa mambo haya. *(Makofi/Kicheko)*

*Parliamentary Practice* ndio maana kuna Kanuni, hata Mwongozo wenyewe unao utaratibu, hata taarifa yenyewe ina utaratibu, hata mambo ya dharura kuna

taratibu. Halafu unaona mnavyofanya, mtu anasimama anataka kumuunga mkono kwenye Mwongozo, mlisikia wapi, haya hayapo! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwatakie sikukuu njema na wanaofuturu waende wafuturu vizuri. Naahirisha Bunge mpaka tarehe 9/8/2012, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.05 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Agosti, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*